

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Hamsini na Nane – Tarehe 3 Julai, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka na Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*]

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*]

**MHE. ESTER M. MMASI – (K.n.y. MHE. DOTTO M. BITEKO  
- MWENYEKITI WA KAMATI YA PAMOJA):**

Maoni ya Kamati ya Pamoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of unconscionable Terms) Bill, 2017*].

Maoni ya Kamati ya Pamoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*].

**MHE. DAVID E. SILINDE – MSEMaji MKUU WA KAMBI  
YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*].

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources Contracts (review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*].

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 478

### Mradi wa Maji Chankolongo – Geita

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa maji wa Chankolongo katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita utakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremia Maselle Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilianza kutekeleza mradi mpya wa maji wa Chankolongo mwaka 2014/2014 ukiwa ni mojawapo ya miradi ya vijiji 10 kwa kufanya usanifu upya na kusaini mikataba ya ujenzi mwezi Machi, 2014 wenye thamani ya shilingi bilioni 4.39 baada ya mradi wa awali wa Nyakagomba kushindikana hadi kuchakaa kwa miundombinu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi unalenga kutumia chanzo cha Ziwa victoria na utahudumia vijiji vinne vya Chankolongo, Chikobe, Chigunga na Kabugozo vyenye wakazi wapatao 24,724. Kazi yote ina mikataba sita iliyoandaliwa na kusimamiwa na *COWI (T) Consulting Engineers and Planners* kwa kushirikiana na *Association with Environmental Consult Limited*. kama Mtaalam Mshauri. Malipo yaliofanyika hdi ssa ni kiasi cha shilingi bilioni 1.99 ambayo ni sawa na asilimia 45.3 ya gharama ya mradi, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulikumbwa na changamoto kutokana na uwezo mdogo wa mkandasi (*Fare*

*Tanzania Limited*) aliyekuwa akijenga choteo na kusambaza mabomba. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imesukuma utekelezaji wa mradi huu ambapo mkandarasi (*Fare Tanzania Limited*) ameingia makubaliano (*sub contract*) na kampuni nyingine iitwayo *Katoma Motor Factors Limited* ambayo inaleta mabomba yote ya mradi pamoja na pampu ndani ya mwezi huu wa Julai 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya sasa mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2017.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu kwa kunipa nafasi niuliza maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kweli kwamba changamoto bado ni kubwa sana katika Mradi huu wa Chankolongo. Pia kutokana na majibu yake na yeye mwenyewe amewahi kufika kwenye huo mradi, mradi huu ni wa muda mrefu sana kiasi kwamba wananchi mpaka sasa hawaelewi kinachoendelea juu ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa pia Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi kwamba, je, ni kweli mwezi Desemba mwaka 2017 mradi huu utakamilika kutokana na changamoto zilizopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa mradi huu unakusudia kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria na ndani ya Jimbo la Busanda wananchi wana tatizo kubwa sana la maji na maji mengi yanayotumika kwa ajili ya uchenjuaji wa dhahabu ni machafu na wananchi wanapenda kupata maji safai na salama; je, mradi huu utawezesha kufikisha maji na katika Jimbo zima la Busanda? Napenda kupata majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mimi na yeye Mbunge tulikwenda jimboni kwake ili kuukagua mradi huu na ni kweli mradi huu tumeukuta una changamoto nyingi sana na ndiyo maana kwa hatua tulizozifanya pale na kutoa maelekezo nilipofika *site* mpaka *Engineer* pale pamoja na Afisa Manunuzi amesimamishwa majukumu kutokana na mradi huu, kwa hiyo hatukulala kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, miezi michache iliyopita tulitoa maagizo kwamba choteo liweze kukamilika na mabomba yaweze kupatika. Kwa taarifa nilizozipata juzi ni kwamba lile choteo limekamilika maji yanatoka katika ziwa mpaka yanafika pale katika *intake* yenyewe, lakini usambaji wa mabomba umekuwa ukisua sua. Ndiyo maana Halmashauri ilivyosukuma, huyu sasa ameingia na hii kampuni nyingine ya *Katoma Motor Factors Limited* ambayo imefanya *commitment* ya kuleta mabomba yote bila hata ya kulipwa hata senti tano. Kwa hiyo mabomba yatafikishwa *site* ndani ya mwezi huu wa saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nilizozipata ni kwamba tayari mabomba haya yapo ndani ya meli na kwamba muda wowote yatafika hapa *site*. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge naomba nikuhakikishie kwamba kwa jinsi nilivyoongea na watendaji katika Halmashauri ya Geita ni kwamba tutasukuma ndani ya mwezi wa 12 mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu agenda ya pili, kwamba mradi huu ikiwezekana ufike kwenye maeneo mengine; wazo ni jema lakini naona kwanza jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba mradi huu unaweza kukamilika katika vile vijiji vya awali. Jambo hili likishakamilika hapa tutaweka mipango mingine ya namna ya kufanya; kwa

sababu chanzo hiki ni kikubwa sana ili kiweze kusaidia wananchi wa Busanda waweze kupata maji kama Mbunge wao anavyohangaika siku zote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Silinde, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la maji nchini ni kubwa na Tanzania ni moja ya nchi ambayo tuna sifa ya kuwa na Maziwa makubwa pamoja na mito mingi; yaani ni nchi ya Maziwa Makuu tofauti na zile nchi za kwenye jangwa kule kama Libya ambao wana maji zaidi ya asilimia 80. Sasa ni kwa nini Serikali isione aibu ya kushindwa kutatua hili tatizo kwa muda mrefu ilhali tuna maji mengi? Sasa hivi ukiangalia moja ya sifa ya nchi yetu ambayo tumekuwa tukijitamba na Serikali mmekuwa mkijisifu kwamba mmekuwa mkikusanya mapato mengi. Ni kwa nini sasa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umeshauliza swali la kwanza umesema kwa nini Serikali isione aibu, ulishamaliza hilo swali, hilo ni la pili na hili ni la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi, kila mwaka inatenga fedha na inazipeleka kwenye Halmashauri. Ni kazi ya Halmashauri kuhakikisha inatumia hiyo hela kuwapatia wananchi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeandaa kitabu kinachoonesha bajeti iliyotengwa katika Halmashauri na kiasi cha fedha ambacho Halmashauri imetumia. Halmashauri nyingi zimeshindwa kutumia fedha zilizotengwa kwenye bajeti. Sasa lawama hii iende kwa nani wakati sisi wenyewe ni Madiwani kwenye hizo Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu ina maji ya kutosha kilichobaki ni kuweka fedha na kusambaza na Serikali inaendelea kuweka fedha. Imeweka fedha mwaka uliopita na mwaka huu fedha tayari ipo kwa ajili ya Halmashauri kuhakikisha kwamba mnamtuambia zile fedha kuwapa wananchi maji na Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeshatoa maelekezo ya jinsi ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaambie Waheshimiwa Wabunge Halmashauri yangu tayari imeshatengeneza mpango kazi leo tarehe 3 Julai, hebu jilize wewe kwenye Halmashauri yako kwenye bajeti mpya je, mpango kazi umeshaanza kufanya? Ndugu zangu naomba sana bajeti ipo tusimamie Halmashauri waweze kutekeleza miradi ya maji hakuna haja ya kulaumiana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, hivi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu katika majimbo yote mawili tulikuwa na mradi wa maji takribani zaidi ya miaka minne na hao wamekosesha Halmashauri zetu kupata mpya za miradi ya maji. Ni kwa nini sasa Serikali isitoe maelekezo ya Waraka kwa Halmashauri za Wilaya kwa jinsi ambavyo watajiondoa katika mikataba ya awali ili wananchi wetu waweze kupata huduma bora na kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Halmashauri yake najua, tena mikataba hiyo imeingiwa wakati na yeye mwenyewe akiwa ni Mwenyekiti wa Halmashauri. Tumeanza kutoa fedha na tumetoa maelekezo kwamba kwanza tukamilishe ile miradi ya awali ambayo ilikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la mikataba ni la Mkurugenzi mwenyewe aliyeingia mikataba, *clauses* za kuhudumia mikataba ziko ndani, *termination* ziko ndani namna gani ziko ndani, suala la mikataba haliwezi kujadiliwa Bungeni, ni la yeye mwenyewe Mkurugenzi ambaye alilingia mikataba hiyo; na *condition* ya mikataba ipo pale na taratibu zote zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge amwambie Mkurugenzi wake aiangalie mikataba vizuri, madirisha ya jinsi ya kutoka yapo ili kuachana na huyo mkandarasi ambaye ameshindwa kazi ili kuweza kuingia na mkandarasi mwingine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Musukuma, swali fupi.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Halmashauri ya Geita DC haina *Engineer* wa maji na Mheshimiwa Naibu Waziri alishuhudia hilo kwamba *Engineer* tuliyekuwa naye hakuwa na cheti cha kuwa *Engineer* wa maji kwenye Halmashauri yetu, na tulimsimamisha mpaka sasa hatuna *Engineer*, je, Serikali ina mpango gani wa kuleta *Engineer* wa maji kwenye Halmashauri ya Geita DC?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWAIA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kutokana na matatizo yaliyojitokeza pale Geita ilionekana kwamba Injiniya yule kipindi kile ilikuwa hatoshi kusimamia miradi ya maji katika Halmashauri ya Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo naomba nimhakikishie kwamba tunafanya harakati. Tumekuwa na changamoto ya mainjiniya katika maeneo mbalimbali lakini eneo la Geita tumelipa kipaumbele kwa sababu kuna miradi hii mikubwa ya maji.



Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali katika eneo lile na ukanda ule ni kutumia Ziwa Victoria, kwa hiyo eneo lake tutalipa kipaumbele. Kwa hiyo Mheshimiwa Musukuma naomba avute subira tu kidogo hili jambo tuliweke vizuri, tutapata injinia mzuri ambaye atatusaidia katika miradi ya maji katika eneo lake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Salma Mohamed Mwasa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 479

### **Ujenzi wa Hospitali Mpya, Dar es Salaam**

**MHE. SALMA M. MWASSA** aliuliza:-

Kumekuwa na mrundikano wa wagonjwa kwenye Hospitali za Mwananyamala, Temeke na Amana:-

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya mpya katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Mohamed Mwasa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 10 katika Kata ya Somangila kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali kubwa ya Wilaya ya Kigamboni. Ujenzi wa Hospitali hiyo unatarajiwa kufanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali ya Morocco. Kwa sasa Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Morocco ili kuanza ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kuboresha Zahanati na vituo vya afya vilivyopo ambapo katika bajeti ya mwaka 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 557.3 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba pamoja na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwasa, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA M. MWASA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, naomba urekebisa kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Mwasa, swali la nyongeza

**MHE. SALMA M. MWASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza swali langu lilikuwa ni Hospitali za Wilaya za Ubungo na Kigamboni, lakini hapa naona limekuja la Kigamboni peke yake. Sasa maswali yangu ya nyongeza ni mawili. La kwanza, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya kwenye Wilaya mpya ya Ubungo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, ni lini Serikali tena itapandisha hadhi kituo cha afya cha Mbezi? Kama huu mchakato wa kujenga Hospitali ya Wilaya utachukua muda basi ipandishe Hospitali ya Mbezi iwe Hospitali ya Wilaya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na tunafahamu hizi Kigamboni pamoja na Ubungo ni Wilaya mpya, zimezaliwa kutoka katika Wilaya mama ya Temeke na Wilaya Kinondoni, tukifahamu kwamba Wilaya ya Ubungo ina changamoto hiyo. Kwa hiyo, jambo la msingi ni kwamba, kwa sababu tumegawanyika si muda mrefu sasa niombe Baraza la Madiwani la Ubungo pamoja na timu yote ya *Management* wafanye utaratibu wa kuandaa hii mipango ya ujenzi wa hospitali mpya ya Ubungo na sisi Serikali katika nafasi yetu tutafanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha kwamba eneo la Ubungo linakuwa na hospitali yake kwa sababu tunajua kwamba *population* ya watu wa Ubungo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kupandisha hadhi kituo cha Mbezi kwa hivi sasa kiweze kutumika, kikubwa zaidi nimuagize Mkurugenzi pamoja na Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ubungo kwamba kama wakiona kinatoshwa waanze kuhakikisha tunaanza harakati za kwanza kukiwezesha kituo hiki kama tulivyofanya kituo cha Vijibweni pale Kigamboni. Tukifanya hivi tutaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasihhi hasa Mkurugenzi na *DMO* wetu, waweze kufanya harakati za haraka na kufanya *analysis* ya kutosha nini kinaweza kufanyika pale ili kuweza kuongeza tija katika Sekta ya Afya katika wilaya ambayo Mheshimiwa Mbunge anaipigania sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Baada ya kupandishwa hadhi Zahanati ya Likombe katika Manispaa ya Mtwara Mikindani kuwa Hospitali ya Wilaya kumekuwa na changamoto kubwa sana ya mrundikano wa wagonjwa hasa katika wodi ya wazazi. Je, ni lini Serikali itapanua wodi ile ili akinamama wale waweze kusitirika wakati wanatimiza haki yao ya msingi kama wanawake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *population* ya Mtwara Mikindani sasa hivi imekuwa kubwa kutokana na kuingiliana na mambo ya gesi. Hata hivyo, hivi sasa tunaenda katika harakati za kufanya ukarabati wa vituo vipatavyo 142. Zoezi hili haliishi hapa; Serikali inajielekeza tena kupanua vituo vingine vipya ambako kuna *population* kubwa. Kituo hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge amekizungumzia hapa tutakichukua kama sehemu ya kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ya Awamu ya Tano ni kufanya *commitment* katika kuwahudumia wananchi. Kwa hiyo, hii tutaweka ni sehemu ya kipaumbele kuwahudumia wananchi wa Mikindani ili waweze kupata afya bora katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Changamoto ya huduma ya afya iliyopo Kigamboni na Ubungo inafanana na ile iliyopo Jimbo la Nanyamba ambako hakuna kituo cha afya hata kimoja, hakuna hospitali ya wilaya, hakuna *ambulance* na hakuna DMO (Mganga Mkuu wa Wilaya). Sasa nataka kujua Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kutatua changamoto hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Mheshimiwa Chikota tulikuwa wote *site* na tulifika eneo ambalo wao wameweka kipaumbele kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakarabati eneo lile ili kupata kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ziara ile nimhakikishie Mheshimiwa Chikota kwamba Serikali imefanya *commitment* ya kutosha na pale muda si mrefu kuanzia sasa tutawekeza fedha nyingi takribani milioni mia saba katika kile kituo chake ambacho alikiwekea kipaumbele siku tulipofika pale. Kwa hiyo, naomba niwaambie wananchi wa Nanyamba kwamba Mbunge wao amepigana na Serikali imesikia na muda si mrefu tutakwenda kufanya uwekezaji mkubwa sana wa sekta ya afya katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la fupi.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami niulize swali fupi. Hospitali yetu ya Makambako ilipandishwa hadhi tangu 2013 na kuwa hospitali kutoka kituo cha afya, lakini mgao wa dawa mpaka sasa tunapata kama kituo cha afya. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kupeleka mgao kama ambavyo ilipandisha kuwa hospitali kwa sababu wataalam, Madaktari wapo na chumba cha kufanyia upasuaji kinaanza mwezi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, nilipofika pale jimboni kwake nikiwa naye ni miongoni mwa watu ambao wame-*invest* pesa zao binafsi kuwasaidia wananchi wao. Mheshimiwa Mbunge hongera sana katika hilo. Changamoto ya mgao wa dawa, kwamba bado unapata kwa mfumo wa kituo cha afya; wakati huo huo ikiwa kwamba Makambako ni *center* kubwa sana ya watu kutoka katika hizi barabara mbili; ya kutoka Ruvuma na kutoka Mbeya; tunajua ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba eneo lile kwa bajeti ya mwaka huu tutaliangalia vizuri. Tutafanya kila liwezekanalo kumwongezea bajeti kwa sababu tunataka ile *centerya* upasuaji ifanye kazi vizuri. Hata hivyo, Serikali tutaangalia tufanyeje ili wananchi wa Makambako waweze kupata huduma vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba niseme kwamba Serikali imelisikia na itakwenda kulifanyia kazi jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Savelina Mwijage, swali fupi.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Bukoba Vijijini, ni hospitali ya *mission* na leo hii walivyotoa *ambulance*

imekwenda kwenye Zahanati ya Kishanje. Ni lini Serikali itapandisha hadhi Hospitali ya *Mission* ambayo tayari wameshakubali kuitoa Serikali, kuwa hospitali ya wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumesikia lile suala la *ambulance* allizungumza nadhani hii ni mara ya pili, kwamba maelekezo ilitakiwa iende katika kituo kingine na nimesema kwamba nitafika kule *site* kufanya *verification*, maagizo yalikuwaje na hii *ambulance* imeenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuhusu mchakato wa kuipandisha hii hospitali tutapitia mikataba, tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya kuangalia nini kilichopo na jambo lipi ambalo ni rafiki zaidi tunaloweza kulifanya kwa mustakabali wa wananchi wa Bukoba. Kwa hiyo, tunachukua haya mawazo lakini lazima tufike *field* pale tuangalie uhalisia wa jambo lilivyo ili tupate majibu muafaka kusaidia wananchi wa Bukoba.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Omary Badwel, sasa aulize swali lake.

Na. 480

### **Posho kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji; hata hivyo Wenyeviti hao wamekuwa wakifanya kazi kwa kujitolea bila kulipwa posho za kujikimu na Serikali imekuwa ikiahidi kuangalia uwezekano wa kuwalipa posho za kujikimu viongozi hao:-

Je, ni lini sasa Serikali itaacha kuendelea kuahidi juu ya malipo hayo na kuanza utekelezaji kwa kuanza kuwalipa viongozi hao posho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inathamini na kutambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na viongozi wa vijiji na mitaa katika kusimamia shughuli za maendeleo katika ngazi ya msingi ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu ambapo posho za viongozi wa Serikali za vijiji na vitongoji zinalipwa na Halmashauri kupitia asilimia 20 iliyotengwa kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri na kurejeshwa kwenye vijiji. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuzisimamia Halmashauri kuhakikisha fedha hizo zinatengwa na kulipwa posho stahiki. Hata hivyo, kutokana na baadhi ya halmashauri kushindwa kutekeleza suala hili kikamilifu, suala la kutenga asilimia 20 litawekwa katika sheria kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ambayo inatarajiwa kuletwa Bungeni ili kurekebisha kasoro zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuendelea kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ili kujenga uwezo mkubwa zaidi wa kulipa posho hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Badwel, swali la nyongeza.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya

nyongeza. Kwa kuwa ni muda mrefu sasa Wenyevitwa wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa wamekuwa wanadai fadha zao na hawajui ni lini watalipwa malimbikizo haya. Je, sasa Serikali iko tayari kuziagiza halmashauri kupitia Wakurugenzi kuandaa idadi ya fedha ambazo kila halmashauri inadaiwa na viongozi hawa ili Serikali baadaye itoe maelekezo ya namna ya kuwalipa viongozi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa sina hakika kama katika maelekezo haya ya kuwalipa Wenyevitwa wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kama pako mahali panaeleza wanalipwa kiasi gani. Je, Serikali sasa iko tayari kutamka hapa kwamba hizo asilimia 20 ambazo zinapelekwa hao Wenyevitwa wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa watalipwa kiasi gani kila mmoja kwa mwezi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna halmashauri zingine zinafanya vizuri lakini kuna zingine ni changamoto kubwa. Ukipita huko kwenye halmashauri nyingine utaona kwamba zile asilimia 20 marejesho hayajarudi vijijini. Hata hivyo, tumetoa maelekezo mbalimbali, lakini naomba tutoe maelekezo tena na tutatoa maelekezo kwa waraka maalum kwamba jinsi gani sasa halmashauri hasa Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokaa katika Kamati ya Fedha katika ajenda ya mapato na matumizi sisi tukiwa wajumbe lazima tuangalie ile *compliance* ya kurudisha zile fedha katika halmashauri zetu. Bahati mbaya sana katika sehemu nyingine utakuta Ma- *DT* wanakuwa kama Miungu watu, hawafanyi maelekezo ya Kamati zao za Fedha wanapofanya maamuzi. Kwa hiyo, jambo hili tutatoa maelekezo mengine ya ziada ili asilimia 20 ya fedha hizi ziwewe kurudi vijijini.



Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika suala zima la kupeleka hizi asilimia 20 mara nyingi zina-*differ* kutoka halmashauri kwa halmashauri, ndiyo maana tumesema kwamba tunafanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ambayo humpa Waziri mwenye dhamana katika kifungu maalum, nadhani katika ibara namba 45, dhamana ya kutoa maelekezo maalum ya namna ya kufanya. Jambo hili lisiwe ni jambo la hiari isipokuwa liwe ni kwa mujibu wa sheria. Lengo kubwa ni kuwasaidia Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa na Vijiji. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Nadhani wote tunatambua umuhimu wa Wenyeviti wa Mitaa na kazi wanazozifanya, lakini kumekuwa na kilio cha muda mrefu sana kuhusiana na maslahi yao kwa kazi kubwa wanayoifanya. Je, Serikali sasa iko tayari kutenga bajeti kwa ajili ya kuwalipa mishahara Wenyeviti wa Mitaa pamoja na Madiwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili nililijibu takribani wiki mbili zilizopita na nikasema kwamba kwa jambo la kulipa mishahara utaratibu wa sasa ni kulipa posho. Pale Bunge litakapoamua vinginevyo, tutaangalia jinsi ya kufanya. Kikubwa zaidi ni kwamba tutaendelea na utaratibu huu, lakini tujue kwamba endapo jambo hili litaingia katika mishahara maana yake ni kuwa *wage bill* lazima itabadilika katika utaratibu wa kiserikali, ambayo vile vile ina changamoto yake. Kwa hiyo lazima tufanye *analysis* ya kutosha juu ya namna ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa utaratibu wa sasa hivi tutaendelea kwa mujibu wa sheria

inavyozungumza. Bunge litakapoamua hapo baadaye tutaenda na maamuzi hayo ambayo Bunge litakuwa limeamua hapo baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe, swali la nyongeza.

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma-Ujiji tuliamua kutumia sehemu ya ushuru ambao manispaa inakusanya kwa ajili ya kuongeza fedha za kuwalipa watu hawa, Wenyeviti wa Mitaa pamoja na kuwalipia Bima ya Afya. Hata hivyo, kutokana na hatua ambayo Serikali Kuu imechukua, mmechukua kodi ya majengo, ushuru wa mabango, haya maelekezo mnayoyotoa kwamba halmashauri zivalipe hawa watu hizi 20 *percent* zitatoka wapi wakati ushuru wote, mapato yote Serikali Kuu inayachukua? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nasema hiyo ni *the best practice* ambayo mmeifanya na tunataka *innovative idea* kama hizo wakati mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, suala la kuchukua fedha Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Waziri wa Fedha alizungumza wazi, kwamba kinachofanywa na Serikali Kuu ni kukusanya baadaye inarudisha katika halmashauri husika; hii ilikuwa ni wazi kabisa, utaratibu wote ambao Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizungumza, kutokana na hamasa nzuri, ndiyo maana leo hii tunaona jinsi ambavyo watu wanapanga foleni *TRA* kwenda kulipa kodi ya majengo. Kwa hiyo kikubwa zaidi naomba tukubaliane na Serikali, lengo la Serikali ni kusukuma mambo yaende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokihitaji ni kwamba tufike Taifa ambalo linaweza kuamua kufanya mambo vizuri zaidi. Kwa hiyo, tutachukua zile *best practice* ambazo

sehemu mbalimbali zipo. Hata hivyo niseme kwamba Serikali haikuwa na nia ya kunyang'anya *authority* ya halmashauri katika kuchukua mapato, isipokuwa ni utaratibu tu unawekwa halafu baadaye tutaona nini faida ya jambo hili ambalo ni jipya, lakini ambalo kwetu lina msingi mkubwa sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, sasa aulize swali lake.

Na. 481

### **Miradi ya *Electricity V* na *REA***

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Serikali imefanikiwa kupeleka umeme katika Wilaya ya Mbogwe kupitia *Electricity V* na *REA* lakini huduma hii haijawafikia wananchi walio wengi;

Je, ni lini Serikali itaongeza usambazaji wa huduma hiyo muhimu kwa wananchi wengi walio tayari kulipia gharama za kufungiwa umeme katika nyumba zao hususan katika Miji ya Masumbwe na Lulembela?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi kabambe wa usambazaji umeme vijijini awamu ya tatu umeanza nchi nzima tangu Mwezi Machi, 2017. Mradi huu utajumuisha vipengele-mradi vitatu vya *Densification*, kwa maana ya vitongoji, *Grid Extention* kwa maana ya vijiji vyote pamoja na *Off- Grid Renewable* katika maeneo ya visiwa. Mradi huu unalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme

katika vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na umeme ikiwa ni pamoja na vitongoji vyote nchi nzima, taasisi zote za umma, mashine za maji pamoja na visiwa vyote nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji ya Lulembela na Masumbwe imewekwa katika utekelezaji wa mradi wa *REA* awamu ya tatu utakaokamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika Miji ya Masumbwe unaojumuisha vijiji vya Budoda, llangale, Masumbwe, Nyakasaluma na Shenda; na katika Lulembela unaojumuisha Vijiji vya Bugomba, Kabanga, Kashelo, Mtakuja, Nyikonga pamoja na maeneo mengine. Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti utapelekwa kwenye maeneo yote yenye urefu wa kilometa 38.7; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 110; ufungaji wa transfoma 20; pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wapya 678. Kazi hii itakamilika mwaka 2020/2021 na itagharimu shilingi bilioni 5.18.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, swali la nyongeza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ambayo imefanyika katika Jimbo la Mbogwe la kusambaza umeme maeneo mengi. Sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme katika Kata Nyasato, Bunigonzi na Vijiji vyote vya Jimbo la Mbogwe ambavyo bado havijapa huduma hii ya umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini sasa mradi wa *REA* awamu ya tatu utaanza katika Mkoa wa Geita na Wilaya ya Mbogwe *in particular?* (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Masele kwa sababu ameshughulikia sana masuala ya umeme katika jimbo lake ambapo kati ya vijiji 72, vijiji 44 vyote vimeshapatiwa umeme. Hongera sana Mheshimiwa Masele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie vijiji vyote vilivyobaki, ameuliza suala la msingi sana ni lini sasa umeme utapelekwa katika Kata za Nyasato pamoja na Budigonzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Masele kwa niaba ya wananchi wa Mbogwe, ni vijiji vyote 28 sasa tunavipelekea, Vijiji hivyo ni pamoja na Budigonzi, Buzigozigo, Mtakuja, Budura pamoja na maeneo mengine ya Kashenda na Nyashimba, yote yatapelekwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini tunazindua Mkoa wa Geita? Nipende kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba tumeanza kuzindua utekelezaji wa mradi wa awamu ya tatu tangu tarehe 24 mwezi huu na tumeanza na Mkoa wa Manyara. Katika Mkoa wa Manyara tumefanya katika Jimbo la Babati na mengine. Tarehe saba na nane tunazindua katika Mkoa wa Kagera, tutakwenda katika Wilaya ya Karagwe. Tarehe 10 tutazindua katika Mkoa wa Geita Mheshimiwa Mbunge; na maeneo ya kuzindua ni maeneo ya Nyangh'wale pamoja na maeneo ya Mbogwe. Kwa hiyo niwahakikishie wananchi wa Mbogwe, wananchi wa Mkoa wa Geita na Wabunge wote wa Mkoa wa Geita basi tushirikiane wote tarehe 8 na 10 tutakapokuwa tunazindua katika Mkoa wa Geita.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wengi mpaka nashindwa kuelewa nani anatakiwa kuonwa. Mheshimiwa Victor Mwambalaswa swali la nyongeza

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nataka niulize Serikali kwa kuwa katika Mkoa wa Mbeya, *REA III* imezinduliwa tayari na mkandarasi yupo aliyeanzia Wilaya ya Rungwe. Sasa ni lini huyo mkandarasi atakwenda Wilaya ya Chunya ili akapeleke

umeme kwenye Kata zilizobaki za Ifumbo, Kasanga, Nkunungu, Lwalaje, Kambi Katoto na Mafyeko?

**NAIBU SPIKA:** Na Rungwe nako hajamaliza, Mheshimiwa Naibu aziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Mwambalaswa nampongeza sana, hata tulipokwenda kule ni kwa sababu pia alishirikiana na sisi sana kwa hiyo hongera kwa kazi hiyo. Nimhakikishie kwa niaba ya wananchi wake; ni kweli kabisa katika Kijiji cha Ifumbwe pamoja na Kasanga bado hatujaenda; lakini tarehe 17 mwezi huu mkandarasi atakuwa kwenye Kijiji cha Kasanga katika jimbo lake. Kwa hiyo, katika maeneo mengine yataendelea kufanya kazi hiyo hiyo na niwaombe sana Wabunge wa Mkoa wa Mbeya tushirikiane kwa kazi hiyo kwa sababu mkandarasi tayari ameshaingia mkoani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joyce Sokombi, swali la nyongeza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo la Mbogwe ni sawa na tatizo lililoko katika Mkoa wa Mara hasa Musoma Vijijini. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuhakikishie kwamba ni lini wananchi wa Musoma Vijijini watapata umeme wa *REA*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa, tulipokwenda katika Mkoa wa Mara wakati tunazindua Mheshimiwa Mbunge alitupa *support* kubwa sana. Hongera sana pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Mara; lakini ni lini sasa umeme vijiji hivyo vitapelekewa; tumeshaanza na kuja kufikia mwezi ujao wakandarasi watakuwa wameingia vijiji 42 katika Mkoa wa Mara na vijiji vilivyokuwa vimebaki

vitakamilika sasa ifikapo mwaka 2020. Hata hivyo, si kwenye vijiji tu na vitongoji vyote Mheshimiwa Sokombi, Taasisi zote za Umma, Makanisa na Misikiti pamoja na visiwa ambavyo viko Mkoa wa Mara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Serikali inaendelea kufanya kazi nzuri kupitia miradi ya *REA*, lakini nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba yako maeneo mengine kwenye miji na majiji bado yanazo sura za vijiji; kwa mfano kwenye Jimbo la Nyamagana iko mitaa inafanana kabisa bado na maeneo ya vijijini kama Fumagila, Rwanima, Isebanda, Kakebe na maeneo mengine kama Nyakagwe. Ni lini Serikali itakuwa na utaratibu wa kuhakikisha na maeneo haya yanapatwa umeme wa *REA* ili yaweze kupata sawasawa na mengine? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mabula. Wakati ananiletea vijiji hivi tulipozungumza aliniletea vijiji vingine ambavyo vilikuwa kwenye hali ya kimtaa, lakini kisura vinaonekana kivijiji na tumeviingiza kwenye Mradi wa *REA*. Katika vijiji ambavyo ametaja hivi ambavyo inaonekana viko mjini, kwanza kabisa kuna mradi ambao unapeleka umeme kwenye miji yote nchi nzima na mradi huu unaitwa *Urban Electrification* na utapeleka katika miji na mitaa 314 kwa nchi nzima. Kwa hiyo, hata vijiji au mitaa ambayo iko mijini bado itapelekewa umeme kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tutakaa katika vijiji ambavyo amesema vya Fumagila pamoja na Kakene tuone hali itakavyokuwa. Nimwombe sana mara baada ya hapa tukutane na Mheshimiwa Mabula ili ikiwezekana vijiji hivi vipelekewe katika Mradi wa *REA*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Ungando, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na mauaji yanayoendelea Wilayani Kibiti bado tunahitaji umeme. Je, Serikali ina mpango gani kupeleka umeme katika vijiji vilivyobakia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, unaombwa uonde giza Kibiti, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze nilienda kwake na tulitembea sana mpaka kwenye Kijiji cha Jaribu Mpakani na tulipeleka umeme Jaribu Mpakani. Hata hivyo, Serikali imekusudia kuangaza umeme vijiji vyote nchi nzima. Napenda nitoe nafasi hiyo kwa sababu, Mheshimiwa Ungando tumeshirikiana sana, lakini niseme tu vijiji vyote vya Jimbo la Kibiti vitapelekewa umeme sasa kupitia Mradi wa REA; hadi kufikia mwaka 2021 vijiji vyake vyote vya Kibiti vitakuwa vimeshapata umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho, Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, Mkoa wa Mtwara na Lindi ndiyo mikoa ambayo ina vijiji vingi sana ambavyo havijapatiwa umeme. Je, ni lini mikoa hii itapewa kipaumbele maalum ili vijiji vingi viweze kupata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kabisa Mikoa ya Mtwara na Lindi maeneo mengi hayajafikiwa na miundombinu ya umeme. Nimhakikishie Mheshimiwa Bwanausi na namshukuru



sana, alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini hapo nyuma, tumeshirikiana sana na amefanya kazi kubwa kwenye jimbo lake, naomba nimpongeze kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tumeipa kipaumbele kikubwa sana mikoa hii miwili. Tarehe 15 hadi tarehe 18 tutakuwa tunafanya kazi ya kuzindua na kuelekeza Wataalam wetu wa *TANESCO* kupeleka umeme katika mikoa hii miwili, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; tunarekebisha miundombinu ya Mtwara. Hivi sasa tunajenga *transmission line* ya kutoka Mtwara umbali wa kilometa 80 na umeme wa *KVA 132*, ili umeme huo upelekwe Mtwara Mkoa mzima na maeneo mengine ya Lindi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bwanausi Serikali imetumia hatua kubwa sana na imegharimu shilingi bilioni mia nane sabini na nane kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Bwanausi, lakini nampa uhakika kwamba, Serikali inaipa vipaumbele sana Mikoa ya Lindi na Mtwara na mwaka 2020 na 2021 vijiji vyote vya Mtwara na Lindi vitakuwa vimepata umeme.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 482

### **Ujenzi wa Mabwawa kwa Ajili ya Kilimo**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Maeneo mengi ya Mkoa wa Simiyu na Mikoa mingine kama vile Dodoma, Singida, Shinyanga na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Tabora na Mwanza yanapata mvua za masika hafifu sana, hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kilimo katika Mikoa hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani mkubwa wa kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilikwishaainisha maeneo yote nchini yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuandaa mpango kabambe wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji wa mwaka 2002. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya ardhi, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inafanya mapitio ya mpango huo ili uhusishe ujenzi wa mabwawa madogo, ya kati na makubwa kwa nchi nzima yakiwemo maeneo yanayopata mvua hafifu za masika. Vilevile mpango huo utahusisha matumizi ya maji ya maziwa makuu, ikiwemo Ziwa Viktoria, kwa ajili ya umwagiliaji wa kutumia teknolojia zinazotumia maji kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupitia mpango huo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2017/2018. Kukamilika kwa mpango huo kutawezesha kufanyika kwa usanifu wa miradi ya mabwawa kwenye maeneo yenye mvua hafifu yaliyotajwa pamoja na maeneo mengine yenye uhaba wa mvua. Katika mpango huo Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji itaanza ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati ya Kidunda, Ndembela na Farkwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, mikoa niliyoitaja inakumbwa na tatizo la upungufu wa chakula mara kwa mara; na kwa kuwa,

Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wanao huo mpango kabambe wa kuanzisha au wa kujenga mabwawa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini. Je, Serikali inaonaje juu ya kuyapa kipaumbele maeneo ya Mikoa hii ya Shinyanga, Mwanza, Singida, Dodoma, Tabora ili kuweza kujenga mabwawa hayo ili wazalishe chakula wakati mvua zinapokuwa hafifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, pia katika Wilaya ya Maswa tuna mabwawa madogo madogo mengi, likiwemo bwawa la Seng'wa, Mwamihanza, Masela, Sola na mengine. Je, Serikali ina mpango gani wa kuyafufua mabwawa haya kwa kuwa, sasa yamejaa mchanga, ili yatumike kuwapatia wananchi wetu maji, lakini pia yatumike kwa kilimo cha mboga mboga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ametaja Mikoa ya Shinyanga, Tabora na mikoa mingine ambayo ina uhaba wa mvua na kwamba, je, Serikali ina mpango gani wa kuipa hii mikoa kipaumbele katika ujenzi wa mabwawa. Sasa ipo timu ya wataalam ambao wanapitia maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yao itatuelekeza sasa ni sehemu gani ambayo inaonekana kuwa na kipaumbele kwa ajili ya kuwekewa hayo mabwawa. Wakishakamilisha hiyo taarifa, mwaka huu wa fedha tulionao basi tafiti zitaelekea kwenye hayo mapendekezo ya maeneo ambayo yanahitaji kujengwa mabwawa na maeneo ambayo yana ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili limezungumzia kuhusu Maswa, wilaya yake na kwamba kuna mabwawa yaliyopo tayari, lakini yameshajaa mchanga. Sasa Serikali ina mpango gani. Tulishasema katika Bunge hili,

tumeelekeza halmashauri kuhakikisha ama zinasanifu kujenga mabwawa kila wilaya, kila halmashauri au kufanya ukarabati wa mabwawa hayo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo wanashindwa tumewaelekeza kwamba, wawasiliane na sisi, ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba, tunafanya ukarabati au tunajenga mabwawa na hasa pale inapokuwa kwamba, mabwawa hayo yanahitajika kwa ajili ya maji safi na salama ya matumizi ya majumbani. Kwa hiyo, niendeleo tena kusisitiza halmashauri zihakikishe kila mwaka zinatenga fedha kwa ajili ya miundombinu ya mabwawa madogo ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa kule katika halmashauri ukiwaeleza jambo hili na wao wanatupia mpira kwenye Wizara, wakati Wananchi wa Maswa wanaendelea kupata tabu ya maji na katika Mradi wa Ziwa Viktoria wako *phase two*, ina maana watachelewa sana kupata maji. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari basi, angalau tushirikiane na ili tuweze kuchagua yale mabwawa muhimu zaidi kwa kutoa huduma kwa wananchi tuanze nayo hata kama ni machache? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe kwanza mfano; Mheshimiwa Bilakwate Halmashauri yake ya Karagwe tayari imeleta mapendekezo ya mabwawa sita na mabwawa hayo tunayafanyia kazi na tunazungumza kati ya halmashauri yake na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili tuweze kuona tunafanya nini kwa kushirikiana kwa sababu Serikali ni hiyo hiyo moja ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Nyongo, Halmashauri yake waanze kufanya kazi kwanza kidogo kule kwao, halafu wawasiliane na sisi tutaona suala la kufanya. Kwa bahati nzuri nimeshatembelea kwenye halmashauri yake na tukaona baadhi ya mabwawa. Basi halmashauri ianze kufanya kazi, Wizara haiwezi kuruka moja kwa moja kuja huko bila yeye mwenyewe. Mapendekezo haya aliyoyazungumza nafikiri wameyasikia, kwa hiyo, wayafanyie kazi, wawasiliane na sisi ili tuweze kufanya kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Matatizo yaliyopo katika Mikoa ya Simiyu, Dodoma na Shinyanga yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Halmashauri ya Temeke, pia hatuna maji. Mheshimiwa Naibu Waziri anakumbuka kwamba, Halmashauri ya Temeke si wanufaika wa maji yanayotoka Mto Ruvu hivyo, hatuna mfumo wa mabomba na tunatumia maji ya kisima na taarifa za wataalam zinasema kwa sababu Halmashauri...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea uliza swali la nyongeza, muda wetu hautoshi! Ukianza kuchangia itakuwa ngumu kidogo, uliza swali!

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, mfumo wa maji taka umechanganyika na mfumo wa maji safi ya kisima tunayotumia Temeke. Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kuhakikisha kwamba, mnatuletea maji ya bomba Temeke, ili tuachane na kunywa haya maji machafu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Temeke kwanza tunao mtambo

wa maji wa Mtoni, ila kweli kwamba, maji yanayotoka pale ni machache. Hata hivyo, tayari tunakamilisha uchimbaji wa visima 20 Kimbiji na Mpera na sasa hivi tunatafuta fedha na tunayo ahadi kutoka Benki ya Dunia, ili tuweze kuweka miundombinu ya usambazaji kuhakikisha kwamba, maeneo yote yale Mheshimiwa Mbunge Temeke na Mbagala yaweze kupata maji safi na salama. Kwa hiyo, ni suala la wakati tu, tayari maji tunayo, tunachoshughulikia ni kupata fedha za kusambaza miundombinu ili wananchi wake waweze kupata maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ajali Akbar, swali la nyongeza.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Newala iliamua kupambana na tatizo hili la maji wakaamua kuchimba bwawa katika Kijiji cha Chilangala, Wilaya ya Newala, lakini kutokana na ufinyu wa fedha lile bwawa hawakulimaliza. Je, Serikali iko tayari kwenda kumalizia lile bwawa ili tuweze kutatua tatizo hili la maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ndiyo kwa mara ya kwanza ananipa taarifa kwamba, kumekuwa na mradi wa bwawa ambao unafanywa na Halmashauri katika maeneo ya Jimbo lake kule Newala. Niseme kwamba, niko tayari tufanye mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo tayari kupitia mkopo wa India ambao tunasubiri *Financial Agreement* isainiwe, hela nyingi imepelekwa kwenye maeneo hayo ili kwenda kuhakikisha kwamba sasa tunachukua maji kutoka Mkunya kule Ruvuma, tunachukua Mitema na kuhakikisha kwamba, maeneo yote ya Newala yanapata maji safi na salama na hasa kwa kuzingatia kwamba, Newala iko juu

sana, huwezi ukachimba kisima ukapata maji. Kwa hiyo, mradi mkubwa unakwenda kwa Mheshimiwa Mbunge, lakini pamoja na hilo bwawa naomba tuwasiliane ili tuweze kuona cha kufanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa, matatizo ya maji yaliyoko huko Maswa Mashariki yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Halmashauri ya Itigi na shida kubwa iko kwa wafugaji katika suala zima la kunywesha mifugo yao. Sasa Serikali kwa maana ya Wizara ya Maji iko tayari kukubaliana na mapendekezo ya Halmashauri ya Itigi kwa ajili ya kuchimba malambo tu madogomadogo katika vijiji vyake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi kabisa ni kwamba, Mheshimiwa Mbunge tuko tayari kushirikiana na halmashauri yake kuhakikisha tunachimba mabwawa madogo madogo kwa ajili ya mifugo. Kwa hiyo, tuendelee kuwasiliana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimwa Cecilia Daniel Paresso.

**MHE. WILFRED M. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali langu, umeliruka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Rwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, sasa aulize swali Lake.

Na. 483

## **Malipo ya Fidia kwa Wakazi wa Kahororo – Bukoba**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali imepanga kuwalipa fidia Wakazi wa eneo la Kifungwa, Kata ya Kahororo, Manispaa ya Bukoba, ambao ardhi zao na mali iliyomo vilichukuliwa na Serikali miaka miwili iliyopita (12/07/2014) kupisha mradi wa maji taka wa *BUWASA*?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji nchini. Katika utekelezaji wa miradi hiyo kuna wananchi ambao walitoa maeneo yao ili kupisha miradi ya maji ikiwemo Mradi wa Maji Bukoba. Kabla ya kuanza ujenzi wa mradi Serikali imeweka utaratibu wa kuwalipa fidia kwa mujibu wa Sheria wamiliki wote wa ardhi na mali nyinginezo zitakazoathiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mradi wa Maji Taka Bukoba Serikali kupitia Wizara ya Maji imetuma fedha za fidia katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka na Usafi wa Mazingira Bukoba, jumla ya Sh.1,960,000,000/= kwa ajili ya malipo ya fidia katika eneo la Kifungwa, Kata ya Kahororo ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba, 2016 wadai wote 194 walilipwa fedha zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, swali la nyongeza.



**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pia niishukuru Serikali kwa kutimiza ahadi yake ya kuwalipa wananchi hawa pale niliposhika Shilingi hapa ndani na wananchi wangu wakawa wamelipwa fedha hizi, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza; ningependa kujua kutoka kwa Serikali hususan Waziri; ni lini wananchi hawa watalipwa riba ya fedha walizolipwa za fidia zaidi ya milioni 200 ambazo wanadai hadi sasa na hawajalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa bahati nzuri wananchi wa Bukoba *Town* wana Mbunge mahiri ambaye anaweza akasimamia na wakalipwa madai yao. Serikali inasemaje kwa watu wa maeneo mengine katika maeneo mbalimbali ya nchi hii ambao hawajalipwa fidia zao? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lwakatare, kwa hiyo hawa wengine siyo Wabunge kama Mbunge wa Bukoba *Town* siyo? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme fidia inalipwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 2001 kupitia Tangazo la Serikali namba 79. Si suala la umahiri wa Mbunge, ni Sheria imewekwa katika utaratibu wa kulipa fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijibu swali lake la kwanza la juu riba. Mheshimiwa Mbunge tarehe 10 Februari, 2017, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Salama BUWASA alileta barua ya kuomba fedha Sh.202, 164, 107.75 kwa ajili ya malipo ya nyongeza baada ya malipo ya fidia kuchelewa zaidi ya miezi sita. Malipo hayo yalichelewa kwa muda wa miezi kumi na sita na sasa hivi Serikali tayari inafanya utaratibu wa kupeleka fedha hiyo ili wananchi waweze kulipwa haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maeneo mengine; utekelezaji wa miradi; na nizingumze kwamba Waheshimiwa Wabunge fidia siyo ajenda yetu, ajenda yetu ni miradi ya maji safi na salama; suala la fidia linaingia katika utaratibu wa kawaida wa kisheria, kwamba unapotekeleza mradi ukikutana na mali ya mwananchi Serikali imeweka Sheria kwamba lazima umlipe fidia kabla utatekeleza huo mradi. Kwa hiyo, Sheria hii inatekeleza kwa nchi mzima na tutaendelea kufanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Singida Jimbo la Iramba Magharibi kuna Mradi wa *World Bank* ambao ulijengwa mwaka 1978 wa matenki ya maji ambayo mpaka leo yamekaa kama sanamu. Naomba Mheshimiwa Waziri aseme ni lini au Serikali ina mkakati gani wa kumaliza mradi huu kwa sababu ni muda mrefu sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa maelekezo, tumeandaa bajeti ya mwaka uliopita kwamba katika bajeti hiyo tuhakikishe kwamba tunatekeleza miradi ile ambayo bado haijakamilika; na tunaendelea hivyo na mwaka huu pia tumeandaa bajeti. Kwa hiyo katika halmashauri yake kama kuna miradi ambayo ilikuwa haijakamilika basi fedha katika mpango kazi wao wahakikishe kwamba wanaiielekeza kwenda kukamilisha miradi ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano anaouzungumzia Mheshimiwa Mbunge nimeukuta Nanyamba ambapo Mheshimiwa Mbunge alinifuata na tukaenda kukaa na halmashauri. Kulikuwa na matenki yamejengwa lakini hayana maji. Sasa hivi Nanyamba tayari wananchi ile fedha

ya mwaka jana wameshaitumia vizuri, wameelekeza kwenye miradi ambayo ilikuwa haijakamilika, wananchi wanapata maji. Naomba na Mheshimiwa Mbunge afanye hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Constantine Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Geita kuna mradi wa maji ambao unafahamika kama *LV WATSAN* ambao unafadhiliwa na *African Development Bank*. Ulitakiwa kuwa umekamilika tangu Novemba mwaka wa jana lakini mpaka leo haujakamilika. Nataka kujua mradi huu utakamilika lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba mradi huo hupo na ni mradi mkubwa unakwenda kwa *phases*. Una *financing* tatu; iko *financing* ya Serikali, watu wa madini wa *GGM*, lakini na *financing* pia kutoka lile fungu la *Lake Victoria Water and Sanitation Project*. Mheshimiwa Mbunge, tunakwenda kwa *phases*, kwa hiyo, kiasi tumeshakamilika na wananchi wanapata maji kama asilimia 30, lakini tunaendelea, hatimaye tuhakikishe tumekamilisha mradi huo ili wananchi wengi waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Swali fupi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayofanya. Nina swali kuhusu mradi wa Rwakajunju namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri awaambie akinamama wa Karagwe ni lini mradi wa Rwakajunju utatekelezwa ili kuwatua ndoo kichwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwatulize wananchi wa jimbo la Mheshimiwa Mbunge kwamba Mradi wa Maji wa Rwakajunju unatekelezwa. Mradi wa maji wa Rwakajunju una *finacing* ya uhakikika kutoka Serikali ya India na tunasubiri sasa hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha asaini mkataba wa fedha. Tayari Wizara tumeshaanza kutafuta Wahandisi Washauri ambao wanahakikisha wanaweka *document* vizuri. Yule Mhandisi anayefanya usanifu wa mradi huu anakaribia kukamilisha. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge tuendelee kuwasiliana, nina imani katika mwaka huu fedha tuliouanza juzi 2017/2018 tutaanza utekelezaji wa Mradi wa Rwakajunju ili tuweze kuwatua wananchi ndoo kichwani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Cecilia Paresso sasa alilize swali lake.

Na. 484

### **Halmashauri kunyang'anywa Uwezo wa Kukusanya Mapato ya Kodi ya Majengo**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Serikali ilitangaza kuzinyang'anya halmashauri uwezo wa kukusanya mapato ya kodi majengo (*property tax*) na Mamlaka ya mapato Tanzania (*TRA*) kupewa jukumu hilo.

(a) Baada ya *TRA* kupewa jukumu hilo je, ufanisi umefikiwa kwa kiasi gani ikilinganishwa na mapato yaliyokuwa yakikusanywa na halmashauri?

(b) Kwa kuwa kodi ya majengo ilikuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri za miji, manispaa

na majiji na majukumu ya kutoa huduma kwa wananchi hayajapunguzwa; Je, Serikali imejipangaje kufidia vyanzo hivyo vilivyopotea?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimia Cecilia Daniel Pareso, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali haijazinyang'anya Halmashauri uwezo wa kukusanya mapato yake hususan kodi ya majengo na badala yake imebadilisha na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo. Mamlaka ya Mapato Tanzania ndiyo yenye jukumu kuu kisheria la kukusanya mapato ya Serikali. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399 kifungu cha 5(1), Waziri wa Fedha na Mipango amepewa mamlaka ya kuikabidhi TRA jukumu lolote linalohusu ukusanyaji wa mapato yoyote kama atakavyoona inafaa kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA ilianza rasmi kukusanya kodi ya majengo kwa halmashauri 30 kati ya 183 kuanzia Oktoba, 2016 baada ya tangazo la Serikali Na. 276 kuchapishwa kwenye gazeti la Serikali tarehe 30 Septemba, 2016. Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2016, Halmashauri zote zilielekezwa kuendelea kukusanya kodi ya majengo wakati TRA ikikamilisha taratibu za kisheria na kimfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho cha Julai, hadi Septemba, 2016, halmashauri 30 ziliweza kukusanya shilingi milioni 3,399 ikiwa ni sawa na asilimia 24 ya lengo la kukusanya milioni 14,502. Ufanisi huu ni sawa na na wastani a shilingi milioni 1,133 kwa mwezi. Aidha, katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2016 hadi Aprili, 2017 jumla ya Shilingi milioni 10,652.6 zilikusanya sawa na ufanisi wa asilimia

22 ya lengo la kukusanya shilingi milioni 48,340.2 katika kipindi husika. Ufanisi huu ni sawa na wastani wa makusanyo ya shilingi milioni 1,521.8 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi ni wazi kwamba *TRA* imekusanya kodi ya majengo kwa ufanisi zaidi ikilinganishwa na halmashauri. Ufanisi wa *TRA* unatarajiwa kuongezeka kwa makusanyo ya mwezi Mei na Juni, 2017 baada ya mifumo yote kukamilika ikiwa ni pamoja na wananchi wengi kupata elimu na kuitikia wito wa kulipa kodi ya majengo kwa hiari kwa tarehe za mwisho wa mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna fidia inayotolewa au itakayotolea na Serikali Kuu badala yake halmashauri zitarejeshewa makusanyo ya kodi ya majengo kulingana na nakisi ya bajeti ya halmashauri husika. Kwa mantiki hiyo, kodi ya majengo itaendelea kuwa ni chanzo cha mapato ya halmashauri na Serikali kwa ujumla kwa mujibu wa sheria na kwamba chanzo hicho hakijapotea bali mfumo wa ukusanyaji umebadilishwa na kuboreshwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikihaidi kwamba itarejeshwa kodi hii ya majengo kwenye halmashauri zetu na ni ukweli kwamba mmekuwa hamrudishi; kwa mfano Halmashauri ya Kinondoni kabla haijagawanyika mliahidi mtarejeshwa bilioni 10 ikiwa ni sehemu ya makisio ya halmashauri husika, lakini mpaka leo hamjarudisha; je, Serikali hamwoni kwamba jambo hili hamliwezi sasa mtamke rasmi kwamba mtabakiwa na hizo kodi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano katika kila mwaka wa fedha imekuwa ikiendelea kuzinyang'anya halmashauri zetu vyanzo vingi vya

mapato kiasi kwamba halmashauri nyingi sasa hivi zinaelekea kushindwa kujiendesha kwa sababu Serikali Kuu inachukua fedha zote; je, Serikali haioni umuhimu sasa mlete mabadiliko ya Katiba hapa Bungeni mzifute rasmi Serikali za Mitaa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa si kwamba hatuwezi jambo hili, hilo nakanusha. Nimesema hapa ufanisi halisi tukilinganisha kati ya halmashauri pamoja na TRA. Katika hili naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba sote sisi ni Watanzania na zote tumeona tarehe za mwisho wa mwezi wa Sita wananchi walivyotoka kwa wingi kwenda kulipia kodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kusema Serikali tumeshindwa si sahihi kabisa na ndiyo maana Serikali kwa kuangalia wananchi wetu jinsi ambavyo wamelipokea jambo hili kwa matokeo mazuri kabisa tumeongeza wiki mbili na naomba mtupime Serikali baada ya hizi wiki mbili ni ambacho tutakuwa tumekifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la kubadilisha Katiba ya Nchi naomba nimwambie Mheshimiwa Cecilia kwamba kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba mamlaka yenye mamlaka halisi ya kukusanya mapato ya nchi yetu ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na ndicho ambacho kwa mujibu wa Sheria Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekifanya na tunaendelea kufanya hatujafanya kitu chochote ambacho kiko kinyume na katiba kinachotupelekea kuleta Mabadiliko ya katika Katiba katika Bunge lako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwisha. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, aulize swali lake.

Na. 485

## Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Njuki – Ilongero – Hydrom

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza:-

Wakati akiwa kwenye Kampeni ya Uchaguzi wa Mwaka 2010 Wilayani Singida Vijijini, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa. Dkt. Jakaya Kikwete aliahidi kuwa Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Njuki – Ilongero – Hydrom lakini ni miaka saba imepita bila utekelezaji wa ahadi hiyo; na Mji wa Ilongero ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Singida Vijijini unakua kwa kasi sana na suala la ujenzi na uboreshaji wa miundombinu yake ni suala la msingi sana kwa sasa:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo iliyotolewa kwa wananchi wa Singida Vijijini ambao wanatarajia barabara hiyo kuwa mkombozi mkubwa wa maendeleo?

**NAIBUWAZIRI WA UJENZI UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Singida kutoka Njuki kuelekea Ilongero hadi Haydom yenye urefu wa kilometa 96.4 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia *TANROADS*. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Manyara. Serikali inaendelea kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Sh.2,851,585,000 zilitumika kujenga kwa kiwango cha lami, jumla ya kilometa 5.6 kuanzia Singida Mjini kuelekea



Ilongero. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sh.1,297.377 zimetumika kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa jumla ya kilomita 2.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika katika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga fedha kwa ajili yakuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Njuki – Ilongero hadi Ngamu tumetenga shilingi milioni 2,043.53 na hizo utazikuta katika ukurasa wa kitabu cha bajeti wa 326 na 345, 365 na 376 Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Sehemu ya Ilongero kupitia Mtinko hadi Nduguti, shilingi milioni 169.76 zimetengwa, rejea ukurasa wa 345 na 376 wa kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Matembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa miundombinu na hasa barabara ni kichocheo kikubwa cha maendeleo; je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara hii kutoka Ilongero Mudida, Kungu Kidarafa hadi Haydom kutoka kilomita 1.6 ambazo zinajengwa kwa sasa kwa mwaka hadi kufikia kilomita tano ili kuharakisha ujenzi huo na kufungua fursa za kiuchumi kwa mikoa ya Manyara, Arusha na Singida?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa ni viongozi wa chama changu ndiyo walitoa ahadi hii nina imani kubwa na Serikali ya chama changu chini ya Jemedari Dkt. John Pombe Magufuli. Je, Waziri yuko tayari sasa kufanya ziara ili kujionea hali halisi ya barabara hii na kuona sehemu iliyofikia ili kuwajengea upya imani wananchi wa Wilaya ya Singida Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Katika jibu lako usisahau kutaja Haydom naona Mbunge wa Mbulu pale yuko *busy* sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ni muhimu sana na kama tulivyoeleza inaunganisha mikoa miwili ya Singida na Manyara; na pale Haydom pana mambo mazito sana ukitoka Haydom unaenda kwenye ile hospitali kubwa ambayo tunategemea sana watu wa maeneo yale kuanzia Singida mpaka Manyara yote. Kwa hiyo, umuhimu wake tunaufahamu na kwa sababu hiyo tutaangalia kuongeza kasi ya kujenga barabara hii kadri tutakavyokuwa tunawezeshwa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, nimjulisha tu Mheshimiwa Mbunge mimi barabara ile nilipita lakini bahati mbaya katika ziara zangu huwa naangalia kazi tu; lakini kwa sababu ni vizuri vile vile kwenda kufanya ziara pamoja na Wabunge, nitaangalia muda mwingine nitakapokwenda katika barabara hiyo nimhusishe na Mbunge ili na yeye ajue kwamba huwa napita katika barabara hiyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tumalizie swali letu la mwisho, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 486

### **Mchango wa Zao la Mbao Katika Pato la Taifa**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Zao la mbao linachangia pato la Taifa katika nchi yetu na zao hili linazalishwa kwa wingi katika Wilaya ya Mufindi katika Mkoa wa Iringa:-

Je, zao hili linaingiza fedha kiasi gani kwa mwaka.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mbao ni miongoni mwa mazao yanayochangia pato la Taifa na pia kutoa ajira kwa wananchi. Zao hili linazalishwa kwa wingi katika Wilaya ya Mufindi kutoka katika shamba la miti la Serikali la *Sao Hill*. Aidha, kiasi cha fedha kinachopatikana kwa mwaka hutegemea kiasi cha meta za ujazo kilichopangwa kuvunwa ambacho nacho kutegemeana na kiasi kinachoruhusiwa kitaalam kuvunwa kwa mwaka kulingana na mpango wa uvunaji wa kila shamba (*annual allowable cut*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mdororo wa uchumi mwanzoni mwa miaka ya 1980, Serikali ilibinafsisha viwanda vyake vikiwemo viwanda vya bidhaa za misitu. Serikali ilibakia na jukumu la kuhifadhi misitu pamoja na kukuza miti katika mashamba yake. Hivyo, Serikali huza miti iliyosimama kwa wawekezaji binafsi ambao huvuna na kuchakata magogo kwa ajili ya mbao, karatasi, nguzo na mazao mengine; shughuli za uchakataji zinabaki kuwa jukumu la sekta binafsi. Kwa kuwa Serikali haihusiki moja kwa moja na uchakataji, takwimu halisi zilizopo wizarani ni za ujazo wa miti inayouzwa kwa wadau mbalimbali na kiasi cha fedha kilichopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2015/2016, jumla ya meta za ujazo wa miti zipatazo 767,946.46 zilivunwa kutoka kwenye mashamba ya Serikali na kuiingizia Serikali jumla ya Sh.58,312,894,416.20. Aidha, kwa mwaka 2016/2017, mashamba ya Serikali yalivunwa na kuuza miti yenye meta za ujazo 754,931 kwa viwanda vya kuzalisha mbao na kuipatia Serikali fedha zipatazo Sh.55,102,043,000.00 ikiwa ni mrabaha na tozo, ushuru wa Halmashauri za Wilaya (*CESS*) na kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa misitu ya asili, mapato yanayotokana na zao la mbao, ni wastani wa shilingi bilioni 18.3 kwa mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Pamoja na Serikali kukiri kuwa zao la mbao linachangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa nchini, lakini barabara zinazolingia katika maeneo ya misitu ni mbovu sana na hazipitiki hasa wakati wa mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka lami katika maeneo hayo ambako mbao hizo zinavunwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa serikali imekuwa ikimuuzia mwekezaji wa nje (*MPM Mgololo*) nusu bei ya magogo, je, iko tayari sasa kuwauzia wajasiliamali wetu bei sawa na hiyo ili kuitikia wito wa uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Ritta kwanza kwa kuonesha nia na dhamira ya kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuendeleza viwanda nchini na hasa viwanda vinvavyopata malighafi yake kupitia misitu; lakini pia nijibu maswali yake ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza la uboreshaji wa miundombinu ya barabara. Kwanza ni jambo ambalo hata upande wa Serikali ni la *interest*, kwamba maeneo ya mashamba yaweze kupitika kirahisi kwa ajili ya kuweza kuyahudumia mashamba yenyewe. Hata hivyo kuhusiana na suala la barabara zainazokwenda kwenye

mashamba yenyewe ambazo zipo kimsingi chini ya Halmashauri ya Wilaya, barabara za makundi haya mawili zinashughulikiwa kwa namna tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara ambazo zipo chini ya Halmashauri; katika Halmashauri ambazo zina mashamba Serikali inachokifanya ni kuweza kuchangia nguvu na uwezo wa kuweza kuhudumia barabara hizo kupitia uazimishaji wa mitambo mbalimbali ya ujenzi wa barabara. Mahali ambapo Serikali za Halmashauri zenyewe huweka mafuta kwenye mitambo hiyo na kuwezesha ujenzi wa barabara hizo. Serikali itaendelea kutumia njia hiyo ili kuweza kuhakikisha kwamba barabara hizo zinaendelea kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa barabara za ndani, tutaendelea kuziboresha kama ambavyo tunaendelea kufanya. Nimshauri tu Mheshimiwa Ritta kwamba haiwezekani kufanya barabara hizo zikafikia kiwango cha lami kwa sasa kwa sababu ya majukumu mengine ya Serikali ya uendelezaji wa miundombinu katika maeneo mengine, hizi za mashambani zitakuwa bora lakini katika kiwango hicho hicho cha barabara za udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la mwekezaji wa Kiwanda cha Karatasi pale Mgojolo (*MPM*); suala hili ni pana, kubwa na la kina na Serikali mara kwa mara imekuwa ikitoa maelezo kuhusu suala hili la mwekezaji huyu ambaye historia yake ni ndefu inaanzia wakati wa Sera ya Ubinafisishaji ya Taifa huko miaka ya nyuma. Hata hivyo, kwa hali ilivyo sasa maelezo ninayoweza kuyatoa hapa kwa sasa hivi ni kwamba kwanza ieleweke kwamba miti ambayo ilikuwa inauzwa au ambayo inauzwa kwa mwekezaji ni magogo yanayotokana na miti ambayo ni ya umri mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umri wa uvunaji wa miti kwa ajili ya bidhaa ya mbao ni miaka 25 na zaidi, lakini magogo haya ambayo yanauzwa kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa ambayo inakwenda kuwa malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa karatasi inayoitwa *pulp* ni miaka kuanzia 14.

Kwa hiyo, si magogo yale yale ambayo anauziwa mwekezaji huyu ambayo wanauziwa wazalishaji wa mbao katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ninachoweza kusema ni kwamba, kwa sababu ya kina cha maelezo katika suala hili, Mheshimiwa Waziri ameandaa maelezo ya kutosha kwa kirefu kuhusiana na suala hili kwa sababu ya kupokea hoja mbalimbali kutoka kwa wananchi wa maeneo hayo hayo na Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kuwa ameungana na wananchi wa maeneo hayo kutaka kujua ni namna gani wananchi wananufaika zaidi na Taifa linanufaika zaidi basi muipe fursa Serikali tuweze kupata nafasi Mheshimiwa Waziri atakuja kutoa maelezo ya kina zaidi katika wakati ambao ataweza kutoa maelekezo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, niwaletee matangazo tuliyonayo. Tutaanza na tangazo la wageni waliopo Bungeni:-

Kundi la kwanza ni la wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni watano wa Mheshimiwa George Simbachawene ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ni watoto wake, watoto wa Mheshimiwa Simbachawene karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni pia 43 wa Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha ambao ni waumini wa Parokia ya Mtakatifu Yohane Paulo wa Pili, Ilazo ya Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambao ni familia yake wakiongozwa na Ndugu Lucy Thomas Malongo ambaye ni mke wa Mheshimiwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tuna wageni waliotembekea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni viongozi kumi wa Serikali za Mitaa

kutoka Kata ya Kikuyu Kusini Maghorofani, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma Mjini, Mkoani Dodoma, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba mpira uliochezwa siku ya Jumamosi tarehe 1 Julai, 2017 kati ya *Bunge Sports Club* na Viongozi wa Dini, matokeo yake ni kama ifuatavyo:-

Mpira wa miguu (*football*) *Bunge Sports Club* ilipata goli moja, Viongozi wa Dini hawakupata goli lolote. Goli la *Bunge Sports Club* lilifungwa na Mheshimiwa Ally Hassan King ambaye pia ndiye aliyekuwa nyota wa mchezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa William Ngeleja anampongeza Kocha Mkuu Mheshimiwa Venance Mwamoto na msaidizi yake Mheshimiwa Ahmed Ngwali. *(Makofi)*

Matokeo ya mpira wa pete (*netball*) *Bunge Queens* walipata magoli sitini na Viongozi wa Dini walipata magoli manne na nyota wa mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Amina Idd Mabrouk ambaye alifunga magoli mengi sana na pongezi zimwendee kocha wa timu hii ambaye ni Ndugu Elionora Mongi. *(Makofi)*

Waheshimiwa wabunge mkiona matokeo mazuri namna hii mjue Mheshimiwa Spika mwenyewe alikuwepo uwanjani, kwa hiyo Mheshimiwa Spika alikuwa mgeni rasmi na sisi vijana wake tusingeweza kumwangusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hayo ndio matangazo tuliyonayo, lakini niwakumbushe sasa hivi kwa sababu tunaingia katika jambo lingine, tuiptie kanuni 66 kuhusu staha ndani ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge ambao huwa mnaongea na simu mkiwa Bungeni, kiti hiki huwa kinaona pande zote, usije ukajikuta umazingira ambayo utatangazwa kwamba wewe unazungumza na simu Bungeni wakati Kanuni ya 66 imekataza, hilo la kwanza.

La pili, unaponyanyuka kwenye kiti chako kwenda kwenye kiti kingine lazima ukumbuke masharti ya kanuni hii, unapaswa kuinamisha kichwa si unaingia kama unaenda mahali kwingine kokote, ndiyo maana kunafika wakati tunakosea heshima humu ndani. Tuzingatie kanuni ya 66 namna inavyotutaka kuenenda humu ndani ili tutunze staha ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutendelea na yaliyopo mbele yetu.

**MHE. JOHN J. MYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, nitaruhusu mwongozo mmoja tu.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru; nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 86(11). Mapema leo asubuhi imetolewa orodha ya shughuli ambayo inaonesha tunajadili Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa mwaka 2017 na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017, Miswada yote hii iko siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii awali ilipaswa kuwasilishwa siku ya kesho kwa mujibu wa ratiba, lakini ghafla jana ratiba ikabadilishwa na hatimaye Miswada hii imeletwa leo kwa hati hiyo ambayo ilikuja mwanzoni ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na Miswada hiyo kuchelewa kuletwa na kubadilika kwa ratiba; kanuni ya 11 inatamka kwamba:-



*“Kamati au Mbunge anaweza kuwasilisha kwa Katibu kwa maandishi mabadiliko anayokusudia kuyafanya katika Muswada huo wakati wa Kamati ya Bunge Zima alionyesha bayana mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika katika ibara inayohusika.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na kanuni hii kutaja bayana kwamba muda wa kuwasilisha *schedules of amendment* yale mabadiliko inaweza ikawa wakati wowote ili mradi tu isiwe kabla ya Bunge kukaa kama Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi Wabunge wafuatao wamewasilisha *schedules of amendment* wakiwakilisha Upinzani; Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Kasuku Bilago, Mheshimiwa Mtolea, Mheshimiwa Mussa, Mheshimiwa Catherine Ruge, Mheshimiwa Japhary Michael na Waheshimiwa wengine wamewasilisha *schedule of amendment* asubuhi kabla ya kikao cha Bunge na wengine kabla hoja hii haijaanza kutolewa na mpaka sasa hoja haijatolewa, lakini katika hali ya kushangaza Katibu wa Bunge amekataa kupokea marekebisho yote haya, maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mlisema awali kwamba tunakwenda kwenye Kamati, tukirudi Waheshimiwa Wabunge mtapata fursa ya kuletea marekebisho yafanyike ili masuala mabovu ndani ya hii Miswada yaweze kurekebishwa, lakini cha kushangaza pamoja na tatizo la hati ya dharura sasa mmefanya hata Miswada isiletewe marekebisho, kinyume kabisa na kanuni na utaratibu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba mwongozo wako ili shughuli hizi zisiendeleo mpaka kwanza hayo marekebisho ya Wabunge hawa mbalimbali wa Kambi ya Upinzani yaweze kupokelewa na Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mnyika ameomba mwongozo na ameenda moja kwa moja kwenye Kanuni ya 86(11), kanuni ambayo inahusu mwongozo pengine kwa sababu ya yeye kwamba anazifahamu sana kanuni hakuona haja ya kutaja. Kanuni ya 68(7) ndiyo inayoombewa mwongozo.

Sasa ametoa maelezo ambayo sina haja ya kuyarejea, ameenda kwenye Kanuni ya 86(11) ambayo inatoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa mapendekezo yao ya marekebisho au mabadiliko ambayo wanaona yafanywe. Sasa fasili ya 11 ambayo Mheshimiwa Mnyika ameisoma na mimi nitairudia ili tuweze kwenda pamoja, inasema hivi:-

*“Kamati au Mbunge anaweza kuwasilisha kwa Katibu kwa maandishi mabadiliko anyokusudia kuyafanya katika Muswada huo wakati wa Kamati ya Bunge Zima akionesha bayana mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika katika kila ibara inayohusika.”*

Mambo mawili ya msingi, la kwanza kuwasilisha kwa Katibu kwa maandishi mabadiliko anayokusudia, siyo awasilishe kwa Katibu wakati zoezi likiendelea. Maana kwa maelezo marefu aliyotoa Mheshimiwa Mnyika ni kana kwamba hata wakati ule Kamati ya Matumizi ikiwa inaendelea hapa bado unaweza kuleta, hapana unapeleka kwa Katibu kwa maandishi yale unayokusudia kuleta hapa Bungeni.

Sasa nitoe maelezo kwa nini nimesema mawili, hilo ni la kwanza, la pili; Bunge hili lilishatoa mwelekeo kwa sababu ya haya mambo ya kuleta marekebisho ama mabadiliko au niseme mapendekezo ya mabadiliko wakati Bunge likiendelea wakati upande ulioleta Muswada uko humu Bungeni ukisikiliza maoni wakati huo huo watu wengine walikuwa wakipeleka kwenye Ofisi ya Katibu hayo mapendekezo yao ya mabadiliko. Bunge hili lilikwisha kutoa mwongozo wa saa ngapi mabadiliko hayo yapelekwe kwa Katibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo ulikuwa umetolewa hapa kwenye kiti hiki ukielekeza Wabunge ni wakati gani wapeleke kwa Katibu. Kwa sababu hiyo, matumizi ya Kanuni ya 86(11) kwa mwongozo huo ambao uliwahi kutolewa hapa ni kwamba mabadiliko hayo ama mapendekezo ya mabadiliko lazima yapelekwe Ofisi ya Katibu ili kuweza kutoa fursa kwa Serikali kuona kama hayo mabadiliko wanaweza wakayafanyia kazi au hapana, hilo ni moja.

La pili, inatoa sasa fursa ya Serikali kukaa humu ndani kusikiliza Waheshimiwa Wabunge wanasema nini badala ya kukimbizana sasa na yale mabadiliko na ndiyo maana lazima yapelekwe kwa mwandishi ili Serikali ipate nafasi ya kuyaangalia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika wakati akimaliza pamoja na kwamba ulikuwa umeombwa mwongozo akasema kwamba zoezi hili tunalotaka kuingia kulifanya tuliache ili tutoe fursa ya Wabunge hawa, mabadiliko yao kuweza kukubaliwa. *(Makofi)*

Sasa mwongozo wangu ni huu, tutaendelea na shughuli iyopo mbele kwa sababu Bunge lilishawahi kutoa mwongozo wa saa ngapi mapendekezo ya mabadiliko yapelekwe Ofisi ya Katibu kwa maandishi. Kwa sababu hiyo tutaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, angeuliza saa ngapi Mheshimiwa Mnyika ningeelewa kwa sababu yeye huwa hayupo mara nyingi Bungeni; Mheshimiwa Shahari ulikuwepo na wote mlikuwepo. Ukiniuliza mimi saa ngapi mwongozo ulishatolewa na kama unataka nirudie kuusema nitausema wakati tukiendelea na shughuli nitakapoletewa hapa kwa sababu ulisemewa hapa ndani kila Mbunge ni lazima anapaswa kufuata huo mwongozo. *(Makofi)*

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili, 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*)**

**na**

**Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi, 2017 (*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*) na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi, 2017 (*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*) sasa usomwe kwa mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitisha Miswada hii na kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maudhui ya Miswada hii, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai, kutujalia afya na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani kubwa aliyoonesha kwangu kwa kuiteua kuwa Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutimiza na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Watanzania wote ni mashahidi wa juhudi kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kuwa nchi inaendeshwa kwa misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na uwajibikaji. Wote tunajionea mafanikio makubwa ambayo nchi yetu imeyapata katika nyanja mbalimbali katika kipindi cha uongozi wake. Namtaka kila la heri na kumwahidi kuwa nitaendelea kuitumikia nchi yangu kwa akili zangu zote na uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe na Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu, Katibu wa Bunge, Makatibu wa Kamati na Watendaji wengine wa Bunge kwa msaada na ushirikiano mkubwa mlioutoa ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ndani ya muda uliopangwa. Pia nalipongeza Bunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa Kikatiba wa kutunga sheria, lakini pia kwa kuishauri na kuisimamia Serikali inapotekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Kwa ujumla, napenda kuwashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoipatia Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Miswada iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa namna ya kipekee, napenda kuzishukuru kwa pamoja Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo; chini ya Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge; na Mheshimiwa Doto Biteko, Mbunge, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kujadili Miswada na maoni waliyoipatia Serikali ambayo kwa kiasi kikubwa imewezesha kuboresha maudhui ya Miswada hiyo. Kazi ya Kamati haikuwa rahisi na kuna wakati palikuwa na mikwaruzano. Tuwiane radhi kwa yote yaliyotokea, lakini sasa tuwe pamoja kuhakikisha tunapitisha Miswada hii ya kihistoria kwa ukombozi wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*) na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi, 2017 (*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*).

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa 2017 unapendekeza kuweka masharti yanayohusianisha misingi iliyomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, mikataba na misingi ya sheria mbalimbali za Kimataifa ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazitambua na ama imesaini au kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inayopendekezwa kupitia Muswada huu ina msingi wake katika Ibara ya 8(1) ya Katiba ambayo inaweka masharti kuwa Tanzania ni nchi inayozingatia msingi wa demokrasia na haki ya kijamii na kwa msingi huo, wananchi wake ndio msingi wa mamlaka yote ya nchi na Serikali inawajibika kwa wananchi wake. Ibara hiyo inaeleza kama ifuatavyo:-

*“Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo: –*

(a) *wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii;*

(b) *lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;*

(c) *Serikali itawajibika kwa wananchi;*

(d) *Wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni nchi yenye uhuru kamili ina haki na mamlaka ya kusimamia maliasili na utajiri wake. Kwa msingi huo, Serikali inayo wajibu wa kulinda maslahi ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mikataba inayoingia kuhusiana na maliasili na utajiri huo kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara hiyo inaeleza kama ifuatavyo:-

*“(1) Kila mtu ana wajibu wa kulinda mali asilia ya Jamhuri ya Muungano, mali ya Mamlaka ya Nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine.*

*(2) Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya Mamlaka ya Nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu, na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia misingi hiyo iliyowekwa na Katiba, Ibara ya 9(1)(c) ya Katiba inaelekeza kuwa shughuli za Serikali zitekelezwe kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa ujumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya maazimio ya Umoja wa Mataifa; Muswada huu unazingatia uwepo wa Sheria ya Kimataifa inayotambua haki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na umiliki wa maliasili. Aidha, Muswada umezingatia kwamba Tanzania imesaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo Azimio la Umoja wa Mataifa Namba 523(vi) la tarehe 12 Januari,

1952; Azimio Namba 626 (vii) la tarehe 21 Desemba, 1952; Azimio Namba 1314 (xiii) la tarehe 12 Desemba, 1958; Azimio Namba 1515 (xv) la tarehe 15 Desemba, 1960; Azimio Namba 1803 (xvii) la tarehe 14 Desemba, 1962; Azimio Namba 2158 (xxi) la tarehe 6 Desemba, 1966; Azimio Namba xxv la tarehe 11 Desemba, 1970; na Azimio Namba 32 la tarehe 12 Desemba, 1974 ambayo inatambua haki ya Jamhuri ya Muungano katika kusimamia rasilimali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hifadhi na ulinzi wa maliasili za nchi; kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika Mikataba ya Kimataifa, Muswada huu unakusudia kuweka masharti yatakayohakikisha kwamba hatua yoyote inayochukuliwa kuhusu uwekezaji wa rasilimali za Taifa inatambua na kuzingatia haki ya Jamhuri ya Muungano kama Taifa huru na lenye mamlaka ya kusimamia na kutumia rasilimali zake kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazopendekezwa katika Muswada huu zinalenga kulinda mali na rasilimali za Taifa na kuondoa aina yoyote ya upotevu au ubadhirifu wa rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpangilio wa maudhui ya Miswada; tuanze na Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili wa mwaka 2017. Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda kueleza kuwa Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili wa 2017, huu ambao una utangulizi mahususi, umegawanyika katika sehemu tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya jumla kama vile jina, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, matumizi ya sheria na ufafanuzi wa msamiati. Katika Ibara ya Pili ya sehemu hii, Muswada unabainisha wazi kwamba sheria inayopendekezwa itatumika kwa pande zote mbili za Muungano bila kuathiri Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar juu ya usimamizi wa rasilimali zake.



Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inaainisha mahitaji ya msingi katika kuhakikisha kwamba mamlaka ya nchi juu ya rasilimali za Taifa yanatambuliwa na kulindwa. Ibara ya Nne inatamka bayana kwamba wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakuwa na mamlaka ya kudumu (*permanent sovereignty*) ya rasilimali na maliasili zote. Aidha, umiliki na udhibiti wa rasilimali na maliasili hizo utasimamiwa kupitia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la masharti haya ni kutambua na kutekeleza masharti ya Ibara ya Nane ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo msingi wa ukuu wa wananchi katika kumiliki na kutumia kwa manufaa yao na nchi kwa ujumla rasilimali zote za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tano inaweka masharti kwamba rasilimali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mali ya kudumu ya wananchi wa Tanzania na kwamba shughuli zote za utafutaji na uendelezaji wa rasilimali hizo utafanywa na Serikali kwa niaba ya Watanzania. Hii italipa Taifa fursa ya kuwa na mamlaka ya umiliki juu ya hatua na bidhaa zote zitokanazo na utafutaji na uendelezaji wa rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Sita ya Muswada inazuia utafutaji na uendelezaji wa rasilimali za Tanzania usiokuwa na tija kwa Watanzania na Taifa kwa ujumla na kwamba uwekezaji wowote katika rasilimali za nchi utazingatia mamlaka ya nchi (*sovereignty*) au kwa Kiswahili ambacho sidhani kama kimekubalika, bado kinafanyiwa kazi; – istikilari, juu ya ya rasilimali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Nane ya Muswada inaweka masharti ya ushiriki wa Watanzania na Serikali katika utafutaji na uendelezaji wa rasilimali za Taifa. Ibara hii inalenga kuhakikisha kwamba Taifa linapata faida kwa kuongeza mapato na kuhakikisha Watanzania wanashiriki na kuendesha rasilimali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tisa ya Muswada inazuia usafirishaji wa rasilimali zisizoongezwa thamani nje ya nchi. Lengo la mapendekezo hayo ni kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani na rasilimali za Tanzania zinafanyika nchini ili kuongeza mapato kwa Taifa na kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Kumi ya Muswada inatamka kuwa mapato ya fedha yote yanayotokana na rasilimali na maliasili hizo yatawekwa hapa nchini katika benki na taasisi za fedha za Tanzania. Naomba nirudie hiyo tena. Ibara ya Kumi ya Muswada inatamka kuwa mapato ya fedha yote yanayotokana na rasilimali na maliasili hizo yatawekwa hapa nchini katika benki na taasisi za fedha za Tanzania; na itakuwa ni kosa kuweka fedha hizo nje ya nchi isipokuwa gawio ambalo mwekezaji ataruhusiwa kutoa nje ya nchi kwa mujibu wa sheria za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu inatambua na kulinda mamlaka ya Jamhuri ya Muungano juu ya rasilimali na inampatia mamlaka Waziri mwenye dhamana ya sheria hii kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji madhubuti wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 inatamka kuwa mashauri kuhusu rasilimali na maliasili ya nchi chini ya mamlaka ya kudumu ya nchi, hayatafanyika katika Mahakama au Mabaraza ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili na Rasilimali za Nchi wa 2017, unapendekeza masharti yanayowezesha wananchi kupitia Bunge kuweza kupokea taarifa ya mikataba inayohusu rasilimali za nchi ambayo imefungana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kujiridhisha endapo masharti, makubaliano na mikataba hiyo haina masharti hasi yanayokinzana na maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa masharti haya ni kutekeleza masharti ya Ibara za 8, 9 na 27 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo nimetangulia kuzisoma, ambazo zinatoa wajibu kwa kila Mtanzania kuhakikisha kwamba anashiriki kikamilifu kulinda mali na rasilimali za nchi kwa maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla. Vilevile sheria inayopendekezwa, imelenga kuyafanya baadhi ya maazimio ya Umoja wa Taifa ambayo nimetangulia kuyataja yote, kuhusu umiliki, uendelezaji na usimamizi wa maliasili za nchi kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia wajibu huo, kila Mtanzania; na kwa kutambua wajibu wa Bunge kama chombo cha uwakilishi, sheria inayopendekezwa imelipa nguvu Bunge kupokea taarifa ya mikataba yote inayohusiana na maliasili za nchi na rasilimali zake ambayo imeingiwa na Jamhuri ya Muungano ili kujiridhisha kuwa masharti yaliyomo katika mikataba hiyo yamezingatia maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla; na endapo masharti hayo hayazingatii maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla, basi Bunge liweze kuishauri Serikali kufanya majadiliano na wahusika wengine katika mikataba kwa lengo la kuondoa masharti hasi yasiyokuwa na manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mapendekezo yaliyomo katika Muswada, endapo utapita kuwa sheria, endapo Serikali haitafikia makubaliano yenye tija kwa wananchi na Taifa ndani ya muda utakaokubaliwa na pande zote, basi masharti yote hasi yatachukuliwa kwamba yamefutwa na siyo sehemu ya mikataba na Serikali haitakuwa na wajibu wowote wa kutekeleza masharti ambayo yamebainika kuwa hasi.

Naomba nirudie tena hapo. Kwa mujibu wa mapendekezo yaliyomo katika Muswada, endapo Serikali haitafikia makubaliano yenye tija kwa wananchi na Taifa ndani ya muda utakaokubaliwa na pande zote, basi masharti yote hasi yatachukuliwa kwamba yamefutwa na siyo sehemu ya mikataba na Serikali haitakuwa na wajibu wowote wa kutekeleza masharti ambayo yamebainika kuwa hasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi wa 2017 umegawanyika katika Sehemu kuu Tatu ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya jumla kama vile jina la sheria na kuanza kutumika kwa sheria inayopendekezwa. Ibara ya Pili ya Muswada inaweka masharti kwamba sheria hii itatumika kwa mikataba iliyoingiwa au kusainiwa kabla au baada ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, mikataba yote ya sasa itapitiwa kwa mujibu wa sheria hii. Naomba nitumie fursa hii kusema kwamba kumekuwa na uongo katika *forum* ya *Jamii Forums* kwamba Waziri huyu aliyesimama hapa amesema mikataba ya zamani haitapitiwa. Mikataba ya zamani itapitiwa; na yeyote ambaye ameisoma sheria hii angejua huo ni uzushi, ni uzandiki na ufitina. (*Makofi*)

Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti yanayolipatia Bunge madaraka na utaratibu wa kupitia makubaliano na mikataba yote inayohusu maliasili za nchi na kuishauri Serikali kufanya majadiliano yatakawezesha kuondoa masharti hasi. Kwa dhati hiyo, Ibara ya 6(1) inaweka utaratibu wa namna ya kuanzisha majadiliano na upande wa pili wa mkataba ili kuondoa masharti hasi kama yalivyobainishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 6(2) ya Muswada. Ibara ya 6(2) ya Muswada imeyaainisha masharti hayo ambayo ni dhahiri au kwa taathira yake ni masharti hasi ambayo yanapaswa kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Nane ya Muswada inampatia Waziri madaraka ya kuandaa kanuni zitakazowezesha utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, majedwali ya marekebisho ya Miswada ya sheria zote mbili yanakusudia kufanya marekebisho katika sehemu mbalimbali za Miswada kwa kuzingatia maoni ya wadau na Kamati za Bunge zilizojadili Miswada hii. Aidha, pamoja

na mambo mengine, marekebisho hayo yanatambua maazimio ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kama yalivyoainishwa kwenye majedwali ya marekebisho kuwa sehemu ya sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii miwili inalenga kuleta mapinduzi makubwa katika kulinda rasilimali na maliasili zetu hapa Tanzania. Dhana ya Miswada hii ni ukombozi wetu. Naomba nimnukuu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika moja ya insha zake tatu za kifalsafa katika Kitabu hiki cha Insha Tatu za Kifalsafa za Mwalimu, alisema:-

*"Mapinduzi haya yanayotakiwa ni kwa wote, siyo kwa wachache. Tulipoonewa, tulionewa wote; tuliponyonywa, tulinyonywa wote; tulipopuuzwa, tulipuuzwa wote; ni unyonge wetu sote kwa pamoja ndiyo uliotufanya tukaonewa, tukanyonywa na tukapuuzwa. Mapinduzi tunayoyataka sasa ni lazima yawe ni yetu wote pamoja ili Mtanzania asiwe mnyonge na unyonge wake ukatumiwa kumnyonya na kumpuuzwa."* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena nukuu ya Mwalimu Nyerere. *"Mapinduzi haya yanayotakiwa ni kwa wote, siyo kwa wachache. Tulipoonewa, tulionewa wote; tuliponyonywa, tulinyonywa wote; tulipopuuzwa, tulipuuzwa wote; ni unyonge wetu sote kwa pamoja ndiyo uliotufanya tukaonewa, tukanyonywa na tukapuuzwa. Mapinduzi tunayoyataka sasa ni lazima yawe ni yetu wote pamoja ili Mtanzania asiwe mnyonge na unyonge wake ukatumiwa kumnyonya na kumpuuzwa."* Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa George Mcheche Masaju kwa ushauri na msaada ambao yeye binafsi amenipatia katika majadiliano kwenye Kamati za Bunge na hatua mbalimbali za maandalizi ya Miswada hii. Kipekee, vile vile natoa shukurani kwa timu ya Waandishi wa Sheria ambao wametoa msaada mkubwa katika Kamati za kudumu za Bunge na maandalizi ya majedwali ya marekebisho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati Maalum ambao waliandaa Miswada yote miwili na kushiriki katika hatua zote za majadiliano wakati wa maandalizi yake. Napenda niwataje; Namshukuru sana Profesa Florence Dominic Andrew Makinika Luoga;, namshukuru sana Ndugu Casmir Sumba Kiuki; namshukuru sana Ndugu Honourous Njole na namshukuru sana Ndugu Said Kalunde kwa msaada wao mkubwa katika kufanya kazi hii adhimu katika historia ya Taifa letu. *(Makofi)*

Miswada hii ni Miswada ya ukombozi. Kwa mara ya kwanza tangu nchi hii ipate uhuru, sasa tunatamka mamlaka ya nchi yetu bayana, bila tashwishi na kwa uwazi na kwa sauti ya jeuri tuliyokuwa nayo wakati wa maisha ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu kujadili Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali wa 2017 *(The Natural Wealth And Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017)* na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikatiba Inayohusu Rasilimali na Maliasili za Nchi 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contract Review and Negotiations of Unconscionable Terms Bill, 2017)*, kisha kuipitisha ili endapo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ataridhia na kuiweka sahihi, ziwe sehemu ya sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***SPECIAL BILL SUPPLEMENT***

***No. 3***

***28<sup>th</sup> June, 2017***

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 4  
Vol. 98 dated 28<sup>th</sup> June, 2017*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of  
Government

---

THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES (PERMANENT  
SOVEREIGNTY) ACT, 2017

ARRANGEMENT OF SECTIONS

PART I  
PRELIMINARY PROVISIONS

<i>Section</i>	<i>Title</i>
1.	Short title and commencement.
2.	Application.
3.	Interpretation.

PART II

PERMANENT SOVEREIGNTY OVER NATURAL WEALTH AND  
RESOURCES

4. Proclamation of permanent sovereignty.
5. Inalienability of natural wealth and resources.
6. Prohibition of exploitation except for the benefit of the People.
7. Guarantee of returns from natural wealth and resources.
8. Participation of the People and Government.
9. Requirement for beneficiation.
10. Retention of earnings.

PART III

PROTECTION OF PERMANENT SOVEREIGNTY

11. Prohibition of proceedings in foreign courts.
12. Review by the National Assembly.
13. Power to make regulations.



—————  
**NOTICE**  
—————

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,  
27<sup>th</sup> June, 2017  
*Cabinet*

JOHN W. H. KIJAZI,  
*Secretary to the*

**PREAMBLE**

WHEREAS, the fundamental objectives and directive principles of state policy enshrined under sub-article (1) of Article 8 of the Constitution, asserts that the United Republic is a State which adheres to the principles of democracy and social justice and, accordingly, sovereignty resides in the People and it is from the People that the Government, through the Constitution, derives all its powers and authority and that the primary objective of the Government shall be the welfare of the People;

AND WHEREAS, international law recognizes the right of the United Republic to assert permanent sovereign right for the purpose of exploring, exploiting and managing its natural resources;

AND RECOGNIZING, that the United Republic is a signatory to the United Nations General Assembly Resolution 1803 (XVIII) of 14<sup>th</sup> December, 1962 and Resolution 3281 (XXIX) of 12 December 1974 and subscribes to the stipulations therein;

AND WHEREAS, the United Republic being a sovereign state has permanent sovereignty over all natural wealth and resources thence imposing on the Government the responsibility of ensuring that interests of the People and the United Republic are paramount and protected in any arrangement or agreement which the Government makes or enters in respect of such natural wealth and resources;

AND WHEREAS, by virtue of Article 27 of the Constitution the protection of natural wealth and resources in the United Republic is charged on the People and the Government and the control of which is entrusted to the President;

AND WHEREAS, the fundamental objectives and directive principles of state policy enshrined under paragraphs (c) and (i) of Article 9 of the Constitution requires all activities of the Government to be conducted in such a manner as to ensure that the national wealth and heritage are harnessed, preserved and applied for the common good, and to prevent exploitation, and that, the use of the national wealth and heritage places emphasis on the development of the People and the Nation, and in particular, geared towards the eradication of poverty, ignorance and diseases;

AND WHEREAS, the Government has resolved to fairly and equitably undertake protracted measures intended to ensure that the natural wealth and resources of the United Republic are used for the greatest benefit and welfare of the People and the United Republic by ensuring that all arrangements or agreements made into by the Government protect interests of the People and the United Republic;

AND WHEREAS, it is necessary to make comprehensive statutory provisions to provide for ownership and control over natural wealth and resources and to provide for the protection of permanent sovereignty over natural wealth and resources;

NOW THEREFORE, be it ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania as follows:

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

Short title and commencement

1. This Act may be cited as the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017, and shall come into operation on such date as the Minister may, by notice published in the *Gazette*, appoint.

Application

2. This Act shall, without prejudice to the authority of the Revolutionary Government of Zanzibar over ownership and control of its own national wealth and resources, apply to Mainland Tanzania .

Interpretation

3. In this Act, unless the context otherwise requires-

“arrangement or agreement” means any contract relating to extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources;

“Minister” means the Minister responsible for constitutional affairs;

“natural wealth and resources” means all materials or substances occurring in nature such as soil, subsoil, gaseous and water resources, and flora, fauna, genetic resources, aquatic resources, micro-organisms, air space, rivers, lakes and maritime space, including the Tanzania’s territorial sea and the continental shelf, living and non-living resources in the Exclusive Economic Zone which can be extracted, exploited or acquired and used for economic gain whether processed or not;

“national jurisdiction” means the authority of judicial system in the United Republic to administer justice over things and persons within the United Republic.

## PART II

### PERMANENT SOVEREIGNTY OVER NATURAL WEALTH AND RESOURCES

Proclamation of permanent sovereignty

**4.**-(1) The People of the United Republic shall have permanent sovereignty over all natural wealth and resources.

(2) The ownership and control over natural wealth and resources shall be exercised by, and through the Government on behalf of the People and the United Republic.

Inalienability of natural wealth and resources

**5.**-(1) The natural wealth and resources shall be inalienable in any manner whatsoever and shall always remain the property of the People of the United Republic.

(2) The natural wealth and resources shall be held in trust by the President on behalf of the People of the United Republic.

(3) For purposes of subsections (1) and (2), all activities and undertakings relating to exploration of natural wealth and resources shall be conducted by the Government on behalf of the People of the United Republic.

Prohibition of exploitation except for the benefit of the People Cap. 2

**6.**-(1) Pursuant to paragraphs (c) and (i) of Article 9 of the Constitution, it shall be unlawful to make any arrangement or agreement for the extraction, exploitation or

acquisition and use of natural wealth and resources except where the interests of the People and the United Republic are fully secured and approved by the National Assembly.

(2) Any arrangement or agreement for international cooperation for the economic and social development involving natural wealth and resources, whether in the form of public or private capital investments, exchange of goods and services, technical assistance or exchange of scientific information shall be such as to further Tanzania's independence based upon respect for permanent sovereignty over natural wealth and resources.

Guarantee of returns from natural wealth and resources

7. In any arrangement or agreement for extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources, there shall be guaranteed returns into the Tanzanian economy from the earnings accrued or derived from such extraction, exploitation or acquisition and use.

Participation of the People and Government

8. Any authorization granted for the extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources, arrangements shall be made or given to ensure that the Government obtains an equitable stake in the venture and the People who are citizens of the United Republic may acquire stakes in the venture.

Requirement of beneficiation

9.-(1) Any arrangement or agreement for the extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources shall

ensure that no raw resources shall be exported for beneficiation outside the United Republic.

(2) For the purpose of subsection (1), any arrangement or agreement for the extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources, there shall be commitment to establish beneficiation facilities within the United Republic.

Retention of earnings

**10.**-(1) Any arrangement or agreement for extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources shall require that earnings from disposal or dealings be retained in the banks and financial institutions established in the United Republic.

(2) For the purpose of subsection (1), it shall be unlawful to keep such earnings in banks or financial institutions outside the United Republic except where distributed profits are repatriated in accordance with the laws of Tanzania.

### PART III

#### PROTECTION OF PERMANENT SOVEREIGNTY

Prohibition of proceedings in foreign courts

**11.**-(1) Pursuant to Article 27 (1) of the Constitution, permanent sovereignty over natural wealth and resources shall not be a subject of proceedings in any foreign court or

tribunal.

(2) For the purpose of subsection (1), disputes relating arising from extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources shall be adjudicated by judicial bodies or other organs established in the United Republic and accordance with laws of Tanzania.

(3) For the implementation of subsection (2), in any arrangement or agreement the jurisdiction of judicial bodies or other bodies established in the United Republic and application of laws of Tanzania shall be acknowledged and incorporated.

Review by the  
National  
Assembly

**12.** All arrangements or agreements entailing extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources may be reviewed by the National Assembly.

Power to make  
regulations

**13.-(1)** The Minister may make regulations for the better carrying out of the provisions of this Act.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), the regulations shall prescribe:

- (a) code of conduct for investors in natural wealth and resources;
- (b) minimum guidelines for inspection, monitoring and evaluation of investments in natural wealth and resources; and
- (c) any thing which is incidental or conducive to the effective

implementation of this Act.

---

OBJECTS AND REASONS

---

This Bill proposes the enactment of the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017 and makes provisions for the integration of the regional and international agreements on the country's permanent sovereignty over natural wealth and resources. The Agreements trace origin in the General Assembly Resolutions 523 (VI) of 12 January 1952 and 626 (VII) of 21 December 1952, Resolution 1314 (XIII) of 12 December 1958,



Resolution 1515 (XV) of 15 December 1960, Resolution 1803 (XVII) of 14 December 1962 Resolution 2158 (xxi) of 6 December 1966, Resolution 2692 (xxv) of 11 December 1970 and Resolution 3281 of 12 December 1974.

In the light of international agreement to which the United Republic is signatory, this Bill seeks to ensure that any measure taken in investments in natural and strategic resources must be based on the recognition of the inalienable right of the country freely to dispose of its natural wealth and resources in accordance with its national interests, and on respect for the economic independence, free from wanton exploitation.

The Bill also seeks to implement the provision of Article 27 of the Constitution of the United Republic, which asserts the duty of every person to protect the natural resources of the United Republic, the property of the state authority and all property collectively owned by the People of the United Republic. The measures stipulated in the Bill are aimed at safeguarding the property of the state authority and all property collectively owned by the People of the United Republic, to combat all forms of waste and squander, and to manage the national economy assiduously with the attitude of people who are masters of the destiny of their nation.

The Bill is divided into Three Parts. Part I provides for preliminary matters including the short title, date of commencement, application and construction of terms.

Part II provides for key requirements in securing permanent sovereignty over natural wealth and resources. Lastly, Part III provides for the protection of permanent sovereignty over natural wealth and resources, and powers of the Minister to make regulations.

---

### **MADHUMUNI NA SABABU**

---

Muswada huu unapendekeza kutungwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili, 2017 kwa kuweka masharti yanayohusianisha misingi iliyomo katika mikataba na itifaki mbalimbali ambazo Jamhuri ya Muungano imetia saini na kuridhia. Baadhi ya masharti yanayopendekezwa katika Muswada huu yanatokana na Azimio la Umoja wa Mataifa Namba 523(VI) la tarehe 12 Januari, 1952 na Azimio Namba 626(VII) la Tarehe 21 Disemba, 1952, Azimio Namba 1314(XIII) la tarehe 12 Disemba, 1958, Azimio Namba 1515(XV) la tarehe 15 Disemba, 1960 Azimio Namba 1803(XVII) la tarehe 14 Disemba, 1962; Azimio Namba 2158(XXI) la tarehe 6 Disemba 1966, Azimio Namba XXV la tarehe 11 Disemba, 1970; na Azimio Na. 32 la tarehe 12 Disemba 1974.

Kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika Mikataba hiyo, Muswada huu unakusudia kuweka masharti yatakayohakikisha

kwamba hatua yoyote inayochukuliwa kuhusu uwekezaji wa rasilimali za Taifa inatambua na kuzingatia haki ya Jamhuri ya Muungano kama Taifa huru na lenye mamlaka kusimamia na kutumia rasilimali zake kwa maslahi ya Taifa. Aidha, Muswada huu unakusudia kutekeleza masharti ya Ibara ya 27 ya Katiba ambayo, pamoja na mambo mengine, inamtaka kila Mtanzania kulinda na kusimamia kikamilifu rasilimali za Nchi kwa masilahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Hatua zinazopendekezwa katika Muswada huu zinalinga kulinda mali na rasilimali za Taifa na kuondoa aina yoyote ya upotevu au ubadhirifu wa rasilimali za Nchi.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya I inahusu masharti ya jumla kama vile jina, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, matumizi ya sheria na ufafanuzi wa misamiati.

Sehemu ya II inaainisha mahitaji ya msingi katika kuhakikisha kwamba mamlaka ya nchi juu ya rasilimali za Taifa yanatambuliwa na kulindwa. Mwisho, Sehemu ya III inatambua na kulinda mamlaka ya Jamhuri ya Muungano juu ya rasilimali na inampatia mamlaka Waziri ya kutengeneza kanuni.

Dar es Salaam,  
23 Juni, 2017

PALAMAGAMBA J.A.M. KABUDI,  
*Waziri wa Katiba na Sheria*

ISSN 0856 – 01001X

---

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***SPECIAL BILL SUPPLEMENT***

***No. 2***

***28<sup>th</sup> June, 2017***

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania  
No. 4 Vol. 98 dated 28<sup>th</sup> June, 2017*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of  
Government

---

THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES CONTRACTS (REVIEW  
AND RE-NEGOTIATION OF UNCONSCIONABLE TERMS) ACT,  
2017

ARRANGEMENT OF SECTIONS

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

<i>Section</i>	<i>Title</i>
1.	Short title and commencement.
2.	Application.
3.	Interpretation.

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

PART II

POWERS OF NATIONAL ASSEMBLY TO REVIEW CONTRACTS

4. Powers to review arrangements or agreements.
5. Procedure for Review.

PART III

GOVERNMENT RE-NEGOTIATION OF UNCONSCIONABLE TERMS

6. Re-negotiation of arrangements and agreements.
7. Rectification and expunge of unconscionable terms.
8. Powers to make regulations.

---

**NOTICE**

---

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with statement of objects and reasons.

Dar es Salaam,  
27<sup>th</sup> June, 2017

JOHN W.H. KIJAZI  
*Secretary to the Cabinet*

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

**PREAMBLE**

WHEREAS, by virtue of Article 27 of the Constitution the protection of natural wealth and resources in the United Republic is charged on the People and the Government the control of which is entrusted to the President;

AND WHEREAS, by virtue of Article 9(c) and (i) of the Constitution requires all activities of the Government to be conducted in such a manner as to ensure that the national wealth and heritage are harnessed, preserved and applied for the common good and to prevent exploitation and that the use of the national wealth and heritage places emphasis on the development of the People and the United Republic and in particular, geared towards the eradication of poverty, ignorance and diseases;

AND WHEREAS, the Government has resolved to fairly and equitably undertake protracted measures intended to ensure that the natural wealth and resources of the United Republic are used for the greatest benefit and welfare of the People and the United Republic by ensuring that all arrangements or agreements by the Government protect interests of the People and the United Republic;

AND WHERE AS, pursuant to International Law, the United Republic has permanent sovereign rights for the purpose of

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

exploring, exploiting and managing its Natural Resources. AND RECOGNISING, that the United Republic is a signatory to the United Nations General Assembly Resolution 1803(XVIII) of 14<sup>th</sup> December, 1962 and subscribes to the stipulations therein;

AND WHEREAS, the United Republic being a sovereign state has permanent sovereignty over all natural wealth and resources thence imposing on the Government the responsibility of ensuring that the interests of the People and the United Republic are paramount and protected in any arrangement or agreement which the Government makes or enters in respect of such natural wealth and resources;

AND WHEREAS, it is necessary to make comprehensive statutory provisions that require all arrangements or agreements on natural wealth and natural resources to be tabled for review by the National Assembly for purposes of ensuring that any unconscionable terms therein is rectified or expunged;

NOW THEREFORE, be it ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania as follows:

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

Short title and commencement

**1.**-(1) This Act may be cited as the Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017.

(2) The Act shall come into operation on such date as the Minister may, by notice published in the *Gazette*, appoint.

Application

**2.**This Act shall, without prejudice to the authority of the Revolutionary Government of Zanzibar over ownership and control of its own national wealth and resources, apply to Mainland Tanzania in respect of all arrangements or agreements made over natural wealth and resources by the Government before or after coming into operation of this Act.

Interpretation

**3.** In this Act, unless the context otherwise requires:

“arrangement or agreement” means any contract relating to extraction, exploitation, acquisition and use of natural wealth and resources;

Cap.2

“Constitution” means the Constitution of the United Republic;

“Minister” means the Minister responsible constitutional affairs;

“natural wealth and resources” means all



*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

materials or substances occurring in nature such as soil, subsoil, gaseous and water resources, and flora, fauna, genetic resources, aquatic resources, micro-organisms, air space, rivers, lakes and maritime space, including the Tanzania's territorial sea and the continental shelf, living and non-living resources in the Exclusive Economic Zone which can be extracted, exploited or acquired and use for economic gain, whether processed or not;

"unconscionable term" means any term in the arrangement or agreement on natural wealth and resources which is contrary to good conscience and the enforceability of which jeopardises or is like to jeopardise the interests of the People and the United Republic.

PART II

POWERS OF NATIONAL ASSEMBLY TO REVIEW CONTRACTS

Powers to  
review  
arrangements or  
agreements  
Cap.2

**4.-(1)** For effective performance of oversight and advisory functions stipulated under Article 63(2) of the Constitution, the National Assembly may review any arrangements or agreement made by the Government relating to natural wealth and resources.

(2) In asserting the principle of permanent sovereignty over natural wealth and resources, there shall be implied in every arrangement or agreement that the negotiation are concluded in good faith and fairly and, at all

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

times, observe the interests of the People and the United Republic.

(3) The principle of permanent sovereignty over natural wealth and resources shall afford fair and equitable treatment to the parties.

(4) The National Assembly shall devise the procedure under the Standing Orders of the National Assembly for reviewing any arrangement or agreement made by the Government over natural wealth and resources.

Procedure for review

**5.-(1)** All arrangements or agreements on natural wealth and resources made by the Government shall, within six sitting days of the National Assembly next following the making of such arrangement or agreements be reported to the National Assembly.

(2) Where upon consideration of the report submitted pursuant to subsection (1), the National Assembly finds that the arrangement or agreement contains unconscionable terms, it may, by resolution, direct the Government to initiate re-negotiation of the arrangement or agreement with a view to rectifying the terms.

(3) Where the National Assembly considers that certain terms of arrangement or agreement on natural wealth and resources or the entire arrangement or agreement on natural wealth and resources

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

made before coming into force of this Act are prejudicial to the interests of the People and the United Republic by reason of unconscionable terms it may, by resolution, direct the Government to initiate re-negotiation of the agreement or arrangement with a view to rectifying the terms.

PART III

GOVERNMENT RE-NEGOTIATION OF UNCONSCIONABLE TERMS

Re-negotiation  
of arrangement  
or agreement

**6.-(1)** The Government shall, within thirty days of the resolution of the National Assembly made in terms of section 5, serve the other party to the arrangement or agreement a notice of intention to re-negotiate the terms which the National Assembly found to be unconscionable.

(2) Terms of the arrangement or agreement shall be deemed to be unconscionable and treated as such if they contain any provision or requirement that:

- (a) aim at restricting the right of the State to exercise full permanent sovereignty over its wealth, natural resources and economic activity;
- (b) are restricting the right of the State to exercise authority over foreign investment within the country and in accordance with the laws of Tanzania;
- (c) are inequitable and onerous to the

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

- state;
- (d) restricts periodic review of arrangement or agreement which purports to last for life time the mining;
  - (e) securing preferential treatment designed to create a separate legal regime to be applied discriminatorily for the benefit of a particular investor;
  - (f) are restricting the right of the State to regulate activities of transnational corporations within the country and to take measures to ensure that such activities comply with the laws of the land;
  - (g) are depriving the people of Tanzania of the economic benefits derived from subjecting natural wealth and resources to beneficiation in the country;
  - (h) are by nature empowering transnational corporations to intervene in the internal affairs of Tanzania;
  - (i) are subjecting the State to the jurisdiction of foreign laws and forum;
  
  - (j) expressly or implicitly are undermining the effectiveness of State measures to protect the environment or the use of environment friendly technology; or
  - (k) aim at doing any other act the effect of which undermines or is injurious to

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

welfare of the People or economic prosperity of the Nation.

(3) In a notice served pursuant to subsection (1), the Government shall state the nature of the unconscionable terms and the intention to expunge the terms from the arrangement or agreement if the re-negotiation is not concluded within a specified period.

(4) Unless the period for the renegotiation is extended by parties on mutual agreement, the period for renegotiation of unconscionable terms shall not exceed ninety days from date of service of notice to the other party.

(5) After completion of re-negotiation, the Government shall prepare a report on the outcome of re-negotiation and lay down the report before the National Assembly.

Rectification  
and expunge of  
unconscionable  
terms

**7.-(1)** Where the Government has served notice of intention to re-negotiate the arrangement or agreement in terms of section 6 and the other party fails to agree to re-negotiate the unconscionable terms or no agreement is reached with regards to unconscionable such terms shall cease to have effect to the extent of unconscionable terms and shall, by operation of this Act, be treated as having been expunged.

(2) For the purpose of subsection (1), the provisions of this Act shall have overriding effect over any other law governing

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

administration and management of natural wealth and resources.

Powers to make regulations

**8.** The Minister may make regulations for the better carrying out of the provisions of this Act.

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

—————  
OBJECTS AND REASONS  
—————

The Bill proposes the enactment of the Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017 in order to provide for a mechanism by the People of Tanzania, through the National Assembly, can review arrangements or agreements made by the Government. The mechanism for review is included to ensure that the terms and conditions of such arrangements or agreements are in line with the interest of the People and the united republic. Once enacted, the proposed law will implement the provisions of Articles 8, 9 and 27 of the Constitution of the United Republic which charge every Tanzanian with the responsibility of protecting natural resources of the United Republic, the property of the state authority and all property collectively owned by the People and the United Republic.

This Bill is divided into Three Parts. Part I provides for preliminary provisions such as the name, commencement date and construction of terms used.

Part II provides for powers of the National Assembly, in the discharge of its oversight role under the Constitution, to review arrangements and agreements made by the Government and, where necessary, direct the Government to re-negotiate any unconscionable terms identified.

Part III provides for the procedure for the initiation of re-negotiation of unconscionable terms and provides a yard stick for unconstitutionality.

*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi. Sheria inayopekezwa inakusudia kuweka utaratibu ambapo wananchi kupitia chombo chao cha uwakilishi yaani Bunge la Jamhuri ya Tanzania kupitia na kujadili makubaliano na mikataba yote inayohusu rasilimali za Nchi ambayo imefungana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kujiridhisha endapo masharti, makubaliano na mikataba hiyo haikinzani na maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Muswada huu unakusudia kutekeleza masharti ya Ibara za 8, 9 na 27 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambazo, pamoja na mambo mengine, zinampa wajibu kila Mtanzania kuhakikisha kwamba anashiriki kikamilifu kulinda mali na rasimali za nchi kwa masilahi ya Watanzania na Jamhuri ya Muungano kwa ujumla.

Kwa kuzingatia wajibu wa kila Mtanzania na kwa kutambua wajibu wa Bunge kama chombo cha uwakilishi, Sheria inayopendekezwa imelipa nguvu Bunge kupitia mikataba yote inayohusina na maliasili za nchi ambayo imeingiwa na Jamhuri ya Muungano ilikujiridhisha kwa masharti yaliyomo katika mikataba hayo yamezingatia maslahi ya watanzania na Taifa kwa ujumla.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu Tatu. Sehemu ya I inahusu masharti ya jumla kama vile jina la sheria na kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya II inalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano nguvu za kisheria ili kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali liweze kupitia makubaliano na mikataba yote



*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*

---

inayohusu maliasili za nchi ambayo imeingiwa na Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kujiridhisha namasharti yaliyomo katika mikataba hiyo. Kwa mujibu wa masharti yanayopendekezwa katika Sehemu hii, baada ya kubaini masharti hasi katika Mikataba hiyo Bunge linaweza kuitaka Serikali kufanya majadiliano upya naupande wa pili wa mkataba ili kuondoa masharti hayo.

Sehemu ya III inaweka utaratibu wa namna ya kuanzisha majadiliano na upande wa pili wa mikataba ili kuondoa masharti hasi kama yalivyobainishwa na Bunge kwa mujibu wa ibara ya 6(2) ya Muswada. Aidha, Sheria inayopendekezwa imeainisha masharti ambayo kwataathira yake ni masharti hasi na hayapaswi kuwemo katika Mikataba inayohusu maliasili za nchi.

Dar es Salaam,  
23 Juni, 2017

PALAMAGAMBA J.A.M. KABUDI  
*Waziri wa Katiba na Sheria*

**NAIBU SPIKA:** Sasa tutamsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya pamoja Mheshimiwa Doto Biteko. *(Makofi)*

**MHE. DOTO M. BITEKO - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA PAMOJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Spika anayo Mamlaka ya kuunda Kamati ya Pamoja itakayojumuisha Kamati za Bunge mbili au zaidi, kwa madhumuni ya kushughulikia jambo ambalo kwa busara zake ataona linahitaji kufanyiwa kazi na Kamati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuzingatia Mamlaka hayo ya Kikanuni, Mheshimiwa Spika aliunda Kamati ya Pamoja inayojumuisha Kamati za Bunge nne zifuatazo:-

- (a) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;
- (b) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria;
- (c) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; na
- (d) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati hiyo ilipewa jukumu la kuchambua, kutoa maoni na mapendekezo kuhusu Miswada miwili ya Sheria iliyowasilishwa Bungeni na Serikali, tarehe 29 Juni, 2017. Miswada hiyo ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa mwaka 2017 na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi ya Mikataba ya Maliasili ya Nchi wa Mwaka, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Pamoja, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umilikaji wa Maliasili wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea Muswada huu tarehe 29 Juni, 2017 na ilikutana mara ya kwanza na Serikali, katika Ukumbi wa Pius Msekwa hapa Dodoma tarehe 30 Juni, 2017 ili kupokea maelezo ya jumla kuhusu Muswada husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusiana na Muswada huu yalitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelezo ya Jumla ya Muswada. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Muswada huu unakusudia kufanya yafuatayo:-

(1) Kutungwa kwa Sheria ambayo itaweka masharti yanayozingatia misingi iliyomo katika Mikataba, Itifaki mbalimbali za Kimataifa kuhusu Mamlaka ya Nchi katika Umilikaji wa Maliasili, ambayo Tanzania imeziridhia;

(2) Kutambua na kuzingatia haki za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Taifa huru lenye mamlaka kamili ya kusimamia na kutumia rasilimali zake kwa maslahi ya Taifa;

(3) Kutekeleza matakwa na masharti ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuweka wajibu kwa kila Mtanzania kulinda kikamilifu rasilimali za nchi;

(4) Kupendekeza hatua zinazolenga kulinda mali na rasilimali za Taifa na kuondoa aina yoyote ya upotevu au ubadhirifu wa rasilimali za nchi kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana na maudhui kuhusu umilikaji wa kudumu (*Permanent Sovereignty*) wa maliasili na rasilimali za nchi; naomba kuwasilisha mapitio ya dhana ya mamlaka ya nchi kuhusiana na umiliki wa maliasili na rasilimali zake kwa lengo la kutoa uelewa wa jumla kwa

Waheshimiwa Wabunge ili waweze kuona mantiki ya Muswada huu unaopendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili na Rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la dhana hii ni katika kipindi cha baada ya Vita ya Pili ya Dunia, hususan miaka ya 1950, ambapo nchi nyingi duniani zilianza kupata uhuru kutoka kwa Wakoloni waliozitawala; na hivyo zilihiti kuwa na umiliki wa maliasili zake. Hatua hii ilitokana na ukweli kwamba Wakoloni mbali na kuonesha utawala wa mabavu, walilenga pia kupora maliasili na rasilimali za nchi walizokuwa wakizitawala ili kujinufaisha kiuchumi katika Mataifa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukomesha unyonyaji huu na kuhakikisha kuwa maliasili na rasilimali za nchi husika zinalindwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi hizo na vizazi vijavyo, Umoja wa Mataifa uliazimia kupitisha maazimio kadhaa kwa lengo la kulinda rasilimali za kila nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa Maazimio hayo ni Azimio Namba 1803 (*Resolution 1803* namba XVII) lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (*United Nations General Assembly*) la tarehe 14 Desemba, 1962.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hilo liliweka masharti kuhusu umilikaji wa kudumu wa maliasili za nchi ili kulinda maliasili ya maendeleo ya nchi hizo husika na watu wake. Pia limeweka misingi kuhusu namna bora ya kuratibu na kusimamia uwekezaji wa kigeni (*foreign investment*) katika rasilimali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa pili ni msingi wa Kikatiba. Maudhui ya Muswada huu yanalenga kuzingatia matakwa ya kisheria ambayo yaliwekwa na Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inatoa wajibu kwa kila Mtanzania kulinda na kusimamia kikamilifu rasilimali za Umma kwa manufaa ya Taifa. Ibara ya 27 (1) inatamka maneno haya na naomba kunukuu:-

*“Kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Jamhuri ya Muungano, mali ya mamlaka za nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine”*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya kuzingatia masharti haya yaliyowekwa kwa mujibu wa Katiba ya Sheria, kila Mtanzania anapaswa kutambua kwamba ni sehemu ya maamuzi haya ya kulinda mali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za Kamati; Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kukutana na wadau mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni. Ili waweze kupata maoni ya wadau, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba orodha ya wadau hawa iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo. Wako pia wadau mbalimbali waliochangia kwa maandishi ambao nao pia naomba waingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuwasilisha uchambuzi wa Muswada uliofanywa na Kamati. Sehemu ya kwanza ya Muswada inahusiana na Ibara ya kwanza (1) hadi ya tatu (3), inaainisha masharti na utangulizi wa sheria; inapendekeza utaratibu wa kutangaza tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na maudhui hayo yaliyo katika sehemu hii, isipokuwa Ibara ya (2) ambayo ilifanyiwa marekebisho na kupendekeza kwamba yaongezwe maneno *“as well as Tanzania Zanzibar”* mwishoni mwa ibara hiyo ili matumizi ya sheria hii yahusishe pia Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inajumuisha Ibara ya nne(4) hadi ibara ya 10, inayopendekeza kuweka masharti ya juu ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na umiliki wa maliasili kwa mujibu wa Ibara ya nne (4) ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya sita (6) ya Muswada inapendekeza kuweka masharti ya kuzuia uvunaji wa rasilimali ambao utatekelezwa kwa manufaa ya Watanzania na kuridhiwa na Bunge. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwani kwa mara ya kwanza wananchi watapata mamlaka ya kudhibiti rasilimali zao kupitia Bunge ambacho ni chombo chao cha uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara hii, ni kosa kisheria kwa Serikali kuingia katika makubaliano ama mipango ya kuhusiana na kutafiti, kuchimba ama kumiliki ama kutumia maliasili na rasilimali za nchi bila kupata ridhaa ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya saba (7) ya Muswada inapendekeza kuweka masharti ya kuhakikisha kwamba mapato yanayopatikana kutokana na uvunaji wa rasilimali yanatumika katika kukuza uchumi wa nchi. Kamati inakubaliana na maudhui ya ibara hii kwa kuwa yanalenga kuongeza thamani ya rasilimali za Taifa na uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nane (8) ya Muswada inapendekeza kuweka masharti ambayo yataiwezesha Serikali kuwa mbia katika utekelezaji wa aina yoyote unaoruhusiwa katika utafutaji, uchimbaji na utumiaji wa maliasili za nchi. Aidha, kwa mujibu wa ibara hii, wananchi wanapewa fursa ya kuwa sehemu ya ubia huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tisa (9) ya Muswada inapendekeza masharti kwa lengo la kuzuia usafirishaji wa malighafi za maliasili kwenda nje ya nchi. Aidha, Ibara hii inapendekeza juu makubaliano au mipango ya uwekezaji katika maliasili na rasilimali, kuambatana na hakikisho la kuanzishwa kwa mitambo ya kuchakata rasilimali ghafi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada ni Ibara ya 11. Katika sehemu hii inaainisha juu ya mamlaka ya nchi katika umiliki wa maliasili na rasilimali, kwa kuzuia mashauri yote yanayohusiana na mamlaka hayo yasipelekwe

katika Mahakama au vyombo vya usuluhishi nje ya nchi. Kwa mantiki hiyo, mashauri yote yatakatwa na utafutaji, uchimbaji au umiliki wa rasilimali za nchi, yataamuliwa na Mahakama na vyombo vya uamuzi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua hii, kwani inazingatia utekelezaji wa Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayosisitiza kwamba, "chombo chenye kauli ya mwisho kuhusu utoaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mahakama zilizopo hapa nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, bada ya uchambuzi huo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(1) Kwa kuwa utekelezaji bora wa Sheria utategemea Kanuni zitakazotungwa na Waziri mwenye dhamana, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha utungaji wa Kanuni husika unafanywa ili kuwe na utekelezaji bora na wa haraka wa kisheria inayotamkwa na Muswada huo.

(2) Serikali ianze haraka mchakato wa ujenzi wa mitambo ya kuchakata, kuchenjua malighafi za rasilimali za nchi ili kuwezesha wavunaji wa rasilimali kupata huduma hiyo hapa nchini.

(3) Kamati inashauri Serikali iimarishe mfumo wa utendaji wa Taasisi za Kibenki, Taasisi za Kifedha ili kuongeza ufanisi wa kutoa huduma kwa Taasisi mbalimbali na Makampuni makubwa ya uwekezaji hapa nchini.

(4) Serikali iboreshe zaidi mifumo na uwezo wa Mahakama na vyombo vingine vya utoaji haki ili viweze kushughulikia mashauri yanayojitokeza na yatakatwa kujitokeza kutokana na masharti ya uwekezaji yanayotamkwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kuona umuhimu wa Muswada huu na kuunda Kamati hii ili tuweze kufanya kazi hii. Hiyo ni ishara kwamba wewe

pamoja na Bunge lako Tukufu, tunaona umuhimu nchi yetu kunufaika ipasavyo kutokana na uwekezaji tunaoufanya katika rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mapendekezo ya Kamati kwenye Muswada wa kwanza, sasa naomba ruhusa yako niweze kutoa mapendekezo ya Kamati kwenye Muswada wa pili ambao ni maoni na ushauri wa Kamati juu ya Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi ya Mikataba ya Maliasili ya Nchi wa Mwaka, 2017 (*The Natural Wealth and Resource Contracts Review and Renegotiations of Unconscionable Terms Bill 2017*).

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya jumla; kwa mujibu wa Muswada huu, Serikali ilitoa maelezo kwa Kamati kuwa:-

(1) Muswada huu unakusudia kuweka utaratibu ambapo wananchi kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watakuwa na mamlaka ya kujadili, makubaliano na mikataba yote inayohusu rasilimali za nchi ambayo inafungana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kujiridhisha endepo masharti na makubaliano ya mikataba hiyo haikiniani na maslahi ya wananchi wa Tanzania kwa ujumla.

(2) Muswada huu unalenga kutekeleza matakwa ya Kikatiba chini ya Ibara ya 8, 9 na 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zinatoa wajibu kwa kila Matanzania kushiriki kikamilifu katika kulinda rasilimali za nchi.

(3) Kwa muktadha huo, Sheria inayopendekezwa inalipa Mamlaka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mikataba yote inayohusiana na maliasili za nchi ambayo imeingiwa na Jamhuri ya Muungano ili kujiridhisha kama masharti yaliyomo katika Mkataba huo yanazingatia maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla.



Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa tumewasikiliza Wadau waliokuja mbele ya Kamati na ambao nimeshawasema, Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada huu na haya ndiyo maoni ya Kamati:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(1) Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huu Kamati inashauri Serikali iharakishe kutunga Kanuni ambapo Waziri mwenye dhamana kwa mujibu wa Ibara ya nane (8) ya Muswada huu inavyoelekeza, utungaji wa Kanuni hizi uzingatie na utawekwa utaratibu wa sheria hii na hivyo kufanikisha azma ya kutungwa kwake ambayo inalenga kulinda rasilimali za nchi kwa maslahi ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Serikali iboreshe utendaji wa vyombo mbalimbali vinavyosimamia sekta mbalimbali za maliasili za nchi ili kuendana na dhamira nzuri ya utungaji wa sheria hii kwa lengo la kuhakikisha rasilimali za nchi na maslahi ya wananchi wa Tanzania. Kamati inaona iwapo vyombo hivi havitasimamiwa na kuboreshwa vizuri, kutapelekea sheria hizi vilevile kutokusimamiwa vizuri. Hivyo, ni muhimu usimamizi wake uwe madhubuti.

(3) Mara baada ya kupitishwa kwa Muswada huu na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa sheria na mchakato wa mapitio ya Mikataba na Makubaliano uanze mara moja ili kuondoa masharti hasi katika Mikataba ya rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana wewe binafsi, kutokana na kuona umuhimu wa Muswada huu na kuamua kuunda Kamati hii kufanya kazi, ambayo ni ishara kwamba Bunge lako Tukufu linaona umuhimu wa Miswada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa moyo wa dhati kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa

Profesa Paramagamba Kabudi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George Masaju kwa ushirikiano wao katika uchambuzi wa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati, pamoja na Wajumbe waalikwa, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kuandaa Taarifa hii. Napenda kuwatambua kwa majina yao yote, lakini kwa sababu ya muda, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah, ambao wamewezesha kazi hii kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati, Ndugu Dickson Bisile na Mkurugenzi Msaidizi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndugu Prudence Rweyongeza, kwa ushirikiano wao kwa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kuwatambua Makatibu wa Kamati ambao ni Ndugu Mwanahamis Munkunda, Ndugu Chacha Timasi Nyakega, Ndugu Stanslaus Kagisa, Ndugu Mkuta Masoli, Ndugu Mariam Mbarouk, Ndugu Elieka Saanya, Ndugu Thomas Shawa na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Gwivaha kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA  
SHERIA YA MAMLAKA YA NCHI KUHUSIANA NA UMILIKI  
WA MALIASILI WA MWAKA 2017 [THE NATURAL WEALTH  
AND RESOURCES (PERMANENT SOVEREIGNTY)] BILL, 2017  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 7 (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Spika anayo mamlaka ya kuunda Kamati ya Pamoja itakayojumuisha Kamati za Bunge mbili au zaidi, kwa madhumuni ya kushughulikia jambo ambalo kwa busara zake ataona linahitaji kufanyiwa kazi na Kamati hizo husika.

Kwa kuzingatia mamlaka hayo ya Kikanuni, Spika, aliunda Kamati ya pamoja iliyojumuisha Kamati za Bunge Nne zifuatazo:

- a) Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;
- b) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria;
- c) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; na
- d) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Aidha, Kamati hiyo ilipewa jukumu la kuchambua, kutoa maoni na mapendekezo kuhusu Miswada miwili ya Sheria iliyowasilishwa Bungeni na Serikali, tarehe 29 Juni, 2017. Miswada hiyo ni:

- a) **Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017** [*The Natural Wealth And Resources (Permanent Sovereignty)*] Bill, 2017; na

**b) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017** [*Natural Wealth and Resource Contracts (Review and Re-negotiations of Unconscionable Terms) Bill 2017*].

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba sasa kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Pamoja, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth And Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*].

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea Muswada huu tarehe 29 Juni, 2017 na ilikutana kwa mara ya kwanza na Serikali, katika Ukumbi wa Pius Msekwa (Ofisi za Bunge), Dodoma mnamo tarehe 30 Juni, 2017 ili kupokea maelezo ya jumla kuhusu Muswada husika. Maelezo kuhusiana na Muswada huo yalitolewa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba J. A. M. Kabudi (Mb).

### **1.1 Maelezo ya Jumla ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Muswada huu unakusudia kufanya yafuatayo:-

(a) Kutungwa kwa Sheria ambayo itaweka masharti yanayozingatia misingi iliyomo katika Mikataba na Itifaki mbalimbali za Kimataifa kuhusu Mamlaka ya Nchi katika Umiliki wa Maliasili, ambayo Tanzania imeziridhia;

(b) Kutambua na kuzingatia haki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Taifa huru lenye mamlaka ya kusimamia na kutumia raslimali zake kwa maslahi ya Taifa;

(c) Kutekeleza matakwa na masharti ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa kuweka wajibu kwa kila Mtanzania wa kulinda kikamilifu raslimali za nchi, na kutangaza bayana kwamba, Watanzania ndio

watakuwa na mamlaka ya kudumu katika umiliki wa maliasili za nchi na Serikali itakuwa ni msimamizi wa maliasili hizo kwa niaba ya Wananchi; na

(d) Kupendekeza hatua zinazolenga kulinda mali na rasilimali za Taifa na kuondoa aina yoyote ya upotevu au ubadhirifu wa rasilimali za nchi kwa manufaa ya Watanzania.

## 1.2 **Dhana na Maudhui kuhusu Umiliki wa Kudumu (Permanent Sovereignty) wa Maliasili na Rasilimali za Nchi**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha mapitio ya dhana ya mamlaka ya nchi kuhusiana na umiliki wa maliasili na rasilimali zake (**The Natural Wealth and Resources (permanent sovereignty)**) kwa lengo la kutoa uelewa wa jumla kwa Waheshimiwa Wabunge, ili waweze kuona mantiki ya Muswada huu unaopendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili na Rasilimali.

Chimbuko la dhana hii ni katika kipindi cha baada ya vita ya pili ya dunia, hususan mwanzoni mwa miaka ya 1950, ambapo nchi nyingi duniani zilianza kupata uhuru kutoka kwa wakoloni waliozitawala, na hivyo zilihitaji kuwa na umiliki wa maliasili zake. Hatua hii ilitokana na ukweli kwamba, Wakoloni mbali na kuonesha utawala wa mabavu, walilenga pia kupora maliasili na rasilimali za nchi walizokuwa wakizitawala, ili kuyanufaisha kiuchumi Mataifa yao.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukomesha unyonyaji huo na kuhakikisha kuwa, maliasili na rasilimali za nchi husika zinalindwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi hizo na ya vizazi vijavyo, Umoja wa Mataifa, uliazimia kupitisha maazimio kadhaa kwa lengo la kulinda rasilimali za kila nchi. Miongoni mwa Maazimio hayo ni Azimio Namba 1803 (XVII) (UNGA Resolution 1803 (XVII)) lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (United Nations General Assembly) tarehe 14 Disemba, 1962.

Azimio hilo limeweka masharti kuhusu umiliki wa kudumu wa maliasili na rasilimali za nchi, ili kulinda maslahi ya maendeleo ya nchi hizo na ustawi wa watu wake. Pia limeweka msingi kuhusu namna bora ya kuratibu na kusimamia wawekezaji wa kigeni (*foreign investors*) katika rasilimali hizo, ambapo pamoja na mambo mengine muhimu, Azimio hilo liliainisha kwamba, haki za wananchi wa kila taifa kuhusu umiliki wa kudumu wa rasilimali za nchi yao ni lazima zipatikane kwa kuzingatia maslahi ya maendeleo ya nchi na ustawi wa kila Mwananchi. Kwa ujumla, dhana inayosisitizwa kupitia Azimio hilo imejikita katika kuhakikisha kuwa, haki na wajibu wa kila taifa vinazingatiwa kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa, pamoja usawa unaotambua mamlaka ya kila nchi (sovereign equality).

### 1.3 Msingi wa Kikatiba

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, maudhui ya Muswada huu yanalenga kuzingatia matakwa ya kisheria ambayo yanawekwa na Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inatoa wajibu kwa kila Mtanzania kulinda na kusimamia kikamilifu rasilimali za umma kwa manufaa ya Taifa.

Ibaya ya 27 kupitia Ibara Ndogo ya (1) inatamka maneno yafuatayo, na hapa ninanukuu:-

***“ Kila mtu ana wajibu wa kulinda  
maliasilia ya Jamhuri ya  
Muungano, mali ya mamlaka ya  
nchi na mali yote inayomilikiwa  
kwa pamoja na Wananchi, na pia  
kuiheshimu mali ya mtu  
mwingine.”***

Kama sehemu ya kuzingatia masharti yanayowekwa na Katiba yetu ambayo ndiyo Sheria Mama, kila Mtanzania anapaswa kutambua kwamba, ni sehemu ya maamuzi ya hali ya baadae ya Taifa letu, hivyo basi anao wajibu wa kuhakikisha anatanza vizuri mali ya nchi, kupiga vita aina

zote za ubadhilifu na kuwa makini katika usimamizi wa uchumi wa Taifa letu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

#### 1.4 Uzoefu kutoka Nchi nyingine:-

**Mheshimiwa Spika**, uzoefu unaonesha kuwa baadhi ya nchi zimezingatia kikamilifu masharti yanayotokana na Maazimio ya Umoja wa Mataifa kuhusu kulinda raslimali za kila nchi. Nchi hizo zimeweka utaratibu mzuri wa kisheria ambao unaziwezesha kunufaika kikamilifu na uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje katika raslimali zake.

Miongoni mwa faida ambazo nchi hizo zimepata ni pamoja na mgawanyo mzuri wa mapato yatokanayo na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (foreign direct investment) katika raslimali zake, ajira kwa wananchi wake, na nguvu ya udhibiti wa kisheria kuhusiana na maamuzi ya usimamizi na udhibiti wa raslimali zake.

Mfano wa nchi hizo ni Thailand ambayo kwa mujibu wa Sheria inayosimamia biashara za kigeni (*Allien Business Law*), umiliki wowote wa biashara na maliasili utakaofanywa na raia wa kigeni, mbali na kupata kibali cha Baraza la Mwaziri ni lazima uridhiwe na Bunge. Aidha Sheria ya umiliki wa majengo ya nchi hiyo (*Land Code and Condominium Act*) inaelekeza kwamba, kibali cha umiliki wa majengo kitakachotolewa na Serikali kwa Wageni kitahitaji kuidhinishwa na Bunge.

Pia, nchi hiyo inalinda ajira kwa raia wake kwa kuzuia wageni kujishughulisha na baadhi ya shughuli ambazo zinaweza kutekelezwa na wazawa. Miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na viwanda vidogo vidogo, biashara ya rejareja, ujenzi wa hoteli, uwakala wa kitalii pamoja na biasahara ya kuuza maji.

Katiba Bara la Afrika pia, zipo nchi ambazo zimeweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo kutokana na mapato yanayotokana na uwekezaji katika maliasili na raslimali za

nchi hizo. Miongoni mwa nchi hizo ni Botswana ambayo kutokana na usimamizi mzuri wa uchimbaji wa madini ya Almas, mwaka 2004 ilivuka kutoka kundi la nchi maskini na kuwa nchi ya kipato cha kati (a middle income country), ikiwa na wastani wa pato la mtu la **Dola za Marekani 9,200 (sawa na Tsh. Milioni 20.6)** kwa mwaka. Nchi hiyo inayokadiriwa kuzalisha takribani robo ya Almasi yote inayozalishwa duniani kwa mwaka, inamiliki hisa 50% katika Kampuni ya Debswana (Debswana Diamond Company Ltd) huku 50% nyingine ya hisa ikimilikiwa na kampuni ya De. Beer ya nchini Afrika Kusini.

Vilevile nchi ya Libya kutokana na kutumia mapato yatokanayo ya uwekezaji katika uchimbaji na uuzaji wa mafuta, kukuza uchumi na kuboresha hali ya maisha ya watu wake. Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Fedha Duniani (IMF) pato la mtu kwa mwaka ni Dola za Marekani 14,000 (sawa na Tsh. Milioni 31.4)

## **1.5 Ushirikishwaji wa Wadau:-**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza kikamilifu sharti la Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kuhusu ushirikishaji wa Wadau katika uchambuzi wa Muswada. Wadau wote waliofika mbele ya Kamati au kutuma maoni yao kwa maandishi walifanya hivyo kufuatia Tangazo la Katibu wa Bunge kwa Umma lililotolewa Tarehe 29 Juni, 2017.

Hivyo, uchambuzi wa Muswada huu ulishirikisha wadau wa aina mbalimbali waliotoa maoni kwa njia ya majadiliano ya moja kwa moja na kwa njia ya maandishi.

### **a) Wadau Waliochangia Moja kwa Moja Ukumbini:**

- (i) Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS);
- (ii) Chuo cha Madini Dodoma;



- (iii) Shirika la Madini Nchini (STAMICO);
- (iv) Baadhi ya Vikundi vya Waendesha Bodada wa Dodoma;
- (v) *Tanzania Chamber of Minerals and Energy*;
- (vi) Chama cha Wachimbaji Wadogo Wadogo wa Madini ya Vito Dodoma;
- (vii) Jumua ya Kikristo nchini;
- (viii) Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira nchini (LEAT);
- (ix) Jukwaa la Asasi za Kiraia zinazojishughulisha na masuala ya Uziduaji nchini (Haki Raslimali);
- (x) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;
- (xi) Jitambue Vijana Dodoma;
- (xii) Ndg. Erasmo Nyika wa Chuo Kikuu cha Abedien uingereza
- (xiii) *Environmental Conservation Society of Tanzania*;
- (xiv) Wawakilishi wa Waganga wa Tiba Asilia nchini;
- (xv) Universal Development Initiative (UDI)
- (xvi) Chama cha Wamachinga wa Dodoma (DOWA);
- (xvii) Tuyatunze Mazingira Dodoma;
- (xviii) Misani ya Hiyari;

- (xix) DAKADAKA Dodoma;
- (xx) LEMKACHEMA 2005 Group;
- (xxi) Ndg. Erasmo Nyika- Mwanafunzi wa Digrii ya Uzamivu;
- (xxii) Ndg. Antidius Kaitu - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (xxiii) Tumaini Hayuma - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (xxiv) Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Wadogo Tanzania (FEMATA).
- (xxv) Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na;
- (xxvi) Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST).

**b) Waliochangia kwa Maandishi:**

- (i) Chama cha ACT Wazalendo (ACT);
- (ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- (iii) Kampuni ya Uchimbaji Mafuta ya Norway (STATOIL)
- (iv) Natural Resources Governance Institute;
- (v) Ndg. Frank Simon Mkoko- Mchimbaji Mdogo;
- (vi) SIBUKA FM;
- (vii) Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya;
- (viii) Ndg. Aziz Mwita (Raia);
- (ix) Ndg. Twahir Abas Kiobya (Raia); na

(x) Ndg. Fadhir C Bwagalilo (Mwanafunzi St. John)  
Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wadau wote walioshiriki kukamilisha zoezi hili kwani maoni yao yamekuwa msaada mkubwa sana kwa Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA:-

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu tatu kama ifuatavyo:-

### 2.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada:

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ambayo inahusisha Ibara ya 1 hadi 3, inaainisha masharti ya utangulizi, jina la Sheria inayopendekezwa na utaratibu wa kutangaza tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria.

Kamati inakubaliana na maudhui yaliyo katika sehemu hii isipokuwa katika Ibara ya 2 mbayo ilifanyiwa mabadiliko kwa kupendekezwa kwamba, yaongezwe maneno *“as well as Tanzania Zanzibar”* mwishoni mwa ibara hiyo ili matumizi ya sheria hii yahusishe Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Sababu ya mabadiliko hayo ni kwamba, Tanzania Bara haiwezi kuwa dola kamili bila kuihusisha Tanzania Zanzibar.

### 2.2 Sehemu ya Pili ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inajumuisha Ibara ya 4 hadi 10, inayopendekeza kuweka masharti juu ya mamlaka ya nchi, kuhusiana na umiliki wa maliasili. Kwa mujibu wa ibara ya 4 ya Muswada, Watanzania ndio watakuwa na mamlaka ya kudumu katika umiliki wa maliasili na raslimali za nchi, na Serikali itakuwa ni msimamizi wa maliasili hizo kwa niaba ya wananchi.

Kamati inakubaliana na maudhui yaliyo katika ibara hii ya Muswada kwani yanalenga kutilia mkazo utekelezaji wa Maazimio mbalimbali ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Mamlaka ya Wananchi juu ya umiliki wa milele wa maliasili zilizomo katika nchi yao kwa maendeleo ya Taifa lao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 5 ya Muswada, rasilimali za Taifa haziwezi kuondolewa kwa namna yoyote na zitaendelea kuwa mali za Watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya usimamizi wa Rais kwa niaba ya Wananchi.

Kamati inakubaliana na maudhui ya ibara hii, kwamba Rais awe ndiye msimamizi wa rasilimali za nchi yetu kwa niaba ya Wananchi. Hii haina tofauti na utaratibu uliowekwa kupitia Sheria ya Ardhi, ambapo ardhi yote ya Tanzania ipo chini ya usimamizi wa Rais, kwa niaba ya Wananchi.

**Mheshimiwa Spika, Ibara 6** ya Muswada inapendekeza kuweka masharti ya kuzuia uvunaji wa rasilimali za nchi, ambao hautatekelezwa kwa manufaa ya Watanzania na kuridhiwa na Bunge.

Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwani kwa mara ya kwanza, Wananchi wamepata mamlaka ya kudhibiti rasilimali zao kupitia Bunge ambacho ni chombo chao cha uwakilishi. Kwa mujibu wa ibara hii, itakuwa ni kosa kisheria kwa Serikali kuingia katika makubaliano au mipango kuhusiana na kutafiti, kuchimba au kumiliki na kutumia maliasili na rasilimali za nchi, bila kupata ridhaa ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 7 ya Muswada inapendekeza kuweka masharti ili kuhakikisha kwamba, mapato yatakayotokana na uvunaji wa rasilimali za Taifa yanatumika katika kukuza uchumi wa Taifa. Kamati inakubaliana na maudhui ya ibara hii kwa kuwa yanalenga kuongeza thamani ya rasilimali za Taifa na kukuza Uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8** ya Muswada inapendekeza kuweka masharti ambayo yataiwezesha Serikali kuwa mbia katika uwekezaji wa aina yoyote utakaoruhusiwa katika utafutaji, uchimbaji na utumiaji wa raslimali za nchi. Aidha, kwa mujibu wa ibara hii, wananchi wanapewa fursa ya kuwa sehemu ya ubia huo.

Kamati inapongeza hatua hii kwani, inatoa fursa kwa Wananchi na Serikali kushiriki katika uendelezaji wa raslimali za nchi kwa lengo la kujenga uchumi wa taifa lao.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9** ya Muswada inapend3ekuweka masharti kwa lengo la kuzuia usafirishaji wa malighafi ya maliasili kwenda nje ya nchi. Aidha, ibara hii inapendekeza juu makubaliano au mipango ya uwekezaji katika maliasili na raslimali kuambatana na hakikisho la kuanzishwa kwa mitambo ya kuchakata raslimali ghafi nchini.

Kamati inakubaliana na maudhui ya ibara hii kwani yanalenga kuongeza thamani ya maliasili na raslimali zinazovunwa, kukuza na kuendeleza viwanda, na kutoa fursa za ajira kwa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10** ya Muswada inapendekeza masharti ya kuhakikisha kwamba, mapato yote yatokanayo na utafutaji, uchimbaji, au umiliki na utumiaji wa rasilimali za Taifa, yanahifadhiwa katika benki na Taasisi za kifedha za ndani ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Aidha, kwa mujibu wa Ibara hii, fedha itakayoruhusiwa kusafirishwa kwenda nje ni ambazo zitatokana na gawio la faida baina ya wabia.

Kamati inapongeza hatua hii kwani itasaidia kudhibiti uhamishaji wa fedha kwenda nje ya nchi, na hivyo kuzifanya benki na taasisi za fedha nchini kukuza mitaji na hivyo kuongeza wigo wa kutoa mikopo kwa wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uzalishaji. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaimarisha mifumo ya kibenki

na taasisi za fedha nchini ili ziweze kumudu kutoa huduma zitakazohitajika kutoka kwa wawekezaji wa nje.

### 2.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya 11 katika sehemu hii inaainisha juu ya mamlaka ya nchi katika umiliki wa maliasili na raslimali, kwa kuzuia mashauri yote yanayohusiana na mamlaka hayo yasipelekwe katika mahakama au vyombo vya usuluhishi vya nje ya nchi. Kwa mantiki hiyo, mashauri yote yatakayotokana na utafutaji, uchimbaji au umiliki na matumizi ya maliasili na raslimali za nchi, yataamriwa na mahakama na vyombo vya uamuzi vya hapa nchini.

Kamati inapongeza hatua hii kwani inazingatia utekelezaji wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayosisitiza kwamba, chombo chenye kauli ya mwisho kuhusu utoaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mahakama zilizopo hapa nchini. Kwa mantiki hiyo, Kamati imejiridhisha kuwa, hatua ya kupeleka nje ya nchi mashauri ambayo chimbuko lake ni maliasili na raslimali za Tanzania zilizopo nchini, ni udhallishaji wa nchi yenye Dola kamili.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza juu ya kuweka masharti ambayo yatalipa Bunge mamlaka ya kuweza kupitia mipango au makubaliano yoyote ya Serikali kuhusiana na utafutaji, uchimbaji, umiliki na matumizi ya raslimali za nchi. Kamati inapongeza hatua hii kwani, itatoa fursa kwa Bunge kuingilia kati kwa lengo la kujiridhisha iwapo mipango au makubaliano hayo yanalinda maslahi ya Wananchi na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya mwisho katika Sehemu hii ni ya 13 ambayo inapendekeza masharti ya kumpatia Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kutunga Kanuni zitakazowezesha utekelezaji bora wa sheria inayokusudiwa kutungwa.

Kamati inakubaliana na maudhui ya Ibara hii hata hivyo, inashauri yaongezwe maneno ***“in consultation with the relevant Sectoral Minister”*** katikati ya maneno ***“Minister”*** na

“May” ili kutoa wigo wa ushirikishwaji kwa Mawaziri wenye dhamana katika sekta mbalimbali zinazohusika.

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi wa Muswada huu, naomba kutoa maoni na ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

1) Kwa kuwa utekelezaji bora wa Sheria hii utategemea Kanuni zitakazotungwa na Waziri mwenye dhamana, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha utungaji wa Kanuni husika unafanyika mapema ili kuwezesha utekelezaji bora na wa haraka wa sheria itakayotokana na Muswada huu;

2) Serikali ianze haraka mchakato wa ujenzi wa mitambo ya kuchakata / kuchenjua mali ghafi za raslimali nchini, ili kuwezesha wavunaji wa raslimali hizo kupata huduma hiyo hapa nchini;

3) Serikali iimarisha mfumo wa utendaji wa benki na taasisi za kifedha ili kuongeza ufanisi katika kuhudumia taasisi mbalimbali na makampuni makubwa ya uwekezaji nchini;

4) Serikali iboreshe zaidi mifumo na uwezo wa Mahakama na vyombo vingine vya utoaji haki nchini ili viweze kushughulikia mashauri yanayojitokeza na yatakayoweza kujitokeza kutokana na masharti ya uwekezaji yanayotamkwa katika Muswada huu;

### 4. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe binafsi, kutokana na kuona umuhimu wa Muswada huu na kuamua kuunda Kamati hii ili iweze kuufanyia kazi. Hiyo ni ishara kwamba, wewe pamoja na Bunge lako Tukufu, tunapenda kuona nchi yetu inanufaika ipasavyo kutokana na uwekezaji unaofanyika katika raslimali na maliasili zetu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Paramagamba J.A.M. Kabudi (Mb), na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. George Masaju Mb, kwa ushirikiano wao katika uchambuzi wa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Pamoja na Wajumbe Waalikwa, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kuweza kuandaa Taarifa hii. Napenda kuwatambua Wajumbe wote wa Kamati hii ya Pamoja kwa kuwataja kwa majina, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kufanya hivyo, na ninaomba majina yao yote yangie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (**Kiambatisho**).

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kasilillah, ambao umewezesha kazi hii kukamilika kwa wakati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati, Ndg. Dickson Bisile na Mkurugenzi Msaidizi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndg. Prudence Rweyongeza, kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Vilevile, napenda kuwatambua Makatibu wa Kamati ambao ni Ndg. Mwanahamis Munkunda, Ndg. Chacha Timasi Nyakega, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Mariam Mbarouk, Ndg. Elieka Saanya, Ndg. Thomas Shawa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Gwivaha kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

.....  
Doto Mashaka Biteko (**Mb**)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA PAMOJA**

3 JULAI, 2017



**KIAMBATISHO**

**ORODHA YA WAJUMBE WA KAMATI YA BUNGE YA PAMOJA**

---

<b>Na.</b>	<b>JINA</b>
1.	Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb.- <b>Mwenyekiti</b>
2.	Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb.
3.	Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb.
4.	Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb.
5.	Mhe. Mauled Said Abdallah Mtulia, Mb.
6.	Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb.
7.	Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb.
8.	Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb.
9.	Mhe. Katani Ahamadi Katani, Mb.
10.	Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb.
11.	Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb.
12.	Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb.
13.	Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb.
14.	Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb.
15.	Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb.
16.	Mhe. Desderius John Mipata, Mb.
17.	Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb.
18.	Mhe. Mohamed Juma Khatibu, Mb.
19.	Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb.
20.	Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb.
21.	Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb.
22.	Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb.
23.	Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb.
24.	Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb.
25.	Mhe. John Wegesa Heche, Mb.
26.	Mhe. Anne K. Malecela, Mb.
27.	Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye, Mb.
28.	Mhe. Kemilembe Julius Lwota, Mb.
29.	Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb.
30.	Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb.
31.	Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb.
32.	Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb.
33.	Mhe. Devotha Mathew Minja, Mb.

34. Mhe. Khalifa Salim Suleimani, Mb.
35. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb.
36. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb.
37. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb.
38. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb.
39. Mhe. Risala Kabongo, Mb.
40. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb.
41. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb.
42. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb.
43. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb.
44. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb.
45. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb.
46. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb.
47. Mhe. Fredy Atupele Mwakibete, Mb.
48. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb.
49. Mhe. Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Mb.
50. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb.
51. Mhe. Neema William Mgaya, Mb.
52. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb.
53. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
54. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb
55. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb.
56. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb.
57. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb.
58. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb.
59. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb.
60. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb.
61. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb.
62. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb.
63. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
64. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb.
65. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb.
66. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb.
67. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb.
68. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb.
69. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb.
70. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb.
71. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
72. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb.
73. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb.

74. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb.
75. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
76. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb.
77. Mhe. Juma Kombo Hamad, Mb.
78. Mhe. Andrew John Chenge, Mb.
79. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb.
80. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb.
81. Mhe. Halima James Mdee, Mb.
82. Mhe. Tundu Antipas Mughway Lissu, Mb.
83. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb.
84. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb.
85. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb.
86. Mhe. Esther Michael Mmasi, Mb.
87. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb.
88. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb.
89. Mhe. Hassani Seleman Kaunje, Mb.
90. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb.
91. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb.
92. Mhe. Hassan Elias Massala Mb.
93. Mhe. Leonidas Tutubert Gama, Mb.
94. Mhe. Almas Athuman Maige, Mb.
95. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb.
96. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb.
97. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA PAMOJA KUHUSU  
MUSWADA WA MAPITIO NA MAJADILIANO KUHUSU  
MASHARTI HASI KATIKA MIKATABA YA MALIASILI ZA NCHI  
WA MWAKA 2017 [*THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES  
CONTRACTS (REVIEW AND RE-NEGOTIATION OF  
UNCONSCIONABLE TERMS)*] BILL, 2017 KAMA  
*ILIVYOWASILISHWA MEZANI***

---

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 7 (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inampa Spika, mamlaka ya kuunda Kamati ya Pamoja itakayojumuisha Kamati mbili au zaidi kwa ajili ya kulifanyia

kazi jambo ambalo kwa busara zake ataona linaweza kufanyiwa kazi na Kamati hizo husika.

Kwa kuzingatia mamlaka hayo ya kikanuni, Mheshimiwa Spika, aliunda Kamati ya pamoja na kuipa majukumu rasmi ya kuchambua, kutoa maoni na mapendekezo kuhusu Muswada wa Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms)*] Bill, 2017 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 29 Juni, 2017. Kamati hiyo ya pamoja ilijumuisha Kamati Nne za Kudumu za Bunge ambazo ni Kamati ya Nishati na Madini, Kamati ya Katiba na Sheria, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Pamoja, kuhusu Muswada wa Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms)*] Bill, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Serikali, katika Ukumbi wa Pius Msekwa (Ofisi za Bunge), Dodoma mnamo tarehe 30 Juni, 2017 ambapo Kamati ilipokea maelezo kuhusu Muswada husika kutoka kwa Waziri wa Katiba na Sheria.

#### 1.1 **Maelezo ya Jumla ya Muswada:-**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea Muswada huu tarehe 30 Juni, 2017 na siku hiyo hiyo Serikali ilifika na kuwasilisha Taarifa kuhusu madhumuni ya muswada huu. Kwa maelezo ya Serikali, muswada huu unakusudia kufanya yafuatayo:-

a) Kuweka utaratibu ambapo Wanachi kupitia Bunge la Jamhuri ya Tanzania watakuwa na Mamlaka ya kupitia na kujadili makubaliano na Mikataba yote inayohusu raslimali za nchi ambayo imefungana na Jamhuri ya Tanzania, kwa lengo la kujiridhisha endapo masharti ya makubaliano na Mikataba hiyo haikinzani na maslahi ya Wanachi na Taifa kwa ujumla.

b) Kutekeleza matakwa ya Kikatiba chini ya Ibara ya 8, 9 na 27 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambazo zinatoa wajibu kwa kila Mtanzania kushiriki kikamilifu kulinda mali na raslimali za nchi kwa maslahi ya Watanzania na Jamhuri ya Muungano kwa ujumla.

c) Kwa muktadha huo, Sheria inayopendekezwa inalipa Mamlaka Bunge kupitia Mikataba yote inayohusiana na maliasili za nchi ambayo imeingiwa na Jamhuri ya Muungano ili kujiridhisha kwa masharti yaliyomo katika Mikataba na kama yamezingatia maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla.

## 1.2 Dhana na Maudhui Muswada

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kuwasilisha mapitio na majadiliano kuhusu masharti hasi katika mikataba inayohusu maliasili za nchi (*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*) ni kuwajulisha Wajumbe dhana ya msingi katika Muswada unaopendekeza kutungiwa Sheria.

Mwanzoni mwa miaka ya 1950, nchi nyingi za Afrika na nchi nyingine Duniani zilianza kupata uhuru kutoka kwa wakoloni. Msingi wa ukoloni ulilenga kuchukua maliasili na rasilimali za nchi zilizotawaliwa ili kuwanufaisha watawala hao kiuchumi na maendeleo ya viwanda.

Kutokana na changamoto ya kuchukuliwa maliasili na rasilimali za nchi zilizotawaliwa na wakoloni, mnamo tarehe 14 Disemba, 1962 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (*United Nations General Assembly*) lilipitisha Azimio Namba

1803 (XVII) (UNGA Resolution 1803 (XVII)) ambalo limeweka masharti ya namna ambavyo Mikatiba inayoingiwa na nchi juu ya rasilimali inapaswa kuwa, kwa mfano Kanuni ya 8 ya Azimio Namba 1803 (XVII) (UNGA Resolution 1803 (XVII)) inaeleza kuwa Mikatiba ya Uwekezaji wa Nje (*Foreign Investment Agreements*) ni lazima iingwiwe kwa nia njema ambapo mataifa na mashirika ya kimataifa yatalazimika kuheshimu mamlaka ya nchi katika maliasili na rasilimali zake kutokana na Mikatiba wa Umoja wa Kimataifa na misingi iliyowekwa katika azimio hili. Misingi wa Kanuni hiyo ya Azimio la Umoja wa Mataifa linafanana na maudhui ya Ibara ya 4 (2) (3) ya Muswada huu ambayo pia inaeleza kwa upana juu ya masuala ya kuzingatia wakati Bunge likipitia Mikatiba na Makubaliano mbalimbali yaliyoingiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, suala la ulinzi wa maliasili za nchi linaonekana katika nchi nyingine za Afrika, kama vile Namibia ambayo kabla ya mwaka 1974 rasilimali za nchi hiyo hazikuwa zinalindwa na kupelekea kupoteza mapato mengi ya nchi hiyo. Mnamo mwaka 1974 Baraza la Umoja wa Mataifa lilitunga Tamko (*Decree No.1*) la ulinzi wa maliasili ya Namibia. Lengo kuu lilikuwa ni kuweka ulinzi madhubuti wa maliasili zilizo ndani ya mipaka ya nchi ya Namibia.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, misingi wa Tamko hilo kwa nchi ya Namibia limesaidia kuweka utaratibu ambao mpaka sasa umendelea kulinda na kusimamia rasilimali za nchi hiyo kwa manufaa ya wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika**, ujio wa Muswada huu wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti hasi katika Mikatiba inayohusu Maliasili za nchi na jitihada zinazofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaifanya Nchi ya Tanzania kuwa ni miongoni mwa Nchi za Afrika zilizochukua jitihada zake binafsi katika kulinda, kusimamia na kuendeleza rasilimali zote za nchi kwa manufaa ya taifa.

**Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa rasilimali za Taifa unaowekwa na Misingi ya Muswada huu wa Sheria, utasaidia

katika kuongeza mapato ya nchi (GDP) na mwananchi mmoja mmoja (Per Capital Income) yanayotokana na rasilimali mbalimbali. Vilevile usimamizi madhubuti wa rasilimali za nchi kupitia Muswada huu wa Sheria utasaidia kuboresha huduma mbalimbali za kiuchumi kama vile ujenzi wa miundombinu, huduma za afya na elimu.

### 1.3 Msingi wa Kikatiba

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Msingi wa Mswada huu unatokana na maudhui ya Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ambayo inalipa Bunge jukumu la kuwa ni chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyote vinavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. Hivyo basi msingi wa upitiaji wa Mikataba ambao unawekwa na Muswada huu wa Sheria utasaidia katika kuishauri Serikali katika eneo hilo na pia kuwawakilisha wananchi katika masuala yanayohusu rasilimali za nchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Lengo la Muswada huu ni kuhakikisha kila mtanzania anashiriki kikamilifu katika ulinzi wa Rasilimali za nchi. Kwa mfano Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 chini ya Ibara ya 8 inasema;

*“Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya Kidemokrasia na Haki ya Kijamii na kwahiyo-*

*a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata Madaraka na Mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii;*

*b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;*

*c) Serikali itawajibika kwa wananchi;*

d) *Wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.*

#### 1.4 Ushirikishwaji wa Wadau:-

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza kikamilifu sharti la Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kuhusu ushirikishaji wa Wadau katika uchambuzi wa Muswada. Wadau wote waliofika mbele ya Kamati au kutuma maoni yao kwa maandishi walifanya hivyo kufuatia Tangazo la Katibu wa Bunge kwa Umma lililotolewa Tarehe 29 Juni, 2017.

Hivyo, uchambuzi wa Muswada huu ulishirikisha wadau wa aina mbalimbali waliotoa maoni kwa njia ya majadiliano ya moja kwa moja na kwa njia ya maandishi.

#### a) **Wadau Waliochangia Moja kwa Moja Ukumbini:**

- (i) Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS);
- (ii) Chuo cha Madini Dodoma;
- (iii) Shirika la Madini Nchini (STAMICO);
- (iv) Baadhi ya Vikundi vya Waendesha Bodaboda wa Dodoma;
- (v) *Tanzania Chamber of Minerals and Energy;*
- (vi) Chama cha Wachimbaji Wadogo Wadogo wa Madini ya Vito Dodoma;
- (vii) Jumua ya Kikristo nchini;
- (viii) Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira nchini (LEAT);
- (ix) Jukwaa la Asasi za Kiraia zinazojishughulisha na masuala ya Uziduaji nchini (Haki Raslimali);



- (x) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;
- (xi) Jitambue Vijana Dodoma;
- (xii) Ndg. Erasmo Nyika wa Chuo Kikuu cha Abedien uingereza
- (xiii) *Environmental Conservation Society of Tanzania;*
- (xiv) Wawakilishi wa Waganga wa Tiba Asilia nchini;
- (xv) Universal Development Initiative (UDI)
- (xvi) Chama cha Wamachinga wa Dodoma (DOWA);
- (xvii) Tuyatunze Mazingira Dodoma;
- (xviii) Misani ya Hiyari;
- (xix) DAKADAKA Dodoma;
- (xx) LEMKACHEMA 2005 Group;
- (xxi) Ndg. Erasmo Nyika- Mwanafunzi wa Digrii ya Uzamivu;
- (xxii) Ndg. Antidius Kaitu- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (xxiii) Tumaini Hayuma- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (xxiv) Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Wadogo Tanzania (FEMATA);
- (xxv) Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na;
- (xxvi) Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST).

b) **Waliochangia kwa Maandishi:**

- (i) Chama cha ACT Wazalendo (ACT);
- (ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- (iii) Kampuni ya Uchimbaji Mafuta ya Norway (STATOIL)
- (iv) Natural Resources Governance Institute;
- (v) Ndg. Frank Simon Mkoko- Mchimbaji Mdogo;
- (vi) SIBUKA FM;
- (vii) Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya;
- (viii) Ndg. Aziz Mwita (Raia);
- (ix) Ndg. Twahir Abas Kiobya (Raia); na
- (x) Ndg. Fadhiri C Bwagalilo (Mwanafunzi St. John)

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wadau wote walioshiriki kukamilisha zoezi hili kwani maoni yao yamekuwa msaada mkubwa sana kwa Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utambulizi wa Taarifa hii, napenda kuwasilisha katika Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ambayo yametokana na uchambuzi wa wajumbe wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada pamoja maoni ya Wadau ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu tatu kama ifuatavyo:

a) Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya jumla kama vile jina la Sheria na kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa.

b) Sehemu ya Pili inalipa Bunge la Jamuhuri ya muungano mamlaka ya kisheria ili kutekeleza wajibu wake wa kusimamia Serikali, kupitia Makubaliano na Mikataba yote inayohusu maliasili za nchi ambayo imeingwiwa na Jamuhuri ya muungano kwa lengo la kujiridhisha na masharti yaliyomo katika Mikataba hiyo. Aidha, kwa muktadha huo Bunge litakuwa uwezo wa kutaka kufanya majadiliano upya na upande wa pili wa mikataba ili kuondoa masharti ambayo yataonekana kuwa ni hasi; na

c) Sehemu ya Tatu inaweka utaratibu wa namna ya kuanzisha majadiliano na upande wa pili wa mikataba ili kuondoa masharti hasi kama yalivyoainishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 6(2) ya Muswada.

## **2.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya kwanza ya Muswada huu ni Utangulizi ambayo imeundwa na Ibara tatu ambazo zinajumuisha, jina la Muswada, mipaka ya Matumizi ya Sheria inayopendekezwa na Tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Ibara ya 2 ya Muswada huu ambayo inatoa mawanda ya matumizi ya Sheria hii, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa imeandikwa bila kuzingatia upande wa Muungano. Ibara 2(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kuwa;

***“Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar, na ni pamoja***

***na sehemu yake ya Bahari ambayo Tanzania inapakana nayo"***

Kwa kuzingatia msingi wa Maudhui ya Ibara hii ya Katiba, Kamati ilishauri Serikali kufanya marekebisho katika Ibara ya 2 ya Muswada huu ili kuweza kuitambua Tanzania Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia Ibara hii ya 2 ya mapendekezo ya Muswada wa Sheria inatoa sharti la matumizi ya Sheria hii katika kupitia Mikataba na makubaliano yaliyokwishaingiwa hapo awali na Serikali kabla ya kutungwa na kuanza kutumika kwa Sheria hii. Mapendekezo ya Muswada katika Ibara hii yataliwezesha Bunge kupitia Mikataba yote ambayo imekwishaingiwa tayari kabla ya kutungwa kwa Sheria hii. Jambo hili litasaidia kuweza kung'amua Masharti yote hasi yanayopatikana katika Mikataba hiyo, hivyo kuiwezesha Serikali kufanya majadiliano mapya na hatimaye kuondoa Masharti hasi katika Mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilichambua Ibara ya 3 ya Muswada huu na kubaini kuwa neno Katiba limetafsiriwa kama Katiba **ya Jamhuri**, hivyo Kamati ilipendekeza tafsiri ya neno Katiba iongezwe maneno "**ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**". Baada ya majadiliano Serikali iliridhia kufanya marekebisho hayo ambayo sasa yatatoa tafsiri halisi ya neno Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ambavyo inapaswa kusomeka.

## **2.2 Sehemu ya Pili ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya pili ya Muswada wa Sheria unaopendekezwa una Ibara mbili (2) yaani Ibara ya Nne (4) na Tano (5). Sehemu hii inalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kisheria ya kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kuishauri Serikali kama ilivyoainishwa katika **Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**.

Kwa msingi huo Bunge litakuwa na uwezo pale linapoonaa inafaa kupitia Mikatiba na Makubaliano yaliyoingiiwa na Serikali kwa lengo la kubaini masharti hasi (*Unconscionable terms*) na kuishauri Serikali kufanya majadiliano upya na upande wa pili wa Mikatiba ili kuondoa masharti ambayo yataonekana kuwa ni hasi.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne (4)** inapendekeza kulipa Bunge Mamlaka ya kupitia Mikatiba pia inaweka sharti la kuhakikisha kwamba Makubaliano yote yanayoingiiwa katika nia njema na usawa kwakuzingatia maslahi ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano Tanzania. Awali utaratibu huu haukuwepo, lakini sasa kupitia mswada huu Bunge linaweza kufanya kuhakikisha maslahi ya nchi na wananchi wake yanalindwa.

Baada ya uchambuzi wa Kamati katika Ibara hii ya 4(1), Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada kama yalivyoletwa na Serikali katika ibara hii, kwa kuwa matumizi ya neno "**May**" yana tija kwa kuwa majukumu na madaraka ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku kama ilivyoelezwa katika Ibara ya **63(2)**. Hivyo, matumizi ya neno "**May**" yanaweka mipaka ya majukumu kati ya Serikali na Bunge.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4(4)** ya Mapendekezo ya Muswada huu wa Sheria inalitaka Bunge kuweka utaratibu wa Kikanuni utakaotumika wakati wa Mapitio ya Mikatiba na Makubaliano yanayoingiiwa na Serikali kwenye maliasili za nchi. Kamati inapendekeza kuondolewa kwa ibara hiyo kwani inaonekana kulilazimisha Bunge kuweka utaratibu mahususi wakati wa kupitia mikatiba iliyoingiiwa na Serikali juu ya rasilimali na maliasili za nchi. Bunge kama muhimili wa dola lina utaratibu wake wa kutekeleza majukumu yake bila kupangiwa na muhimili mwingine.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5** kwa ujumla wake inatoa utaratibu wa jinsi gani Serikali itaanzisha majadiliano na upande wa pili wa Mikatiba ili kuondoa masharti hasi yatakayojitokeza katika Mikatiba au makubaliano

yaliyoingiwa na Serikali kwa maslahi ya nchi. Ibara hii kwa kweli italetwa maana halisi ya umilikiwa wa maliasili za nchi kuwa nchi ya Wananchi na hii sas inaliapa Bunge nguvu ya kumiliki.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa Kamati katika Ibara hiyo, Kamati iliona kuwa Mapendezo hayo hayana tija kwa kuwa majukumu na madaraka ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku kama ilivyoolezwa katika Ibara ya **63(2)**. Hivyo basi maudhui ya Ibara ya Tano (5) yataliongezea Bunge nguvu ya Kisheria ya kufanya marekebisha na siyo kuingilia kazi ya Serikali ya kuingia Mikataba na makubaliano mbalimbali.

### 2.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ya Tatu ina Ibara tatu yaani ibara ya 6, Ibara ya 7 na Ibara ya 8. Lengo la sehemu hii ya Muswada ni kutoa utaratibu wa namna gani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaanzisha majadiliano na makubaliano na upande wa pili wa Mikataba kwa lengo la kuondoa masharti hasi kama yatakavyobainishwa na Bunge. Sehemu hii pia imeainisha masuala kwa muonekano wake yatachukuliwa kuwa ni hasi hayatapaswa kuonekana katika Mikataba.

Kamati ilifanya uchambuzi wa **Ibara ya 6** na kubaini kuwa uandhishi wa Ibara ya 6(2(d) umetumia neno **Mining** kubeba maana ya Rasilimali zote za nchi. Kamati inapendekeza neno "**Mining**" *liondolewe* katika Ibara hiyo na badala yake yatumike maneno "**Natural Resources**". Sababu kubwa ya mapendekezo hayo ni kwamba maneno natural resources yanajumuisha rasilimali nyingi ziadi ya madini. Baada ya mashauriano, Serikali ilipokea ushauri wa Kamati na kukubali mabadiliko yaliyopendekezwa.

Msingi wa mabadiliko ya maneno hayo katika Ibara ya 6(2) (d) sasa yataweka tafsiri ya neno rasilimali na hivyo

kuingiza aina mbalimbali za rasilimali kama zinavyofafanuliwa katika Ibara ya 3 ya Muswada huu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi katika Ibara ya 7(1) ilibaini makosa madogo ya uandishi yaliyopelekea matumizi yasiyo sahihi ya neno *Unconscionable* lililo kati ya maneno *regards to* na *such terms* badala yake litumike neno *Unconscionability of terms*. Hivyo basi matumizi ya neno hili litasaidia kuleta maana halisi iliyokusudiwa katika kifungu hicho. Aidha, kifungu kidogo cha pili cha ibara hiyo kimeridhiwa na Kamati kama kilivyoainishwa katika muswada.

Katika Ibara ya 8 Kamati ilichambua Muswada na kupendekeza yaongezwe maneno "*upon consultation with the relevant sectoral Ministries*" mwanzoni mwa Ibara hii. Msingi wa mapendekezo haya unatokana na ukweli kwamba jinsi ibara hii ilivyoandikwa inatoa Mamlaka yote kwa Waziri wa Katiba na Sheria, wakati Sheria hii itagusa Wizara tofauti katika utekelezaji wake.

### 3.0 MAONI YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi wa Muswada huu Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo:-

a) Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huu Kamati inashauri Serikali iharakishe kutunga Kanuni kama ambavyo Waziri mwenye dhamana kwa mujibu wa Ibara ya Nane (8) ya Muswada inavyoelekeza. Utungaji wa Kanuni hizi utaweka utaratibu wa utekelezaji wa Sheria hii na hivyo kufanikisha adhama ya kutungwa kwake ambayo inalenga kulinda rasilimali za nchi kwa maslahi ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Kwamba Serikali iboresha utendaji wa vyombo mbalimbali vinavyosimamia sekta ya maliasili za nchi ili kuendana na dhamira nzuri ya utungaji wa Sheria hii kwa lengo la kuhakikisha rasilimali za nchi na maslahi ya wananchi wa Tanzania. Kamati inaona iwapo vyombo hivi

havitasimamiwa na kuboreshwa kutapelekea Sheria hizi kutosimamiwa vema na hivyo kuondoa umuhimu wa utungwaji wake.

c) Kwamba, mara baada ya kupitishwa kwa Muswada huu na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa Sheria, mchakato wa mapitio ya Mikataba na Makubaliano uanze mara moja ili kuondoa masharti hasi katika Mikataba ya rasilimali za nchi.

#### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe binafsi, kutokana na kuona umuhimu wa Muswada huu na kuamua kuunda Kamati hii ili iweze kuufanyia kazi. Hiyo ni ishara kwamba, wewe pamoja na Bunge lako Tukufu, tunapenda kuona nchi yetu inanufaika ipasavyo kutokana na uwekezaji unaofanyika katika rasilimali na maliasili zetu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Paramagamba J.A.M. Kabudi (Mb), na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. George Masaju Mb, kwa ushirikiano wao katika uchambuzi wa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Pamoja na Wajumbe Waalikwa, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kuweza kuandaa Taarifa hii. Napenda kuwatambua Wajumbe wote wa Kamati hii ya Pamoja kwa kuwataja kwa majina, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kufanya hivyo, na ninaomba majina yao yote yangie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (**Kiambatisho**).

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kasilillah, ambao umewezesha kazi hii kukamilika kwa wakati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athman Hussein, Mkurugenzi



Msaidizi wa Kamati, Ndg. Dickson Bisile na Mkurugenzi Msaidizi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndg. Prudence Rweyongeza, kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Vilevile, napenda kuwatambua Makatibu wa Kamati ambao ni Ndg. Mwanahamis Munkunda, Ndg. Chacha Timasi Nyakega, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Mariam Mbarouk, Ndg. Elieka Saanya, Ndg. Thomas Shawa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Gwivaha kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamlika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

.....  
**Doto Mashaka Biteko**  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA PAMOJA**  
3 JULAI, 2017

**KIAMBATISHO**

**ORODHA YA WAJUMBE WA KAMATI YA BUNGE YA PAMOJA**

---

<b>Na.</b>	<b>JINA</b>
1.	Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb.- <b>Mwenyekiti</b>
2.	Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb.
3.	Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb.
4.	Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb.
5.	Mhe. Mauled Said Abdallah Mtulia, Mb.
6.	Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb.
7.	Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb.
8.	Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb.
9.	Mhe. Katani Ahamadi Katani, Mb.
10.	Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb.
11.	Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb.

12. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb.
13. Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb.
14. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb.
15. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb.
16. Mhe. Desderius John Mipata, Mb.
17. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb.
18. Mhe. Mohamed Juma Khatibu, Mb.
19. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb.
20. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb.
21. Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb.
22. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb.
23. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb.
24. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb.
25. Mhe. John Wegesa Heche, Mb.
26. Mhe. Anne K. Malecela, Mb.
27. Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye, Mb.
28. Mhe. Kemilembe Julius Lwota, Mb.
29. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb.
30. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb.
31. Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb.
32. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb.
33. Mhe. Devotha Mathew Minja, Mb.
34. Mhe. Khalifa Salim Suleimani, Mb.
35. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb.
36. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb.
37. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb.
38. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb.
39. Mhe. Risala Kabongo, Mb.
40. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb.
41. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb.
42. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb.
43. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb.
44. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb.
45. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb.
46. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb.
47. Mhe. Fredy Atupele Mwakibete, Mb.
48. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb.
49. Mhe. Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Mb.
50. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb.
51. Mhe. Neema William Mgya, Mb.

52. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb.
53. Mhe. Mohamed Omary Mchengera, Mb
54. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb
55. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb.
56. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb.
57. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb.
58. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb.
59. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb.
60. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb.
61. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb.
62. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb.
63. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
64. Mhe. Makame Mashaka Foun, Mb.
65. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb.
66. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb.
67. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb.
68. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb.
69. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb.
70. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb.
71. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
72. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb.
73. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb.
74. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb.
75. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
76. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb.
77. Mhe. Juma Kombo Hamad, Mb.
78. Mhe. Andrew John Chenge, Mb.
79. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb.
80. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb.
81. Mhe. Halima James Mdee, Mb.
82. Mhe. Tundu Antipas Mughway Lissu, Mb.
83. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb.
84. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb.
85. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb.
86. Mhe. Esther Michael Mmasi, Mb.
87. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb.
88. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb.
89. Mhe. Hassani Seleman Kaunje, Mb.
90. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb.
91. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb.

92. Mhe. Hassan Elias Massala Mb.
93. Mhe. Leonidas Tutubert Gama, Mb.
94. Mhe. Almas Athuman Maige, Mb.
95. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb.
96. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb.
97. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ni suala la utaratibu, naomba nipewe nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Mnyika. Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. TUNDU A.M. LISSU - MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naomba pia utambue tuna hotuba mbili tofauti, nami nitawasilisha hotuba Muswada wa kwanza wa *Permanent Sovereignty* na Mheshimiwa Heche atawasilisha Muswada wa pili.

**NAIBU SPIKA:** Mtajua ninyi namna mtakavyogawana, lakini kwa jumla mna nusu saa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MBUNGE FULANI:** Hoja hizi ni mbili tofauti.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwenyekiti, hoja hizi ni mbili tofauti, ambazo kila moja inapaswa ipewe nusu kwa mujibu wa utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae. Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae! Mheshimiwa Cecilia Paresso, naomba uendelee kusoma.

**MBUNGE FULANI:** Mbona mnatuburuza sana jamani!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la utaratibu hilo! Hoja ni mbili tofauti.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae. Naomba mkae! Mheshimiwa Lema tafuta kiti ukae, nimeagiza mkae. Kwa hiyo, tafuta kiti, ukae.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani kama wote tunavyofahamu, kiti kikiwa kimeagiza jambo, kama ulikuwepo ama hukuwepo ndicho kinachopaswa kufuatwa. Mheshimiwa Spika, aliunda Kamati yenye Kamati nne ndani yake, akaagiza Mheshimiwa Doto Biteko kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo kushughulika na Miswada miwili kwa pamoja. *(Makofi)*

Zile Kamati nne zilivyounganishwa pamoja, hazijadai muda wa kuleta kila watu jambo lao. Hapa tumemsikia Mwenyekiti akileta yote mawili, tumeisikia Serikali ikileta yote mawili na Kambi Rasmi ya Upinzani pia italeta yote mawili kwa sababu Mheshimiwa Spika alikuwa ameagiza mambo haya yafanywe kwa pamoja na Kamati moja. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu tutakaotumia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, tutagawana dakika 15 na Mheshimiwa Heche atakuja kumalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kuwa umuhimu wa rasilimali na maliasili kama madini, mafuta, gesi, milima, wanyamapori, maji na rasilimali nyingine ni hazina kwa Taifa kwa manufaa ya sasa na ya baadaye. Kwamba Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kwa rasilimali na utajiri wa asili ni hoja isiyokuwa ya mjadala. Hivyo hatuna budi kama Taifa kuhakikisha kuwa tunatengeneza sheria nzuri ambazo zinaweza kutunufaisha kwa miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nchi yetu imekabiliwa na changamoto kubwa ya kuzimudu, kuzisimamia na kunufaika na rasilimali hizo. Tutakumbuka kuwa mnamo miaka ya 1990 nchi yetu kwa haraka haraka na kufuata Sera za Kiliberali za uchumi huria ilikubali kubinafsisha Sekta ya Madini. Ubinafsishaji huu ulichagizwa na mkakati wa madini wa Afrika wa mwaka 1992, uliotolewa na Benki ya Dunia. Mkakati huu ulitaka nchi za Afrika ikiwemo Tanzania kubinafsisha Sekta ya Madini kwa kisingizio kwamba Mashirika ya Madini ya Serikali yalishindwa kuiendesha sekta hiyo, kwani yalikuwa yanaendeshwa kwa misingi ya kisiasa na siyo ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika haya pia yalisingiziwa kuwa hayafanyi shughuli za utafutaji madini na kupanua migodi, hayakuwa na mitaji ya kutosha pamoja na wataalam wabobezi. Kibaya zaidi hayakuwa yamejifungamanisha na soko la madini la dunia. Hali hiyo haikuwa kwa kampuni za nje ambazo zina mtaji wa kutosha, zina utaalum wa kutafuta na kuendesha migodi na ni sehemu ya Soko la Madini la Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Dunia iliendelea kusema kuwa Afrika ingeweza kunufaika tu na rasilimali ya madini kama itabinafsisha sekta hiyo na kuikabidhi kwa kampuni za madini za nje. Hilo lingewezekana tu pale ambapo nchi hizi zitakapotunga sera na sheria rafiki za madini ambazo zitatoa vivutio vya kisheria, uwekezaji, vya kifedha na kodi. Serikali ilitakiwa ibakie kuwa msimamizi wa mali wa mbali wa Sekta ya Madini kwa kutunga sheria na kanuni na kutoza kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 1994 hadi 1997 jumbe 17 za Wataalam wa Benki ya Dunia zilitembelea Tanzania kwa lengo la kuchagiza na kuongoza mabadiliko ya sera na sheria zote zinazogusa Sekta ya Madini. Matokeo yake ni kupitishwa kwa Sera na Sheria ya Madini ya Mwaka 1997 na kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria za Fedha Na. 27 ya Mwaka 1997, pamoja na Sheria ya Madini ya Mwaka 1998. Wakati hayo yakitokea, nchi yetu ilishuhudia kufukuzwa kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya Bulyankulu Kahama, Shinyanga na Lusu Nzega, Tabora mwaka 1996 na huko Mkoani Mara.

Wachimbaji wadogo wa Bulyankulu walifukuzwa licha ya kuwepo zuiu la Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Tabora katika Kesi Na.12 ya 1995 iliyokuwa imefunguliwa na Kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited* katika Mahakama Kuu iliyokuwa ikimilikiwa na Kampuni ya *Sutton Resources Limited* ya Canada. Matokeo yake ni kuondolewa kwa wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wadogo na familia zao wapatao 400,000. Kwa maana hiyo nchi yetu ilipoteza ajira za wachimbaji wadogo wasiopungua milioni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 ilimpa Waziri wa Madini madaraka makubwa ya kusaini mikataba ya uendelezaji madini na kuingilia hata sekta ambazo hazihusiani na madini. Mikataba hii imeyapa kinga kubwa sana makampuni ya madini ambazo zimesaini mikataba na Serikali ikiwa ni pamoja na kuzuia kutumika kwa sheria mpya ambazo zinapitishwa na Bunge kwa kampuni hizo kuanzia mikataba hiyo inaposainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwamba migogoro yote kati ya Serikali na kampuni hiyo iamuliwe na mabaraza ya usuluhishi wa migogoro ya wawekezaji kama vile *International Centre for Settlement of Investment Disputes*, *London Court of International Arbitration* na *International Chamber of Commerce*. Kwa misingi hiyo, Mamlaka ya Mahakama za nchi juu ya migogoro kati ya Serikali na

kampuni hizi inaamuliwa na mabaraza ya nje na siyo Mahakama zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji wa Sekta ya Madini ambao ulikuwa na ahadi kwa nchi yetu itanufaika kupitia kodi na mrabaha, mwisho wa siku ilibainika kuwa ni ahadi hewa. Kwa mfano, kuanzia mwaka 1997 hadi 2009 hakuna hata kampuni moja iliyolipa kodi ya mapato na hivyo nchi kupata tu tozo ya mrabaha ambayo ilipatikana baada ya kutoa gharama za uzalishaji. Kampuni ya *Resolute* iliyokuwa inachimba dhahabu katika mgodi wa Lusu ililipa kodi kwa miaka miwili tu licha ya kuchimba dhahabu kwa zaidi ya miaka 14 na kufunga uzalishaji mwaka 2012. Kampuni za madini pia zimeimbikiza hasara kwa miaka mingi na hivyo kusababisha kutolipwa kwa kodi ya mapato kwa miaka karibu yote ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kampuni hizo zilipewa nafuu kubwa za kifedha, kodi na tozo. Tume ya Jaji Warioba ilibaini kuwa Tanzania ilipoteza au kusamehe dola milioni 8.7 na dola milioni 24 kati ya mwaka 2006 hadi 2008 kama tozo ya mafuta. Aidha, Serikali ya Tanzania ilisamehe dola milioni 60 kwa lita milioni 178 zilizouzwa kwa kampuni sita za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa misingi hiyo, Sera na Sheria za Madini ambazo zilipitishwa na Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi kuanzia miaka ya 1990 hadi hivi sasa zimesababisha nchi yetu kugawa bure rasilimali zake kwa wachukuaji hawa. Mwisho wa siku nchi yetu haijanufaika hata kidogo na uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa misingi hiyo tunapenda kusema kuwa, Miswada hii ni ushahidi wa wazi kuwa Serikali ilishindwa na imeshindwa kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie, “ni kwa misingi hiyo Miswada hii ambayo inajadiliwa leo ni ushahidi wa wazi kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilishindwa



na imeshindwa kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia sekta ya madini." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na hali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema, utungwaji wa sheria kwa hati ya dharura hatuwezi kutibu mfumo mbovu wa Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema kuwa, utungwaji wa sheria kwa hati za dharura, hakuwezi kutibu mfumo mbovu wa sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza kabisa kuona leo hii tunarudia kosa lile lile la kupitisha Miswada hii kwa hati ya dharura wakati nchi haipo katika hatari ya vita na wala rasilimali zetu hazitoweki kwa kujipa angalau muda wa kukusanya maoni ya wadau kutoka katika Majimbo yetu, wataalam mbalimbali na pia kupata uzoefu katika nchi nyingine ili kuhakikisha tunatengeneza sheria bora na zenye tija kwa maslahi ya muda mrefu wa Taifa hili. Mfumo mzuri wa sheria na kitaasisi unaweza kuletwa kwa kukaa pamoja na kupitia kwa kina na kimo udhaifu mzima wa sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Miswada; Azimio Namba 1803 la Mwaka 1962 na Azimio Namba 3281 la Mwaka 1979; licha ya kuzitaja katika dibaji ya Muswada huu wa Sheria na licha ya kuwa kifungu cha 25 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria mbalimbali kuwa ni sehemu ya tamko, lakini sheria hii kama sehemu tu ya kuweka msingi wa kuelewa lengo la sheria, lakini siyo kifungu ambacho kinaweza kutumika kupata au kupigania haki au kumwadhibu mtu anayekiuka kile kilichotajwa katika utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa Maazimio haya mawili lazima yawekwe kwenye majedwali ya Muswada huu wa Sheria, kufanya hivyo kutaweza kuyaasili na kuyafanya kuwa sehemu za sheria zetu za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha (2) cha Muswada huu wa sheria kinachotamka kuwa sheria hii itatumika Tanzania Bara pekee ni kifungu kilichokosa uhalali kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni kwa sababu Tanganyika imejivika koti la Muungano kwa mujibu wa Muswada huu, hususan Kifungu cha 4 (1) kinachosema: *"The people of the United Republic shall have permanent sovereignty over all natural wealth and resources. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la kushangaza kabisa kwa kuwa Tanzania Bara haina mamlaka kamili bila Tanzania Zanzibar. Pamoja na hilo, rasilimali kama gesi ni jambo la Muungano na lipo kikatiba kama ilivyoelezwa kwenye Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo la kushangaza ni kuwa Zanzibar inatengwa katika Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali. Hata hivyo, Tanzania Zanzibar ina sehemu yake ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta ya gesi asilia ya mwaka 2016, kinyume kabisa na Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hizi zimelenga kutumika Tanzania Bara pekee. Kwa tafsiri rahisi ni kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imegawanywa vipande viwili katika suala la umiliki na usimamizi wa rasilimali za maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* lakini nifanye hitimisho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwakumbusha Wabunge wote wa CCM kuacha kutumia jeuri ya wingi wao waliopitisha sheria ambazo leo zinaonekana kuliingiza Taifa katika hasara kubwa. Ni vyema sasa Bunge hili likawa ni Bunge la tofauti, ni Bunge ambalo litakumbukwa katika historia kwa kuweka pembeni ushabiki

wa itikadi za kisiasa na kuamua kuwatendea Watanzania haki kwa kutengeneza sheria bora zenye manufaa kwa sasa na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Hivyo basi, Wabunge wa pande zote mbili, yaani wa Upinzani na wa Chama cha Mapinduzi, tutapimwa kwa namna ambayo tutachagua leo hii kulisimamia Taifa letu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inawasihi Wabunge wa CCM wasirudie tena makosa ya kutumia wingi wao kulisulubu Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ya CCM kurudisha mchakato wa Katiba Mpya ambao umetumia fedha nyingi za walipa kodi ili sasa maoni ya wananchi waliyoyatoa kupitia Tume ya Warioba kuhusu usimamizi wa rasilimali zao yawekwe kuwa sehemu ya Katiba mpya na kuhakikisha kuwa Taifa hili linanufaika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAMLAKA YA NCHI KUHUSIANA NA UMILIKI WA MALIASILI WA MWAKA 2017 (THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES [PERMANENT SOVEREIGNTY]) BILL, 2017 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*( Yanatolewa chini ya Kanuni ya 86 (6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ,toleo la Mwaka 2016)*

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, nianze kwa kusema kuwa umuhimu wa rasilimali na maliasili kama madini, mafuta, gesi , milima , wanyamapori, maji na rasilimali nyingine ni hazina kwa taifa kwa manufaa ya sasa na ya baadae. Kwamba Tanzania ni

nchi iliyobarikiwa kwa rasilimali na utajiri wa asili ni hoja isiyo ya mjadala. Hivyo hatuna budi kama taifa kuhakikisa kuwa tunatengeneza sheria nzuri ambazo zinaweza kutunufaisha kwa miaka mingi ijayo.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo nchi yetu imekabiliwa na changamoto kubwa ya kuzimudu, kuzisimamia na kunufaika na rasilimali hizo. Tutakumbuka kuwa mnamo miaka ya tisini nchi yetu kwa haraka haraka na kufuata sera za kiliberali za uchumi huria ilikubali kubinafsisha sekta ya madini. Ubinafsishaji huu ulichagizwa na mkakati wa madini wa Afrika wa mwaka 1992, (The Strategy for African Mining) uliotolewa na Benki ya Dunia. Mkakati huu ulitaka nchi za Afrika ikiwemo Tanzania kubinafsisha sekta ya madini kwa kisingizio kwamba mashirika ya madini ya Serikali yalishindwa kuiendesha sekta hiyo kwani yalikuwa yanaendeshwa kwa misingi ya kisiasa na si ya kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, Mashirika haya pia yalisingiziwa kuwa hayafanyi shughuli za utafutaji madini na kupanua migodi, hayakuwa na mitaji ya kutosha pamoja na wataalamu wabobezi. Na kibaya zaidi hayakuwa yamejifungamanisha na soko la madini ya dunia. Hali hiyo haikuwa kwa kampuni za nje ambazo zina mtaji wa kutosha, zina utaalamu wa kutafuta na kuendesha migodi, na ni sehemu ya soko la madini la dunia.

**Mheshimiwa Spika**, Benki ya Dunia iliendelea kusema kuwa Afrika ingeweza kunufaika tu na rasilimali ya madini kama itabinafsisha sekta hiyo na kuikabidhi kwa kampuni za madini za nje. Hilo lingewezekana tu pale ambapo nchi hizi zitakapotunga sera na sheria rafiki za madini ambazo zitatoa vivutio vya kisheria, uwekezaji, vya kifedha na kodi. Serikali ilitakiwa ibakie kuwa msimamizi wa mbali wa sekta kwa misingi ya kutunga sheria na kanuni na kutoza kodi. Kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 1994 hadi 1997 jumbe 17 za Wataalamu wa Benki wa Dunia zilitembelea Tanzania kwa lengo la kuchagiza na kuongoza mabadiliko ya sera na sheria zote zinagusa sekta ya madini. Matokeo yake ni kupitishwa

kwa Sera ya Madini ya Mwaka 1997, kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria za Fedha Namba 27 ya Mwaka 1997, na Sheria ya Madini ya Mwaka 1998.

**Mheshimiwa Spika**, wakati hayo yakitokea nchi yetu ilishuhudia kufukuzwa kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya Bulyanhulu Kahama Shinyanga na Lusu Nzega Tabora mwaka 1996 na huko mkoani Mara. Wachimbaji wadogo wa Bulyanhulu walifukuzwa licha ya kuwepo zui la Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Tabora katika Kesi Namba 12 ya 1995 iliyokuwa imefunguliwa na Kampuni ya Kahama Mining Corporation Limited katika Mahakama Kuu iliyokuwa ikimilikiwa na kampuni ya Sutton Resources Limited ya Canada. Matokeo yake ni kuondolewa kwa wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wadogo na familia zao wapatao 400,000. Kwa maana hiyo nchi yetu ilipoteza ajira za wachimbaji wadogo wasiopungua milioni moja.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 ilimpa Waziri wa Madini madaraka makubwa ya kusaini mikataba ya uendelezaji madini (Mineral Development Agreements (MDA) na kuingilia hata sekta ambazo hazihusiani na madini. Mikataba hii imezipa kinga kubwa sana kampuni za madini ambazo zimesaini mikataba na Serikali na ikiwa ni pamoja na kuzuia kutumika kwa sheria mpya ambazo zinapitishwa na Bunge kwa kampuni hizo kuanzia mikataba hiyo inaposainiwa. Aidha, kwamba migogoro yote kati ya Serikali na kampuni hizi iamuliwe na mabaraza ya usuluhishi wa migogoro ya wawekezaji kama vile International Centre for Settlement of Investment Disputes (ICSID), London Court of International Arbitration (LCIA), International Chamber of Commerce (ICC). Kwa misingi hiyo, mamlaka ya Mahakama za nchi juu ya migogoro kati ya Serikali na kampuni hizi inaamuliwa na mabaraza ya nje na si mahakama zetu. Hii ni kinyume na Ibara 107 A(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kinataka migogoro yote iamuliwe na Mahakama zetu.

**Mheshimiwa Spika**, Ubinafsishaji wa sekta ya madini ambao ulikuwa na ahadi kuwa nchi yetu itanufaika kwa kupitia kodi

na mrabaha mwisho wa siku ulibainika kuwa ni ahadi hewa. Kwa mfano, kuanzia mwaka 1997 hadi 2009 hakuna hata kampuni moja iliyolipa kodi ya mapato na hivyo nchi kupata tu tozo la mrabaha ambalo lilipatikana baada ya kutoa gharama za uzalishaji. Kampuni ya Resolute iliyokuwa inachimba dhahabu katika mgodi wa Lusu ililipakodi kwa miaka miwili tu licha ya kuchimba dhahabu kwa zaidi ya miaka 14 na kufunga uzalishaji mwaka 2012. Kampuni za madini pia zimelimbikiza hasara kwa miaka nyingi na hivyo kusababisha kutolipwa kwa kodi ya mapato kwa miaka karibu yote ya uzalishaji.

Aidha, kampuni hizi zilipewa nafuu kubwa za kifedha, kodi na tozo. Tume ya Jaji Bomani ilibaini kuwa Tanzania ilipoteza au kusamehe dola milioni 8.7 na dola milioni 24.4 kati ya mwaka 2006/7 na 2007/8 kama tozo ya mafuta. Aidha, Serikali ya Tanzania ilisamehe dola milioni 60 kwa lita milioni 178 zilizouzwa kwa kampuni sita za madini.

**Mheshimiwa Spika**, ni kwa misingi hiyo, sera na sheria za madini ambazo zilipitishwa na Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi kuanzia miaka ya tisini hadi hivi sasa zimesababisha nchi yetu kugawa bure rasilimali zake kwa wachukuaji hawa. Mwisho wa siku nchi yetu haijanufaika hata kidogo na uchimbaji huu.

**Mheshimiwa Spika**, ni kwa misingi hiyo tunapenda kusema kuwa Miswada hii ni ushahidi wa wazi kuwa Serikali ilishindwa na imeshindwa kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia sekta hii. Kuondokana na hali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema kuwa, utungwaji wa sheria kwa hati ya dharura hakuwezi kutibu mfumo mbovu wa sekta ya madini.

**Mheshimiwa Spika**, ni jambo la kushangaza kabisa kuona leo hii tunarudia kosa lile lile la kupitisha miswada hii kwa hati ya dharura wakati nchi hii haipo kwenye hatari ya vita na wala rasilimali zetu hazitoweki kwa kujipa walau muda wa kukusanya maoni ya wadau kutoka katika majimbo yetu, wataalamu mbalimbali na pia kupata uzoefu kutoka katika nchi nyingine ili kuhakikisha tunatengeneza sheria bora na

zenye tija kwa maslahi ya muda mrefu ya taifa hili. Mfumo mzuri wa kisheria na kitaasisi unaweza kuletwa kwa kukaa pamoja na kupitia kwa kina na kimo udhaifu mzima wa sekta hii.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa “The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act 2017” unataja Azimio Namba 1803 la Mwaka 1962 na Azimio Namba 3281 la Mwaka 1974. Licha ya kuzitaja katika dibaji ya Muswada huu wa Sheria na licha ya kuwa kifungu cha 25 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria za Nchi (Interpretation of Laws Act Cap 1) kusema kuwa Tamko la Awali (Preamble) ni sehemu ya sheria lakini ni sehemu ya sheria tu kwa misingi ya kuelewa lengo la sheria hiyo lakini si kifungu ambacho kinaweza kutumika kupata au kupigania haki au kumuadhibu mtu anayekiuka kile kilichotajwa katika utangulizi.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo basi Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa Maazimio haya mawili lazima yawekwe kwenye majedwali ya Muswada huu wa Sheria, kufanya hivyo kutaweza kuyaasili na kuyafanya kuwa sehemu za sheria za nchi yetu. Pili Azimio Namba 1803 la Mwaka 1962 limetambuliwa kuwa ni kanuni ya asili ya sheria za kimataifa na hii inatupatia msingi wa kuzipa mahakama zetu mamlaka ya kuamua migogoro yote inayotokana na matumizi ya rasilimali zetu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kifungu cha 2 cha muswada huu wa sheria kinachotamka kuwa sheria hii itatumika Tanzania Bara pekee ni kifungu kilichokosa uhalali kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Hii ni kwa sababu Tanganyika imejivika koti la Muungano kwa mujibu wa muswada huu hususani katika kifungu cha 4 (1) kinachosema “The people of the United Republic shall have permanent sovereignty over all natural wealth and resources.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili ni la kushangaza kabisa kwa kuwa Tanzania bara haina mamlaka kamili bila Tanzania Zanzibar "Mainland Tanzania *cannot claim sovereignty* without Zanzibar as per constitution. Tunatambua wazi kuwa kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu Ibara ya 2(1) inasema *"Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar, na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania imepakana nayo"*. Kwa kuwa muswada huu wa Sheria inawatambua watu wa Jamhuri wa Muungano kuwa na mamlaka ya kuamua juu ya rasilimali zao basi ni lazima Wazanzibari waweze kujumuishwa katika muswada huu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hilo, rasilimali kama gesi ni jambo la Muungano na lipo kikatiba kama ilivyoelezwa kwenye Nyongeza ya kwanza ya Katiba hii inayosema *"Maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasisochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa na gesi asilia*. Jambo la kushangaza ni kuwa Zanzibar inatengwa katika Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali. Hata hivyo, Tanzania Zanzibar ina sheria yake ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta ya gesi asilia ya Mwaka 2016 (Zanzibar Oil and Gas (Upstream) Act 2016"). Kinyume kabisa na Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2015 Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria tatu kuhusiana na rasilimali za mafuta na gesi. Sheria hizo ni ;

- Sheria ya uwazi na uwajibikaji katika rasilimali za nchi, mafuta na gesi asilia Tanzania,
- Sheria ya mafuta
- Sheria ya Usimamizi wa mapato yatokanayo na mafuta na gesi.

Sheria hizi zimelenga kutumika Tanzania Bara pekee. Kwa tafsiri rahisi ni kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imegawanywa vipande viwili katika suala la umiliki na usimamizi wa rasilimali na maliasili kinyume na katiba yetu ya nchi ambayo ndiyo msingi Mkuu wa sheria nyingine yoyote



inayotungwa. Hivyo ni dhahiri hata muswada huu wa sheria hii inakiuka katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuruhusu Tanzania Bara kujipa mamlaka kamili na kujivika koti la Muungano. ***Na endapo sheria yoyote iliyotungwa inakiuka katiba ya Jamhuri ya Muungano basi sheria hiyo ni batili.***

**Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 5 (2) cha muswada huu ambacho kimeweka umiliki wa rasilimali na maliasili za nchi mikononi mwa Rais kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kifungu hatari sana ambacho kinaweza kuleta madhara makubwa kwa taifa kisipoangaliwa kwa nidhamu ya hali ya juu na kwa uzalendo uliotukuka.

**Mheshimiwa Spika**, tunatambua cheo cha "Rais" ni mamlaka anayopewa 'mtu'. Mamlaka haya ni makubwa sana na yenye athari chanya au hasi pale yanapotumiwa vibaya. Endapo binadamu huyu aliyepewa cheo kikubwa hivi akiyatumia madaraka yake vibaya anaweza kuleta hatari kubwa katika taifa. Watafiti wakubwa duniani Hysom na Kane waliofanya utafiti kuhusu maliasili ya mafuta na tawala za nchi mbalimbali katika nchi za Nigeria ,Congo, Ecuador, Cuba, Somalia, Syria, Iran, Norway, Urusi na nchi nyingine nyingi waliungwa mkono na Duncan Clarke katika kauli aliyoitoa kuhusu utajiri wa rasilimali na mfumo wa mtawala unavyokwenda sambamba. Alisema ***"utajiri wa maliasili katika nchi unaweza ukasababisha nchi ikatumbukia katika lindi la umaskini, vita na migogoro endapo utawala utakosa hekima, lakini alikwenda mbali zaidi na kusema utajiri wa maliasili unaweza kuwa neema na baraka katika nchi endapo utawala unaweza kuzitumia vyema katika kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi"***.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maneno hayo ya busara ya Hysom, Kane na Duncan Clarke yanatuweka wazi kuwa binadamu hatabiriki, na kwa kuwa kama taifa tuna uwezo wa kuamua namna bora zaidi ya usimamizi wa maliasili zetu basi ni vyema usimamizi huu uwe chini ya mamlaka ya Bunge badala ya Rais. Kwani Bunge ndio chombo kikuu cha kuwasemea wananchi ambao ndio wamiliki wakuu wa rasilimali hizi

badala ya kuwa chini ya Mamlaka ya mtu mmoja. ***Ni vyema kesho yetu tukaiamua leo.*** Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha inaendeleza mchakato wa Katiba Mpya ili sasa maoni ya wananchi kuhusu usimamamizi wa maliasili na rasilimalia asilia yaweze kuingizwa kwenye katiba .

**Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 6 (1) cha muswada huu kinachoweka katazo kuhusu shughuli ya aina yoyote inayolenga uzinduaji na uchimbaji wa rasilimali na maliasili pasipo kuweka maslahi ya umma mbele. Katika kifungu hiki neno maslahi ya umma ***“interests of the people”*** ni lazima liweze kupewa maana ya wazi (clear definition). Kumekuwepo na tabia ya baadhi ya viongozi wa Serikali kutumia kivuli cha neno maslahi mapana ya umma kujinufaisha wenyewe. Tumeshuhudia mikataba mingi ikisainiwa kwa usiri mkubwa kwa kivuli cha maslahi ya umma huku watu wachache wakijinufaisha. Matokeo ya mikataba kama Buzwagi, Escrow na mingine mingi imekuwa ikisainiwa katika kivuli hicho hicho cha maslahi ya umma na matokeo yake leo hii Serikali inatumia fedha nyingi na kuingia katika hasara zisizo na sababu kutokana na sheria na mikataba iliyopitishwa kiholela kwa mwamvuli wa maslahi ya umma. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuja na maana ya maslahi ya umma ili kuondoa utata katika kifungu hiki.

**Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 9 (1) cha muswada huu kimeweka masharti kuwa shughuli zote za uzinduaji, uchimbaji na upatikanaji au utumiaji wa rasilimali utahakikisha kuwa hakuna rasilimali ghafi itakayosafirishwa nje ya Tanzania. Katika kifungu hiki Serikali inapaswa kueleza wazi ni aina gani ya rasilimali ambazo hazitasafirishwa nje ya nchi zikiwa ghafi. Hii ni kutokana na baadhi ya rasilimali ambazo zimetajwa katika maana ya maliasili na rasilimali asilai kuwa haziwezi kuchakatwa na pengine uchakataji wake unaweza kuwa na athari kwa mazingira, afya za watuamijaji na hata kuharibu thamani ya bidhaa husika. Mfano, Madini kama Uranium ambayo yana athari za moja kwa moja za kimazingira na pia ni hatari kwa viumbe hai

watakaozunguka jirani na maeneo hayo ya uchimbaji, baadhi ya maliasili ambazo ni viumbe vidogo vidogo (micro-organisms), viumbe wa baharini nk. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza maana halisi ya rasilimali ghafi "raw resources".

**Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 10 (1) na (2) ni muhimu vifungu hivi vikawa na maelezo ya ziada. Kifungu cha 10 (1) kinapaswa kueleza bayana ni asilimia ngapi ya mapato inapaswa kubaki katika benki zetu au taasisi za fedha. Vilevile, kifungu cha 10 (2) kinalenga kukatiza uhamishaji wa mapato yatokanayo na mauzo ya rasilimali na kwa kusema kuwa kitendo hicho ni kinyume na sheria.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kuwa kitendo hicho kitakuwa ni kinyume cha sheria kama kifungu hiki kinavyosema lakini pia muswada huu haujaonyesha kuwa endapo kosa lolote la kisheria limefanywa kinyume na kifungu hiki adhabu yake itakuwa nini.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile kifungu hiki kiweke bayana je, ni benki au taasisi zipi za fedha ndani ya nchi yetu zitakuwa na sifa na uwezo wa kufanya biashara na wawekezaji hawa katika sekta hii ya maliasili. Hii ni kwa sababu ndani ya nchi yetu kuna benki au taasisi za fedha ambazo kimsingi ni za kigeni ila zina matawi hapa nchini Tanzania. Pamoja na hilo ni vyema Serikali ikafanya tathimini ya kina kuhusu uwezo wa mabanki yetu katika kufanya biashara na wawekezaji wakubwa katika sekta ya maliasili na rasilimali asilia.

**Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 11 (1) na (2) kinakatiza migogoro yote ya uchukuaji wa rasilimali na utajiri wa asili iamuriwe na mahakama zetu. Hata hivyo, sheria haizungumzii juu ya mikataba ya pande mbili au pande nyingi (*bilateral or multilateral investment treaties (BITs) / (MITs)*) ambayo nchi yetu imesaini na mataifa ya nje kwa lengo la kutoa hakikisho la uwekezaji na utaratibu wa kusuluhisha migogoro katika mabaraza ya kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo licha ya sheria hii bila kuweka utaratibu wakurekebisha mikataba hiyo na mataifa tuliyosaini mikataba hiyo bado nchi yetu itaendelea kutokuwa na himaya ya milele kwa rasilimali zake. Hivyo malengo ya sheria hii yatabaki kuwa ni matamko yasiyokuwa na maana yoyote. Sheria hii ni lazima itamke kuwa Serikali lazima ianze mchakato wa kujadiliana na mataifa hayo na kuhakikisha kuwa inaendana na matakwa ya Azimio la Namba 1803 ya Mwaka 1962 na Azimio Namba 3281 ya Mwaka 1974.

**Mheshimiwa Spika**, aidha ili matakwa ya sheria kutimilika ya kuzipa mahakama zetu mamlaka juu ya migogoro ya rasilimali na utajiri wa asili ni lazima kujitoa katika maagano ya kimataifa inayohusiana na migogoro na bima za uwekezaji. Maagano hayo ni kama Convention on International Centre for Settlement of Investment Disputes ya Mwaka 1965 na Convention on Multilateral Investment Guarantee Agency ya Mwaka 1985.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutunza na kukazia mamlaka ya nchi yetu juu ya rasilimali zetu Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa sheria zetu zipige marufuku usainiwaji wa mikataba ya matumizi ya rasilimali za asili baina ya Serikali na kampuni yoyote ya nje au ya ndani. Sheria iweke mfumo wa utoaji wa leseni kwa wawekezaji, wachukuaji au wachimbaji wa rasilimali zetu. Hii itahakikisha kuwa Serikali yetu haijidhalilishi kwa kujadiliana na kampuni moja moja bali yenyewe itakuwa na mamlaka ya kupitia maombi ya leseni na kutoa au kutotoa leseni. Kampuni zitabanwa na sheria pamoja na mashariti ya leseni.

Aidha hii itaondoa mwanya wa rushwa na hivyo kutoa nafasi kwa vyombo vya Umuduji kutenda kazi zao kwa mujibu wa sheria na si kwa mikataba ya pande mbili.

### **3.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu bado ni changa sana katika sekta binafsi za kizalendo. Mpaka sasa Serikali haijaweza

kutengeneza mifumo thabiti ya kuweza kutafuta, kuwajenga na kuwawezesha wawekezaji wazawa. Jambo ambalo linapelekea makampuni makubwa kwenye sekta ya madini, mafuta, gesi, na maliasili ya wanyamapori kuendeshwa na makampuni ya nje.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hilo makampuni haya ya nje bado hayajawekewa mikakati mizuri ili kuhakikisha yananufaisha taifa. Mpaka sasa kuna ombwe kubwa katika utekelezaji na usimamizi wa sheria mbalimbali ambapo kama sheria hizi zingesimamiwa ipasavyo basi zingeweza kulinufaisha taifa. Badala yake kumekuwa na ushabiki na ujinga uliopindukia katika ushindani wa kisiasa usio na tija ambapo badala ya kuja pamoja kama taifa ili kuhakikisha tunajenga taifa lenye nguvu kubwa kiuchumi na hali ya maisha ya wananchi wetu yanaboreka badala ya malumbano na ubabe wa kisiasa ambao umelifanya taifa hili kushindwa kujikwamua mikononi mwa maadui watatu yaani ujinga, umaskini na maradhi tangu taifa hili limepata uhuru.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kusema hayo Kambi Rasmi inatoa rai kwa Bunge lako na wananchi kwa ujumla kuhakikisha wanafuatilia kwa makini mjadala huu wa kupitisha sheria hizi za maliasili na rasilimali asilia ili siku za mbeleni waweze kujua ni nani hasa adui anayewakwamisha kuwatoa katika lindi hili la umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwakumbusha wabunge wote wa wa CCM kuacha kutumia jeuri ya wingi wao walipitisha Sheria ambazo leo hii zimeonekana kuliingiza taifa katika hasara kubwa. Ni vyema sasa Bunge hili likawa ni Bunge la tofauti, bunge ambalo litakumbukwa katika historia kwa kuweka pembeni ushabiki wa itikadi za kisiasa na kuamua kuwatendea haki Watanzania kwa kutengeneza sheria bora yenye manufaa kwa sasa na vizazi vijavyo.

Hivyo basi, sisi kama Wabunge wa pande mbili yaani Wabunge wa upinzani na Wabunge wa chama tawala

tutapimwa kwa namna ambayo tutachagua leo hii kulisimamia taifa letu kwa sababu hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani inawasihi wabunge wa CCM wasirudie tena makosa ya kutumia wingi wao kulisulubu taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ya CCM kurudisha mchakato wa Katiba Mpya ambao umetumia fedha nyingi za walipa kodi ili sasa maoni ya wananchi waliyoyotoa kupitia tume ya Jaji Warioba kuhusu usimamizi wa rasilimali zao yaweze kuwa sehemu ya Katiba mpya na kuhakikisha kuwa taifa hili linanufaika ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha,

.....  
Cecilia Daniel Pareso(Mb)  
K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni  
Wizara ya Katiba na Sheria

**03.07.2017**

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE (K.n.y. MHE. TUNDU A.M. LISSU - MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGE KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa sababu muda ni mdogo sana na kwa sababu haya mambo yameletwa kwa kuburuza buruza muda, naomba na ule muda wa Cecilia aliouacha hapo uzingatiwe kwangu ili niweze kumaliza maoni haya kama nitaweza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Lissu, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano, kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, Serikali imeleta Muswada wa Sheria Bungeni kwa hati za dharura ili Bunge litunge sheria kwa dharura kurekebisha makosa yaliyoisababishia nchi hasara kubwa kutokana na udhaifu wa Sheria za Madini, Petrol na Tasnia ya Uzindujaji (TEITI) ambazo zilipitishwa kwa hati za dharura kutokana na kuwasilishwa kwa hati ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahenga wetu walisema kuwa, sikio la kufa halisikii dawa. Nasema hivi kwa sababu kwa miaka yote ya uhai wa Bunge la Tisa, Bunge la Kumi na sasa Bunge la Kumi na Moja, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikikemea vikali suala la kuleta Miswada ya Sheria Bungeni kwa hati za dharura, hususan Miswada ya Sheria zenye athari katika maslahi ya kiuchumi kwa Taifa; lakini Serikali hii ya CCM imekuwa ikiweka pamba masikioni na matokeo yake Taifa limepata hasara kubwa kutokana na ukaidi huo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo kinachofanywa sasa na Serikali hii cha kujidai kwamba ina uchungu na rasilimali za nchi; na kujidai kuleta haraka haraka Miswada hii ili kufanya mapitio ya mikataba yenye masharti hasi inayohusu maliasili za nchi yetu, ni sawa na kula matapishi yake. Kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishatoa rai kwa Serikali kufanya hivyo kwa takriban miaka 15. Sasa leo baada ya miaka 15 ndiyo mnaelewa kwamba tulikuwa tumefanya makosa makubwa. Serikali iling'ang'ania kwamba mikataba hiyo iko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka yote hiyo niliyotaja, ilikuwa ikiitaka Serikali kuleta mikataba yote inayohusu rasilimali za nchi yetu ambayo Serikali inaingia na wawekezaji ili ijadiliwe na kuridhiwa na Bunge, lakini mara zote Serikali ilikataa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haipaswi kujisifu wala kujinasibu kwamba ni ya kizalendo kwa kuleta Muswada huu kwa kupitia mikataba yenye masharti hasi sasa; kwa kuwa si

jambo jipya. Inatekeleza ushauri uliotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani uliotolewa takriban miaka 15 iliyopita. Hata hivyo, Serikali imeanza vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia, "hata hivyo Serikali imeanza vibaya kutekeleza ushauri huo kwa kuwa.. samahani kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Ahsante kwa makofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeshagutuka kwamba Taifa lilikuwa linanyonywa kutokana na mikataba mibovu iliyotokana na sheria dhaifu zilizopitishwa kishabiki kwa haraka haraka na Wabunge walio wengi wa CCM, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea kwamba safari hii Serikali ingetulia kuandaa Muswada wa Sheria kwa umakini na kuwashirikisha wadau wote na kwa muda unaotosha ili kuziba mianya yote ya kinyonyaji iliyokuwepo kutokana na uharaka haraka katika utungaji wa sheria husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume na matarajio hayo, Serikali inarudia makosa yale yale ambayo yaliisababishia nchi hasara kubwa. Tunataka tuyarekebishe leo kwa kutumia njia zile zile na akili zile zile, hatuwezi kupata matokeo tofauti hata hivyo. Mwanafalsafa Albert Einstein aliwahi kusema:

*"We can't solve the problems by using the same kind of thinking we used when we created them."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango kile kile cha akili kilichosababisha matatizo kwa kuleta mikataba kwa uharaka haraka kimerudia tena kuleta sheria hii kwa uharaka. Kwa hiyo, tutatengeneza matatizo mengine makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe tu kusema kwamba Serikali inabidi ikiri kwamba ilikosea kuliingiza Taifa katika mikataba ya kinyonyaji iliyotokana na sheria dhaifu na hivyo kulisababishia hasara na kwamba sasa inatakiwa kufanya



*retreat* ili kubaini ilipokosea na kujirekebisha. Ili Serikali ifanikiwe katika *retreat* hiyo, haitakiwi kuwa na pupa wala papara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitoe maoni ya jumla kuhusu Muswada ulioko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 2.1 Dibaji (*Preamble*); tofauti na utaratibu wa kawaida uliozoeleka wa uandishi wa Miswada ya Sheria, Muswada huu una Dibaji, ambayo mwandishi amejitahidi sana kupamba maneno yanayoashiria utafa, uzalendo na nguvu ya wananchi katika kumiliki na kulinda rasilimali za nchi. Ikumbukwe kwamba ni Serikali hii hii ya CCM iliyoingia mikataba ya kinyonyaji na wawekezaji, wananchi wakafukuzwa katika maeneo yao, tena bila fidia na wengine wakauawa kwa kupigwa risasi hususan katika maeneo yaliyo karibu na migodi ikiwemo Jimboni kwangu Tarime. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya dibaji hii na vitendo halisi wanavyofanyiwa wananchi walioko karibu na maliasili za nchi yetu, vinafanana kabisa na ile methali inayosema “ utamu wa nanasi, ndani kipande cha mti.” Kama kweli Serikali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho, mbona imewanyima haki na uhuru wao wa kikatiba wa kupata habari kwa kuzuia kurushwa moja kwa moja kwa mijadala ya Bunge lao; na kuwawekea sheria ngumu na kandamizi ya makosa ya kimtandao inayowanyima uhuru wa habari. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho, mbona imewanyima haki yao ya kikatiba ya kukusanyika na kujiunga na vikundi au vyama vya siasa kwa kupiga marufuku mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho; mbona inawazuia wananchi wasiuze mazao yao ya kilimo nje ya nchi ili wapate

faida? Kama kweli Serikali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho, mbona wananchi wanaoishi katika maeneo ya machimbo ya madini wanaendelea kuwa maskini na kunyanyaswa na kuuawa mpaka leo? Hii mfano wake ni juzi Tarime walikamatwa watu zaidi ya 68 wako ndani kwa *armed robbery*, baada ya kujaribu kutetea rasilimali za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi mabaya wanayofanyiwa wananchi na Serikali hii inaona na wala haichukui hatua. Hivyo kuja kuwahadaa wananchi kwamba wao ndio wenye mamlaka kwa kutumia maneno matamu ya utangulizi na wakati kinachofanyika ni kinyume na maneno hayo, haikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya sheria, ibara ya pili ya Muswada wa Sheria inayopendekezwa inasema kwamba sheria hiyo itatumika Tanzania Bara, bila kuathiri mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar juu ya umiliki na uhibiti wa rasilimali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba iliyopo sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala ya mafuta na gesi ni miongoni mwa mambo ya Muungano yaliyoorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba. Pamoja na takwa hili la kikatiba Serikali hii ya CCM ikishirikiana Wabunge wake ilitunga Sheria ya Gesi na Petroli ya mwaka 2015 inayoipa Zanzibar mamlaka juu ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi Zanzibar kuwa na mamlaka juu ya rasilimali zake isipokuwa mihimili ya Bunge na Serikali iwe makini vya kutosha ili kuepuka kutunga sheria zinazokinzana na Katiba kama hii ambayo tunaenda kuipitisha sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa upungufu mkubwa ya Muswada wa Sheria inayopendekezwa ni kwamba inalenga kuifunga mikono Mahakama isiweze kushughulikia shauri la mtu atakayeonewa au kutendewa visivyo na sheria hii. Dibaji ya Sheria hii imefanya rejea ya Ibara

za (8) na (9) zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo kwa mujibu wa Katiba hiyo, haziwezi kutiliwa nguvu na Mahakama yoyote ya nchi. Kwa hiyo, hii inaweza kuwa ni geresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba "Masharti ya sehemu hii, yaani Sehemu ya Pili ya Katiba hayatatiliwa nguvu ya kisheria na Mahakama yoyote. Mahakama yoyote nchini haitakuwa na uwezo wa kuamua juu ya suala kama kutenda au kukosa kutenda jambo kwa mtu au Mahakama yoyote, au kama sheria au hukumu yoyote inaambatana na masharti ya sehemu hii."

Mheshimiwa Naibu Spika, yale mambo yote mazuri yaliyotajwa kwenye dibaji ya Muswada wa Sheria hii, ikiwa hayatastekelezwa na Serikali au ikiwa Serikali itakwenda kinyume nayo, au ikiwa mtu yeyote ataathirika kwa namna moja au nyingine wakati wa utekelezaji wa masuala hayo, basi hakuna shauri lolote linaloweza kufunguliwa kwa minajili ya kufanya madai na wala hakuna Mahakama yoyote itakayoweza kushughulikia jambo hilo. Kwa maneno mengine zile ahadi nzuri zinazotelewa na ule utangulizi ni *cosmetic*, kwa kuwa hakuna haki inayoweza kutolewa ikiwa kuna ukiukwaji wa haki umetokea katika sehemu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kengele imeshagonga, niende kwenye hitimisho, lakini naomba hotuba yangu yote kama ilivyo hapa iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hitimisho, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusisitiza kwamba nchi yetu inaangamia kutokana na mifumo mibovu ya kiutawala. Mifumo yetu ingekuwa thabiti kusingekuwa na tabia hii ya kuleta Miswada ya Sheria kwa Hati ya Dharura hata kwa mambo yasiyo ya dharura. Hati za dharura hutolewa iwapo kweli kuna jambo la dharura kwa mfano, nchi iko vitani; au kuna hali ya hatari katika nchi au kuna mlipuko wa magonjwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ungekuja Muswada wa Sheria ya Kudhibiti mambo yanayoendelea huko Rufiji na Kibiti kwa hati ya dharura, tusingeshangaa na tungeunga mkono. Kuleta Miswada ya sheria ya mambo makubwa yanayohusu utajiri na rasilimali za nchi kwa hati za dharura ni matumizi mabaya ya hati hizo. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inakutegemea upige marufuku tabia hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesisitiza kwamba...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Kengelee ya pili imegonga. Nakuongeza sekunde thelathini, malizia.

**MHE. JOHN W. HECHE (K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGE KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesisitiza kwamba ili Taifa hili liondokane na shimo hili la uharibifu, ni lazima kuanzia sasa tuamini katika mifumo ya kitaasisi kuliko kuamini katika mtu au watu. Ukiangalia Miswada ya Sheria iliyoletwa mbele ya Bunge lako utagundua kwamba kinachotafutwa ni utukufu wa mtu, yaani *Glorification of a Person*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Heche huwezi kusikia tena, kwa sababu nimezima *microphone* hapa.

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAPITIO NA MAJADILIANO, KUHUSU MASHARTI HASI KATIKA MIKATABA YA MALIASILI ZA NCHI WA MWAKA 2017 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Lissu (Mb), naomba kuwasilisha maoni ya

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano, kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena, Serikali imeleta Muswada wa Sheria Bungeni kwa hati ya dharura; ili bunge litunge sheria kwa dharura kurekebisha makosa yaliyoisababishia nchi hasara kubwa kutokana na udhaifu wa sheria za madini, petroli na tasnia ya uzinduaaji (TEITI) ambazo zilipitishwa kwa dharura kutokana na kuwasilishwa kwa hati ya dharura.

**Mheshimiwa Spika**, wahenga wetu walishasema kuwa, sikio la kufa halisikii dawa. Nasema hivi kwa sababu kwa miaka yote ya uhai wa bunge la tisa, bunge la kumi na sasa bunge la kumi na moja, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikemea vikali suala la kuleta miswada ya sheria Bungeni kwa hati ya dharura, hususan miswada ya sheria zenye athari katika maslahi ya kiuchumi kwa taifa; lakini Serikali hii ya CCM imekuwa ikweka pamba masikioni; na matokeo yake Taifa limepata hasara kubwa kutokana na ukaidi huo wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo kinachofanywa sasa na serikali hii cha kujidai kwamba ina uchungu na rasilimali za nchi hii; na kujidai kuleta harakaharaka miswada hii ili kufanya mapitio ya mikataba yenye masharti hasi inayohusu maliasili za nchi yetu, ni sawa na kula matapishi yake; kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishatoa rai kwa Serikali kufanya hivyo kwa takriban miaka 15 iliyopita; lakini Serikali ikawa inang'ang'ania kwamba mikataba hiyo iko sawa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka yote hiyo niliyotaja, ilikuwa ikiitaka Serikali kuleta mikataba yote inayohusu rasilimali za nchi yetu ambayo Serikali inaingia na wawekezaji ili ijadiliwe na kuridhiwa na Bunge, lakini mara zote Serikali ilikataa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali haipaswi kujisifu wala kujinasibu kwamba ni ya kizalendo zaidi kwa kuleta muswada huu wa kupitia mikataba yenye masharti hasi sasa; kwa kuwa si jambo jipya. Inatekeleza ushauri uliotolewa na Kambi Rasmi

ya Upinzani uliotolewa takriban miaka 15 iliyopita. Hata hivyo Serikali imeanza vibaya kutekeleza ushauri huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Serikali imeshagutuka kwamba; Taifa lilikuwa linanyonywa kutokana na mikataba mibovu iliyotokana na sheria dhaifu zilizopitishwa kishabiki na kwa harakaharaka; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea kwamba; safari hii Serikali ingetulia na kuandaa muswada wa sheria kwa umakini na kuwashirikisha wadau wote na kwa muda unaotosha; ili kuziba mianya yote ya kinyonyaji iliyokuwepo kutokana na uharakaharaka katika utungaji wa sheria husika.

**Mheshimiwa Spika**, kinyume na matarajio hayo; Serikali inarudia makosa yaleyale ambayo yaliisababishia nchi hasara; tunataka tuyarekebishe leo kwa kutumia njia zile zile na akili zilezile. Hatuwezi kupata matokeo tofauti kwa kufanya hivyo!!!!!! *“We can’t solve problems by using the same kind of thinking we used when we created them (Albert Einstein)*. Kwa maneno ya mwanafalsafa huyu, ni kwamba kuna haja ya Serikali kubadili mbinu na mfumo mzima wa kushughulikia jambo hili.

**Mheshimiwa Spika**, itoshe tu kusema kwamba; Serikali inabidi ikiri kwamba ilikosea kuliingiza taifa katika mikataba ya kinyonyaji iliyotokana na sheria dhaifu na hivyo kulisababishia hasara; na kwamba sasa inatakiwa kufanya *retreat* ili kubaini ilipokosea na kujirekebisha. Na ili Serikali ifanikiwe katika *retreat* hiyo, haitakiwi kuwa na pupa wala papara.

## 2. MAONI YA JUMLA KUHUSU MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitoe maoni ya jumla kuhusu Muswada ulioko mezani.

### 2.1. Dibaji (Preamble) ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, tofauti na utaratibu wa kawaida uliozoeleka wa uandishi wa Miswada ya Sheria, Muswada huu una Dibaji, ambayo mwandishi amejitahidi sana kuupamba kwa maneno yanayoashiria utaifa, uzalendo na

nguvu ya wananchi katika kumiliki na kulinda rasilimali za nchi; lakini ikumbukwe kwamba ni Serikali hii hii ya CCM iliyoingia mikataba ya kinyonyaji na wawekezaji, wananchi wakafukuzwa katika maeneo yao tena bila fidia na wengine wakauwawa kwa kupigwa risasi hususan katika maeneo yaliyo karibu na migodi ya madini.

**Mheshimiwa Spika**, maudhui ya dibaji hii, na vitendo halisi wanavyofanyiwa wananchi walio karibu na mali asili za nchi yetu vinafanana kabisa na ile methali inayosema *“utamu wa nanasi, ndani kipande cha mti”* Kama kweli Serikali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho, mbona imewanyima haki na uhuru wao wa kikatiba wa kupata habari kwa kuzuia kurushwa moja kwa moja kwa mijadala ya Bunge lao; na kuwawekea sheria ngumu na kandamizi ya makosa ya kimtandao inayowanyima uhuru wa habari?; Kama kweli Serikali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho; mbona imewanyima haki yao ya kikatiba ya kukusanyika, na kujiunga na vikundi au vyama vya siasa kwa kupiga marufuku mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa?; Kama kweli Seriali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho; mbona inawazuia wananchi wasiuze mazao yao ya kilimo nje ya nchi ili wapate faida?; Kama kweli Serikali hii ina mapenzi na wananchi kwa kiasi hicho, mbona wananchi wanaoishi katika maeneo ya machimbo ya madini wanaendelea kuwa masikini, kunyanyaswa na kuuwawa mpaka leo?

**Mheshimiwa Spika**, yapo mambo mengi mabaya wanayofanyiwa wananchi, na Serikali hii inaona na wala haichukui hatua. Hivyo kuja kuwahadaa wananchi kwamba wao ndio wenye mamlaka kwa kutumia maneno matamu ya utangulizi na wakati kinachofanyika ni kinyume na maneno hayo, haikubaliki.

## 2.2. Matumizi ya Sheria Inayopendekezwa

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya pili ya Muswada wa Sheria inayopendekezwa inasema kwamba; sheria hiyo itatumika Tanzania Bara, bila kuathiri mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar juu ya umiliki na udhibiti wa rasilimali zake za taifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Katiba iliyopo sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; masuala ya mafuta na gesi ni miongoni mwa mambo ya Muungano yaliyoorodheshwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba. Pamoja na takwa hili la kikatiba; Serikali hii ya CCM ikishirikiana wabunge wake; ilitunga sheria ya Gesi na Petrolu ya mwaka 2015 inayoipa Zanzibar mamlaka juu ya mafuta na gesi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi Zanzibar kuwa na mamlaka juu ya rasilimali zake; isipokuwa mihilimili ya Bunge na Serikali iwe makini vya kutosha ili kuepuka kutunga sheria zinazokinzana na Katiba.

### **2.3. Mahakama Kufungwa Mikono katika Kuamua Mashauri Yanayotokana na Sheria Inayopendekezwa.**

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa mapungufu makubwa ya Muswada wa Sheria inayopendekezwa ni kwamba inalenga kuifunga mahakama mikono isiweze kushughulikia shauri la mtu atakayeonewa au kutendewa visivyo na sheria hii. Dibaji ya Sheria hii imefanya rejea ya ibara za 8 na 9 zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ambazo kwa mujibu wa Katiba hiyo, haviwezi kutiliwa nguvu na mahakama yoyote nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya 7(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba: *“Masharti ya sehemu hii (yaani sehemu ya pili ya Katiba) hayatatiliwa nguvu ya kisheria na mahakama yoyote. Mahakama yoyote nchini haitakuwa na uwezo wa kuamua juu ya usuala kama kutenda au kukosa kutenda jambo kwa mtu au mahakama yoyote, au kama sheria au hukumu yoyote inaambatana na masharti ya Sehemu ya Sura hii”*

**Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika**, yale mambo yote mazuri yaliyotajwa kwenye dibaji ya Muswada wa Sheria hii, ikiwa hayatatekelezwa na Serikali au ikiwa Serikali itakwenda



kinyume nayo, au ikiwa mtu ataadhirika kwa namna moja au nyingine wakati wa utekelezaji wa masuala hayo; basi hakuna shauri lolote linaloweza kufunguliwa kwa minajili ya kufanya madai, na wala hakuna mahakama yoyote itakayoweza kushughulikia jambo hilo. Kwa maneno mengine zile ahadi nzuri zinazotelewa na ule utangulizi ni **Cosmetic**, kwa kuwa hakuna haki inayoweza kutolewa ikiwa kuna ukiukwaji wa haki umetokea katika sehemu hiyo.

#### **2.4. Marekebisho ya Sheria Mbalimbali kwa Kuzingatia Maudhui ya Muswada wa Sheria Inayopendekezwa.**

**Mheshimiwa Spika**, Dhana ya “Utajiri na Rasilimali za Asili” ni pana sana, na kwa vyovyote vile haiwezi kuhusishwa na madini au mafuta na gesi peke yake. Kwa mujibu wa tafsiri iliyotolewa na muswada huu, **Rasilimali za Asili** ni vitu vyote vinavyotokea kiasili, kuanzia ardhini, majini na hata angani vyenye thamani ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na upana wa dhana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitegemea kwamba Serikali ingeleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ili sheria zote zinazohusu maliasili na utajiri wa asili zifanyiwe marekebisho ili ziendane na maudhui ya Sheria hii inayopendekezwa. Lakini cha ajabu ni kwamba Serikali imeleta Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali namba 4 ukiwa na marekebisho ya sheria mbili tu zinazohusu utajiri na maliasili za nchi - yaani Sheria ya Madini na Petroli, pamoja na sheria zingine za mapato na kodi. Lakini sheria nyingine zinazohusika katika maeneo ya utajiri na rasilimali za asili kama vile wanyamapori, utalii, ardhi, uvuvi, uhifadhi wa mazingira nk. hazijaletwa kufanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba ili sheria hii inayopendekezwa iwe na tija, ni lazima sheria nyingine zinazohusika na masuala hayo zifanyiwe marekebisho.

## 2.5. Mamlaka ya Bunge katika Kupitia Mikataba

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mikataba ya Rasilimali za Nchi, ukitazama kwa kwa juu juu, inaonekana kama ina nia nzuri; lakini haiweki mfumo madhubuti wa kujadiliana mikataba hiyo. Aidha, Bunge linapewa madaraka pale tu mikataba hiyo inapokuwa imejadiliwa na kuanza kutelezwa bila kuzungumzia mikataba mipya inayojadiliwa. Aidha, sheria haiagizi kuwa mikataba yote iwasilishwe Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kama itakiwavyo na Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inayoagiza kuwa mikataba yote isainiwayo na serikali lazima iwasilishwe na kuridhiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 4 cha Muswada huu kinasema kwamba; Bunge linaweza kupitia upya mikataba ya rasilimali za nchi kuhusu Masharti hasi katika Mikataba inayohusu rasilimali hizo. Hata hivyo, ukisoma kwa makini ni kuwa, bado serikali itakuwa na mamlaka ya kuingia mikataba ya uvunaji wa rasilimali isipokuwa Bunge linaweza kuipitia upya mikataba hiyo baada ya kuingiwa na serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba, Serikali isiingie mkataba wowote unaohusu rasilimali asili za nchi mpaka mikataba hiyo itakapojadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

## 2.6. Haki ya Wananchi Kushirikishwa katika Uamuzi juu ya Rasilimali za Nchi

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu hauna kifungu cha kinachotoa haki kwa wananchi ya kushirikishwa, kuhusishwa na kutaarifiwa kuhusu maamuzi yote yanayohusu utafutaji au uvunaji wa rasilimali za umma. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba licha ya Bunge kuwa na nafasi ya kujadili mikataba hiyo; lakini pia wananchi wa eneo lenye rasilimali hizo washirikishwe kupitia serikali zao za mitaa, vijiji na vitongoji. Aidh, Kamati ya Bunge itakayokuwa inashughulikia masuala hayo, ikusanye maoni kutoka kwa wananchi hao, ili maoni hayo yalisaidie Bunge katika kufanya mapitio ya Mikataba hiyo.

## 2.7. Ukosefu wa Vyombo au Taasisi za Kufanya Majadiliano ya Mitakaba Hasi.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada hauzungumzii au hauundi chombo au taasisi yoyote ile ya serikali ambayo itahusika na mazungumzo ya mikataba hasi. Huu ni usahaulifu wa ajabu na kwa kweli ni kutokana na kuandikwa kwa miswada hii kwa haraka. Ili kuweza kuwa na majadiliano mazuri ni lazima kuwepo kwa Timu Bobezi ya Kitaalamu kuweza kujadiliana na Kampuni za uwekezaji katika maliasili za nchi yetu. Hivyo Muswada huu lazima uwe na kifungu kinachounda Timu Bobezi ambayo inajumuisha watu wa kada mbalimbali wakiwemo wanauchumi, wanasheria, watoza kodi, wahasibu, wanajiolojia, wanamazingira, walandisi, wanasayansi (ikiwemo wanahisabati, wafizikia na wakemia), watakwimu na wataalamu wa TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba; wataalamu watakaoiunda Timu hii wawe watu ambao ni wabobezi na ambao mapenzi yao kwa nchi yetu hayatiliwi mashaka. Watoke ndani na nje ya serikali na pale ambapo mtaalamu wa kada fulani hayupo nchini basi atafutwe kutoka nje. Mfumo huu umetumiwa kwa mafanikio makubwa na Kamati ya Madini ya Botswana.

## 2.8. Kutokuwepo kwa Vifungu vya Adhabu:

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unalipa Bunge madaraka ya kutoa maazimio juu ya mikataba yenye mashariti hasi; lakini hausemi ni adhabu ipi Bunge litatoa kwa Kiongozi au Ofisa wa Serikali anayekiuka azimio la Bunge. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa sheria itamke kwa uwazi kabisa kuwa Waziri au Mtendaji yeyote yule wa serikali anayeshindwa kutekeleza azimio la Bunge anatenda kosa la jinai na adhabu yake ni kushitakiwa mahakamani kwa kosa hilo licha ya adhabu ya kinidhamu.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya Sheria kutoa fursa ya majadiliano ya upitiaji wa masharti hasi sheria inaonekana kuwa kandamizi kwani inalazimisha matokeo ya majadiliano. Ni

rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa pale kunapotokea kutokuelewana basi suala hili lipelekwe Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara. Aidha, sheria isifunge orodha ya vifungu vya mashariti hasi na itoe nafasi kuwa jambo lolote lile ambalo kutokana na mabadiliko ya sheria au mazingira ya utendaji basi sharti hasi linapojitokeza nalo liweze kuchagiza majadiliano mapya.

### 3. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusisitiza kwamba nchi yetu inaangamia kutokana na mifumo mibovu ya kiutawala. Mifumo yetu ingekuwa thabiti kusingekuwa na tabia hii ya kuleta miswada ya sheria kwa hati ya dharura hata kwa mambo yasiyo ya dharura. Hati za dharura hutolewa iwapo kweli kuna jambo la dharura kwa mfano nchi iko vitani; au kuna hali ya hatari katika nchi au kuna mlipuko wa gonjwa hatari nk.

**Mheshimiwa Spika**, ungekuja Muswada wa Sheria ya kudhibiti mambo yanayoendelea huko Rufiji na Kibiti kwa hati ya dharura tusingeshangaa na tungeunga mkono; lakini kuleta miswada ya sheria ya mambo makubwa yanayohusu utajiri na rasilimali za nchi hati za dharura ni matumizi mabaya ya hati hizo; na Mheshimiwa Spika, Kambi Rasi ya Upinzani Bungeni inakutegemea upige marufuku tabia hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Nimesisitiza kwamba; ili taifa hili liondoke katika shimo la uharibifu, ni lazima kuanzia sasa tuamini katika mifumo ya kitaasisi kuliko kuamini katika mtu au watu. Ukiangalia miswada ya sheria iliyoletwa mbele ya Bunge lako utagundua kwamba kinachotafutwa ni utukufu wa mtu (Glorification of a person) na sio utukufu wa taasisi. Hii ni hatari kubwa sana kwa kuwa, mtu huyo anayetafutiwa utukufu katika sheria hizi ikiwa hayupo, na akitokea mwingine ambaye hapendi utukufu huo; maana yake ni kwamba; sheria hizi zitakuwa *redundant* na nchi itaparaganyika kwa kuwa, kutakuwa hakuna mifumo ya kitaasisi iliyojengwa kusimamia nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha

John Wegesa Heche (Mb)

**KNY: MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI, KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

3 Julai, 2017

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uwasilishaji. Ninayo majina hapa ya uchangiaji kwa kadri ya uwiano tulionao. Nina majina machache, kulingana na muda yataitwa siyo kwa uwiano lakini kwa sababu wapo Wabunge ambao Vyama vyao haviwezi kupata nafasi kama hatutawapa hiyo fursa. Tutaanza na Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Adamson Mwakasaka na Mheshimiwa John John Mnyika, ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niwe wa kwanza kuchangia katika Miswada hii miwili. La kwanza, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuja na Miswada hii miwili. Miswada hii ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tulikuwa tuna sheria nyingi zinazotambua rasilimali zetu za Taifa, lakini hizi zilikuwa hazijaunganishwa. Kulikuwa na Sheria za Ardhi, kuna Sheria za misitu na sheria nyingi tu; lakini sasa Serikali imeamua kuja na Miswada ambayo tunazitambua kwa pamoja maliasili zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili ambazo tunazitungumzia sasa hapa, hatuzungumzii tu madini, tunazungumzia udongo wote wa kila namna, tunazungumzia hewa, tunazungumzia maji, tunazungumzia milima yote, maziwa yote tuliyonayo, tunazungumzia viumbe vyote vyenye uhai na visivyokuwa na uhai, tunazungumzia kila kitu ambacho kiko katika nchi yetu. Tulikuwa hatuna sheria moja

ambayo inatambua maliasili zote hizo ili tuweze kuzilinda kwa pamoja, sheria hii sasa imekuja kutambua vyote kwa pamoja. Hii ni hatua nzuri sana na tutapiga kasi sana katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii Sheria ya Maliasili zetu hizi, imeweka misingi mizuri sana ambayo sasa sheria nyingine zinazohusu maeneo mbalimbali zitakuwa zinatungwa kwa kuzingatia hii Sheria muhimu. Nami niseme nawashukuru hata Wapinzani, ukiangalia hotuba yao, wanakubaliana na hizi sheria. Wanachobaki kusema, ni kwamba muda hautoshi, tumekimbia haraka; lakini wanakubaliana kwamba kuna matatizo ambayo lazima yawe *addressed*. Sasa hatuwezi kusubiri kwamba tuwe na muda wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeibiwa vya kutosha, maliasili zimepotea kwa muda mrefu, hatuwezi. Lazima wakati huu tunaanzia hapa, kama kutakuwa na upungufu tutaendelea kushughulikia kadri muda unavyoendelea. Leo hii tuseme tunasubiti eti tuwe na muda muafaka, muda muafaka upi? Huu ndiyo muda muafaka sasa wa kushughulikia rasilimali za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imeweka utaratibu mzuri sana katika kila namna. Kwanza wanasema, labda nizungumzie kwenye Sheria hii ya Madini. Wanasema, Serikali sasa itahakikisha kwamba inasimamia utafiti. Utafiti huu utatuwezesha kujua kwamba maliasili tulizonazo zina thamani ya kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba labda hapa nieleze kidogo, watu wengi wanafikiri uwekezaji kwenye madini, uwekezaji kwenye hizi rasilimali ni sawasawa na uwekezaji mwingine. Kuna utafauti mkubwa. Kwenye hii sekta tunachosema, Serikali ikiwekeza ikafanya utafiti inakwambia kwenye eneo lako hapa kuna utajiri wa kiasi fulani. Sasa ukishajua utajiri ulionao ndiyo anza kutafuta utaratibu sasa wa kuanza ku-*extract* kutoka kwenye hiyo mali uliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zilizokuwepo zilikuwa hazina utaratibu mzuri. Mali ni zetu kila kitu ni chetu, eti kwa sababu mtu ana mtaji, ana vifaa vya kuchimba, anakuja anachukua mali zote, sisi tunabaki hatuna kitu. Kwa hiyo, sheria hii sasa inaweka utaratibu, inasema anayetaka kuja kuwekeza, tukishajua mali zetu ziko hivi, ndiyo maana tunasema sasa tunaanza kumiliki asilimia angalau kwanza 16; tunaanzia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hiyo 16 ni ndogo, kwa sababu kama haya madini ni yetu, huyu mtu anakuja tu na mtaji kuchimba, utampaje zaidi? Tunachochimba kinatakiwa kwanza kiukweli kabisa tugawane nusu kwa nusu. Wewe njoo na mtaji, mimi nina mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunachosema sasa, ukiangalia utaratibu huu ni kwamba hisa lazima ziwekwe kwetu, zitambuliwe na sisi tuwe nazo; utaratibu huu umetumika na nchi nyingi. Tumeona Ivory Coast wamefanya, wanamiliki *free hold* wanazo pale Ivory Coast; lakini tumeona pia Niger wanazo. Tunaona nchi nyingi wanao huu utaratibu wa namna hii na Afrika Kusini nao walipitia mikataba yao. Kwa hiyo, tunasema na sisi katika utaratibu huu tulionao, lazima na sisi sasa mali zetu tufaidike, ndio maana tunasema lazima wananchi tumiliki sasa, tutakuwa na hisa na tutakuwa tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Sheria inaweka utaratibu mzuri sana. Inasema sasa wananchi wote tutakuwa tunamiliki hisa kwenye hii makampuni na hisa zetu hizi kwa kuanzia zitakuwa zinasimamiwa na Serikali kupitia Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, aliyechaguliwa na wananchi wote. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kwa kura nyingi.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alichaguliwa na wananchi ndiyo maana tunampa

mamlaka kwamba hebu simamia kwa niaba yetu. Tutaendelea kuweka utaratibu mzuri na kuendelea kuitumia hiyo maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inaweka utaratibu mzuri sana; na ni Serikali ya Awamu ya Tano imeona hilo; nashangaa kama kuna mtu anaipinga. Wajibu, ukiangalia kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu kuna Serikali, kuna Bunge na kuna Mahakama. Kila chombo kina kazi yake. Serikali ya Awamu ya Tano inasema hivi, pamoja na kwamba ni wajibu wa Serikali kuingia kwenye mikataba, lakini pia mhimili wa Bunge upate nafasi pale unapooni ni muhimu upitie hiyo mikataba; hii sheria imeweka utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sheria hizi sasa, baadhi ya mikataba tukiihitaji tutakuwa tunapata, tunapitia, tunaishauri Serikali, tunaielekeza maeneo ya kwenda kurekebisha. Sasa hatukuwa na sheria kama hiyo, Sheria hii imekuja na ni Awamu ya Tano imeweka huo utaratibu, ambao ni utaratibu mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imeweka utaratibu kwamba kwenye mikataba inayohusu mali zetu, tunapoingia kwenye migogoro ya kutokuelewana na mwekezaji, basi Mahakama za kwetu za humu ndani kama mhimili mwingine, ndiyo utumike katika kutatua hii migogoro. Kwa nini tuchukue fedha nyingi; mabilioni ya mapesa tunaenda kupeleka nje kwenye mali ambazo ni za kwetu? Kwa hiyo, sheria hii imekataa na imesema kwamba sasa tutakuwa tunamaliza humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nitashangaa sana kama mtu mwenye akili timamu, mtu yoyote mwenye nia njema na maendeleo ya nchi hii, atakuwa anasema eti hapana, kukiwa na migogoro tupeleke huko. Huko wapi? Nadhani utaratibu uliwekwa sasa hivi ni utaratibu mzuri sana ambao unatupa madaraka ya kuweza kufanya vizuri na kuweza kuiendeleza nchi yetu na kupata faida kubwa inayotokana na rasilimali za nchi yetu.



Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hapa, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, hizi sheria ni nzuri. Hizi sheria tunaziwekea sasa msingi. Hakuna sheria ambayo inaweza ikawa *hundred percent perfect*; baadaye kama kuna upungufu tutaita tena, lakini lazima tuwe na mahali pa kuanzia. Kwa hali tuliyonayo ambayo tunataka hapa kazi na lazima tukimbie, hii ndiyo sheria tuliyokuwa tunaisubiri kwa muda mrefu. Naipongeza sana Serikali kwa kuja na hii sheria na nawaomba kila mtu aiunge mkono ili angalau tupate maendeleo ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi sheria pia zimeweka utaratibu mzuri, kwamba katika maeneo yale ambayo yatakuwa na wawekezaji, iwe sasa ni lazima kwa wawekezaji kuingia ile tunaita *cooperate social responsibility*, iwe ni wajibu wa kampuni, wakae na wananchi wa eneo lile waone ni maeneo gani wanatakiwa kupata huo msaada. Zamani ilikuwa ni hiyari, sasa siyo hiyari kwa mujibu wa sheria hii, itakuwa ni lazima sasa wananchi wanufaike na rasilimali zilizopo katika maeneo haya. Kwa hiyo, nadhani huu ni utaratibu mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wenzangu hasa ambao wako upande wa pili wale wanaoanza kudai *TV Live*, tumedai sijui kilimo, huu siyo wakati wake. Hatuzungumzii kilimo wala *TV Live* leo, tunachozungumzia hapa ni rasilimali za Taifa hili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia Sheria...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja za Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Adamson Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa John John Mnyika na Mheshimiwa Godbles Lema ajiandae.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia hili jambo muhimu sana kwa maslahi ya nchi yetu, kwa kuletwa marekebisho haya ya sheria mpya ya *The Natural Wealth and Resources Act of 2017*. Naipongeza sana Serikali kwa kutuletea huu Muswada mpya tuweze kuupitia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu vifungu vichache tu kwa jinsi vilivyo. Tumekuwa kweli tukiibiwa sana na nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo na kuliwekea mkakati ambao kama nchi ni lazima tunatakiwa tuwe pamoja kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu kwa ujumla. Ite Sheria yetu Na. 10 ilikuwa haina vitu vingi ambavyo sasa vimeletwa kwenye hii sheria mpya. Kwa mfano, Waziri sasa ambaye alikuwa ndiye Waziri wa Nishati na Madini amepunguziwa madaraka mengi, yamepelekwa kwenye *Commission*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Commission* ile ina watu mbalimbali ambao wana utaalum mwingi lakini *Commission* hii imewekwa ili kuondoa ule upungufu ambao ulikuwepo kwenye sheria ya kwanza na sasa zile *discretionary powers* za Waziri alizokuwa nazo zimepelekwa kwenye *Commission* ambapo sasa *Commission* hii itakuwa na uwezo wa kufikiria kutoa leseni na hata kuifuta leseni ya madini kitu ambacho hakikuwepo mwanzoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na mikataba ambayo kwa mfano, hawa wenzetu wawekezaji walikuwa wakishaingia mikataba, huwezi kubadilisha chochote hapa katikati mpaka mkataba utakapoisha hasa kwenye masuala ya kodi, lakini sasa kuna vipengele vya kuweza ku-review mikataba hiyo, kitu ambacho kitaisaidia sana nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kifungu namba 10 (1) na (2), pale kuna masuala ya pesa ambazo zinatakiwa kuhifadhiwa na hawa wawekezaji. Pesa nyingi walikuwa wanapeleka nje, lakini sasa sheria hii mpya inawataka wawekezaji wote kwamba sasa pesa zao, isipokuwa *dividend* waweke hapa nchini. Sasa kwa kuweka pesa nchini, pesa hizi zikiwa kwenye mabenki yetu zitasaidia hata mzunguko wa kifedha wa nchi katika mabenki yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasikiliza kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani walikuwa wanaongea kwamba usimamizi wa Serikali unatakiwa uwe mbali katika masuala ya madini. Nasikitika sana kwa usemi huo, sikuutegemea kabisa! Wakati nchi imeingia kwenye matatizo makubwa, *Hansard* ipo, usimamizi wa *Government* uwe mbali.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa! Tumefika hapa tulipo kwa sababu na kutokuwa na *close supervision*; tulikuwa hatuna, kiasi ambacho tumeibiwa sana. Sasa Serikali inabana, wenzetu wanasema Serikali isiwe moja kwa moja. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, la pili...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, kwa muda tulionao na kwa idadi ya watu hapa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huwa mnakumbushwa siku zote, kwa nini hamjifunzi kwa Kiongozi

wa Upinzani Bungeni na ndiyo kiongozi wenu? Kwa nini hamjifunzi kutoka kwake? Mkiambiwa msikilize, mnazomea, kwa sababu zipi za msingi? Kwa sababu zipi mnazomea? Nasema hivi, taarifa sitapokea, nitapokea kuhusu utaratibu. Mheshimiwa Adam Mwakasaka endelea.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri *Hansard* zipo nirudi kwenye hizo taarifa walizozisoma...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, naomba ukae, kuhusu utaratibu, Kanuni ipi imevunjwa?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu Kanuni ya 64(1) Mbunge hatatoa Bungeni maneno ya uongo. Anachozungumza Mheshimiwa Mwakasaka hatuja-*surface* popote kwenye hotuba zetu kwamba Serikali isisimamie, wala hakipo popote mtu yeyote amezungumza. Sisi miaka yote tumekuwa tunapigania Serikali iwe makini na rasilimali za nchi hii. Kwa hiyo, naomba umwombe afute hiyo kauli, asipotoshe wananchi kwa makusudi au athibitisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, hayo maneno umeyasikia kwenye taarifa za leo ama yako wapi?

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kwamba nimesikia na *Hansard* zipo. Lipo la pili, wameongelea hii *certificate* kuletwa *under emergence* kwamba nchi haiko kwenye vita, imeongelewa hapo pia. Vita gani wanaitaka wao? Hapa tupo kwenye vita kubwa ya kuokoa rasilimali zetu za nchi. Wao wanaposema kwamba nchi haiko kwenye vita, wanaongelea vita gani? (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, tumalize moja kwanza. Hili la vita hata mimi nimelisikia, hilo sidhani kama wao watabisha. Ila hilo la kwanza ndilo ambalo walisimama hapa kuomba utaratibu. Kama huna uhakika sana na wapi liko, lifute ili uendelee na hilo lingine la vita.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba nifute hilo, labda nitakuwa nimei-*misheard* lakini ninaomba pia *Hansard* zirejewe kwa sababu nilikuwa nimelisikia, ila nafuta ili niweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hili la pili la kwamba nchi hii haiko kwenye vita, kwa hiyo, hii *certificate of emergence* haikutakiwa kuletwa hapa Bungeni. Hiki siyo kweli kwa sababu suala hili la sisi kuibiwa hizi rasilimali zetu siyo tu kwamba sisi tumetikisika, hata wenzetu waliotuhumiwa tuliona wamekuja hapa kwa sababu ilikuwa ni suala ambalo limegusa wengi. Linagusa kodi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashangaa wenzetu wakisema wao wanataka *certificate of emergence* zije wakati kuna vita. Vita gani zaidi ya hii ambayo tunapigania uchumi wetu? Kwa hiyo, wasiendelee kuwadanganya wananchi kwa vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala hili la Kifungu Na. 12; kuna suala la wao wenzetu kulazimisha kwamba tuweke neno "*shall*" badala ya "*may*" kwenye suala la Bunge kupitia hii mikataba. Ninavyofahamu ni kwamba Bunge kazi yake kubwa ni kuishauri Serikali. Sasa Bunge likiwa lenyewe ni *part of decisions*, sijui litaishauri vipi Serikali wakati na Bunge lenyewe lilishiriki kwenye kutoa maamuzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutakubaliana na wao ina maana kwamba Bunge sasa litakuwa halina nguvu kuja ku-*review* mambo ambayo na lenyewe lilikuwa miongoni mwa kujadili. Kwa hiyo, nadhani ibaki vile vile kama ilivyo.

Hili neno " *may*" libaki kwa sababu kisheria linatoa muda wa Bunge kujiridhisha halafu ndiyo kuitisha ku-*review*; siyo kila kitu kiwe *reviewed* na Bunge halikutani kila mara na ndiyo maana vyombo vingine vimepewa mamlaka kuweza kushughulikia vitu ambavyo haviwezi kuletwa Bungeni kila mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hiki Kifungu Na. 11 kuhusiana na hizi kesi ambazo kukitokea *dispute* yoyote na hawa wawekezaji kwamba kesi hizi zierendeshwe ndani ya Mahakama zetu. Naunga mkono kifungu hiki kwa sababu kwanza sisi tuna *Prominent Lawyers* wengi tu, nchini kwetu. Siyo lazima kila kesi, kuna mgogoro kidogo tu uende nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *International Court of Arbitration*, kwanza ni kesi chache sana zinazokwenda kule. Pia kwa nini tuzidharau Mahakama zetu ambazo zina uwezo mkubwa sana wa kisheria? Kwa hiyo, napenda kifungu hiki kibaki ili pia kuzipa hadhi Mahakama zetu. Tunao Majaji, tunao Wanasheria ambao wanakwenda kuhudhuria kesi nyingine nje ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunao Majaji, tunao Mahakimu wazuri sana nchini mwetu ambao wanaweza wakashughulikia kesi hizi mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba nchi ni kweli kwa sasa hivi ilikuwa inazihitaji sana hizi sheria zilizoletwa hapa kwa sababu ya hali halisi ambayo ipo nchini kwetu na kwamba wananchi wasidanganywe na wenzetu kwamba kila siku Serikali ya CCM ndiyo imekuwa ikileta hizi *certificate of emergence* hapa. Labda niwakumbushe kwamba hata huko kwao, leo kuna viongozi ambao walishiriki kwenye maamuzi haya, huku nyuma, wako kwao leo ambao leo wao wanawaona wa maana. Sasa wasiwachanganye wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, naomba kusema, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa John John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Asubuhi ulianza kutuongoza na Dua; Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba Mbingu na Dunia, umeweka katika Dunia Serikali za wanadamu na Mabunge ya Mataifa ili haki yako itendeke. Ni kwa bahati mbaya sana tunasali tunataja jina la Mungu kwamba haki itendeke lakini haki haitendeke kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunalitaja jina la Mungu, huku haki haitendeke, maana yake tunalitaja bure jina la Mungu na tunatenda dhambi. Siku chache zilizopita tumetoka kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Mwezi wa toba, lakini badala ya kutubu, mnarudia makosa yale yale ya kulitaja bure jina la Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ameiumba nchi hii ikiwa na rasilimali nyingi sana. Ukiitazama ile nembo ya Taifa pale, unaweza kuona rasilimali moja baada ya nyingine zikiwakilishwa na rangi mbalimbali na kauli mbiu ya Taifa letu ikiwa ni Uhuru na Umoja lakini bahati mbaya wenzetu ninyi wa CCM, hamna uhuru kwenye Chama chenu na matokeo yake mmesababisha Bunge halina umoja kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhambi hii ya kulitaja bure jina la Mungu maana yake ni kwamba ni wazi inaambatana na matumizi mabaya ya rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu amejalia Taifa letu. Kwa bahati mbaya, badala ya kurekebisha hali hiyo kwa kuleta sheria bora na kufikiria kwa muda mrefu tukae tuzijadili kwa umakini, mmeamua kutenda dhambi ile ile ya kuleta Miswada kwa Hati ya Dharura; miwili ijadiliwe kwa siku moja na matokeo yake hatutafanya kazi ya maana inayotajwa kwenye sala hii. Hii ni dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ulituambia tukipita hapa, tuwe tunainama, maana mjadala huu umeibuka kutokana na *report* ya Rais ya masuala ya Makinikia kuhusu dhahabu na pale kuna siwa inayofanana kidogo na dhahabu, lakini siyo dhahabu, kwa maneno mengine inawezekana ni sehemu ya makinikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya mjadala tullonao, ilipaswa kabla hatujajadili Miswada hii, Bunge liletewe *report* zote mbili za Rais juu ya makinikia tuzijadili kwa kina, tuielekeze Serikali ikafanye nini, Serikali ndiyo ilete Miswada inayofikiri miaka 50 ijayo, inayofikiri miaka 500 ijayo inayofikiri mbele sana juu ya mustakabali wa Taifa letu, lakini ninyi mmeleta Muswada wa kufikiria miaka mitano tu ya kuelekea uchaguzi. Kuna mtu aliwahi kusema, *Politicians think about election; Leaders, think about generation*. Ni bahati mbaya sana Mheshimiwa Rais ameamua kuwa mwanasiasa badala ya kiongozi, anafikiria uchaguzi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, kuhusu utaratibu. Kanuni iliyovunjwa!

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64 (1) kanuni (d) na (g). Naomba utaratibu unaotumika ndani ya Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge yoyote kwanza anapotaja jina la Mheshimiwa Rais, hatakiwi kulitaja kwa dhihaka katika mjadala kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mfumo anaoenda nao Mheshimiwa Mnyika ni mfumo ambao unavunja kabisa kanuni hiyo niliyoisema; lakini hatatumia maneno ya kuudhi



na ya kudhalilisha watu wengine. Ameanza kwa kusema hapa maneno kwa mfano, anasema Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na Chama chao katika kuleta Muswada huu Bungeni, wamekiuka uhuru, wanaendeshwa bila uhuru ndani ya Chama kitu ambacho siyo kweli. Naye sio mwanachama wa Chama cha Mapinduzi; na anaelewa kabisa mfumo wa kikanuni.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema hapa Sehemu ya Nane ya kanuni zetu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambazo zilileta Muswada huu ndani na Muswada huu ilifuata matakwa yote ya kikanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza maneno ya kumdhalilisha Rais ayafute, lakini pili aendelee kuchangia humu ndani ya Bunge akiwa anachangia kwa kuthamini uwepo na utu wa Wabunge wengine na ajikite kwenye hoja zake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya mambo tunayazungumza kila wakati, lakini inabidi kuyarudia ili tuweze kwenda vizuri. Umeombwa utaratibu kuhusu kanuni ya 64 na nimetajiwa fasili ya (1)(d) na (g). Nianze na (g); matumizi ya lugha ya kuudhi na kudhalilisha watu wengine, nadhani hilo lizingatiwe, kwa kuwa humu ndani tunafanya mjadala kwa kuheshimiana. Yale mambo tusiyoyajua, ya nyumba nyingine tuyaache, tushughulike na yale ya nyumba zetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika, uhuru wa Wabunge wa CCM wanaojua ni wao kama wanao ama hawana. Nina uhakika pia, Wabunge wa Vyama vya Upinzani wao ndio wanaojua kama vyama vyao vinawapa uhuru ama haviwapi. Kwa hiyo, hayo naomba yasijitokeze hapa ili yasitupotezee muda wa mjadala. Tujadili hoja iliyoko mezani, kila mtu ameingia humu ndani kupitia tiketi ya chama alichona kinafaa.

Kwenye fasili ya (1)(d); kuhusu matumizi ya jina la Rais kwa dhihaka, Mheshimiwa Mnyika na pia kwa Wabunge wote, Mheshimiwa Rais pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, maana yake...

Mheshimiwa Bwege, tafadhali! Mheshimiwa Bwege tafadhali, Mheshimiwa Bwege mara ya mwisho hiyo, unaitwa!

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunapozungumza mambo, tufuate utaratibu ambao uko kikatiba. Kama Katiba inamtambua Rais kwamba atapitia chama fulani kuomba kura, basi tujue yeye ni mwanasiasa wa chama hicho. Kwa kuwa amepigiwa kura na nchi nzima, ni Rais wa watu wote hata ambao hawakumpigia kura, yeye ndiye aliyepata kwa wingi, kwa hiyo ni kiongozi wa namna hiyo. (*Makofi/Vigelegele*)

Nimesema kila chama kiangalie ya ndani kwake kwa sababu Katiba ya CCM inasema Rais atakuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hayo tuwaachie wa Chama cha Mapinduzi tuendelee na yaliyopo mbele yetu hapa Bungeni sasa.

Mheshimiwa Mnyika na Wabunge wengine mtakaoendelea kuchangia, tafadhali tuzingatie Kanuni, muda wetu hautatutosha kuzungumza kwa wale wote ambao wamepanga hapa kuchangia ili kuboresha hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Juu ya Muswada wa Sheria ya kuhusiana na Umiliki wa Maliasili, nitaomba muda wangu ambao umeuchukua, ulindwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, mimi naruhusiwa kuzungumza muda wowote; na hata nikisimama hapa, bado

nitazungumza. Kwa hiyo, wewe endelea kuchangia, achana na hayo mambo. Tulishayazungumza wiki iliyopita alipokuwa amesimama Mheshimiwa Gekul, sasa msitake turudie jambo moja kila wakati. Wewe endelea na hoja, Makatibu wako, Mezani wanafanya kazi yao.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Sheria hii imetoa mamlaka makubwa sana kwa Rais kuhusiana na masuala ya umiliki wa rasilimali za nchi. Sheria hii imedhihirisha ni kwa nini sisi Wapinzani na wananchi tulioungana pamoja kutaka rasimu ya Warioba ili kupunguza mamlaka ya Rais kwenye masuala mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia...

**MBUNGE FULANI:** Kwa sababu hamna Serikali!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga kanuni iliyovunjwa.

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 149 na vipengele vyake, mavazi yasiyoruhusiwa Bungeni. Mheshimiwa Mnyika amevaa nguo za *traffic* ambayo hairuhusiwi Bungeni. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane!

Mheshimiwa Mlinga ameleta hoja kwamba Kanuni ya 149 Mheshimiwa Mnyika ameivunja kwa sababu fasili ya (3) inazungumzia mavazi ambayo wanapaswa kuvaa wanaume. Sasa ukiipitia hii Kanuni, fasili ya (1) inasema:-

*“Suti ya kiafrika au safari ya mikono mirefu au mifupi yenye ukosi au shingo ya mviringo na yenye fulana au bila fulana ndani, ya rangi moja, isiyokuwa na nakshi, pamoja au bila baragashia.”*

Kwa hiyo, Kanuni yetu pamoja na kwamba ukiisoma yote kwa pamoja inakataza mavazi ya kung’aa lakini Mheshimiwa Mnyika amevaa suti kwa mujibu wa hii fasili tuliyonayo hapa. Mheshimiwa Mnyika endelea. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ukiangalia ile Nembo ya Taifa kuna rasilimali yetu mojawapo, zile pembe za ndovu zina rangi nyeupe. Ndiyo maana nasema ninyi, samahani sana, kuna miongoni mwenu mnaabudu miungu badala ya Mungu. Mimi nawashauri mtubu, msafishike muwe weupe kama theluji. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa nimezuia, huu ni muda anaochangia Mheshimiwa Mnyika, hayo anayochangia ndiyo aliyoona yanafaa. Kwa hiyo, muacheni Mheshimiwa Mnyika amalizie muda wake. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

Kuhusu Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti katika Mikataba ya Maliasili kwa nchi ya mwaka 2017, sisi tumedai mikataba mara nyingi sana, tumedai mikataba muda mrefu sana. Sasa mmeleta sheria ya kuleta mikataba lakini sheria hiyo mmeleta kwanza mmetumia neno “may” kwa maana ni hiari lakini pili mnaileta mikataba siyo kwa majadiliano kwa mapitio ya moja kwa moja kwa sababu mikataba hii hamjaweka kifungu chenye

kuonesha kwamba Bunge linapaswa kuiridhia mikataba hiyo. Kwa maneno mengine kifungu hiki kitafanya mambo yawe yale yale kama ya miaka 50 iliyopita na Taifa litakuwa pale pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwaka 2008 kwenye Maazimio ya Bunge kuhusu *Richmond* kulikuwa na Azimio ambalo lilisema bayana toka mwaka 2008 kwamba kuanzia mwaka 2008 Kamati za Bunge za Kisekta na hili nililikumbushia wakati wa mjadala wa *Escrow* nilileta mapendekezo ya marekebisho, Kamati za Bunge za Kisekta ziwe zinapewa mikataba na Serikali kabla ya Serikali kwenda kuridhia mikataba husika. Hata hivyo, kwenye marekebisho ya sheria hii hamjaleta kifungu cha namna hiyo na kwa bahati mbaya mmetubana tusilete marekebisho, mmekataa marekebisho yetu asubuhi tulivyoyaleta, kwa hiyo mmeamua kabisa kutunga sheria hovy hovy. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Marekebisho yapo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yameletwa machache, mengi yamekataliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ya namna hii, namkumbuka Mzee wangu Dkt. Emmanuel Makaidi, kabla hajafariki tarehe 30 Machi, 2014 tukiwa kwenye Bunge la Katiba alinikabidhi *Emma's Encyclopedia Tanzania of National Records*, aliweka *records* za toka mwaka 1497 mpaka mwaka 1995; za miaka 498 ambazo nyingine zimegusa masuala ya rasilimali nchi yetu inaelekea wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Viongozi, kati ya mambo ambayo yalitokea katika Taifa letu ni Vita ya Majimaji ya mwaka 1905 mpaka 1907 wananchi wakikataa kuporwa rasilimali zao. Kama ninyi mnasema mmeanzisha vita ya kiuchumi basi ni wakati sasa wa kuwa na Vita ya Majimaji ya kuwaondoa ninyi madarakani. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Siyo rahisi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa sababu katika hali iliyopo Watanzania hawawezi tena kuitegemea CCM hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, Kanuni unazifahamu. Usitake kutumia mgongo wa kuwa humu Bungeni kufanya makosa ambayo unafahamu wazi ni kinyume na Katiba na sheria. Huwezi kuwa wewe unataka kutengeneza mazingira ya kuanzisha vita na wewe unafahamu wazi kwamba wakati wa Vita vya Majimaji kuna watu walikufa. Kwa hiyo, naomba tutoke huko Mheshimiwa Mnyika. Tafadhali tufuate Katiba na sheria.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na vita ya silaha, hii itakuwa ni vita ya kisiasa na kiuchumi, wananchi wakihamasishwa kutumia silaha yao kuu (sanduku la kura) kuiondoa CCM madarakani mwaka 2019 na mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mmeonesha wazi hamtaki kutuletea Katiba Mpya, mmeikataa Rasimu ya Warioba iliyotaka maadili...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Iliyotaka uadilifu, iliyotaka wananchi wanufaike na rasilimali, mmeikataa na hamtaki kuwa na Katiba Mpya...

**MBUNGE FULANI:** CCM Oyeeee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Tutawaiondoa madarakani pamoja...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nani huyo aliyekuwa anazungumza huko?

**WABUNGE FULANI:** Agness, Agness, Agness.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tafadhali sana.

**MBUNGE FULANI:** Apelekwe kwenye Kamati ya Maadili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa maneno ambayo yameandikwa katika Biblia ya Mfalme Nebukadneza ambaye yeye aliamua kuisifu miungu iliyotengenezwa kwa fedha, dhahabu, shaba, chuma, miti na mawe. Miungu ambayo haioni wala haisikii, haijui lolote lakini Mungu ambaye uhai wako uko mkononi mwake na njia zako zi wazi mbele yako hukumheshimu basi Mungu ametuma mkono uandike maandishi haya, maandishi yenyewe ni haya; *“Mene Mene Tekeli Peresi”* na hii ndiyo maana yake. Mene maana yake Mungu amehesabu siku za ufalme wako na kuukomesha. Tekeli maana yake wewe umepimwa katika mizani nawe ukaonekana huna uzito wowote. Peresi maana yake ufalme wako umegawanywa kati ya Wamedi na Waajemi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**WABUNGE FULANI:** Eheeeeeeeeeeee. *(Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Godbless Lema atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Bunge linapokaa kutunga sheria nafikiri ndiyo wakati *sensitive* kwa Wabunge kuliko nyakati nyingine zote katika mijadala ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi na Wabunge wote sisi ni mashahidi kwamba Muswada huu umeletwa kwa Hati ya Dharura sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yetu toka mwanzo ilikuwa ni muda wa kutosha, siyo Wabunge wa Upinzani wa kupitia wala wadau. Ni muda wa Wabunge wote kuwa na *concentration* ya kutosha juu ya mjadala muhimu kama huu ambao unakwenda kutengeneza sheria ya rasilimali za Taifa hili ya watoto wetu, wajukuu na vitukuu. Kwa bahati mbaya sana, pande zote, ushabiki katika masuala ya utungaji wa sheria umekuwa ni muhimu na umekuwa thabiti kuliko umuhimu wa sheria wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili hili tulipitisha Sheria ya *Money Laundering* hapa, kelele zikapigwa hapa ikawa kama wanatungiwa upande mmoja, leo sheria zile zinakula watu wa upande huu kuliko watu wa upande huu. Kwa hiyo, utungaji wa sheria ni *issue sensitive* siyo *issue* ya kishabiki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ukiangalia Ripoti ya Makinikia wakati Mheshimiwa Rais anaipokea ulikuwa ukisikiliza hotuba ya Rais unaelewa kwamba analalamika kwamba uongozi uliopita maana yake ni pamoja na Bunge lilifanya makosa makubwa katika utungaji wa Sheria za Madini. Ukimuangalia Rais alikuwa analalamika anasema, jamani tumelipeleka Taifa mahali pabaya, tumetunga sheria mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama leo tuko *serious* na kubadilisha sheria hizi kwa ajili ya utawala bora wa Taifa hili, ingekuwa ni vyema Chama cha Mapinduzi ambako kuna Wabunge wengi Muswada wa kwanza ambao mngeuleta kwa dharura ungekuwa ni Muswada wa kuondoa kinga ya viongozi wanapokuwa madarakani. Imethibitika kwamba kwa sababu viongozi wengi wana *immunity* hiyo ndiyo imesababisha viongozi wengi kufanya maamuzi yasiyozingatia haki katika Taifa hili. (Makofi)

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji



anayeongea kwanza anajaribu kuzungumza akikiuka Kanuni ya 80(4),(5) na (6) ambayo inaweka utaratibu wa Miswada inayoletwa kwa Hati ya Rais ili itungwe sheria kwa ajili ya kufanya jambo linalopaswa kufanyika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hizi zinaeleza hatua ya Muswada huo kukubalika ili uweze kuja huku Bungeni. Moja kati ya vipengele muhimu ni pale ambapo Hati na Muswada huo utapelekwa kwa Spika na Spika ataitisha Kamati ya Uongozi ya Bunge ambayo ina pande zote za Bunge. Huko ndiko walikoamua Muswada huu uje hapa, huku mnakuja kutuambia kitu gani? Mlikaa huko mkaamua Muswada uje huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wanatumia sasa wajibu wao wa kutunga sheria na ndiyo kazi yao, wanaambiwa hapa wanafanya kazi ambayo haifai na wanalaumiwa. Kwa nini tulaumiwe wakati mlikaa huko Kamati ya Uongozi na Spika na pande zote, Kiongozi wa Upinzani na Kiongozi wa upande wa Serikali mkakubali Muswada uje Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwaje hapa tena turudishwe kwenye zoezi ambalo sio lenyewe? Hapa tulipofika kwa kuwa huko imeshapita sasa tusaidiane tutunge sheria. Bunge hili ndiyo kazi yake kutunga sheria. Sasa ukisema tukitunga sheria leo tumalize kabisa kesho tutafanya kazi gani? Hii sheria tunayoitunga leo tukija hata Bunge lijalo tunaweza tukarekebisha, zikija nyingine tutarekebisha, ndiyo kazi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba niseme, Kanuni hii inakiukwa na ninasikitika kwamba imekuwa kila mmoja anasema, naomba utoe maelekezo juu ya suala hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Simbachawene anatumkumbusha masharti ya kutunga sheria hasa yale yanayohusu Miswada ya Dharura. Wote tunajua utaratibu wakati Miswada hii akiipeleka wenye Kamati alitoa

maelezo ya namna Miswada hii ilivyoletwa na kwamba Kanuni zetu zinataka Mheshimiwa Rais ndiyo amuandikie Spika na alifanya hivyo. Mheshimiwa Spika alipokea akaitisha Kamati ya Uongozi ambayo kama Serikali inavyosema ama Mheshimiwa Simbachawene, ni kweli Kamati ya Uongozi ikiongozwa na Spika kuna uwakilishi wa pande zote.

Waheshimiwa Wabunge, mimi niwasihi tena tufuate Kanuni zetu. Kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge anasimama hapa anasema mabadiliko yamekataliwa wakati mimi niko nayo hapa Mezani haya hapa. Sasa ukisimama ukasema yamekataliwa unataka mimi nisimame kila wakati nikuziue kuzungumza niseme ninayo yako hapa. Sasa hebu tufuate utaratibu tuache haya maneno ambayo hayatusaidii kuboresha hoja iliyoko Mezani kwa sababu lengo letu hapa tulipokaa sasa hivi tunataka kuboresha hoja ya Mheshimiwa Waziri ili tutunge sheria vizuri. Sasa tusipofanya hivyo tutakuwa sisi wenyewe hatujitendei haki, lakini pia wale tunaowawakilisha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo naomba sana tuzingatie Kanuni. Maneno ya kwamba mabadiliko yamekataliwa siyo kweli na kuanzia sasa hivi naomba tafadhali nisisasikie kwa sababu niko nayo hapa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, yapo yaliyokataliwa.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Heche. Nikiwa nazungumza huwezi kuzungumza, ninyi mnasoma hizi Kanuni vipi? Nikiwa mimi nimesimama nazungumza Wabunge mnapaswa kuwa kimya mnanisikiliza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, marekebisho ninayo hapa yale yaliyofuata utaratibu ambao nimeshauleza saa ya kuomba miongozo asubuhi yako hapa, kwa hiyo, hoja hiyo haipo.

Waheshimiwa Wabunge, hii hoja ya kuhusu Hati ya Dharura unaweza ukaichangia kwa namna ya tofauti

uonavyo wewe lakini tuzingatie masharti haya kwamba humu ndani tunavyojadili hatujadili ile Hati ya Dharura kwa sababu Hati ya Dharura hailetwi humu ndani. Kwa mujibu wa Kanuni tulizotunga wenyewe, inapelekwa Kamati ya Uongozi, wakishaamua kule wanatuletea huku. Kwa hiyo, naomba tusipoteze muda tuboreshe hii sheria tunayoitunga leo hapa ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu ambao wametutuma kuwawakilisha humu ndani. Sasa tukiwa tunazungumza mambo ambayo hayahusiani na uboreshaji wa hii sheria sijui tunatunga sheria gani na sisi ndiyo Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tutumie muda wetu vizuri. Naomba tuendelee na naamini tutafuata Kanuni zetu. Mheshimiwa Lema naomba umalize muda wako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Hatutarajii kuwashinda sana humu ndani kwa sasa, lakini wakati wa Mungu ukifika mtashindwa na watu wengine.

**MBUNGE FULANI:** Haupo.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wengine wanataka kuhamishwa Wizara ndiyo maana kila nikisimama wanasimama, kwa sababu wanajua umuhimu wa hizo Wizara. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda hujafahamishwa, hizi hapa zote zimekataliwa na majina yao yako hapa nitakukabidhi baadaye. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, nizungumze tena. Nimezungumza wakati wa Miongozo. Mwongozo ulishatoka namna ya uwasilishaji wa hayo mabadiliko, ni muda gani. Kwa hiyo, kama yametoka nje ya utaratibu hata ukizungumza hapa ndani haitusaidii kwa sababu ninayo ambayo yamepokelewa, kwa nini yapokelewe haya na mengine yakataliwe? Hapa ninayo ya Serikali na ninayo ya Wabunge wa Upinzani. Kwa nini Mheshimiwa Cecilia Paresso ya kwake

yamepokelewa, Mheshimiwa Pendo Peneza ya kwake yamepokelewa, Mheshimiwa Bilago ya kwake yamepokelewa na hayo kwa nini yachaguliwe kukataliwa? Hebu tuendeleeni tumalizieni hoja iliyoko Mezani. Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nilikuwa nasema ulikuwa ukimuangalia Rais wakati akipokea Ripoti ya Makinikia lawama yake na maelekezo aliyotoa baadhi ya watu kuwajibishwa unagundua kwamba kuna makosa yalifanyika katika mfumo wa utawala huko nyuma. Ndiyo nasema pamoja na Muswada huu kuja kwa haraka, Muswada wa kwanza ambao ungepaswa kuletwa kwa haraka ni wa kuondoa kinga ya viongozi wakuu wa nchi wakiwa madarakani ili mambo haya ambayo yamefanyika huko...

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(c), Mbunge anyezungumza anazungumzia jambo ambalo lilishajadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano huu. Mheshimiwa Spika alishaeleza na kuagiza Wabunge wote kwenye Bunge hili kutowachokonoa viongozi wetu wastaafu. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Wewe.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia alieleza. Naomba umkumbushe Mheshimiwa Lema kwa kuwa yeye ni mtoro wa kuja humu Bungeni moja na wengine wote kwamba Mheshimiwa Spika alishatoa maelekezo na kuwaeleza Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya jambo hili. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, naomba uzingatie matakwa ya hiyo Kanuni hiyo ya 64(1)(c).

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa sababu umemuelewa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kutengeneza sheria bila kutafuta *reference* za kusaidia Wabunge kufanya maamuzi. Tunanukuu hotuba za Rais wakati anapokea Ripoti ya Makinikia alivyokuwa anasema huko nyuma tumefanya makosa makubwa na ndiyo maana mmeleta Muswada huu kwa Dharura. Dharura ya Muswada huu ni kwamba makosa yasiendelee kufanyika. Sasa tunajenga hoja kwa kuangalia *reference*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, habari ya *IPTL* ni Wabunge hawa na Simbachawene huyu aliyesema hela sio za Serikali, hela ni za watu binafsi, leo mmekamata watu mmepeleka magereza. Sasa tunapojenga hoja, mkae kimya. Wote sisi ni Watanzania. Humu tunafanya nini? Wote sisi humu ni Watanzania tunaongea kwa manufaa yetu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani mimi nanukuu maneno ya Rais unanyanyuka unasema tusingelee viongozi wa zamani, tumuongee nani? Shetani wa zamani? Tumuongee nani? Mungu wa zamani? Tumuongee nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa sisi tunatawala mngetusema. Sisi hamuwezi kutusema sana kwa sababu hatutawali, ninyi ndiyo mnatawala, tupeni fursa ya kuwarekebisha na hapa ndiyo pa kusemea. Wewe pia unataka Uwaziri, unaweza ukakaa sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye hoja za msingi. Nataka niamini, nataka nifanye *assumption* Rais tuliye naye ni mzalendo, nataka niwe na hiyo *assumption*. Nataka niwe na *assumption* kwamba Rais tuliye naye anapenda watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Magufuli alisema hivi, alikuwa ana-*beep* watu wakapokea. Najiuliza kwa *power* mliyompa Rais ya kusimamia rasilimali za za nchi hii, siku moja anakuja Rais ambaye sio mzalendo kama Magufuli, nataka niamini hivyo, anatokea hata upande huu, inawezekana akatokea hata CHADEMA kwa sababu huku hawako malaika, anaweza akatokea CUF kwa sababu CUF hakuna malaika, akatokea Rais siyo mwaminifu mmempa *power* ya ku-*manage* na kusimamia rasilimali zote na mkawekea Bunge masharti nafuu kuhusu usimamizi huo, Taifa hili litauzwa. Mnapotunga sheria hamtungi sheria kwa kumwangualia Rais aliyeko madarakani, bali mnatunga sheria kwa *assumption* kwamba anaweza akaja Rais ambaye si malaika kama mliye naye na siku moja Taifa hili likaingia mahali pabaya na hili ndilo angalizo tunataka mliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiongea mnafikiri tunawachukia, tunawachukiaje? Ninyi wote nyie tukikaa kantini maneno mnayoongea ni tofauti kabisa na mnavyo-*behave* huku na sijui kwa nini. Kama tungekuwa tunawarekodi ninyi maneno tunayoongea kwenye kantini tunampelekea Magufuli, kwenye Kamati tukitoka nje mnaongea tofauti, lisaidieni Taifa hili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge awamu ya pili, Wabunge wote unaowaona hapa asilimia 70 ni wageni, pengine hamtarudi tena kuwa Wabunge ninyi na kama hamtarudi kuwa Wabunge...

**MHE. SEIF KHAMIS S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Sipokei taarifa Mheshimiwa Seif, napokea Kuhusu Taratibu tu.

**MHE. SEIF KHAMIS S. GULAMALI:** Basi Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote ninyi 70% hapa ni wageni, tunasema hivi

tutunge sheria hata kama siku moja mtoto wako hatakuwa Waziri, hatakuwa Mbunge, hata kama hautarudi Bungeni sheria hizi bado zinaweza zika ku-*protect* hata kama huna-*influence* ama huna *connection* na mtu yeyote. Sisi tukileta mawazo haya ndugu zangu mkubali kwamba *opinion* zetu siyo kwa sababu ya kuwashinda bali ni kwa sababu ya kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapoanza kulalamikia kwamba hii Miswaada inakuja kwa njia ya Dharura na wakati kuna muda, leo makinikia yamezuia Bandari ya Dar es Salaam, Rais ana mamlaka. Ukweli ni kwamba kutokuuamini Taasisi ya Urais siyo jambo la maana hata kidogo, kutokumwamini Rais siyo jambo la maana hata kidogo, lakini kwa mazingira ya mataifa ya Afrika na demokrasia ilivyo Taasisi ya Urais lazima iwekewe *check and balance* ili Taifa hili liweze kwenda salama kwa sababu anaweza akaja mtu, siyo kama huyu malika tuliye naye. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza naunga mkono mambo yote yaliyozungumzwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe wenzangu, nimewasikiliza wachangiaji walionitangulia wamezungumza sana kuhusiana na suala la Hati ya Dharura. Hata hivyo, nataka niwakumbushe tu kwa upendo mkubwa, uchaguzi wa mwaka 2015 Mgombea Urais wa upande wao alipatikana kwa Hati ya Dharura. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeh. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, alipatikana kwa Hati ya Dharura kwa kuwa wao wenyewe walimuona anafaa kwa dharura waliokuwa nayo na Watanzania hawakuwahoji. Kwa hiyo, tunapozungumza suala la dharura mimi nadhani tungeungana mkono kwa sababu hata wao waliiona dharura na kumchukua mtu ambaye hawakufanya *vetting*, hajui mambo ya CHADEMA, hajui chochote wakampa dharura ya Urais. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashangaa Wabunge wenzangu mnalalamika tunawaburuza katika kutunga hizi sheria, wewe ulituletea mtu ambaye unataka tumkabidhi nchi.

**MBUNGE FULANI:** Halafu mgonjwa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Sitaki kusema mgonjwa hayo ni ya kwenu, tumkabidhi nchi halafu hajui chochote kuhusu CHADEMA...*(Kicheko)*

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Hajui chochote kuhusu Serikali.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Utaratibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Kwa vile wao walifanya hivyo mimi nadhani tungeendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara kanuni iliyovunjwa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Kanuni iliyovunjwa ni kwamba hata Mheshimiwa Magufuli alipatikana kwa Hati ya Dharura. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.



**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Bungara watu wote wanamjua humu, inawezekana hajui kama Magufuli alipatikana kwa *procedure* ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunaunga mkono Hati ya Dharura ya Serikali tuweze kupitisha sheria hii ambayo imeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nimesikia wanalalamika sana wanasema tulichelewa kufanya mabadiliko. Nakubali tulichelewa kwa sababu dunia inabadilika na CCM inabadilika, watu waliokuwa wanatuchelewesha wote mmewakumbatia nyie huko. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Serikali hii ilikuwa inaongozwa na Lowassa na Sumaye ndiyo mmewakumbatia kwetu, sisi tulipoona hawafai nyie mmechukua kwa Hati ya Dharura. Kwa hiyo, sasa mtulie tumeamua kufanya mabadiliko kwa Mheshimiwa Majaliwa na kwa Mheshimiwa Magufuli. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia wenzetu wanalalamika kuhusu kufanya mabadiliko ya sheria haraka haraka, hebu niwakumbushe 1992 na ninyi wazee mlioko upande wa pili mliokuwepo 1992 kwenye siasa. Bila mabadiliko yaliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ninyi msingekuwa humu, ingekuwa CCM yote humu. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Kwa hiyo, mabadiliko yanakuja na faida mtulie baadaye tutaona faida ya mabadiliko haya yanayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie sasa kwenye Muswada wenyewe. Marekebisho ya Sheria ya Serikali wanasema wanataka kuwa na *share* asilimia 16. Naomba tu Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atueleze hii asilimia 16 imetuchukua na sisi wachimbaji wadogo ama ni kwa ajili ya makampuni ya kigeni. Mimi sijawahi kuona hata ukienda Dubai, ukienda China Serikali hailingii hisa kwa wazawa inaingia kwa wageni.

Kwa hiyo, muangalie mtakapokuwa mnataka kuingia kwetu wachimbaji wadogo kwa asilimia 16 ni sawa na mnataka kutufuta wachimbe wachimbaji wakubwa peke yake. Kwa hiyo, ushauri wangu nadhani hii sheria tutunge lakini kwa wawekezaji wageni, lakini sio wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusiana na ile kodi ya asilimia sita. Naomba sana na Wabunge wenzetu mtusaidie sisi wenzenu tunaotoka kwenye machimbo, utakapochukua asilimia sita ya kodi, tunaomba sana asilimia moja angalau ibaki maeneo yanakochimbwa yale madini, kwa sababu ukisema tupate 0.3% peke yake haisaidii. Sisi wengine tunaoka kwenye machimbo tumekuwa tukilalamika kwamba tuna migodi mikubwa lakini mji ni mchafu, sasa mkituachia ile 1% angalau na sisi tutakuwa na mipango mikubwa ambayo tutaipanga kuiendesha Halmashauri yetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yalifanyika Mtwara na Ngorongoro wala siyo kitu cha ajabu. Mjifunze mlifanyaje Ngorongoro wao wanapewa chakula, wanalipwa, wanasomeshewa watoto na sisi tunaotoka kwenye machimbo tunaomba hiyo *offer* Serikali iweze kutufanyia hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine suala la sheria hii kifungu cha 10 wanasema kuanzia tarehe 20 madini yote hayatasafirishwa bila kuchakatwa Tanzania. Tanzania hatuna *refinery* na leo ni tarehe 3 Julai, 2017 maana yake bado tuna siku 17. Ukisema kuanzia tarehe 20 tusisafirishe, kwa wenzetu wale wachimbaji wakubwa kama *GGM, Acacia* na wengine

wao wana mitaji sio shida kwenda kununua *refinery*, *refinery* moja ya hali ya chini ni dola milioni mbili kwa sisi wachimbaji wadogo, pengine mpaka muanze kuzungumza na mabenki na mikopo mingine itatuchukua zaidi ya miezi mitatu mpaka hata miezi sita, mnafahamu taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa wachimbaji wadogo hii sheria isitubane. Hatukatai kulipa kodi lakini Serikali iangalie kama ninyi mnajenga hiyo *refinery* mtuambie. Ukisema tarehe 20 tusisafirisha maana yake kuanzia kesho tusichimbe na tusiwashe hiyo mitambo midogo midogo inayozalisha. Kwa sababu mitaji tuliyonayo tunapochimba siku mbili tunauza tunapata hela za kulipa madeni na wafanyakazi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri...

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga Kanuni iliyovyunjwa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mchangiaji alikuwa anapongeza sasa hivi anaanza kulalamika sasa sijajua taratibu zikoje.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni gani imevunjwa? Mheshimiwa Haonga nadhani unatafuta kubadilishwa jina humu ndani. Mheshimiwa Musukuma endelea. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, namheshimu mwalimu wangu wa darasa la kwanza, kule kwao anafundisha darasa la kwanza kwa taarifa niliyonayo, kwa hiyo, msimshangae hii ni mifano. Ninapozungumza hapa silalamiki naboresha.

Ninachozungumza hapa mimi silalamiki naipongeza Serikali kwa kuboresha, wewe unasema nalalamika, nalalamika kitu gani na Serikali ni ya CCM na mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, ebo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuboresha pale ambapo tulipokuwa tunafanya kazi za kibajeti kwenye Halmashauri migodi yote ilikuwa haishiriki kwenye bajeti. Sasa tulivyopitisha hii sheria tunashukuru kwamba tutashiriki nao kwenye bajeti hata yale tutakayokuwa tunayapanga tukiwapa wafanye 1,2,3 litakuwa ni la kimkataba na Waziri anasaini na sisi tutawadai kama wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa nasema hawa wenzetu hawaelewiki na ninaangalia huko naona wengi sana wasomi rafiki zangu, nakushukuru Mchungaji umesogea chini ili unisikie vizuri kule husikii. Wengine wote wakiongea dakika mbili wanakimbia tusiwajibu, hapa tunazungumzia Muswada wa Madini, mtu msomi, mwalimu ameshaaenda kantini. Mtu msomi kabisa ana *masters* yake ya sheria badala ya kukaa humu kutushauri, tunazungumza Muswada wa Madini ananyanyuka anazungumzia *tv*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshauri Waziri sisi wanyonge na watu tunaotaka mabadiliko ya nchi hii hakuna mtu anayelalamika. Ha hata hawa, jaribuni kufanya mikutano kwenye majimbo yenu watu hawako na ninyi ...

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Yaani ni kakundi kenu tu mnapiga kelele. Unasimama hapa unaomba zile Taarifa za Tume tuletewe humu kwani Tume imeshakamilisha kazi yake, si bado kuna majadiliano. Amepokea Taarifa ya Tume, anafanya majadiliano turalipwa, halafu tunaweza kuja kujadili ameshakamilisha kazi yake. Humu hakuna mtu aliyegundua suala la makinikia nilishasema ni suala la Rais tukae kimya amalize kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Sanga na utachangia kwa dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Mngwali atakayechangia kwa dakika 10 atafuatia Mheshimiwa Zitto Kabwe ambaye atachangia kwa dakika saba.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kuipongeza Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuleta Miswada hii ya Dharura ambayo ndiyo tulikuwa tunaitaka sasa Serikali imetimiza, tunaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unajua mtoto wa kambo hata ungemlisha, ukampa nyama za aina gani atalalamika kwamba hatunzwi. Kwa hiyo, hii sio kitu kigeni, ni kitu cha kawaida tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii kwa kweli ni mizuri sana. Sheria hizi ambazo zitapitishwa Bungeni hapa, sheria zinatoa nafasi kurekebisha hata baada ya kuanza utekelezaji wa mikataba hii. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo jema sana ambalo tumelizungumza sana siku za nyuma. Bunge lililopita tumezungumza juu ya mikataba hii kwamba tunaibiwa, Rais amegundua ametuletea sasa tunataka nini, si ndiyo sasa tuiptishe hapa. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sheria inawapa wananchi kunufaika moja kwa moja na ajira na bima. Pia Halmashauri zetu zitazungumza na mwekezaji kuhusu mahitaji yao, sasa tunataka nini? Kwa kweli jambo hili ni jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile udhibiti wa maliasili inayopatikana, nia ya Rais wetu kufanya marekebisho kuja haraka inasaidia sana na ndiyo maana leo imeletwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Miswada hii juzi na jana wadau mbalimbali tumekaa nao pale kwenye ukumbi wa Pius Msekwa. Idadi kubwa ya wadau wameunga mkono sana jitihada za Serikali. Sasa watu wanasema imeletwa kwa dharura lakini imeungwa mkono na wadau mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe tu, Miswada ya Habari imezungumzwa zaidi ya miaka 15 na ndiyo juzi juzi tumepitisha hapa, sasa tunataka na hii iwe hivyo? Mimi naunga mkono kabisa Muswada huu ambao umeletwa kwa sababu utaleta manufaa kwa wananchi na kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine hapa wanasema Serikali ya CCM 2019/2020 wataingia wengine thubutu, thubutu. Wananchi jambo hili wamelipokea kwa mikono miwili... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sana.

**MHE. DEO K. SANGA:** ...sana, kila unapopita, kwanza wanaona tunachelwa. Wananchi wamelipokea jambo hili vizuri na sisi kama Wabunge tuungane ili jambo hili liweze kuanza kwa sababu liko vizuri. Kwanza tunategemea hata zile fedha za makinikia tutapata maji, barabara na kadhalika, kwa hiyo, tumuunge mkono Rais na Wizara kwa ujumla, tusiwakatishe tamaa, sisi tuwe nyuma yao kuhakikisha tunaunga mkono jitihada za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi hapa, unajua wakati fulani huwa nashindwa niseme nini maana Serikali ikileta jambo jema tunasema hapana, sasa tunataka Serikali ifanye nini?

Kuna usemi mmoja unasema shukrani ya nini, sitaki niseme huko, tuiunge mkono Serikali kwa jitihada inazozifanya ili kuhakikisha tunawaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yes.

**MHE. DEO K. SANGA:** Ili tuhakikishe reli inajengwa, bandari jana tumeona na kadhalika, tunataka tutoke hapo ili tupate uchumi wa kati na mkubwa kwa nchi yetu, kwa hiyo, ni lazima tuiunge mkono Serikali. Kwanza, tunampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa kuleta Muswada huu na sisi tupo nyuma yako. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yameisha.

**MHE. DEO K. SANGA:** Yamekwisha, yako mengi hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza imezungumzwa katika sheria hii kwamba itafanya pesa zisipotee kiholela. Vilevile benki za hapa nchini zitatumika kulinda uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. DEO K. SANGA:** Kwa hiyo, ni jambo jema sana.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. DEO K. SANGA:** Huna jipya acha wewe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga muda wako umekwisha. Kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia 400. *(Makofi)*

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64 kuhusu kusema uongo kwamba yale anayoyazungumza yapo katika Muswada wa kesho leo tunazungumzia maliasili ya Taifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde hii ya leo Mheshimiwa Waziri hapa alituambia kwamba fedha zitatunzwa hapa nchini ama mimi ndiyo sijamuelewa Mheshimiwa? Hilo la kutunza fedha nchini liko kwenye yale yanayozungumzwa leo. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) naongeza muda wa nusu saa lakini fasili hii inanitaka niwahoji ili tukubaliane. Kwa hiyo, nitawahoji kuhusu hoja hii.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafikiwa Kuongeza Muda wa Nusu Saa)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, tunaendelea. Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali atachangia kwa dakika 10 lakini Waheshimiwa Wabunge wote nitakaowataja baada ya hapo kwa saababu muda wetu umekwenda na ili uwiano ukae sawa watachangia kwa dakika tano, tano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Esther Mmasi na Mheshimiwa Peter Serukamba wajiandae.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia mjadala huu unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka taarifa ile ya Katibu wa Bunge kusema sasa wadau watoe maoni ilipotolewa nilikuwa nashangaa na naendelea kushangaa namna hili jambo zito sana lilivyoshughulikiwa. Mheshimiwa Profesa Kabudi kaka yangu anajua tulikuwa wote kwenye Tume ya Warioba namna gani Watanzania walisema kwa uchungu mkubwa kuhusu rasilimali hizi. Namna gani tulikwenda mpaka Buhemba tukaona mahandaki yale yaliyoachwa pale, watu wameachwa dhalili kuliko udhalili wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lilipotolewa lile tangazo nikasema Alhamisi tangazo, Jumamosi utampata vipi mtu wa Buhemba, utampata vipi mtu wa Mahenge, hawa ndio



walioko kule, waje watoe maoni yao? Nikasikia kauli tena kutoka mamlaka ileile kwamba niliowaalika mimi nimewapa barua na nakala za Miswada, kumbe kuna watu *selected few* ndiyo tuliowataka kwenye zoezi hili? Sidhani kama tunawatendea haki Watanzania, sidhani kama tunajitendea haki sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchanganyikiwa kote huku napata faraja kwenye maneno ya Mwenyezi Mungu, anasema hakika wale wanaoharibu wakiambiwa mnaharibu kwa kiburi wanasema sisi tunatengeneza. Tunaharibu. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Swadakta.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mnaharibu wenye mamlaka mnaharibu na tunawaambia mnaharibu. Fungeni macho kama yale aliyonifundisha mwalimu wangu *Mrs. Seif*, fungua macho *internalize*.

*My former boss* Profesa Safari aliwahi kuandika makala anasema, '*Liberating the Court Language*', kwamba ile Mahakama Kuu acheni kusema kiingereza semeni kiswahili kwa sababu ndiyo lugha ya Watanzania ili twende pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuja watu tukawaonyesha kwamba wao ni dhalili kwa kulalamikia lugha tu. Hili suala linawagusa wao, limeletwa katika lugha ambayo haieleweki kwao, lakini pia si lugha ya Taifa lao, wapeni haya masuala kwenye lugha yao, wa-*internalize*, waweze ku-*participate fully*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikutarajia katika maisha yangu kuona Mbunge anamdhalilisha mpiga kura. Wale wananchi waliokuja pale tukawadhililisha ni wapiga kura, ni wananchi wa Tanzania. Tunashangaa vipi hizi taasisi nyingine kama polisi na kadhalika kutudhalilisha sisi? Sisi wenyewe tunadhililisha Watanzania. Ni msiba mkubwa na imenisikitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda haupo wa kutosha kujadili suala hili muhimu. Nilitarajia tungepata uelewa wa pamoja kwanza kwamba *what are the issues in debate* kuhusu matatizo haya. *Grievance* za wananchi ni zipi hasa? Sisi wote tupate uelewa wa pamoja kisha tuambiwe hizi sheria zilizopo kwani simekosea nini na zina upungufu gani, tulete hayo mapendekezo mapya tuone yanaleta nini hasa ambayo ni *so substantial* ambayo kweli ita-*take care of the limitation* ambazo ziko sasa hivi lakini hatufanyi haya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala madogo tu, tunaulizana je, hii sheria tunayoitengeneza ita-*apply retrospectively*? Hilo peke yake wengine wanasema ndiyo, wengine wanasema siyo uelewa wa hilo pia hatuna. Pia katika wataalam kuna waliotuambia kwamba mbona hii mikataba yenyewe ya sasa hivi inaruhusu *reviews, why we didn't do the reviews?* Hilo pia hatuna uelewa, jamani tunafanya nini? Tunaleta ushabiki kwenye suala hili? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaambia hamjafika Buhemba mkawaona wananchi dhalili walioachiwa mashimo yale. Mwanangu Mheshimiwa Bashe aliwahi kusema hapa wameachiwa mashimo ambayo hayatojaa mpaka kwa miaka 200, nchi bado ipo? Jamani tuwe *serious* na masuala haya. Hayahitaji kupigana vijembe, hayahitaji kuonyeshana ushabiki na siku moja nilikuwa kusema hapa kwamba hayahitaji kujificha *behind technicalities*. Wenye mamlaka wanatuambia ndiyo Kikatiba, kitaratibu, kikanuni tunawakaribisha wadau lakini hatulazimiki kuwasikiliza wala hatulazimiki kufuata wanayosema. *Come on are we serious, wasting time?* Wabunge wanakaa hapa Jumamosi na Jumapili watu waje waseme eti lakini *after all* hatulazimiki kuwasikiliza au kufuata wanayosema, ya nini tunafanya hayo? Mimi sidhani kama kweli hiyo nia aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kutuletea mabadiliko tumeitendea haki, hatukuitendea haki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika waandishi waliowahi kuandika kuhusu vita vya Rwanda, alishangaa akauliza, *how could all these people agree to kill but how all these people*

*accept to be killed?* Watu walishawishiwa tu wakaambiwa kwamba ueni wakaua na maelfu tena malaki yanakaribia milioni na wao wakakubali wakauliwa. Kwa sababu anatoa *scenario* ambayo Mchungaji au Kiongozi mkubwa wa Kanisa anamwandikia meseji mtu mkubwa wa mamlaka anamwambia, *we wish to inform you that tomorrow we will be killed.* Yaani wamefungiwa Kanisani wanajua wanakuja kuuliwa kesho na anapeleka hiyo *note*. Sasa mwandishi akashangaa *how could all these people agree to kill but how all these people accept to be killed?* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mimi nauliza hivyo hivyo, *how could all of us accept to be fooled and how all of us accepted to be robbed?* (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tumekaa...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Tukapumbazwa tu kwamba hatukuelewa mikataba inasema nini, sheria zinasema nini, halafu tukakubali tuibiwe hivi hivi mchana kweupe?

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Hatukuelewa tunaibiwa, ni nini kimetendeka hapa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo Kanuni iliyovunjwa?

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1), naona Mheshimiwa hapo kidogo anatutwisha maneno ambayo siyo. Hakuna Mbunge hata mmoja aliyekubali kuwa *fooled* hapa...

**MBUNGE FULANI:** Yeye ndiyo amekubali.

**MHE. STANLAUS H. NYONGO:** Labda kama ni yeye mwenyewe kakubali kuwa *fooled*. Kwa utaratibu ni kwamba ilikuja *certificate of urgency* na Spika alivyopokea sisi tulikwenda kwenye Kamati ya Uongozi tukapitisha pamoja na Kambi ya Upinzani hizo siku tatu za kusikiliza maoni ya wadau na tumepitisha kwa pamoja na sasa hivi tunajadili hoja ya kuboresha Miswada hii, hakuna Mbunge hata mmoja aliyekubali kuwa *fooled*. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Nyongo ametoka kutoa utaratibu, labda kama unataka kuonyesha kwamba yeye ndiyo kavunja Kanuni kwa sababu ndiye aliyezungumza kabla yako. Mheshimiwa Riziki Shahari naomba umalize mchango wako.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikuzungumzia suala la juzi na leo, nimezungumzia *all that time* kwamba wakati huo wote vipi sisi tulikubali kupumbazwa na mikataba tuliyoingia na tukakubali kuibiwa na mikataba tuliyoingia, sikuzungumzia hili la leo. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mnisamehe kwa hilo, kama mmenielewa vibaya sikuzungumzia hilo, nimezungumzia *how..*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma Kanuni iliyovunjwa.

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni hiyohiyo Kanuni ya 64, mchangiaji amelalamika anasema

sheria zimeandikwa Kingereza lakini yeye pia anazungumza kiingereza kwenye Bunge la watu ambao wengine hatujui kiingereza. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shahari naomba umalize mchango wako.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kila niliposema hilo la kiingereza lilifuatia la kiswahili pamoja na nilipotoa ufafanuzi kwamba namna gani tulikubali kupumbazwa na namna gani tulikubali kuibiwa kwa mikataba ambayo tuliingia sisi wenyewe tukiwa na wataalamu wetu na tukiwa na akili zetu timamu.

**MBUNGE FULANI:** Wanageuzageuza maneno.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio hicho nilichosema mwanzo, hili si suala la ushabiki wala si suala la kushindana kwa *semantics*, misamiati ambayo haitupi tija. Tunajadili suala hili naamini ndani ya moyo wangu kabisa kwamba huu mchakato ulihitaji muda wa kutosha tuwape nafasi walioguswa moja kwa moja na siyo mimi na ninyi tunaosikia kupitia kwa mtu mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msisitizo kabisa kwamba mchakato huu hatukuutendea haki na yanaonekana hapa. Katika kauli ambayo imenipa ukakasi zaidi ni ile ya kusema *after all* tunatengeneza si tutabadilisha tu. Hiyo peke yake ni *false start* yaani ni mwanzo mbaya sana huo kwamba mnatunga sheria kwa sababu kuna nafasi ya kurekebisha, hiyo siyo sababu ya kutunga sheria. Tunatunga sheria mioyo yetu ikiamini kabisa ni katika yale maamuzi ambayo Bunge hili kama yalivyo Mabunge mengine duniani yamepewa mamlaka kwa niaba ya wananchi kutengeneza vitu pamoja na sheria ambazo ni makini sana ama ikitokea kasoro ndiyo tunasema ni *human error* kwamba ni binadamu hatuko wakamilifu, lakini siyo kwa makusudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kusema hapa tunafanya mambo ya kanyaga twende, hapana haifai, sisi

ni watu muhimu bana, hii taasisi ni muhimu sana. Tumetumwa hapa kwa kazi maalum na hilo la utungaji wa sheria ndiyo haswa kazi yenyewe. Kwa hiyo, tunapoitekeleza kazi hii ni lazima tuwe makini sana na zaidi jamani tunaswali hapa kila asubuhi, *unless* kama tunafanyia stihizai Mwenyezi Mungu. Kama kweli hii swala tunayoimba hapa asubuhi kweli tunaitia ndani ya mioyo yetu naamini tutabadilika na tutafanya kazi zile ambazo tunatakiwa kufanya. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shahari muda wako umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamruhusu mzungumzaji anayefuata, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa na chombo chetu kisije kikajikuta katika mazingira yasiyofaa, Mheshimiwa Shahari hapo ametoa mfano wa ulinganifu ambao unaruhusiwa kisomi, lakini mfano alioutumia wa watu wa Rwanda kuuawa na sisi kudanganywa hauwezi kuiweka pamoja, zile ni roho za watu zilipotea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mfano huo naagiza hapa Makatibu na watu mnaotunza huko kumbukumbu uanzie pale anapoeleza kuhusu sisi kudanganywa mambo ya Rwanda yatoke pale kwa sababu ya muktadha uliotolewa, tusije tukajikuta mazingira ambayo tunafananisha vitu viwili ambavyo havifanani. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Mmasi na Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae.

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa muda ambao umenipa maana uliniambia dakika saba baadaye ukasema tano, kutokana na mambo ambayo nimeyapanga kuzungumza nitaangalia yale

ambayo nitakayoweza kuzungumza na mengine labda nitaweka kwa maandishi.

**MBUNGE FULANI:** Sawa.

**MHE. ZITTO Z.R. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo napenda nilizungumze ni nasaha tu kwa Bunge. Kazi ambayo tunaifanya hapa ni kubwa sana lakini aina ya mjadala yaani *quality of debate* ambayo tunayo hailingani na uzito wa jambo ambalo tunalifanya hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwasihia Wabunge wa pande zote mbili, bahati nzuri nina hiyo *moral authority* maana pande zote mbili mimi niko mwenyewe, mwenzangu naona wewe uko UKAWA. Kwa hiyo, nawasihia tufanye jambo hili kwa utulivu ili tuweze kutunga sheria ambayo itakuwa na manufaa kwa nchi. Hii kubishana, kurushiana maneno na kadhalika yanatupotezea muda muhimu sana sisi kama nchi kuweza kufanya kazi hiyo kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa ujumla hii seti ina sheria tatu. Sheria moja ndiyo kubwa sana ile ya mabadiliko ya *The Mining Act*, kwa hiyo, tunaweza tukahitaji muda wa kutosha sana kule. Sheria mbili hizi, hii ya *re-negotiation* na hii ya *sovereignty* ni *statements of intent*. Ni mambo ambayo tulipaswa tuyafanye toka mwaka 1962, hatujafanya. Kwa hiyo, tunakuja hapa kwa ajili ya ku-*correct* hayo makosa ambayo tumeyafanya huko nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani hizi sheria mbili ya *re-negotiation* ya mikataba na Bunge kuwa na mamlaka ya kutazama mikataba na Sheria ya *Sovereignty* ya kuweka maliasili yetu kuwa yetu, hizi tuzimalize tupate muda wa kutosha tuje kujadili ile ambayo ni kubwa ambayo hata nimeona Mheshimiwa Musukuma anachangia sheria ambayo haipo hapa kwenye mjadala. Hizo 16% na kadhalika ziko kule siyo hapa, hizi ni *statement of intents*, tuzikamilishe tumalize tupate muda wa kushughulika na jambo kubwa

zaidi ambalo liko kwenye *Mining Act* ambayo sijui itakuja lini kama ni kesho au siku gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo napenda kuzungumzia ni je, sheria hizi mbili ni za kimapinduzi (*revolutionary*)? *Yes*. Kwa sababu gani? Kwa mara ya kwanza tumekuwa nchi ya kwanza ya kiafrika kutamka kwenye sheria kwamba chochote kilichopo chini na juu ya ardhi ya nchi yetu ni chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni *transformative*? *No!* Kwa sababu licha ya kutamka hivyo hatujagusa mfumo wa uzalishaji. Mfumo wa uzalishaji bado ni ule ule ambao tunazungumza kwamba tunataka kuutatua. Kwa mfano, Wabunge hapa mnazungumzia umiliki wa 16% na baadaye muende mpaka 50% siyo jambo jipya. Sheria iliyopita ina umiliki, hii sheria ambayo tunataka kui-*amend* ina umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya mwaka 1979 ilikuwa ina umiliki na mpaka sasa kuna migodi ya Almasi, Mwadui tunamiliki 25%, kwa hiyo siyo jambo jipya. Jambo jipya ni nini? Jambo jipya tubadilishe mfumo wa uzalishaji. Mwekezaji awe mkandarasi, awe *contractor*. Sisi tuna madini, unajua una mashapo kadhaa Buzwagi akija *Acacia*, unakubaliana naye achimbe kwa niaba yako, aondoe gharama zake, kile kinachobakia mgawane kwa makubaliano maalum, hiyo ndio *transformative*, hatufanyi hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili siyo jambo jipya, tunalifanya hili kwenye mikataba ya gesi sasa hivi. Ndiyo maana hamuoni malalamiko makubwa ya kimapato kwenye gesi kwa sababu kwenye gesi mwekezaji ni mkandarasi.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Mmasi



atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na dakika zetu za mwisho atamalizia Mheshimiwa Shanif Mansoor.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Waziri mwenye dhamana kwa hiki alichotuletea mezani. Sheria hizi mbili kimsingi zimelenga kuleta ukombozi wa kiuchumi nchini Tanzania. Sheria hizi mbili zimejaribu kuleta uhalali wa umiliki wa maliasili ya Tanzania pia zimejaribu kuweka umuhimu wa Bunge kuwa kama chombo pekee cha kupitia mikataba yote yenye masharti hasi na mikataba yote isiyo na masharti hasi ili kuendana na Azimio ambalo Tanzania kama nchi tumeridhia, Azimio Namba 1803 lililoazimiwa na *United Nation General Assembly 1962*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu sheria hizi mbili zimelipa Bunge dhamana kubwa ya kupitia mikataba hii ili kuweza kulinda maslahi mapana ya Taifa. Sheria hizi pia zinaendana na Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo pia inasema kwamba Bunge litakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyote ili viweze kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. Kupitia wasilisho la Miswada hii miwili ya sheria ni kwamba sasa Bunge linapewa hati na mamlaka kamili ya kuweza kupitia mikataba ambayo itakuwa inaletwa Bungeni kwa maslahi mapana ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, zimekuja *opinions*, tunafikiri kwamba Bunge pamoja na kupitia pia waweze ku-*ratify*, nadhani hii ni *double standard*. Ukiangalia Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumepewa nafasi ya kuweza kuisimamia na kuishauri Serikali. Tunapoenda kusema tunataka tu-*ratify*, sisi Wabunge tuna dhamana ya ku-*ratify International Conventions* tu kwa nafasi zetu katika Bunge lako Tukufu. (Makofi)

Kwa hiyo, mimi bado napinga na ninasema kwamba hapana tuna kila sababu ya kuona kwamba Muswada huu ni mzuri na una maslahi mapana ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *opinion* nyingine ilikuwa suala la muda. Niseme tu tofauti na watu wote waliosimama kupinga Miswada hii kutokana na suala la muda kwa kufuta kumbukumbu zao juu ya Muswada wa Sheria ya Habari ambao ndiyo hawa walitusumbua lakini ukapita. Pamoja na hao waliochangia, watu wengine walioweza kuchangia wakifanana na sura zao au mitizamo yao ilikuwa ni Chama cha Bodaboda Dodoma, wauza mitumba nafikiri *Dakadaka Group* na *Lamkachema Group*. Ukisoma ripoti ya Kamati, ukurasa wa 10 utaona mawazo yao hayo yote yanafanana na hiki ambacho wamekisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekuja wadau na wadau ambao sisi tuliweza kuwaelewa kwa ukaribu na pengine mimi kwa hofu yangu, nilifikiri wangeweza wakatukana kwenye hili. *TLS* ambao wao ndio wamemtoa Rais nafikiri wa Dunia au ni Rais wa Tanzania wa upande huo wa sheria walikuja wakai-*support* Serikali. Mimi niko tayari kupokea adhabu yoyote kutoka kwenye Kiti chako, *TLS* walianza kusema wamepata muda wa kutosha, wanashukuru Serikali imewapa muda wa kutosha katika kufanya uchambuzi wa sheria hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sheria hizi, hii *Permanent Sovereignty* ina vifungu nane tu lakini ni *A3* iliyotumika hapa, kuna *page* mbili ukitoa *preamble, two pages!* Hebu tuwe wa kweli na tuache wizi, huu ni wizi. Unakaa hapa unalipwa posho kusoma kurasa mbili za *A3*, unaniambia kwamba unahitaji *some ages?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inanisikitisha, muda tuliotoa unatosha. Mheshimiwa Mnyika atakumbuka tumeanza ku-*discuss* Ijumaa, tulikuwa na Kamati ya Mheshimiwa Mchengerwa, tulikuwa na Kamati ya Mheshimiwa Doto Biteko lakini hata yeye tunafahamu alikuwa na Kamati yake ambapo aliendesha mpaka usiku

wa manane jana. Sasa huu muda tunaolalamika hautoshi ni muda upi tena? (*Makofi*)212

Mheshimiwa Naibu Spika, tuisahau, Mheshimiwa...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mdogo, lakini Waheshimiwa Wabunge leo ni siku muhimu sana, ni siku ya mapinduzi ya kiuchumi. Ukisoma sheria zile mbili ni siku ambayo Watanzania tumeamua kwa sauti moja kwamba mali zilizopo Tanzania ni za kwetu. Kwa namna yoyote ile maamuzi haya lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Magufuli amefanya kazi hii, amezidi kuthibitisha uzalendo wake lakini amezidi kuonesha nia njema ya kutaka kuliendeleza Taifa letu. Nilisema siku ile wakati nachangia Wizara ya Ujenzi kwamba naamini watakaokuja kuandika historia ya Tanzania, jina la Rais Magufuli litaandikwa kwa wino wa dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nataka nimpe angalizo Waziri wa Sheria. Waziri wa Sheria tunatunga sheria hii leo, hizi ndogo mbili, ambazo tunakwenda kutambua ukuu na mali za Tanzania. Ninayo hakika wakubwa duniani watalalamika, wawekezaji wakubwa watalalamika, *Bretton Woods Institutions* zitalalamika, nikuombe Waziri Profesa usije ukaenda ukapata *pressure* za hao wakubwa ukaja hapa kufanya *amendments*, nitaongoza kukupinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena, tunatunga sheria hizi ambazo ni ukombozi wa nchi yetu, muende huko mkakutane na wakubwa halafu Waziri wa Sheria uje kutaka kufanya *amendment*, nina-*registernitakupinga*. Ni vizuri tuwe

tayari yatakayotokea tujifunge mkanda. Mwalimu wa Taifa alituambia sisi ni Taifa lazima tuwe tayari kujifunga mkanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wanaosema wakubwa watanuna, sawa, wanune, waende, mali ni yetu. Watakuja watachimba hata watoto wa watoto wangu. Maana haya tumeamua, haya ni maamuzi makubwa, amesema Mheshimiwa Zitto kwamba haya ni maamuzi makubwa na mimi nasema leo Bunge hili tumeingia kwenye historia kufanya maamuzi makubwa.

Naombeni Wabunge tusirudi nyuma, wanaosema tuna haraka, mlitaka tuanze lini? Tumeibiwa vya kutosha, hili jambo halitakiwi tuulizane kuhusu dharura, kwanza limechelewa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, yamekuwepo malalamiko kwamba tunaibiwa na tatu tumepewa *opportunity* ya kwenda ku-*renegotiate* mikataba yote iliyokwishapita, tunataka nini kama Bunge? Tumepewa *opportunity* kama Taifa, naombeni Bunge tufanye kazi yetu tuhakikishe tunakwenda ku-*renegotiate*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema tunakwenda kupata *shareholding*, mimi nataka muende mbali zaidi Mheshimiwa Waziri, naomba tukubaliane hapa kama Bunge madini yote yaliyobaki tufanye *exploration* wenyewe. Tukifanya *exploration* wenyewe anayekuja tuta-*determine* sisi tuwe na *percent* ngapi. Nafuu kila hata baada ya miaka mitano tufanye *exploration* moja, tuanze mgodi mmoja, lakini tutaanza na asilimia 50 tutapata fedha nyingi kama Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa suala la kuamua watu wote wanaofanya biashara ya *resources* Tanzania wafungue akaunti zao hapa. Maana yake ni nini? Fedha watakazoweka kwenye benki zetu na sisi Wabunge tutazitumia, tutakwenda kukopa, ndiyo *banking* inavyofanya kazi, kwa hiyo, uchumi

wetu utachanganya kwa wao kuweka fedha zao kwenye akaunti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wanaosema wamechukua mikopo duniani, *yes!* Mikopo wamechukua, bado hata ukikopa nje unaweza ukalipa kutokea kwenye benki ya Tanzania, *it is normal*, ni *TISS* tu. Kwa hiyo, tunachosema sisi kopeni huko nje, lakini fedha leta weka Tanzania ili na sisi Watanzania tufaidike na fedha hizo ambazo ziko kwenye uchumi wetu. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta hili na kwenye Ripoti ya Bomani najua hili lilikuwa moja ya sharti la Ripoti ya Bomani kwamba lazima wafungue akaunti zao hapa Tanzania. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba. Mheshimiwa Shanif Mansoor atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru umenipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa busara na ujasiri wake wa kuleta Muswada huu wa Marekebisho ya Masharti Hasi yanayohusu maliasili ya nchi. Naomba pia nimuombee Mwenyezi Mungu ampe afya njema na maisha marefu Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mengi lakini muda hautoshi lakini naomba nishauri mambo yafuatayo kwa Serikali yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, hapa tunajadili masuala ya wawekezaji, sisi tuna wawekezaji wa aina mbili kwenye Miswada hii tunayojadili. Kuna wawekezaji wa zamani ambao tuna mikataba mibovu na tuna wawekezaji wapya. Mimi ningependa kushauri kwa Serikali yetu kwamba

wale ambao wana mikataba mibovu wana zaidi ya miaka 20, walipofika kuwekeza ndani ya nchi yetu walikuja na *business plan* yao ambayo ilikuwa inasema ndani ya miaka mingapi watakuwa wamesharudisha faida yao. Sasa hivi kwa taarifa nilizonazo wale wote tena sio wawekezaji, wameshapata faida zao maradufu sasa hivi wale watu ni waendeshaji tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa kufanyika sasa hivi ni Serikali ichukue migodi yote ambayo ina zaidi ya miaka 20 kwa sababu *business plan* zao zimesha-*expire* na wameshapata faida zao, sasa hivi wale watakuwa ni waendeshaji tu. Serikali tunatakiwa tuwe na asilimia zaidi ya 75 kwenye hiyo migodi ambayo ina zaidi ya miaka 20. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine ni kwamba migodi mipya tusiwe chini ya asilimia 50 na zaidi. Nakubaliana na Mheshimiwa Zitto aliyosema kwamba wale wawe waendeshaji tu, wasijekuwa ndiyo wawekezaji, wawe waendeshaji wa migodi ambayo inaendelea ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishauri Serikali Serikali yangu kwamba tuna misamaha ya Kodi ya Forodha na VAT kwa wawekezaji. Naomba hilo suala nalo lifutwe kusiwe na misamaha yoyote. Misamaha yote iende kwenye Kodi ya Mapato, misamaha ya Kodi ya Forodha ifutwe, sisi tunataka fedha za kuendesha bajeti yetu, hatuwezi kusubiri mpaka mwekezaji apate faida ndiyo sisi tuanze kupata fedha. Tunataka fedha siku ya kwanza akija atupe fedha ili sisi tutoe huduma za jamii za maji, barabara na afya kwa wananchi wetu, kwa hiyo, hakuna misamaha. Tufute misamaha yote hata kwenye mafuta tufute misamaha yote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri amesema kwamba watafungua akaunti yao ya biashara hapa nchini. Sio akaunti tu, napenda pia madini yanayotoka hapa yasipelekwe kwenye maeneo yao,

yauzwe kutoka Tanzania. Madini ya Tanzania mpaka leo hayatoki *the invoice*, yanatoka madini peke yake. Ningeshuri dhahabu itoke na *invoice* iende kwa mnunujaji tujue kodi ya mapato tunayopoteza. Sasa hivi madini yote yanatoka hapa yanaenda Afrika Kusini huko ndiyo wanakouza tunapoteza mapato mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa madini yetu yatoke na *invoice* na ningeshuri pesa zote zile zirudi ndani ya nchi yetu, kama Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wafungue akaunti. Mimi ningependa isiwe akaunti ya kuongeza *earnings* pia akaunti ya kulipa madeni yote ya mgodi yalipwe kutoka Tanzania. Wakifanya manunuzi wanunue kutoka Tanzania. Mimi ningependa hilo lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho ambalo napenda kushauri kwa Serikali, tumesema *by laws* zitategenezwa na Waziri. Mimi napenda tusimuachie Waziri peke yake mwenye dhamana kwa kazi hiyo, baada ya *by laws* kutengenezwa na Mheshimiwa Waziri ningeshuri hizo *by laws* zipitishwe katika *cabinet* au na Bunge ili tusirudi huko tunakotoka leo. Tusimuachie Waziri akategeneza *by laws* peke yake lazima tushirikishe *cabinet* au Bunge kuhakikisha kwamba ziko sawasawa *otherwise* tutakuwa tunarudi palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi.

Kwanza hili la uchangiaji tumemaliza, kwa hiyo, mchana wataendelea na ratiba nyingine kwa maana ya kumaliza wale wachangiaji kwa upande wakamilishaji wa hoja na pia kuingia kwenye utungaji sasa wa sheria na hayo marekebisho yataangaliwa mchana.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.38 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge liliirudia)*

*Spika (Mhe. Job Y. Nduga) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na uchangiaji uliisha asubuhi, kwa jinsi hiyo sasa naomba nimwiite mtoa hoja Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Kabudi ili ahitimishe hoja yake kwa kupitia maelezo ya Waheshimiwa Wabunge na maoni yao. Mheshimiwa Waziri, karibu tafadhali, karibu sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili wa 2017 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017)* na Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Rasilimali na Maliasili za Nchi kwa mwaka 2017 *(The Natural Wealth and Resource Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms), Bill 2017)*

Mheshimiwa Spika, umeongoza mjadala wa Miswada hii kwa umahiri na maoni na michango iliyotolewa imeiwezesha Serikali kuboresha maudhui ya Miswada hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nazishukuru kwa pamoja Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Kamati ya Sheria Ndogo waliokuwa chini ya Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa



Rufiji na Mheshimiwa Doto Biteko, Mbunge wa Bukombe, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kujadili Miswada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Doto Biteko ambaye alisoma maoni kwa niaba ya Kamati ya Maalum kwa kutoa maelezo mazuri ya ufafanuzi juu ya maudhui ya Miswada hii pamoja na mapendekezo ya marekebisho kwenye Miswada. Naamini maelezo yake yamewasaidia Waheshimiwa Wabunge na wananchi waliomsikiliza kuelewa vema maudhui ya Miswada iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu. Maoni ambayo Kamati Maalum imeyatoa kwa Serikali yamewezesha kwa kiasi kikubwa kuboresha maudhui ya Miswada hiyo kama Majedwali ya Marekebisho yanavyosomeka.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA na Mheshimiwa John Heche, Mbunge pia wa Chama cha CHADEMA kwa hotuba yaliyoitoa kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Wizara ya Katiba na Sheria na kwa zile Kamati nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano waliotuonyesha mimi pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa maandalizi na majadiliano ya Miswada hii katika hatua zote. Pia nawashukuru watendaji wa Wizara zote zilizoshiriki kwenye hatua za maandalizi na majadiliano ya Miswada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa Miswada hii, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 12 wamechangia Miswada hii. Kwa namna ya pekee niwashukuru Mheshimwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge wa Bukombe kwa niaba ya Kamati Maalum; Mheshimwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA na Mheshimiwa John Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Vwawa; Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini; Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba;

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma; Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, Mbunge wa Viti Maalum - CUF; Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha Mjini; Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako; Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum - CCM; Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita na Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mbunge wa Kwimba - CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri waliyoitoa wakati wa majadiliano ya kwenye Kamati. Tumepokea maoni mazuri ambayo yamelenga kuboresha Miswada hii. Kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia Miswada hii ni ushahidi kwamba Bunge hili linatambua umuhimu wa mapendekezo ya kutungwa kwa sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kuona Wabunge wote wanakubaliana kwamba Miswada hii ni muhimu kwa nchi yetu. Hakuna hata Mbunge mmoja aliyesema kwamba Miswada hii siyo muhimu kwa nchi yetu. Hilo limenipa faraja kubwa sana kutambua kumbe sheria hizi zimefika kwa wakati muafaka. Yale madogo madogo yaliyokuwepo yasitoe katika azma hiyo ya pamoja kwamba Miswada hii ni yetu sote, ni ya mapinduzi makubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Nimshukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa kusema hilo ambalo niliogopa kulisema ili isionekane Serikali inajisifia. Hii ni Miswada ya kwanza ya sheria kutungwa katika Bara la Afrika. Hakuna nchi nyingine katika Bara la Afrika ambayo imethubutu kutunga Miswada ya Sheria ya aina hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Watanzania tuna kila haki ya kujisifu na kujipambanua kwamba tumethubutu pale ambapo wengine hawakuthubutu, tumejaribu pale ambapo wengine hawakujaribu. Kama nilivyoeleza hapo awali hatujidanganyi, tunapambana na miamba wenye nguvu, wenye kila aina ya silaha, lakini silaha yetu kubwa ni uzalendo wetu, ni umoja

wetu, ni nia yetu ya kulinda mali hii kwa ajili yetu sisi na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe kwa kulisema hilo ambalo nilichelea kusema ili nisije nikajivuna na kama anavyosema Mtume Paul na mimi nikaanguka, lakini nashukuru sana kwa hayo yaliyosemwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge tusingependa kuingia kwenye malumbano, ni kweli sheria hii ilistahili pia kuwa na Muswada wa tafsiri ya kiswahili. Jambo hilo naahidi litafanyika mara moja ili sheria hii itapopitishwa na Bunge tutakuwa na sheria hii ya kiingereza lakini pia tutakuwa na tafsiri yake ya kiswahili. Shughuli ya kutafsiri imeanza.

Mheshimiwa Spika, Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge jana mimi mwenyewe nimeondoka katika hivi viwanja vya Bunge saa kumi na moja karoso dakika kumi alfajiri na vijana wale bado wanafanya kazi. Hata hivyo, tutafsiri kwa kiswahili ili sheria hii pia ipatikane kwa Watanzania wote kwa lugha ya kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatufanyi hivyo kwa sababu Watanzania hawajui kiingereza, la hasha! Tunafanya hivyo kwa sababu kiswahili ni lugha yao na tunapozungumzia rasilimali na mali zao ni pamoja na lugha yao adhimu ya kiswahili. Kwa sababu ya dharura ndiyo maana tulileta Muswada huu kwa lugha moja tu. Kwa hiyo, niwaombe radhi Watanzania kwamba hatukuweza kufanya hivyo kwa sababu hii ni vita na vita hii ilibidi silaha hizi zitumike sasa lakini watapata tafsiri ya kiswahili kwa sababu haki yao na sisi Serikali ni wajibu wetu kuwapatia tafsiri hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo machache ambayo ningependa kuyafafanua. Ukisoma Miswada hii miwili, Rais hapewi umiliki wa mali hizi. Hakuna mahali Rais anapewa umiliki wa mali hizi. Neno lililotumika ni *trust* yaani yeye ni mdhamini. Umiliki wa mali hii ni wa wananchi wote wa

Tanzania, yeye ni mdhamini. Unapokuwa na mdhamini ina maana wako ambao ni *beneficiaries* au wanaofaidika na udhamini huo, nao ni wananchi wote wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme ingawa mara nyingi nimeanza kushtumiwa au kukumbushwa kwamba hili siyo darasa na kweli hilo darasa ni Bunge. Suala la udhamini katika historia ya nchi yetu na hasa upande wa Tanzania Bara lilianza mwaka 1919 katika Mkataba wa *Versailles* baada ya Wajerumani kushindwa katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na koloni lao la Deutsch-Ostafrika ambalo lilikuwa Tanzania Bara ya leo Rwanda na Burundi kuwekwa chini ya usimamizi wa *League of Nations*.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huo wa *Versailles* kwa mara ya kwanza ndiyo unaotumia neno *trust* ambao ulisema ardhi yote iliyo katika eneo la Ujerumani ya Afrika Mashariki ni mali ya wenyeji na itakuwa katika dhamana ya *League of Nations*, *trust of the League of Nations*.

Mheshimiwa Spika, lugha hiyo hiyo, ndiyo inayotumika kwenye Sheria ya Ardhi ya mwaka 1923 inayosema kwamba ardhi yote ya Tanganyika ni mali ya wenyeji (*natives*) na itakuwa katika dhamana ya Malkia kwa niaba ya wananchi. Ndiyo maana kwa sababu hiyo Waheshimiwa Wabunge sisi tofauti na Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya ardhi yetu yote ilitangazwe kuwa *public land* yaani ardhi ya umma iliyowekwa katika dhamana ya Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo miaka ya 50, Waingereza walipojaribu kuchukua ardhi ya Wameru kwa sababu ni ardhi nzuri yenye rutuba na kuwaondoa wenyeji, kiongozi wa wananchi wa Meru Japhet Kirilo akisaidiwa na Mwanasheria kutoka Bermuda, Mkaribiani mweusi Earle Seaton ambaye baadaye alikuja kuwa Jaji katika Mahakama Kuu ya Tanganyika na Tanzania walikwenda kwenye Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa na kukataa ardhi hiyo isichukuliwe na ardhi hiyo haikuchukuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, isingekuwa Wajerumani kushindwa katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na sisi kuwekwa katika udhamini wa *League fo Nations* na baadaye udhamini wa Umoja wa Mataifa, watu wetu wanaoishi Makete leo wangehamishwa. Kwa sababu hali ya hewa ya Makete ni hali ya hewa ya Ulaya na Wajerumani walikuwa wamejipanga kwenda kuishi kule. Ndiyo maana wale Wakinga na Wabena walipelekwa manamba ili waondoke kwenye ardhi nzuri. Hivyo hivyo, kwa watu wa Kasulu nao walipelekwa manamba ili baadaye ardhi hiyo waichukue Wazungu. Lakini Mungu bariki baada ya Wajerumani kushindwa na udhamini kuja ardhi hiyo imebaki kwa wenyeji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najua watu wanatoa mfano wa Sheria ya Ardhi kwamba udhamini upo chini ya Rais, lakini ardhi mbona haiendi inavyotakiwa. Iko tofauti kubwa na hiyo nitaizungumza kesho kwenye Muswada huo. Hata hivyo, nataka niwakumbushe Watanzania yuko Mtanzania ambaye Rais alitumia mamlaka yake kupitia Kamishna wa Ardhi kumfutia hati yake ya ardhi, alikwenda mahakamani mpaka Mahakama ya Rufaa katika kesi ya *Partman Garments* na Mahakama ikasema ingawa Rais ana mamlaka hayo haruhusiwi kuyatumia *arbitrary* na lazima *observe principles of natural justice*. *Partman Garments* eneo la *Nyerere Road* alirudishiwa ardhi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimetoa mfano huu kuonyesha kwamba si kweli kwamba Rais ni mmiliki wa ardhi, yeye ni msimamizi na anapotokea amesimamia isivyotakiwa kwa mujibu wa sheria kwa mujibu wa maamuzi ya Mahakama ya Rufaa ya Tanzania hukumu ya Marehemu Jaji Mwakasendo haruhusiwi kuyatumia madaraka yao *arbitrary* na ni lazima *a-observe principles of natural justice*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, duniani kote udhamini wa mali ya pamoja upo kwa Mkuu wa Nchi (*Head of State*). Sasa mimi naomba Watanzania wanisaidie *Head ya State* wa Tanzania

anaitwa nani. Kwa sababu duniani kote anayepewa udhamini wa mali ya pamoja ni Mkuu wa Nchi. Sasa niambiwe Mkuu wa Nchi wa Tanzania Kikatiba anaitwa nani?

**WABUNGE FULANI:** Rais.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kama anaitwa Rais hatuna njia ya kuliepuka hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wako Marais wa aina nyingine ambao siyo mjadala wa hapa. Zipo nchi zenye Marais ambao ni *ceremonial*, lakini bado wamepewa mamlaka ya udhamini. Soma Katiba ya Ethiopia aliyepewa mamlaka ya udhamini ni Rais wa Ethiopia tofauti yake na wa kwetu yeye siyo Rais Mtendaji. Soma Katiba ya India aliyepewa udhamini wa mali yote ya India ni Rais wa India kwa sababu ni Mkuu wa nchi tofauti yake yeye siyo mtendaji kama hapa. Soma sheria mbalimbali za Uingereza, mali zote za Uingereza zimewekwa chini ya Mkuu wa nchi ambaye ni Malkia tofauti yake na hapa Malkia siyo Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la udhamini kuwa chini ya Rais ningepomba lisiwe suala la mjadala kwa sababu ndiyo utaratibu wa dunia nzima. Hata hivyo, nimeenda mbali kuonesha mahakama zetu zimechukua hatua wakati Taasisi ya Urais ilipotumia mamlaka zaidi ya yale iliyopewa. Nimetoa mfano wa Sheria za Ardhi, lakini ningeweza kutoa mifano mingine mingi ambapo mahakama iliingilia mamlaka ya Rais kama Mkuu wa Serikali alipokuwa amekwenda au mamlaka yake yametumika isivyokuwa na kawaida.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo huo upo, tunaweza kuutumia mahakamani kutumia kitu kinaitwa *Judiciary Review of Administrative Action* au tukaenda kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kulalamika kuhusu *abuse of power*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahahakikishie Watanzania kilichofanyika katika sheria hii ya kumpa Rais kuwa Mkuu wa Nchi ndiyo duniani kote. Kwa sasa kwa

sababu Mkuu wa nchi yetu anaitwa Rais, haitwi jina lingine ataendelea kuwepo katika sheria kama mdhamini. Kama nitakavyoeleza kesho kwenye Muswada unaofuata si kweli kwamba amepewa madaraka makubwa, mtaona kule jinsi madaraka ya Rais yalivyopunguzwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nirudie kusema azma ya kupunguza Madaraka ya Rais yalitolewa na Chama cha Mapinduzi mwaka 1983 na 1984 wakati Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokuwa anang'atuka. Moja ya mambo aliyotamka bayana ni kwamba sasa naondoka lazima Watanzania tupunguze madaraka ya Rais na yalipunguzwa kwa namna mbili. Moja, vipindi viwili vya Urais lakini pia kuwa na Waziri Mkuu Mtendaji ambaye anaidhinishwa na Bunge. Kwa hiyo, tusiwafanye Watanzania waogope Taasisi ya Urais tukifanya hivyo hatumdhalilishi Rais tunaidhalilisha yetu wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie kwa haya yaliyoelezwa, ni suala zima la matumizi ya sheria hii. Moja, nashukuru katika michango jana ilidhihirika wazi kwa wengi kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha *Cap.1, preamble* ni sehemu ya sheria. Siku ile lilipotolewa na rafiki yangu Mheshimiwa Mtolea na leo niliseme hadharani nilikaa kimya kwa sababu Mheshimiwa Mtolea namheshimu niliona nisimwonyeshe kwamba hajasoma vizuri sheria na yeye namshukuru alikuwa muungwana. (Makofi)

La pili, ni hili suala, je, sheria hii ni *retrospective*? Unajua tunachanganya vitu viwili na napenda nifafanue sasa. Sheria hii siyo *retrospective* maana yake itaanza kutumika siku itapokuwa imetiwa saina lakini *effect* yake kuhusu mikataba ni *retrospective* kwa sababu inasema mikataba yote iliyoingiwa kabla ya sheria hii kutungwa na baada ya sheria hii kutungwa yote itapitiwa na kujadiliwa upya. (Makofi)

Kwa hiyo, ambacho ni *retrospective* siyo sheria bali ni matumizi ya sheria hiyo kuhusu kuangalia mikataba hiyo na imetamka bayana ni mikataba iliyoingiwa kabla ya sheria hii na itakayoingiwa baada ya sheria hii. Maana yake nini? Mikataba yote ya zamani kwa mujibu wa sheria hii itaangaliwa upya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuangalia upya mikataba hiyo kitakuwa baada ya sheria kupita. Kwa hiyo, mimi hilo halinipi wasiwasi na ambaye anajipanga kwenda mahakamani kuliongelea hilo hata akienda kwenye *International Court of Justice* tutampiga chini kwa sababu tutamwonyesha maamuzi ya nchi mbalimbali ikiwemo Marekani inapochukua hatua kama hizi zinakuwa *retrospective*, ingawa sheria yenyewe siyo *retrospective*.

Mheshimiwa Spika, nisiwaingize katika darasa la *jurisprudence* wala *statutory interpretation*. Kwa sababau tuna tatizo moja wanasheria na hasa tuliosoma zamani bado tunatumia *Canons of interpretation* za zamani. Someni kesi ya Warioba vs Wasira maamuzi ya Mahakama ya Rufaa, hukumu ya Jaji Kisanga inasema katika mazingira ya sasa tuna *approach* mbili za kutafsiri sharia, *the purposive approach and the literal approach*. Unapokwenda kwenye *purposive approach* unaangalia *the purpose of the enactment of that law*, ndiyo maana ndani ya ile sheria kwa mara ya kwanza Mahakama ya Rufaa ili ijue *the purpose* ya ile Sheria ya Rushwa ya Uchaguzi ina maana gani, kwa mara ya kwanza Mahakama ya Rufaa ili angalia *objects and reasons* kwenye *Bill*.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza Mahakama ya Rufaa ilikwenda kwenye *Hansard* na uamuzi huo wa Jaji Kisanga wa Mahakama ya Rufaa katika kesi hiyo ulirudi rejea katika kesi nyingi za *House of Lords*. Labda niwakumbushe wenzangu waliosoma zamani, *House of Lords* sasa siyo tena Mahakama ya mwisho ya Uingereza, siku hizi kuna *Supreme Court of England and Wales* kwa sababu najua watu wanasoma vitabu vya zamani wanaweza kuwa haya mapya hawajayajua. (Makofi)



Kwa hiyo, tunavyotafsiri sheria hii tusitumie *literal approach*, tutumie *purposive approach*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninafarijika sana kwamba michango mingi iliyotolewa imekuwa ni ya kujenga, kuboresha na kutufanya tufikie azma yetu. Yapo maswali yaliyoulizwa na wengine kwa mfano, suala la *check and balances* za Rais, Katiba yetu imeweka *checks and balances* za kutosha kuhusu madaraka ya Rais wetu ikiwa ni pamoja na *impeachment*. Kwa hiyo, hilo halinipi shida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yale aliyoongea Mheshimiwa Musukuma naomba tuyajibu kesho kwa sababu yapo katika Muswada wa kesho wa je, hizo asilimia 16 za *share* zinawahusu pia wachimbaji wadogo wadogo, ningeomba hilo tulijibu kesho kwa sababu kazi hiyo ipo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Muswada huu hauna *controversy* (hauna ubishi), ubishi haupo katika maudhui ya Muswada, ubishi uko katika mawanda na mimi nayaelewa ni mawanda ya kisiasa.

Sasa mawanda ya kisiasa yasitoe katika maudhui ya Muswada huu ambayo hakuna hata Mbunge mmoja niliyemsikiliza haungi mkono Muswada huu. Basi kwa sababu Wabunge wote mmeunga mkono Muswada huu, kwa niaba ya wananchi wa Tanzania, hilo ni jambo la wote kusimama pamoja kusema kwamba tumeitendea nchi yetu haki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE  
HON. PALAMAGAMBA J.A.M. KABUDI, THE MINISTER FOR  
CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE SECOND  
READING OF A BILL ENTITLED "THE NATURAL WEALTH AND  
RESOURCES (PERMANENT SOVEREIGNTY) ACT, 2017"**

-----  
*(Made under S.O 86(10)(b))*  
-----

A Bill entitled "The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017" is amended as follows:

**A:** In the Preamble, by-

(a)

inserting immediately after the words "Article 8" the words "and Article 9(f)" appearing in the first paragraph;

(b)

deleting the third recital and substituting for it the following:

"AND RECOGNISING, that the United Republic is a signatory to the United Nations Universal Declaration of Human Rights and the African Charter on Human and Peoples Rights and subscribes to Articles 17 and 21 respectively;"

**B:** In Clause 2, by inserting the words "as well as Tanzania Zanzibar" at the end of that Clause;

**C:** In Clause 4, by adding after subclause (2), the following new subclause:

"(3) The First Schedule and the Second Schedule shall have effect in relation to assertion by the People and the United Republic over permanent sovereignty over natural wealth and resources."

**D:** In Clause 5, by adding immediately after sub-clause (3) the following:

"(4) Without prejudice to subsection (3), the Government may, where it considers necessary, authorise any

person to perform functions or undertakings relating to exploration of natural wealth and resources in accordance with laws of Tanzania.”;

**E:** In Clause 6, by-

(a) deleting the phrase “be such as to further Tanzanian’s independence” appearing in subclause (2) and substituting for it the phrase “aim at furthering independence and self reliance of the People of the United Republic of Tanzania”;

(b) adding immediately after subclause (2) the following:

“(3) For purposes of subsections (1) and (2), it shall be the duty and responsibility of the Government, all organs and persons or authorities exercising executive, legislative or judicial functions to take cognizance of, observe and apply the provisions of this Act.”;

**F:** In Clause 8, by deleting the phrase “who are citizens”;

**G:** In Clause 9, by-

(a) deleting the words “shall be” appearing in subclause (1) and substituting for them the word “are”;

(b) inserting the word “in” between a comma and the word “any” appearing in subclause (2)”;

**H:** In Clause 11-

(a) in sub clause (2) by-

(i) deleting the word “relating” appearing in the second line; and

(ii) inserting the word “in” between the word “and” and the word “accordance”:

(b) by deleting sub clause (3) and substituting for it the following:

“(3) For the purpose of implementation of subsection (2), judicial bodies or other bodies established in the United

Republic and application of laws of Tanzania shall be acknowledged and incorporated in any arrangement or agreement.”

I: By inserting after Clause 13 the following Schedules:

---

**FIRST SCHEDULE**

---

*(Made under section 4(3))*

---

1962 UN GENERAL ASSEMBLY RESOLUTION ON PERMANENT SOVEREIGNTY OVER NATURAL RESOURCES (GAR 1803)

The General Assembly,

Recalling its resolutions 523(VI) of 12 January 1952 and 626(VII) of 21 December 1952,

Bearing in mind its resolution 1314(XIII) of 12 December 1958, by which it established the Commission on Permanent Sovereignty over Natural Resources and instructed it to conduct a full survey of the status of permanent sovereignty over natural wealth and resources as a basic constituent of the right to self-determination, with recommendations, where necessary, for its strengthening, and decided further that, in the conduct of the full survey of the status of the permanent sovereignty of peoples and nations over their natural wealth and resources, due regard should be paid to the rights and duties of States under international law and to the importance of encouraging international co-operation in the economic development of developing countries,

Bearing in mind its resolution 1515(XV) of 15 December 1960, in which it recommended that the sovereign right of every State to dispose of its wealth and its natural resources should be respected,

Considering that any measure in this respect must be based on the recognition of the inalienable right of all States freely to dispose of their natural wealth and resources in accordance with their national interests, and on respect for the economic independence of States,

Considering that nothing in paragraph 4 below in any way prejudices the position of any Member State on any aspect of the question of the rights and obligations of successor States and Governments in respect of property acquired before the accession to complete sovereignty of countries formerly under colonial rule,

Noting that the subject of succession of States and Governments is being examined as a matter of priority by the International Law Commission,

Considering that it is desirable to promote international co-operation for the economic development of developing countries, and that economic and financial agreements between the developed and the developing countries must be based on the principles of equality and of the right of peoples and nations to self-determination,

Considering that the provision of economic and technical assistance, loans and increased foreign investment must not be subject to conditions which conflict with the interests of the recipient State,

Considering the benefits to be derived from exchanges of technical and scientific information likely to promote the development and use of such resources and wealth, and the important part which the United Nations and other international organizations are called upon to play in that connection,

Attaching particular importance to the question of promoting the economic development of developing countries and securing their economic independence,

Noting that the creation and strengthening of the inalienable sovereignty of States over their natural wealth and resources reinforces their economic independence,

Desiring that there should be further consideration by the United Nations of the subject of permanent sovereignty over natural resources in the spirit of international co-operation in the field of economic development, particularly that of the developing countries.

## **PART I**

Declares that:

1. The right of peoples and nations to permanent sovereignty over their natural wealth and resources must be exercised in the interest of their national development and of the well-being of the people of the State concerned.

2. The exploration, development and disposition of such resources, as well as the import of the foreign capital required for these purposes, should be in conformity with the rules and conditions which the peoples and nations freely consider to be necessary or desirable with regard to the authorization, restriction or prohibition of such activities.

3. In cases where authorization is granted, the capital imported and the earnings on that capital shall be governed by the terms thereof, by the national legislation in force, and by international law. The profits derived must be shared in the proportions freely agreed upon, in each case, between the investors and the recipient State, due care being taken to ensure that there is no impairment, for any reason, of that State's sovereignty over its natural wealth and resources.

4. Nationalization, expropriation or requisitioning shall be based on grounds or reasons of public utility, security or the national interest which are recognized as overriding purely individual or private interests, both domestic and

foreign. In such cases the owner shall be paid appropriate compensation, in accordance with the rules in force in the State taking such measures in the exercise of its sovereignty and in accordance with international law. In any case where the question of compensation gives rise to a controversy, the national jurisdiction of the State taking such measures shall be exhausted. However, upon agreement by sovereign States and other parties concerned, settlement of the dispute should be made through arbitration or international adjudication.

5. The free and beneficial exercise of the sovereignty of peoples and nations over their natural resources must be furthered by the mutual respect of States based on their sovereign equality.

6. International co-operation for the economic development of developing countries, whether in the form of public or private capital investments, exchange of goods and services, technical assistance, or exchange of scientific information, shall be such as to further their independent national development and shall be based upon respect for their sovereignty over their natural wealth and resources.

7. Violation of the rights of peoples and nations to sovereignty over their natural wealth and resources is contrary to the spirit and principles of the Charter of the United Nations and hinders the development of international co-operation and the maintenance of peace.

8. Foreign investment agreements freely entered into by or between sovereign States shall be observed in good faith; States and international organizations shall strictly and conscientiously respect the sovereignty of peoples and nations over their natural wealth and resources in accordance with the Charter and the principles set forth in the present resolution.

## PART II

Welcomes the decision of the International Law Commission to speed up its work on the codification of the topic of responsibility of States for the consideration of the General Assembly.

## PART III

Requests the Secretary-General to continue the study of the various aspects of permanent sovereignty over natural resources, taking into account the desire of Member States to ensure the protection of their sovereign rights while encouraging international co-operation in the field of economic development, and to report to the Economic and Social Council and to the General Assembly, if possible at its eighteenth session.

---

## SECOND SCHEDULE

---

*(Made under section 4(3))*

---

### **CHARTER OF ECONOMIC RIGHTS AND DUTIES OF STATES GA Res. 3281(xxix), UN GAOR, 29th Sess., Supp. No. 31 (1974) 50**

The General Assembly,

RECALLING that the United Nations Conference on Trade and Development, in its resolution 45(III) of 18 May 1972, stressed the urgency to establish generally accepted norms to govern international economic relations systematically and recognized that it is not feasible to establish a just order and a stable worked as long as a charger to protect the rights of all countries, and in particular the developing States, is not formulated.



RECALLING FURTHER that in the same resolution it was decided to establish a Working Group of governmental representatives to draw up a draft Charter of Economic Rights and Duties of States, which the General Assembly, in its resolution 3037(XXVII) of 19 December 1972, decided should be composed of forty Member States.

NOTING that, in its resolution 3082(XXVIII) of 6 December 1973, it reaffirmed its conviction of the urgent need to establish or improve norms of universal application for the development of international economic relations on a just and equitable basis and urged the Working Group on the Charter of Economic Rights and Duties of States to complete, as the first step in the codification and development of the matter, the elaboration of a final draft Charter of Economic Rights and Duties of States, to be considered and approved by the General Assembly at its twenty-ninth session.

BEARING IN MIND the spirit and terms of its resolutions 3201(S-VI) and 3202(S-VI) of 1 May 1974, containing, respectively, the Declaration and the Programmed of Action on the Establishment of a New International Economic Order, which underlined the vital importance of the Charter to be adopted by the General Assembly at its twenty-ninth session and stressed the fact that the Charter shall constitute an effective instrument towards the establishment of a new system of international economic relations based on equity, sovereign equality and interdependence of the interests of developed and developing countries.

HAVING EXAMINED the report of the Working Group on the Charter of Economic Rights and Duties of States on its fourth session, transmitted to the Generally Assembly by the Trade and Development Board at its fourteenth session.

EXPRESSING ITS APPRECIATION to the Working Group on the Charter of Economic Rights and Duties of States which, as a

result of the task performed in its four sessions held between February 1973 and June 1974, assembled the elements required for the completion and adoption of the Charter of Economic Rights and Duties at the twenty-ninth session of the General Assembly, as previously recommended.

ADOPTS AND SOLEMNLY PROCLAIMS the following Charter:

### **Charter of economic rights and duties of states**

Preamble

The General Assembly,

REAFFIRMING the fundamental purposes of the United Nations, in particular the maintenance of international peace and security, the development of friendly relations among nations and the achievement of international co-operation in solving international problems in the economic and social fields,

AFFIRMING the need for strengthening international co-operation for development,

DECLARING that it is a fundamental purpose of the present Charter to promote the establishment of the new international economic order, based on equality, sovereign equality, interdependence, common interest and co-operation among all States, irrespective of their economic and social systems,

Desirous of contributing to the criterion of conditions for:

(a) the attainment of wider prosperity among all countries and of higher standards of living for all peoples;

(b) the promotion by the entire international community of the economic and social progress of all countries, especially developing countries;

(c) the encouragement of co-operation, on the basis of mutual advantage and equitable benefits for all peace-loving States which are willing to carry out the provisions of the present Charter, in the economic, trade, scientific and technical fields, regardless of political, economic or social systems;

(d) the overcoming of main obstacles in the way of economic development of the developing countries;

(e) the acceleration of the economic growth of developing countries with a view to bridging the economic gap between developing and developed countries;

(f) the protection, preservation and enhancement of the environment.

MINDFUL of the need to establish and maintain a just and equitable economic and social order through:

(a) the achievement of more rational and equitable international economic relations and the encouragement of structural changes in the world economy;

(b) the creation of conditions which permit the further expansion of trade and intensification of economic co-operation among all nations;

(c) the strengthening of the economic independence of developing countries;

(d) the establishment and promotion of international economic relations, taking into account the agreed differences in development of the developing countries and their specific needs,

DETERMINED to promote collective economic security for development, in particular of the developing countries, with strict respect for the sovereign equality of each State and through the co-operation of the entire international community,

CONSIDERING that genuine co-operation among States, based on joint consideration of and concerted action regarding international economic problems, is essential for fulfilling the international community's common desire to achieve a just and rational development of all parts of the world.

STRESSING the importance of ensuring appropriate conditions for the conduct of normal economic relations among all States, irrespective of differences in social and economic systems, and for the full respect of the rights of all peoples, as well as strengthening instruments of international economic co-operation as a means for the consolidation of peace for the benefit of all.

CONVINCED of the need to develop a system of international economic relations on the basis of sovereign equality, mutual and equitable benefit and the close interrelationship of the interests of all States,

REITERATING that the responsibility for the development of every country rests primarily upon itself but that concomitant and effective international cooperation is an essential factor for the full achievement of its own development goals.

FIRMLY CONVINCED of the urgent need to evolve a substantially improved system of international economic relations,

SOLEMNLY ADOPTS the present Charter of Economic Rights and Duties of States.

## **CHAPTER I Fundamentals of international economic relations**

Economic as well as political and other relations among States shall be governed, *inter alia*, by the following principles:

- (a) Sovereignty, territorial integrity and political independence of States;
- (b) Sovereign equality of all States;
- (c) Non-aggression;
- (d) Non-intervention;
- (e) Mutual and equitable benefit;
- (f) Peaceful coexistence;
- (g) Equal rights and self-determination of peoples;
- (h) Peaceful settlement of disputes;
- (i) Remedying of injustices which have been brought about by force and which deprive a nation of the natural means necessary for its normal development;
- (j) Fulfillment in good faith of international obligations;
- (k) Respect for human rights and international obligations;
- (l) No attempt to seek hegemony and spheres of influence;
- (m) Promotion of international social justice;
- (n) International co-operation for development;
- (o) Free access to and from the sea by land-locked countries within the framework of the above principles.

## **CHAPTER II Economic rights and duties of states**

### **Article 1**

Every State has the sovereign and inalienable right to choose its economic system as well as its political, social and cultural systems in accordance with the will of its people, without outside interference, coercion or threat in any form whatsoever.

## **Article 2**

1. Every State has and shall freely exercise full permanent sovereignty, including possession, use and disposal, over all its wealth, natural resources and economic activities.

2. Each State has the right:

(a) to regulate and exercise authority over foreign investment within its national jurisdiction in accordance with its laws and regulations and in conformity with its national objectives and priorities. No State shall be compelled to grant preferential treatment to foreign investment;

(b) to regulate and supervise the activities of transnational corporations within its national jurisdiction and take measures to ensure that such activities comply with its laws, rules and regulations and conform with its economic and social policies. Transnational corporations shall not intervene in the internal affairs of a host State. Every State should, with full regard for its sovereign rights, cooperate with other States in the exercise of the right set forth in this subparagraph.

(c) to nationalize, expropriate or transfer ownership of foreign property, in which case appropriate compensation should be paid by the State adopting such measures, taking into account its relevant laws and regulations and all circumstances that the State considers pertinent. In any case where the question of compensation gives rise to a controversy, it shall be settled under the domestic law of the nationalizing State and by its tribunals, unless it is freely and mutually agreed by all States concerned that other peaceful means be sought on the basis of the sovereign equality of States and in accordance with the principle of free choice of means.

## **Article 3**

In the exploitation of natural resources shared by two or more countries, each State must co-operate on the basis of a system

of information and prior consultations in order to achieve optimum use of such resources without causing damage to the legitimate interest of others.

**Article 4**

Every State has the right to engage in international trade and other forms of economic co-operation irrespective of any differences in political, economic and social systems. No State shall be subjected to discrimination of any kind based solely on such differences. In the pursuit of international trade and other forms of economic co-operation, every State is free to choose the forms of organization of its foreign economic relations and to enter into bilateral and multilateral arrangements consistent with its international obligations and with the needs of international economic co-operation.

**Article 5**

All States have the right to associate in organizations of primary commodity producers in order to develop their national economies, to achieve stable financing for their development and, in pursuance of their aims, to assist in the promotion of sustained growth of the world economy. In particular accelerating the development of developing countries. Correspondingly, all States have the duty to respect that right by refraining from applying economic and political measures that would limit it.

**Article 6**

It is the duty of States to contribute to the development of international trade of goods, particularly by means of arrangements and by the conclusion of long-term multilateral commodity agreements, where appropriate, and taking into account the interest of producers and consumers. All States share the responsibility to promote the regular flow and access of all commercial goods traded at stable, remunerative and equitable prices, thus contributing to the equitable development of the world economy, taking into account, in particular, the interests of developing countries.

### **Article 7**

Every State has the primary responsibility to promote the economic, social and cultural development of its people. To this end, each State has the right and the responsibility to choose its means and goals of development, fully to mobilize and use its resources, to implement progressive economic and social reforms and to ensure the full participation of its people in the process and benefits of development. All States have the duty, individually and collectively, to co-operate in eliminating obstacles that hinder such mobilization and use.

### **Article 8**

States should co-operate in facilitating more rational and equitable international economic relations and in encouraging structural changes in the context of a balanced world economy in harmony with the needs and interests of all countries, especially developing countries, and should take appropriate measures to this end.

### **Article 9**

All States have the responsibility to co-operate in the economic, social, cultural, scientific and technological fields for the promotion of economic and social progress throughout the world, especially that of the developing countries.

### **Article 10**

All States are juridically equal and, as equal members of the international community, have the right to participate fully and effectively in the international decision-making process in the solution of world economic, financial and monetary problems, *inter alia*, through the appropriate international organizations in accordance with their existing and evolving rules, and to share in the benefits resulting therefrom.

### **Article 11**

All States should co-operate to strengthen and continuously improve the efficiency of international organizations in implementing measures to stimulate the general economic



progress of all countries, particularly of developing countries, and therefore should co-operate to adapt them, when appropriate, to the changing needs of international economic co-operation.

## Article 12

1. States have the right, in agreement with the parties concerned, to participate in subregional, regional interregional co-operation in the pursuit of their economic and social development. All States engaged in such co-operation have the duty to ensure that the policies of those groupings to which they belong correspond to the provisions of the present Charter and are outward-looking, consistent with their international obligations and with the needs of international economic co-operation, and have full regard for the legitimate interests of third countries, especially developing countries.

2. In the case of groupings to which the States concerned have transferred or may transfer certain competences as regards matters that come within the scope of the present Charter, its provisions shall also apply to those groupings in regard to such matters, consistent with the responsibilities of such States as members of such groupings. Those States shall co-operate in the observance by the groupings of the provisions of this Charter.

## Article 13

1. Every State has the right to benefit from the advances and development in science and technology for the acceleration of its economic and social development.

2. All States should promote international scientific and technological co-operation and the transfer of technology, with proper regard for all legitimate interests including, *inter alia*, the rights and duties of holders, suppliers and recipients of technology. In particular, all States should facilitate the

access of developing countries to the achievements of modern science and technology, the transfer of technology and the creation of indigenous technology for the benefit of the developing countries in forms and in accordance with procedures which are suited to their economies and their needs.

3. Accordingly, developed countries should co-operate with the developing countries in the establishment, strengthening and development of their scientific and technological infrastructures and their scientific research and technological activities so as to help to expand and transform the economies of developing countries.

4. All States should co-operate in research with a view to evolving further internationally accepted guidelines or regulations for the transfer of technology, taking fully into account the interest of developing countries.

#### **Article 14**

Every State has the duty to co-operate in promoting a steady and increasing expansion and liberalization of world trade and an improvement in the welfare and living standards of all peoples, in particular those of developing countries. Accordingly, all States should co-operate, *inter alia*, towards the progressive dismantling of obstacles to trade and the improvement of the international framework for the conduct of world trade and, to these ends, co-ordinated efforts shall be made to solve in an equitable way the trade problems of all countries, taking into account the specific trade problems of the developing countries. In this connexion, States shall take measures aimed at securing additional benefits for the international trade of developing countries so as to achieve a substantial increase in their foreign exchange earnings, the diversification of their exports, the acceleration of the rate of growth of their trade, taking into account their development needs, an improvement in the possibilities for these countries to participate in the expansion of world trade and a balance more favourable to developing countries in the sharing of the advantages result-

ing from this expansion, through, in the largest possible measure, a substantial improvement in the conditions of access for the products of interest to the developing countries and, wherever appropriate, measures designed to attain stable, equitable and remunerative prices for primary products.

### **Article 15**

All States have the duty to promote the achievement of general and complete disarmament under effective international control and to utilize the resources released by effective disarmament measures for the economic and social development of countries, allocating a substantial portion of such resources as additional means for the development needs of developing countries.

### **Article 16**

1. It is the right and duty of all States, individually and collectively, to eliminate colonialism, *apartheid*, racial discrimination, neo-colonialism and all forms of foreign aggression, occupation and domination, and the economic and social consequences thereof, as a prerequisite for development. States which practise such coercive policies are economically responsible to the countries, territories and peoples affected for the restitution and full compensation for the exploitation and depletion of, and damages to, the natural and all other resources of those countries, territories and peoples. It is the duty of all States to extend assistance to them.

2. No State has the right to promote or encourage investments that may constitute an obstacle to the liberation of a territory occupied by force.

### **Article 17**

International co-operation for development in the shared goal and common duty of all States. Every State should co-operate with the efforts of developing countries to

accelerate their economic and social development by providing favourable external conditions and by extending active assistance to them, consistent with their development needs and objectives, with strict respect for the sovereign equality of States and free of any conditions derogating from their sovereignty.

### **Article 18**

Developed countries should extend, improve and enlarge the system of generalized non-reciprocal and non-discriminatory tariff preferences to the developing countries consistent with the relevant agreed conclusions and relevant decisions as adopted on this subject, in the framework of the competent international organizations. Developed countries should also give serious consideration to the adoption of other differential measures, in areas where this is feasible and appropriate and in ways which will provide special and more favourable treatment, in order to meet the trade and development needs of the developing countries. In the conduct of international economic relations the developed countries should endeavour to avoid measures having a negative effect on the development of the national economies of the developing countries, as promoted by generalized tariff preferences and other generally agreed differential measures in their favour.

### **Article 19**

With a view to accelerating the economic growth of developing countries and bridging the economic gap between developed and developing countries, developed countries should grant generalized preferential, non-reciprocal and non-discriminatory treatment to developing countries in those fields of international economic cooperation where it may be feasible.

## **Article 20**

Developing countries should, in their efforts to increase their over-all trade, give due attention to the possibility of expanding their trade with socialist countries, by granting to these countries conditions for trade not inferior to those granted normally to the developed market economy countries.

## **Article 21**

Developing countries should endeavour to promote the expansion of their mutual trade and to this end may, in accordance with the existing and evolving provisions and procedures of international agreements where applicable, grant trade preferences to other developing countries without being obliged to extend such preferences to developed countries, provided these arrangements do not constitute an impediment to general trade liberalization and expansion.

## **Article 22**

1. All States should respond to the generally recognized or mutually agreed development needs and objectives of developing countries by promoting increased net flows of real resources to the developing countries from all sources, taking into account any obligations and commitments undertaken by the States concerned, in order to reinforce the efforts of developing countries to accelerate their economic and social development.

2. In this context, consistent with the aims and objectives mentioned above and taking into account any obligations and commitments undertaken in this regard, it should be their endeavour to increase the net amount of financial flows from official sources to developing countries and to improve the terms and conditions thereof.

3. The flow of development assistance resources should include economic and technical assistance.

### **Article 23**

To enhance the effective mobilization of their own resources, the developing countries should strengthen their economic co-operation and expand their mutual trade so as to accelerate their economic and social development. All countries, especially developed countries, individually as well as through the competent international organizations of which they are members, should provide appropriate and effective support and co-operation.

### **Article 24**

All States have the duty to conduct their mutual economic relations in a manner which takes into account the interest of other countries. In particular, all States should avoid prejudicing the interests of developing countries.

### **Article 25**

In furtherance of world economic development, the international community, especially its developed members, shall pay special attention to the particular needs and problems of the least developed among the developing countries, of land-locked developing countries and also island developing countries, with a view to helping them to overcome their particular difficulties and thus contribute to their economic and social development.

### **Article 26**

All States have the duty to coexist in tolerance and live together in peace, irrespective of differences in political, economic, social and cultural systems, and to facilitate trade between States having different economic and social systems. International trade should be conducted without prejudice to generalized non-discriminatory and non-reciprocal preferences in favour of developing countries, on the basis of mutual advantage, equitable benefits and the exchange of most-favoured-nation treatment.

## **Article 27**

1. Every State has the right to enjoy fully the benefits of world invisible trade and to engage in the expansion of such trade.

2. World invisible trade, based on efficiency and mutual and equitable benefit, furthering the expansion of the world economy, is the common goal of all States. The role of developing countries in world invisible trade should be enhanced and strengthened consistent with the above objectives, particular attention being paid to the special needs of developing countries.

3. All States should co-operate with developing countries in their endeavours to increase their capacity to earn foreign exchange from invisible transactions, in accordance with the potential and needs of each developing country and consistent with the objectives mentioned above.

## **Article 28**

All States have the duty to co-operate in achieving adjustments in the prices of exports of developing countries in relation to prices of their imports so as to promote just and equitable terms of trade for them, in a manner which is remunerative for producers and equitable for producers and consumers.

## **Chapter III Common responsibilities towards the international community**

### **Article 29**

The sea-bed and ocean floor and the subsoil thereof, beyond the limits of national jurisdiction, as well as the resources of the area, are the common heritage of mankind. On the basis of the principles adopted by the General Assembly in resolution 2749 (XXV) of 17 December 1970, all States

shall ensure that the exploration of the area and exploitation of its resources are carried out exclusively for peaceful purposes and that the benefits derived therefore are shared equitably by all States, taking into account the particular interest and needs of developing countries; an international regime applying to the area and its resources and including appropriate international machinery to give effect to its provisions shall be established by an international treaty of a universal character, generally agreed upon.

### **Article 30**

The protection, preservation and enhancement of the environment for the present and future generations is the responsibility of all States. All States shall endeavour to establish their own environment and development policies in conformity with such responsibility. The environmental policies of all States should enhance and not adversely affect the present and future development potential of developing countries. All States have the responsibility to ensure that activities within their jurisdiction or control do not cause damage to the environment of other States or of areas beyond the limits of national jurisdiction. All States should cooperate in evolving international norms and regulations in the field of the environment.

## **Chapter IV Final provisions**

### **Article 31**

All States have the duty to contribute to the balanced expansion of the world economy, taking duly into account the close interrelationship between the well-being of the developed countries and the growth and development of the developing countries, and the fact that the prosperity of the international community as a whole depends upon the prosperity of its constituent parts.



### **Article 32**

No State may use or encourage the use of economic, political or any other type of measures to coerce another State in order to obtain from it the subordination of the exercise of its sovereign rights.

### **Article 33**

1. Nothing in the present Charter shall be construed as impairing or derogating from the provisions of the Charter of the United Nations or actions taken into pursuance thereof.

2. IN their interpretation and application, the provisions of the present Charter are interrelated and each provision should be construed in the context of the other provisions.

### **Article 34**

An item on the Charter of Economic Rights and Duties of Sates shall be included in the agenda of the General Assembly at its thirtieth session, and thereafter on the agenda of every fifth session, In this way a systematic and comprehensive consideration of the implementation of the Charter, covering both progress achieved and any improvement and additions which might become necessary, would be carried out and appropriate measures recommended. Such consideration should take into account the evolution of all the economic, social, legal and other factors related to the principles upon which the present Charter is based and on its purpose." .

Dodoma,  
3<sup>rd</sup> July, 2017

PJAMK  
MoCLA

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY  
THE HON. PALAMAGAMBA J.A.M. KABUDI, THE MINISTER  
FOR CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE NATURAL  
WEALTH AND RESOURCES (PERMANENT SOVEREIGNTY)  
ACT, 2017"**

-----  
*(Made under S.O 88(6))*  
-----

The Bill entitled "The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017" is further amended as follows:

**A:** By adding immediately after paragraph **B** of the Schedule of Amendment a new paragraph **C** as follows:

"**C:** In Clause 3 by adding in its appropriate alphabetical order the following new definition:

" "Government" means the Government of the United Republic or the Revolutionary Government of Zanzibar as the case may be, and the corresponding Constitutions and institutions of the United Republic and Tanzania Zanzibar exercising powers or performing functions in relation to natural wealth and resources." "

**B:** By deleting the proposed paragraph B of the Schedule of amendment and substituting for it the following:

"**B:** by deleting Clause 2 the substituting for it the following:

"Application                    **2.** This Act shall, without prejudice to the authority of the Revolutionary Government of Zanzibar over ownership and control of its own national wealth and resources in accordance with the Constitution and the laws of Tanzania Zanzibar in relation to natural wealth and resources, apply to Mainland Tanzania as well as Tanzania Zanzibar." .

C: By renumbering paragraph C to paragraph I as paragraphs D to J respectively.

Dodoma,  
..... 2017

PJAMK  
MoCLA

**FURTHER FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED  
BY THE HON. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI, THE MINISTER  
FOR CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE SECOND  
READING OF THE BILL ENTITLED "THE NATURAL WEALTH AND  
RESOURCES (PERMANENT SOVEREIGNTY) ACT, 2017"**

-----  
*(Made under S.O 88(6))*  
-----

A Bill entitled "The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017." is further amended as follows:

A: In Clause 6(1) by deleting the words "and approved by the National Assembly" appearing after the word "secured".

Dodoma,  
3<sup>rd</sup> July, 2017

PJAMK  
MoCLA

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana kwa maelezo hayo. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*)**

*Preamble*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli nilileta marekebisho hayo kidogo kuongezea nguvu kwenye *preamble* ya Mheshimiwa Waziri japo alikuwa ameamini kwamba siitaki *preamble*, lakini nilileta marekebisho ya kuitia nguvu zaidi. Nimeona kwenye marekebisho ya Mheshimiwa Waziri ame-*incorporate* hiki ambacho nilikuwa nataka kiingizwe.

Kwa hiyo, tayari nakiona kwenye marekebisho ya Mheshimiwa Waziri ambapo hiyo *African Charter* aliacha nyuma na kwa umuhimu wake tuliona na yenyewe iingie, nashukuru. (*Makoff*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hivi, kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza na mimi mtu yeyote muungwana mtanizoea na upungufu wangu. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mtolea, aliniambia mara tu baada ya mjadala huu kuanza na namshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu yupo upande wa pili na nataka kuwa-*compliment* watu wa upande wa pili ambao Mungu amewajalia hekima na busara. Tumeongeza pia Ibara ya 17 na Ibara ya 21 ili kuboresha zaidi ambacho Mheshimiwa Mtolea alituletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. *(Makofi)*

*(Preamble iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda nichukue fursa hii kumshukuru Waziri kwa kufanya marekebisho ya yale ambayo niliyapendekeza. Kwa hiyo, namshukuru Waziri na naondoa hoja yangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, amekubali. Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mabadiliko ya Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe haupo kwenye...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** *No*, kifungu si tunachangia, si tunaruhusiwa kuchangia?

**MWENYEKITI:** Hapana, ni walioleta marekebisho kama wangetaka tuchangie ndiyo tungeingia kwenye mchango.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Nachangia marekebisho ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Hapana. Hayo ninayahoji tu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** *No, nachangia marekebisho ya Serikali nahitaji ufafanuzi.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in clause four* nilileta marekebisho ya kusema kwamba *in sub clause two of the clause four by deleting the words on behalf appearing before the word government and;* sasa kwenye *schedule* imekuja *before* lakini ni *after* ndiyo inatakiwa ikae hapa.

Kwa hiyo, naomba isomeke hivyo na kwa maana hiyo basi kifungu hicho kidogo cha pili kisomeke *the ownership and control of the natural wealth and resources shall be exercised by, and through the government in the interest of the people and the United Republic.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kutaka mapendekezo haya, naomba kifungu hiki kipokelewe na Serikali kama nilivyorekebisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sina hakika kama umeelewewa na Serikali. Mheshimiwa Waziri tafadhali ufafanuzi. Kabla ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kabwe Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi na nadhani utatuongoza vizuri pia

kuweza kufahamu kwamba hata kama hakuna *schedule of opinion*, kama Mheshimiwa Mbunge anahitaji ufafanuzi wa jambo kutoka kwa yeyote *whether* Serikali au Mbunge mwenye hoja anapaswa kupata huo ufafanuzi. Kifungu hiki cha 4(2)...

**MWENYEKITI:** Hapo hapo kabla hujaendelea hebu tujiweke sawa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** *Unless* nimesahau kidogo. Matarajio yangu ni kwamba *schedule of amendment* ya Serikali ni maeneo ambayo wameshakubaliana Serikali na Kamati kwa niaba yetu, kwamba Serikali haijapita tu dirishani kuja hapa. Ni vitu ambayo wamekaa, wakajadili, wakakubaliana na ndiyo ikaja hapa. Endelea tu. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ufafanuzi ninaouomba kwenye Kifungu hiki, kwenye sekta ya madini *ownership* kisheria ipo kwenye *mineral rights*. *Mineral right* inapotolewa ama kwa mtu au kwa kampuni ndiyo anakuwa *owner*. Namna ambavyo kifungu hiki kimekaa bado *exercising* ya hiyo *sovereignty* itakuwa *limited*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto *with due respect* nakuomba ukae tu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Naomba nipate ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto ninakuomba sana. Kwa sababu kilichoko mezani ni hoja ya Mheshimiwa Sabreena ambayo ndiyo iko hapa, sasa wewe unaanzisha nyingine sijui tuchukue hii ya kwako, yule ambaye ame-*submit* kabisa rasmi tumuache, hapo ndiyo taabu inapokuja. Kwa sababu suala lako nilidhani lina-*qualify* lile la Mheshimiwa Sabreena ndiyo maana nikakuruhusu labda ulitaka kuliweka vizuri zaidi. Kwa hiyo, tumuache kwanza Mheshimiwa

Sabreena apate majibu kwanza ya *issue* yake, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kutoa ufafanuzi.

Hoja ya Mheshimiwa Zitto anaiwahisha kwa sababu hapa hatujadili Muswada wa Madini, hiyo ni ya kesho ndiyo tunaweza tukajadili mambo ya *mineral rights* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini tunatumia neno *on behalf* kwa niaba, haya ni masharti ya Kikatiba. Kwa hiyo, mkiisoma hii *preamble* inazungumza juu ya Ibara ya 8, Ibara ya 9 na Ibara ya 27 za Katiba. Sasa kwenye Ibara ya 8(1) ya Katiba inasema hivi: (a) wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata Madaraka na Mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii. Kwa hiyo, tayari wananchi ni hii Serikali ndiyo wameikasimu madaraka kufanya kwa niaba yao, ndiyo msingi wa kusema kwamba kwa niaba ya wananchi, ndiyo msingi wa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Sabreena Sungura uikubali hoja ya Serikali kama ilivyo kwenye mapendekezo ya Muswada ambayo kama ulivyosema kwamba Kamati yote mlkubaliana jana, naomba kushauri.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu hayo kwa kweli bado sija kubaliana nayo na ni kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu miaka mingi tumekuwa tukitumia sheria zetu tunaandika *on behalf* lakini tumeshuhudia kabisa Watanzania sehemu mbalimbali wakiathirika na makubaliano yanayofanyika kwenye mikataba ya madini, tumeshuhudia Watanzania wakifa, wakiumwa, wakibakia na ulemavu na kupata madhara mbalimbali kutokana na mikataba hii.



Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kwa kuwa tumekuwa tukitumia *on behalf* hata kwenye Kamati zako za Bunge, tumesema Kamati za Bunge zitakuwa zinafanya kazi kwa niaba ya Bunge zima, lakini ukiangalia kwa jicho la undani zaidi, unaona kabisa kwamba hata Kamati za Bunge zina-*ownership*, anapokuja Mjumbe kutoka nje ya Kamati ile kuna haki nyingine bado anakuwa hapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitumia *in the interest*, kwa maslahi italetwa maana zaidi kuliko tukitumia *on behalf*, lakini hata tukiangalia Sheria yetu ya Ardhi *Cap. 113* tumempa mamlaka Mheshimiwa Rais ya kumiliki...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sabreena kidogo tu nikusaidie, nitakupa tu nafasi uendele. Kama nimemuelewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, neno hili lililotumika ni la Kikatiba sasa kama hivyo ndivyo, sasa unaweza ukaendelea.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hiyo Ibara ya Katiba ambayo inatoa *requirement* kwamba kwenye sheria zetu tutumie *on behalf*, mimi sijaiona labda angeweza kutusaidia kama ana maelezo zaidi ili niweze kukubaliana na hilo, mimi binafsi Katiba ninayo hapa sijaiona, ndiyo maana nataka nitoe hoja kwamba suala hili lijadiliwe na Bunge lako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali urudie kwa mara nyingine.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hivi, ukisoma huu Muswada na Muswada mwingine wowote hata unaokuja kuna maelezo ya utangulizi pale kwa kiingereza wanaita *preamble*. Pale tumefanya rejea kwenye Ibara kadhaa za Katiba. Moja ni Ibara ya 8, Ibara ya 9 na Ibara ya 27; ukisoma hizo Ibara zote *in its totality* unaona jinsi Serikali inavyopaswa kufanya na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia ustawi wa wananchi. Hata hii Ibara ya 8(1)(a) inasema wananchi ndiyo msingi wa Mamlaka yote na Serikali itapata Madaraka na Mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa

Katiba hii. (b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi.

*So, that is the interest ambayo anaizungumza, (c) Serikali itawajibika kwa wananchi; na (d) wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali kwa mujibu wa Katiba hii, ndiyo sasa ninyi Wabunge mnawawakilisha. That is the essence of our submission. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri Mheshimiwa Sabreena Sungura, msomi Mwanasheria, hiki kitu kinakushindaje kukielewa? (Makofi)

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuendelee, nakubaliana na hilo. (Makofi)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hiki cha tano nahitaji marekebisho yanayokusudia kumpunguzia Rais madaraka yake na hivyo madaraka hayo kuyakabidhi kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 8 ambayo ameinukuu sasa hivi, rafiki yangu Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwamba wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka wananchi wakabidhi Serikali madaraka yote haya, kwamba mali zote za nchi hii, wananchi wazikabidhi kwa Serikali yao. Hili tunazungumza leo, tukiwa tuna Rais ambaye ana uzalendo, hapo baadaye tunaweza tukafika hatua tukaingia kwenye mikono ya Rais asiye na uzalendo na mali zile tukawa tumemkabidhi yeye akazifanya za kwake badala ya kuwa mali ya wananchi...

**MWENYEKITI:** Mwalimu samahani kidogo, hii ya kwako si ndiyo ile ile ya Sabreena? Mlikuwa mnaandika mpo pamoja au ilikuwaje? Maana yake *theme* ni ile sijui kama ni kitu kipya, wote mnasisitiza neno *in the interest*. Hebu endelea kusema. Someni wale ambao mnazo.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niisome *in sub clause two of clause five by deleting the word President*, hapa na-*delete President*, Sabreena haku-*delete President*; nina-*delete President appearing before the word on*, and after the word *the*, and replacing it with the word *government*; hapo ndipo inapokaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *five* na ya Mheshimiwa Sabreena ilikuwa *four...* (Makofi)

**MWENYEKITI:** Endelea kusoma mpaka mwisho.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** *Yes, and also by deleting the word, on behalf appearing after the word President and before the word of, and replace it with the word in the interest kwenye clause five.* (Makofi)

**MWENYEKITI:** Sasa na Mheshimiwa Sabreena anasema *delete the words on behalf and replace it with the words in the interest*, ndiyo maana nikasema kama vile mlikuwa pamoja. (Kicheko)

Kwa hiyo, hili la pili Bunge lilikwishaamua kulikubali hatutalijadili. Basi tu-*discuss* lile la *government*. Nilichoshangaa tu ni kwa nini vitu hivi viwe *so parallel* kama vile, na mimi sina taarifa, mimi ndiyo Spika wenu, sina taarifa.

Mheshimiwa Mwalimu, endelea na lile la kwanza la *Government*.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa hapa ni namna ambavyo tunaweza tukawa na Rais baadaye huko mbele akaja akawa kama Iddi Amin au akina Mobutu Sese kule Congo jirani zangu,

ambao walifanya mali za nchi zikawa za kwao binafsi, kwa sababu tu zilikuwa zinataja ziwe mali zao. Sasa hili ni vema tukakabidhi mali hizi kwenye Serikali, wananchi wakabidhiwe mali zao kwa mujibu wa Katiba hii wazikabidhi kwenye Serikali itakayokuwa madarakani na siyo lazima atajwe Rais, ili Rais asiye aka-*monopolise*.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka. Nadhani Waheshimiwa kwa sababu tunakwenda wote kwa pamoja, ningependa sana mjadala huu uwe wa wote. Anachosema Mheshimiwa Mwalimu, pale liondoke neno Rais ambalo yeye hana imani nalo, lakini tuweke neno Serikali, likiwekwa neno Serikali yeye anakuwa *comfortable* zaidi.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri hivi; pengine Mheshimiwa Bilago angekuwa ameisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 33 ambayo inasema hivi;

(1) Kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, (2) Rais atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Tafsiri ya Serikali imefanywa kwenye Ibara ya 152. Kwa hiyo, hata unakosema Serikali, huyo ndiyo Kiongozi wa Serikali na ndiyo Mkuu wa Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefafanua vizuri sana wakati wa *winding up*, na kwa nini Rais? Rais ndiyo Mkuu wa Nchi (*Head of State*). Hapa ni mkataba unaozungumza *sovereignty*, mamlaka ya nchi, *interface* ya wananchi wa Tanzania na Mataifa mengine katika Jumuiya ya Kimataifa ni Rais, siyo Bunge wala nini. Rais kama *Head of State*, Rais kama Mkuu wa Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba kushauri, Mheshimiwa Mwalimu Bilago ni mtu makini sana na ndiyo

maana ni mwalimu, amefundisha wanafunzi wengi hata humu ndani. Naomba kushauri Mheshimiwa Bilago aizingatie hii hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, hapa Rais siyo mmiliki na Waziri amefafanua ni mdhamini tu kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ahsante sana. Mwalimu nafikiri...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa, kama vyombo vyote vinafanya kazi vizuri, Bunge na Mahakama vinafanya kazi vizuri, Rais akikabidhiwa hizi mali aka-*misbehave*, kuna jambo litafanyika juu yake, lakini kama vyombo hivi vitakuwa dhaifu tunaweza tukapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili lijadiliwe, naomba kutoa hoja.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Sasa mnataka kujadili nini? Sijaelewa kabisa. Kaeni, nawaona, lakini tuelewane kidogo, si mnajua mbele kuna *guillotine*, huenda kuna mambo ya maana humu. Kwa hiyo, yako mambo kaeni tu mimi nimeshawaona wote mliosimama. Angalau ungekuwa unasema, mfano tu, kwamba liondolewe neno Rais liwekwe neno Bunge, lakini unasema liondolewe neno Rais liwekwe neno Serikali wakati Rais ni Mkuu wa Serikali hiyo hiyo, halafu mnataka tujadili. Unataka uonekane tu umeshinda? Sasa hiyo Serikali mkubwa wake nani? Sasa tukimtaja huyo mkubwa unasema aah, tumtaje mdogo. (*Makofi/Kicheko*)

Haya mnaotaka kujadili simameni tena sasa, na upande huu nimewaona. Huku nitachukua wawili na upande huu nitachukua wawili. Haya, nichukue mwanamke na

mwanaume. Nitachukua kwa CHADEMA nimeshataja Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Zitto Kabwe vyama tofauti *at least*, halafu na huku atakuwa Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais. Mheshimiwa Pauline.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Bilago kwamba Serikali wakubali kutoa neno Rais waweke neno Serikali kwa sababu Serikali ni *collectively*, Baraza la Mawaziri ni Serikali, badala ya kuacha kwa taasisi moja ya Rais. Najua Rais ni kiongozi wa Serikali, lakini mnaona siku hizi kadri siku zinavyoenda hata matamshi ya Serikali ni ya nani yanabadilika. Imefikia hatua mtu anasema Serikali yangu wala siyo ya chama ambacho ametokana nacho.

Kwa hiyo, ili kuangalia haya yote, hebu udhamini huu wa rasilimali za wananchi wa Tanzania tuwape Serikali iliyopo madarakani *collectively*, isiwe ni mtu mmoja na isiwe ni Taasisi ya Urais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Mwalimu, kutoa hilo neno la Urais tuweke Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Hoja ya Mheshimiwa Pauline ni kwamba anataka *collectivity*, kwa sababu kuna Baraza la Mawaziri ambalo hakuliona tu ni kwamba Baraza la Mawaziri linamshauri tu Rais, wala halina *role* nyingine.

Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kabudi atakuwa anakumbuka Ripoti ya Tume ya Shivji kuhusu ardhi na mjadala mpana sana kuhusiana na *radical title*, mjadala ule bado haujafa kwa sababu yeye ni sehemu ya wataalam wa Hakiardhi wakati ule na nadhani bado anafuatilia masuala ya Hakiardhi. Kwa

hiyo, suala la kuanza taratibu kuondoa *trust* (dhamana) kuwa kwa Rais ni jambo ambalo linapaswa lianze kutekelezwa, kwa sababu huko tunakokwenda *supremacy* ya nchi haitakuwa tena *a Head of State, supremacy* ya nchi itakuwa ni wawakilishi wa wananchi ambao ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwalimu Bilago yeye anaomba kwamba ile *trust* tu-*move* kutoka kwa Rais twende Serikali kuelekea kwenda kwenye Bunge. Nitamkumbusha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kifungu cha Katiba ambacho ametuambia tusome kuhusu Serikali ni nini. Kifungu cha 34(2) kinasema; “Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatahusu utekelezaji na hifadhi ya Katiba.” Kwa hiyo hata Katiba hii haijawekwa kwenye *trust* ya Rais, imewekwa kwenye mamlaka ya Serikali, hifadhi ya Katiba imewekwa kwenye mamlaka ya Serikali. Sasa kwa *spirit* ile ya wataalam wetu, akina Mheshimiwa Profesa Kabudi kwenye *radical title* kwenye ardhi, tuanze kuchukua wazo la Mheshimiwa Mwalimu Bilago...

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa naipokea, Mheshimiwa Mbunge wa Sikonge.

## T A A R I F A

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Msemaji anayeendelea kuzungumza kwamba anaposoma 34(2) asome na 34(3) ambayo nadhani akiisoma itakuwa vizuri zaidi ili Bunge liweze kuelewa vizuri kuliko anavyoendelea kupotosha. Ahsante sana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba atoe maneno kupotosha, mimi sipotoshi hapa. Atoe kwanza neno kupotosha mimi ninachangia kama

Mbunge tafadhali, ninakuheshimu sana Mheshimiwa Kakunda, futa hiyo kupotosha kwanza, tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge wa Sikonge.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapotosha anaposoma kipengele hicho tu, bila kumalizia kile cha (3) kinachosema mamlaka yote ya nchi yatakuwa mikononi mwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ninakuomba Mheshimiwa Kakunda, wewe usome cha kifungu cha (2) na usome kifungu cha (3), wewe mwenyewe kwanza ili utuweke sawa. Nakuomba usome kwa sababu siyo kila mtu ana Katiba hapa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo Katiba.

**MWENYEKITI:** Endelea, kile alichokisoma Mheshimiwa Zitto na hicho unachotaka kusema na uongeze na kifungu cha (4).

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosoma Mheshimiwa Zitto, 34(2); "Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatahusu utekelezaji na hifadhi ya Katiba hii na pia mambo mengineyo yote ambayo Bunge lina mamlaka ya kuyatungia sharia. Kifungu cha 34(3) kinasema: Mamlaka yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano, na pia juu ya mambo mengineyo yote yahusuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Rais wa Jamhuri ya Muungano" *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani niishie hapo.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mbunge wa Sikonge asome kifungu cha Katiba 34(5)(b)...



(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

**MWENYEKITI:** Sasa na wewe usome kama alivyosoma yeye.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsomea, ninaomba tu Waheshimiwa Wabunge tuheshimu mijadala, tunajadiliana hapa, haya mambo ya kuzomeazomea ni tabia za hovyoy kabisa.

**MWENYEKITI:** Mimi ndiyo nimekuruhusu, endelea Mheshimiwa Zitto usiwafuate hawa Wabunge...

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Kifungu cha 34(5)kinasomeka: "Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Ibara hii hayatahesabiwa kwamba; (b) yanalizuia Bunge kukabidhi madaraka yoyote ya kisheria mikononi mwa mtu au watu au mamlaka yoyote ambayo siyo Rais." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili linataka kukabidhi hili kwa Serikali na Katiba imetamka wazi, tunayo hayo mamlaka. Kwa hiyo, wazo la Mheshimiwa Mwalimu Bilago ni kukabidhi huko, tunapopaswa kuelekea mamlaka ya namna hii yanapaswa kukabidhiwa kwa Bunge, kwa sababu tunakwenda kwenye *Parliamentary Supremacy* na siyo *Presidential Supremacy* ambayo tunataka kuiendeleza katika Bunge hili, kama ningekuwa na mamlaka ya kufanya *amendment* ya wazo la Mheshimiwa Mwalimu Bilago ningesema hapa neno liwe Bunge na siyo Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda umeshapita. Ndiyo maana nilimwambia Mheshimiwa Mwalimu mwanzoni, kwamba ungekuwa umeweka neno Bunge kungekuwa na hoja lakini hoja ya Rais na Serikali, ni hoja iko *very weak*.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nilikuruhusu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo hapa ni tafsiri ya neno *trusteeship*. Neno hili lilitumika zamani kidogo, na mtu wa kwanza kuasisi neno hili na matumizi yake ni Gandhi. *Trusteeship* haimaanishi mtu huyo anapewa, yeye anahifadhi, anatumiza, anaweka salama. Sasa, hapa kinachochanganya ni kwamba wanadhani kama mtu ni *trustee* anaweza akafanya anavyotaka, ndiyo maana Mheshimiwa Profesa Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria anasema zipo kesi, na ni kesi ile ya *Patman Garments* ambayo imewahi ku-*override* uamuzi wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tusipate hofu kwa sababu huyu Rais anayezungumzwa hapatikani kienyeji, anapatikana kwa mchakato na anakuwa ameridhiwa na kuaminika kuliko yeyote yule katika nchi. Nazungumzia nchi ya kidemokrasia kama ya Tanzania, ambayo upatikanaji wa Rais hauwi wa mapinduzi, anapatikana kwa njia ya kidemokrasia na ameaminika kuliko mtu yeyote. Huyu ndiye Rais ninayemzungumzia hapa, ambaye kwenye sheria nyingine, kwa mfano Sheria ya Ardhi kifungu cha nne, tumemkabidhi ardhi yote ya Tanzania kuwa *trustee*, kwa sababu hiyo anapotokea mtu yeyote anataka kufanya visivyo kwenye ardhi yeye kwa dhamana ile aliyopewa anairejesha, umesikia Rais anafuta hati anairejesha Serikalini, hafanyi hovy, ndiye anayeaminika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninyi mnasema tu-*trust* sijui Bunge, tu-*trust*, huyu anasema for *people's interest, trusts*. *You know* maana yake ni nini? ikitokea la kutokea mitishe *referendum* ili muweze kubadilisha huo uamuzi maana *interest* bado ina watu, hakukabidhiwa mtu anayeweza akaamua kwa haraka na mara moja kulinda yale maslahi. Sijui ninaeleweka? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika hoja hii aliyotoa Mheshimiwa Zitto, alipo-*cite* Ibara ya 34(4) kuhusiana na madaraka ya Mheshimiwa Rais, hapa yeye ame-*cite* madaraka lakini ukiangalia tunaongelea mamlaka, na mamlaka ya Serikali yako chini ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia dhana nzima duniani kote ya masuala ya udhamini wa rasilimali za Taifa na maliasili, yamewekwa chini ya Mkuu wa nchi na kiongozi wa nchi. Ukiangalia kwetu Mkuu wetu wa nchi hata ukiangalia Ibara ya 33 (2) ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, niombe sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kweli hatuna haja ya kupoteza muda kwenye eneo hili, tuwe na imani, tuamini Mheshimiwa Rais anayo hayo mamlaka na tumempa wenyewe Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Rais ni taasisi hatekelezi mwenyewe, mwisho wa siku ikitokea kuna lolote, zipo *power za impeachment* ikitokea kuna mambo yoyote hayajaenda sawa. Tumuumini anashikilia tu kwa udhamini kwa niaba ya wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mapendekezo ya Serikali kama yalivyowasilishwa ndiyo yaweze kuchukuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu, nafikiri umeridhika kwamba hoja yako imejadiliwa sana kwa mapana, sasa kwa muda mfupi tafadhali, unasemaje.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu bado iko palepale kwamba nilitaka dhamana hii kubwa ipewe Serikali, chombo kama taasisi. Kwa hiyo, naomba iamuliwe kwa kura.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, umeshaeleweka maana yake ulishafafanua. Sasa ni wakati wa Wajumbe kuamua.

Nitawahoji kwa wanaoafiki hoja ya mtoa hoja kwanza, Mheshimiwa Mwalimu Bilago, waseme ndiyo, halafu baadaye nitawahoji wasioafikiana naye, nadhani tumeelewana.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi hoja yangu ipo katika Ibara ya tano ya Muswada na ninaomba niisome kama ifuatavyo na inasema; *in sub-clause three of clause five, by deleting the word on behalf appearing before the word government and after the word of, and replace it with the word in the interest, and also by adding the words in consultation with the Local Authority where the natural resources are found.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisema hii kwa sababu yamejitokeza maeneo mengi panapojitokeza madini wananchi wamekuwa...

**MWENYEKITI:** Hebu ngoja kidogo Mheshimiwa Mbarouk. Ili twende vizuri nadhani angeanza Mheshimiwa Upendo Peneza kwa sababu ya kwake ni 5(2).

Mheshimiwa Mbarouk, nadhani tunakubaliana. Maana yake mabadiliko yako ni kama yapo mbele zaidi kidogo. Ahsante sana. Mheshimiwa Upendo ungeanza kwanza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi la kwangu ni katika hiyohiyo *sub-clause two* katika *clause five* na *suggestion* yangu ni kutoa neno *the President* na ku-*replace* na neno *the government*. Hoja yangu hapa ni pamoja maneno ambayo

ameyasema Mheshimiwa Waziri kwamba Rais ni mtu ambaye ameaminika kuliko...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo, hilo limekwishaamuliwa, *by default* limekwishaamuliwa tayari, kwa sababu mjadala ni ule. Lile la Mheshimiwa Mwalimu Bilago limefanya hata kwako, maana yake ni yaleyale kabisa.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk sasa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwanza, maana yangu ni kuwa kwa nini nimeongeza haya maneno au *sentence; in consultation with the Local Authority where the natural resources are found*. Kwa sababu mara nyingi imejitokeza, kwanza wananchi au wachimbaji wadogo ndiyo ambao wanakuwa wagunduzi wa madini, lakini matokeo yake wakati mwingine wanaondolewa wanapokuja wawekezaji wakubwa, pia maeneo mengi wale wananchi wa maeneo husika yanapogundulika madini hawashirikishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa nataka wananchi katika maeneo ambayo madini yanagundulika nao washirikishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk, bado kidogo ili tuelewane vizuri, rudia tu kwa kifupi sana. Ninapotaka utufafanulie kwa kifupi tu kwamba hata hawa wananchi wa chini huku, sio kupitia Serikali zao za Mitaa ndiyo Serikali hiyo hiyo au? Hebu iweke vizuri.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine mambo yanaanzia juu, kule chini yanapelekwa wakati wale wananchi hawashirikishwi moja

kwa moja. Sasa mimi nataka pale ambapo madini yanagundulika basi wale wananchi wa eneo husika panapogundulika madini na wao washirikishwe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kupitia taasisi ipi, huko kwa wananchi? Ukisema wananchi tu itakuwa haieleweki, kupitia taasisi ipi?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *Local Government*.

**MWENYEKITI:** Kupitia *Local Government*.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Eeeh.

**MWENYEKITI:** Ambayo ni Serikali hiyo hiyo. Haya, Mheshimiwa Waziri...

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maana hiyo.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba maneno hayo yasiongezwe, ndiyo. Teende tuangalie *interpretation ya natural wealth and resources*, hivyo *air space* utashauri *Local Government* ipi? *Exclusive Economic Zone* utashauriana na Serikali ya Mitaa ipi? *Genetic resources* utashauriana na Serikali ya Mitaa ipi? Bahari.

Kwa hiyo, ukiangalia tafsiri ya mali, hiyo ya madini isubiri kesho na kule utaratibu upo, hapa hatuzungumzii madini. *Micro-organisms* tumeziweka hapa utashauriwa na Serikali ya Mitaa ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ya madini yanakwenda kwenye sheria sekta. Sheria hii Waheshimiwa Wabunge ni *normative law* siyo *prescriptive law* inaweka *norms*, inaweka *standards*, mambo ya *operation* ni kwenye sheria ya sekta sasa hapa *air space*, hii ya Dodoma tutakaa

na wananchi wa Dodoma kwamba hii *air space* yetu, hizo *satellite* hizo zikaaje? *Demarcation* ya mwisho ya Mamlaka ya Halmashauri ya Dodoma Mjini kuhusu *air space* yanaishia wapi na ya Jamhuri ya Muungano yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia maji ya baharini angalia *Exclusive economic Zone*, rudi kwenye Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act 1982*, Mamlaka yale amepewa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naamini kabisa Mheshimiwa Mbarouk ameelewa. Mheshimiwa Mbarouk tafadhali tuokolee muda.

**MHE. BAKARI M. MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi pia napenda tutumie muda vizuri, ukisikiliza haya maneno kwa makini labda Mheshimiwa Waziri hakuyasikiliza maneno yangu naomba niyarudie: "*In consultation with the Local Authority where the natural resouces,*" sikutaja madini peke yake, ukitaja *natural resources* maana yake ni rasilimali nyingi sasa labda anielewe vizuri hapo.

**MWENYEKITI:** Ni kweli maelezo hayo Mheshimiwa Mbarouk hujaelewa? Majirani hamuwezi kumwambia kweli? Si ndiyo hizo umetolewa mfano *natural resouces*/Kwa mfano, *micro-organisms* haya mimi nakupa moja. Wakisema *micro-organisms* wana maana ya *fungus*, wana maana ya *virus*, wana maana ya *bacteria*, haya niambie sasa hapo! Mambo mengine muwe mnakubali jamani tunaokoa muda.

Hii yaani inaweka ile *frame work*, *point* yako ni *point* kabisa ila siyo mahali pake, labda angalia pale kesho unaweza ukaiweka mahali yaani hakuna Mbunge atakataa habari ya wananchi kushirikishwa. Ushirikishwaji wa wananchi ndiyo sera yetu, Wabunge wote hawa lakini hapa kidogo siyo mahali pake kwa maana hiyo. Hatukatai hoja yako hapana.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nitasubiri mpaka kesho. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

**MWENYEKITI:** Nayaomba hayo marekebisho niyaone kabla sijawapa nafasi. Yanataka kufanana sana lakini yana tofauti ndogo sana lakini hii “*shall*” iko kote kote. Kwa hiyo, tukijadili mahali pamoja tutakuwa tumevuka, basi tuanze na ambae hajaongea sijui ni nani kati yao, haya mlivyojipanga aanze yeyote yule kati yenu.



**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Katika mabadiliko yangu nilitaka kutoa sehemu ambapo kumewekwa neno “*may*” katikati ya *resources* na *be* na badala yake ku-*replace* na neno “*shall*”, halafu katikati ya “*be*” na “*reviewed*” kuweka neno “*approved*” na kwa ujumla itasomeka; “*All arrangements or agreements entailing extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources shall be approved or reviewed by the National Assembly.*”

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeeleweka kabisa. *Almost* hapo hapo ambapo Mheshimiwa Cecilia Paresso ana *point* yake hapo hapo naomba na wewe uongeze hapo ili ijadiliwe kwa pamoja maana yake *almost* ni kitu hicho kama una tofauti au nini. Naona *almost point* inataka kufanana hivi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli napendekeza kwamba isomeke “*shall be reviewed and approved*” kwa hiyo, totafuti itauwepo pale kwa Mheshimiwa Peneza yeye amesema “*or review*” lakini mimi napendekeza “*shall be reviewed and approved by the National Assembly.*”

**MWENYEKITI:** Basi sasa mmojawapo aibebe, mmefanana kwa kweli pendekezo lenu ni zuri tu lakini limefanana. Kwa hiyo, mmoja alibebe sasa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tumeleta mapendekezo haya kwa sababu huko nyuma tumeshuhudia mara nyingi mikataba hii imekuwa ikiingiwa na Serikali kwa usiri mkubwa ambapo Bunge lilikuwa halina taarifa.

Na kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti wewe kama Spika wakati unatueleza kuhusu Miswada hii ulituambia sasa Muswada huu ni jambo zuri Bunge litakuwa lina taarifa na kwa vile mapendekezo ambayo yameletwa kwenye

Muswada huu inaweka neno “*may*” ambalo halina nguvu ya moja kwa moja kwa Serikali kuweza kuwajibika na kuleta Miswada hii ndani ya Bunge, ndiyo maana napendekeza isomeke neno la kisheria ambalo litakuwa na nguvu, liwekwe “*shall be approved and reviewed by the National Assembly*” kwa msingi ule kwamba mikataba mingi imekuwa ikifanyika, Bunge halifahamu kwa hiyo, ukija hapa tukiipitia na ku-*approve* basi Serikali itaendelea na utaratibu mwingine.

**MWENYEKITI:** Natumaini hoja yake tumeisikia. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hapa mara kadhaa kwamba hii ni sheria inaweka tu misingi (*frame work*), ukiangalia hii sheria sasa siyo ya *operations*. Hapa tunafanya *opening* Bunge kupata fursa ya ku-*review* hii mikataba utakuja kuiona hii kwenye sheria hii nyingine inayokuja, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hatuwezi kuliambisha Bunge ndiyo maana tunachosema “*may*” sasa tunaliambisha Bunge? Bunge lina namna yake yenyewe ya kufanya kazi, ndiyo msingi wenyewe huo. Pia hapa sasa inatoa *opening* kwa Bunge, lakini Bunge hili kuja ku-*review* mikataba ni wapi itakuwa ni hii sheria nyingine inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi rasilimali ambazo sasa zimekuwa *vested* kwa Rais kwa niaba ya wananchi, wananchi hao bado wa *surveillance* kupitia Bunge lao, ndiyo sababu tunafanya *opening* hapa, kwamba hizi rasilimali madaraka msiyaweke kwa Rais tu na wananchi pia kupitia Bunge lao. Hivyo, tunasema “*may*” *when necessary*. *When pale inapolazimika*, kwa hiyo ingekuwa na shida kwamba Bunge limefungwa kabisa ungesema “*shall not,*” sasa ukishapewa “*may*” si unaweza ku-*exercise when necessary, then how do you exercise this? You go to the other law* ambayo sasa inaweka na utaratibu mwingine wote kwenye hii sheria nyingine, ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, hivi mikataba hapa tuanze ku-*negotiate* hapa, halafu *oversight role* unaitoa wapi? Lazima tu-*maintain separation of power and then, if you want this then we are done*. Kwa sababu *there is no way now you can exonerate yourself whatever, bad agreement might get in* na ninyi mtakuwemo, sisi hatuko tayari kuona maslahi ya nchi hii yanafungwa. Halafu Bunge lenyewe kwanza mmegawanyika, *you have got so many interest*. Mko kwenye maslahi ya vyama, maslahi sijui ya Majimbo, *how did you negotiate?* Hata hapo naona mnajadili kwenye kitu cha msingi sana mmegawanyika, *how can we so much entrusted* na ku-*approve* mikataba na ku-*negotiate*, *the time is there?* (Makofi)

Naomba kushauri, hoja kama ilivyoletwa kwenye mapendekezo ya Serikali ni hoja nzuri na naomba sana Waheshimiwa Wabunge muikubali hii hoja ya Serikali na fursa hiyo mnayo kwa sababu *opening* inawekwa sasa, lakini kwenye Muswada huu unaofuatia wa *review* na *negotiation* ndiyo unaona sasa Bunge litakavyotekeleza Waziri atakapowaletea taarifa na Bunge mnakuwa na mamlaka ya kusema aah, ninyi bwana huu mkataba mlingia mkataba mbovu, nendeni una-*questionable terms*. Ahsante.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Gekul.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Parreso mwenye hoja yako.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi sijaridhika na maelezo ya AG na naomba Wabunge wachangie kwa sababu sijamuelewa anachokieleza, naomba nafasi Wabunge pia wachangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilitaka kidogo tumpe nafasi mtoa hoja kwa muda mfupi sana, nitatoa nafasi kama mtakuwa bado hamjaridhika kwa sababu Mheshimiwa Cecilia amesema neno moja kwamba hakuelewa yale maelezo ya mwanzo huenda yakifafanuliwa akaelewa anaweza akafikiri tofauti, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kwenye *concept ya supremacy of Parliament* tumekwenda kwenye *concept ya sovereignty of Parliament*. Sasa kwa sababu Bunge ni *sovereign*, haliwezi kutunga sheria ya kujiambia lenyewe “*shall*” hii ni *drafting* na naomba mnisamehe kwa unyenyekevu mkubwa sana. *Drafting* ni taaluma, kila *Drafter* ni Mwanasheria lakini siyo kila Mwanasheria ni *Drafter*, kwa unyenyekevu mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bunge haliwezi kusema ‘*shall*’ huwezi kuli amuru Bunge ni *sovereign* yaani ninyi mnataka mji amuru? Mshurutishwe? Haijatokea duniani chombo chenye mamlaka yake kikajiamuru, kwa sababu hiyo hili neno “*may*” ni heshima kwa Bunge. Bunge huwezi ukaliambia lazima, ukishaliambia “*may*” Bunge limebaki na mamlaka yake ya kudai chochote. Sheria hii inatungwa na Bunge. Ingekuwa ni Sheria ya Serikali ingeliambia Bunge “*shall*” lakini Bunge haliwezi kujiambia lenyewe “*shall*” inakuwa na ukakasi katika uandishi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa umeeleweka kabisa

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tu ni *sovereignty of the Parliament*, ndiyo maana tumeweka *the Parliament may*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba taarifa kidogo tupate ufafanuzi zaidi tunajielemisha, taarifa kidogo. Sasa nadhani Waziri kama *concept* ya *sovereignty of Parliament* ndiyo ambayo inachukuliwa *into this provision*, katika hii *bill* nzima hakuna mahali ambapo panataja hiyo *sovereignty of Parliament*. Tunaomba utusaidie ni kufungu gani katika hii *bill* ambacho angalau *even for influence* kinataja hiyo *sovereignty of Parliament* kwa sababu *with that sovereignty of Parliament* maelezo yako yanakuwa ni sahihi kabisa. Wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri atusaidie.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 63(2) imeeleza suala hili ni suala la Katiba, kwenye Muswada huu tumeandika *article* 63(2) na inasema hivi; "Sehemu ya Pili ya Bunge itakuwa ndiyo chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii." *Should we need to set this here?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaja vifungu vya Katiba kwenye *preambles* ndiyo maana huhitaji tena kuanza kuyanukuu yale yote pale, *you just go to the Constitution* na Katiba ndiyo sheria mama.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja Wabunge waweze kujadili.

**MWENYEKITI:** Aah, ama kweli! Ahsante nitawachukua ambao hawajaongea mpaka sasa. Mheshimiwa Shahari, Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hili kidogo linaingia kwenye ile *point* ambayo asubuhi nilizungumza hapa kuhusu uelewa wa pamoja, haya ndiyo mambo ambayo yalitakiwa yawe kwenye zoezi la mwanzo kabisa. Kwa sababu wakati mwingine tunakubali kweli *drafting* ni *profession* ya aina yake, lakini sisi wote ambao ni *Drafters* tulitaka kueleweshwa mapema. Je, kwa mfano, inapokuja *verb in a passive form* kama hii kwamba *it refer something else shall be done by somebody else*, sasa sisi tunaichukulia ile kwamba yanalazimishwa yale masuala na silazimishwi Mbunge, ndiyo *concept* ambayo sisi tumeielewa. Kwa hiyo, haya masuala mengine yote tunayalazimisha yapite kwenye Bunge na hutulazimishi Bunge lifanye, tulitaka hata *concept* kama hizi zieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mimi bado naona hili suala linahitaji kuwa katika *form* hiyo ambayo mtoa hoja amesema kwamba mikataba *shall be reviewed and approved by the Parliament*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo Mheshimiwa Shahari hata tunapopata *professional advice* bado tunaikataa tu? Mheshimiwa Heche.

**MHE JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 12 kinasema; *“All arrangement and agreement entailing extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources may be reviewed by the National Assembly” “may”*. Tunajua mikataba yote siku zote inaingwiwa na Serikali, hoja ambayo ipo hapa, ili mikataba inapoingwiwa na Serikali, mikataba hii Bunge liwe linaweza kuulazimisha Serikali iilete Bungeni kui-*review*, Bunge liwe na uwezo wa kupitia na ku-*review* ndiyo hoja ambayo iko hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, tatizo ni kwamba sijui kama tunasikilizana vizuri mwanzo hadi mwisho.

*Concept* ni hiyo unayosema, hakuna mtu anayebisha hilo unalolisema, unanielewa? Kilichoko hapa ni *professionalism* tu, kwamba wewe huwezi kujilazimishia yaani katika uandishi huwezi kujiamulia yaani unajipa amri kuwa mimi Heche kula, sasa unajiamrishaje? Ndiyo hoja iliyoko hapa.

Vinginevyo kama wewe unabisha utupe neno la kuweka pale yaani *professionally* haikubaliki wewe kujiamrisha, yaani sisi Bunge kujiamrisha sisi kwa sisi ndiyo tatizo lingine liko hapa ni tatizo la kiuandishi tu ndicho kinachoongelewa hapa. Pale unaposema basi mimi nakataa hilo, unatupa neno lingine la mbadala wake ili usionekane unajiamrisha sasa usemeje?

Mheshimiwa Heche bado nafasi ni ya kwako kama unataka kuongea kama umeridhika basi tumuite mwingine. Lugha iweje ili usionekane umejiamrisha wewe Bunge.

**MHE JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mimi kichwa changu kinagoma hayo maelezo unayonipa sikuelewi. Unaposema "*National Assembly may*" ina maana ni *option* iko pale kwamba inaweza ika-*review* au isi-*review*, lakini hii mikataba inaingiwa na Serikali siyo Bunge, sijui kama mimi naelewa vizuri na ninachokizungumza. Wanaoingia mikataba na wanaofanya *agreements* hizi na nini ni Serikali, sasa Bunge liwe na hiyo nafasi ya ulazima pale linapohitaji ku-*review* liagize lete hapa, lakini hao wanaweza kutumbia hatuleti kwa sababu hamna kitu kinacholazimisha hapa kuleta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche ni hivi, unachokisema ndiyo tunachokitaka sisi wote pamoja na Waziri, unanielewa? Ila hapa ni utamaduni wa wenzetu Waingereza, utamaduni wa Mwingereza ana lugha laini kwa Mheshimiwa. Mnaelewa ni kama lugha yenu na wa Kenya kwa mfano, jirani zetu, wapendwa wetu. Mkenya anasema "lete chai hapa", Mtanzania anasema "tafadhali naomba kikombe cha chai." (*Kicheko*)

Sasa Mwingereza ndiyo tafadhali yake hii *may*, kwa mtu mkubwa kama Bunge, mtu mkubwa kama Bunge haaambiwi *shall*, yaani ndiyo utamaduni tu unaongelewa hapa. Mheshimiwa Mpina. (Makofi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa maelezo yale ya matumizi ya *may* na *shall* nadhani yamewekwa vizuri na yameeleweka vizuri sana. Ninachotaka kukiongea hapa ni lile suala ambalo Mheshimiwa mtoa hoja analolozungumza la ku-*approve*, kwamba Bunge lipewe nafasi ya kua-*approve* mikataba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia suala la *oversight*, *oversight function* ipo kwa Bunge na imetajwa kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 63(2) ambayo inalipa mamlaka Bunge ku-*play* ile *oversight function*. Sasa ukishajingiza na wewe Bunge kwenye ku-*approve* mikataba, kwamba mikataba hii sasa inakuwa *approved* na Bunge, nani mwisho wa siku ata-*play oversight function*? *Suppose* Bunge limekosea nani ata-*play oversight function*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hapa tulichokifanya, nimeingia bungeni hapa 2005 nimekuta Wabunge wenzetu wakilalamikia hili, tukiwa na kina Mheshimiwa Zitto Kabwe wakilalamikia hili. Leo nafurahi kwamba niko miongoni hapa mwa Wabunge na Serikali kwamba hili jambo limeletwa walau Bunge sasa, linaweza lika-*review* mikataba. Kama tulivyoitengeneza *The Public Procurement Act* ambayo inawaruhusu watendaji wa Serikali kuendelea na manunuzi na kuendelea na mikataba, mwisho wa siku *Local Government* zinapitia ile mikataba kuona kama kuna makosa yoyote yamefanyika au kama kuna kasoro yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kukitokea na kasoro yoyote, Serikali yetu leo imefungua milango kwamba kama Bunge linaweza kuja kuona tatizo mahsusni linaweza sasa kuiagiza Serikali kwenda kufanya marekebisho. Leo marekebisho haya yanayopendekezwa ndiyo yanayojenga



msingi wa malalamiko baada ya kugundua kasoro. Bunge lisiingie kwenye *operation* badala yake libakize suala la *oversight function*, ukifanya hivyo utakuwa umevunja sheria na Katiba ya nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Cecilia kwa mara ya mwisho sasa. Hapa unatujibu tu kama unakubali au unakataa ili tupige kura. Kama umeafiki umerudisha au kama bado huafiki ili tunahoji tu.

**MHE: CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka kumuelewa kidogo Profesa pale, lakini hiyo *provision* ya Katiba anayosema ya 63 mfano inge-*appear* kabisa hapa pia ingeleta maana au ingekuwa kwenye *preamble* ili kuonesha hiyo Mamlaka ya Bunge katika masuala hayo, lakini hi haipo. Kwa hiyo, Bunge lako liamue.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kama tulivyofanya mwanzo, nitaanza na wanaoafiki na hoja na inayosimamiwa badiliko linalopendekezwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso na baadae nitahoji wale wanaokataa yaani wanaokataa badiliko hilo.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 13

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea, bado unaendelea au umeshakifuta, maana ulionyesha uungwana tangu mwanzo.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Waziri ani-*convince* kwa nini tusikiongeze hiki kifungu kama ambavyo nimependekeza hapo.

**MWENYEKITI:** Kama hauna pendekezo kuna kipande kipo hapa. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kimeshaingia kwenye *preamble* na ninaomba *Cap. 1*. Tukienda kwenye *Cap. 1* kifungu cha 25 kinasema: *"The preamble to a written law form part of the written law and shall be construed as a part thereof, intended to assist in explaining its purport and its object."* Sasa maadam tayari tumeshaikua hiyo na kimeshaingia kwenye *preamble* naomba kibaki kwenye *preamble* na hatuna sababu tena ya kukiingiza ndani, kwa sababu *preamble* kwa mujibu wa kifungu hiki ni sehemu ya sheria.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ndiyo nilitaka hayo maneno yaingie kwenye *Hansard* ili yaweze kuwa *record* kwamba sasa kifungu hiki kimepita kwenye *Preamble*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Siyo umetulia muda tu bure bwana. Hilo limekataliwa la kuongeza. (*Kicheko*)

*(Ibara Mpya ya 13 ilikataliwa kwa sababu ilishaingizwa kwenye preamble)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali Jipya la Kwanza

Jedwali Jipya la Pili

*(Majedwali Mapya yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge zima imemaliza kazi yake kwa Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resource (Permanent for the Sovereignty) Bill, 2017*).

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri Taarifa.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017*) Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria wa Mamlaka ya nchi, kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili wa mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*, kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsante sana. Katibu (*Makofi*)

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili na Kuweka

Masharti Yanahusianisha Misingi Iliyomo Katika Mkataba na Itifaki Mbalimbali ambazo Jamhuri ya Muungano Imetia Saini na Kuridhia *(A Bill for an Act to Make Provisions for the Integration of the Regional and International Agreements of the Country Permanent Sovereignty of the Natural Wealth and Resources.*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Taratibu zote za utungaji wa sheria sasa umekamilika, bado tu kupeleka Muswada huo mbele ya Mheshimiwa wa Rais wa Jamhuri ili ikimpendeza akiweka baraka zake, basi iweze kuwa ni sheria kamili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Katibu sasa tuendelee.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

*Preamble*

*(Preamble iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina marekebisho kwenye *title*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uwe na utulivu tu kidogo tutakufikia. Katibu.

Ibara ya 1

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo Peneza, nafikiri hapo ni sawa sasa tunaanzia kwako. Kifungu cha kwanza? Sawa endelea. (*Kicheko*)

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kurekebisha kwenye Jina la Muswada na kuongeza neno *approval*, halafu na *comma* (,) *comma as comma* siyo koma kwa maneno. *Comma* kama alama ya koma, na kisha isomeke *The National Wealth and Resources Contracts, (Approval, Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms, Act, 2017)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza mabadiliko haya kuanzia hapa kwenye *title* kama ambavyo tumekwisha ongelea katika *Bill* ambayo tumeshaipitisha hapa. Lengo langu ni kwamba Bunge kiwe ni chombo ambacho kinakuwa na uwezo wa kuweza ku-*approve* mikataba. Ndiyo maana nimependekeza kwamba tuanzie kwenye mabadiliko ya jina na huku ndani pia nimeweza kuongeza kifungu ambacho kitaweza ku-*support* hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa Upendo ili tuweke vizuri sasa, natumaini kila mtu ameshafungua vizuri, pendekezo lako tuweke vizuri, hatujakuelewa kabisa. Jaribu sasa kuliweka sawa sawa. Tunayo wote unataka hapa pasomeke vipi sasa, au lieleze unavyoona sawa wewe mwenyewe.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nafanya mabadiliko kwenye *title*, ambapo nimesema ninaongeza nena *approval* kwenye ile *heading* ambayo kwa maana yangu kwamba itakuwa *The Natural Wealth and Resources Contracts (Approval, Review and Re-negotiation*

of Unconscionable Terms) Act, 2017). Maana yangu ya kufanya hivyo ni kuhakikisha ya kwamba Bunge linakuwa na wajibu wa kuweza *ku-approve* mikataba hii. Ukisoma kwa ndani utaona ya kwamba mikataba hii inaletwa baada ya kuwe imeshasainiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mikataba inaletwa ndani ya Bunge, ikishasainiwa na Serikali, maana yake ni kwamba inawezekana kwamba wameshasaini mikataba ikiwa tayari ina matatizo. Kwa hiyo, bora basi Bunge ikawa ni chombo ambacho mikataba hii tutaridhia zile *terms*, tutaridhia mambo yote ambayo tutataka yasainiwe ndipo ambapo Serikali ikasaini na baadae sasa Serikali iweze kurudisha kwa ajili ya *review*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo, maneno ya *approval*/tulijadili kwenye hoja ya Mheshimiwa Cecilia Paresso ambaye mli-*share* pamoja hili jambo la *approval* tumekwisha limaliza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima zote kwako, nadhani huu ni Muswada Mpya na mjadala ni mpya, tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto tangu lini unakuwa na fujo tena na wewe kama umekuja...eeh! Kuna watu wanaruhusiwa kufanya fujo na wengine hawaruhusiwi. Ninyi hamuoni Mheshimiwa Mbowe ametulia jamani! Huo ndiyo mfano wa Mbunge mkongwe. (*Makofi/Kicheko*)

Haya, nafikiri Mheshimiwa Waziri tufafanulie tena. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba, *short title* ibaki ilivyo. Unajua *short title* haitakiwi kuwa *tautologous*, hiyo ni *tautology* unarudia jambo ambalo liko tayari *implicit*, sasa kwa nini Bunge lisi-*approve* hiyo mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wake ni Ibara ya 63, unajua unapo *approve* kitu, umekuwa sehemu ya ule uamuzi

huwezi tena kuja ukasema kina kasoro. Ni lazima ukae pembeni ili u-*exercise your oversight, once you approve, you are part and parcel of that decision, you can't vacate*. Ndiyo maana kwenye sheria tunawashauri Majaji wasi-*descend on the scene*, yaani asishuke kwenye tope. Sasa Bunge lishishuke kwenye tope, libaki pembeni liambie wewe Serikali umekosea karekebishe, kanawe. Bunge likiingia litakuwa sehemu ya tope hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge tayari litakuwa limejinyima nafasi ya kukosoa, kwa sababu limekuwa sehemu ya mchakato huo, sehemu ya maamuzi hayo, sehemu ya upuuzi huo, sehemu ya uhovyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Bunge lisi-*descend on the scene* inabidi libaki linatazama kwa sababu lina *role ya oversight* kazi ya kuingia na ku-*approve* ni kazi ya *Executive*. Ndiyo maana soma tena Ibara ya 63 inayolipa Bunge kazi ya kuwa *oversight*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Bunge limeamua liache kuwa *Oversight Institution* liwe *Executive* litakuwa ni Bunge la kwanza duniani kufanya hivyo ni hatari. Mimi siwezi kukubali kuwa Mbunge kwenye Bunge ambalo linaingia kwenye tope, acha Serikali iingie kwenye tope kwa nini? Ikiingia kwenye tope unaweza hata kumpigia *vote of no confidence* Waziri Mkuu Bunge utalipigia *vote of no confidence* wapi likikosea? *You can't*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chombo gani juu ya Bunge ambacho sasa Bunge limeingia topeni tunaliambia hicho chombo jamani hebu lishughulikieni Bunge. Bunge lina uwezo wa kuishughulikia Serikali, hata ukiipigia kura ya kutokuwa na imani.

Kwa hiyo, vitu vingine ndugu zangu kwa unyenyekevu mkubwa tuwaachie na tuwaamini tuliowapa dhamana ya kuandika hizi sheria.

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Upendo umeelewa kwa nini nilisema hili jambo shule ilishatolewa ya kutosha.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Hii shule ya leo muhimu sana kwa sababu siyo wengi wanajua haya mambo, ndiyo maana mnaona wengine wanakimbia kimbia huko barabarani huko wanajaribu kushtaki Bunge, hawajui Bunge ni kitu gani? Kwa hiyo, ni muhimu sana hii shule. *(Kicheko)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kichwa cha Sehemu ya Pili ya Muswada

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza hapo huna neno si ndiyo imebaki ya Serikali nisije nikakuruka.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *withdraw*. Ahsante.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*



Ibara ya 4

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yangu (c), (d), (e) na (f) naomba niyaondoe kwa sababu yote yanahusu masuala ya *approval*. Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

**MWENYEKITI:** Hiyo ya tano umetoa au bado? Mheshimiwa Upendo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana sijatoa. Hapa nataka kutoa neno *may* na kuweka neno *shall* ambayo *in clause 5(2) by the deleting the word "may" appears between the words it and a comma (,) kwenye it and a comma substuting it with the world shall.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki sasa kitasomeka; *"Where upon consideration of the report submitted pursuant to the subsection (1), the National Assembly finds that arrangement or contains uncounscionable terms, it shall by resolution, direct the government Initiate re- negotiation of the arrangement or agreement with a view to rectifying the terms."*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo hiyo si ndiyo tumetoka kujadili tena kwa undani kabisa, ndiyo ile ambayo mlijadili wote hapa hata Mheshimiwa Heche alisimama sana ni hiyo *shall* na *may* inayohusu Bunge.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la tofauti kwa sababu hapa tunachozungumzia sasa ni *report* ambayo itakuwa *submitted* kutoka kwenye upande wa Serikali kuja kwetu. Sasa tuseme kwamba ni *shall* lazima sasa ili Serikali iweze kuifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Kwani Mheshimiwa Upendo anaposema *it shall* anayeambiwa *it shall* ni nani? Jibu mwenyewe anayeambiwa *it shall* ni nani?

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kitu ambacho ningependa tuelewane kidogo hiki cha *yes*, sawa kwamba hatusemi kwamba *may* kwa maelezo ya Waziri aliyokuwa anatoa ni kwa upande wetu sasa kama *discussion* inakuja kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotoa hapa sasa ni makubaliano ambayo sisi Bunge tumefanya, ambayo tunai-*direct* Serikali kufanya baada ya kugundua kwamba kuna makosa ambayo yamefanyika kwenye mkataba. Sasa hatuwezi tukasema ni *may* kwa sababu tunataka sasa hizo *uncounsciounable terms* ziweze kubadilishwa, kwa hiyo nadhani itabidi iwe *shall*.

**MWENYEKITI:** Mjadala ni ule ule Mheshimiwa Upendo, mantiki ni ile ile, kitu ni kile kile, kutolilazimisha Bunge kwa kusema maneno shall. Tumeshafanya maamuzi na hilo tayari.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana. Hili hatulazimishi Bunge hili tunailazimisha Serikali sasa, ndiyo vitu viwili tofauti hapo, baada ya *discussion* kwa hiyo Bunge sasa tunailazimisha Serikali sasa ili iweze kufanyia kazi hayo mapendekezo ambayo yametolewa. Kwa hiyo, siyo upande wa Bunge.

**MWENYEKITI:** *The National Assembly .....it may*, wewe unasema *the National Assembly it shall*, si unalazimisha *National Assembly*?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, labda kwenye Muswada niusome kidogo, nisome tu hapo ulipoanzia, *the National Assembly*...

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo kuna taarifa hapo.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Upendo Peneza ana maudhui yale yale, lakini hasomi tu kwa utulivu ili aone anayeambiwa hiyo *mayna shall* ni nani? Sasa labda kwa faida tu ya wote niisome.

*"Where upon consideration of the report submitted pursuant to the subsection (1), the National Assembly finds that arrangements or agreements contain uncounscionable terms, it may, by resolution, direct the government."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hapa kuna maudhui makubwa sana, sasa ukisema *shall* sasa unalazimisha Bunge kwa hiyo maudhi anayosema Spika ndiyo yale, lakini *may* kwa tasfiri ya kisheria ni heshima kweli, yaani ni heshima sana, kwamba inampa sasa, maana jamani unajua hizi *resources* ni nyingi ziko kubwa, ndogo, ziko nyingi.

**MBUNGE FULANI:** Inatosha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Inatosha?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Ahsante sana.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana, ahsante Mheshimiwa Upendo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mwalimu bado upo? Karibu tuendeleo.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hichi cha 7 nilitaka kiongezwe. Kwanza niseme Muswada wote wa rafiki yangu Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria hakuna ulipotaja chombo kitakachoshughulika na masuala ya majadiliano. Kwa hiyo, nilitaka kiongezwe kifungu pale kitachoelekeza ni chombo gani kishiriki katika masuala ya majadiliano (*negotiation*) katika shughuli za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nataka isomeke namna hii, kwa heshima yako *in clause 7(a) by introducing a new clause 8 as follows: "8(1) There shall be a negotiation committee of not less than ten members appointed by the Minister after consultation with the respective Minister or Ministers responsible the matter to be negotiated upon."*

*"(2) The negotiation committee shall comprise of:*

*(1) one Member representing the Attorney General;*

*(2) one member representing Tanganyika Law Society;*

*(3) two members representing umbrella of mining companies;*

*(4) one member representing Tanzania National Parks;*

*(5) one member representing the Ministry of Lands;*

*(6) one IT expert from the government;*

*(7) Senior Accountant; and*

*(8) two members from Ministry of Natural Resources.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mapendekezo yangu.

**MWENYEKITI:** Mwalimu hapa umechanganya madawa, yaani wewe ninavyojaribu kukuelewa, umejaribu kuleta kifungu kipya ambacho ungependa kiitwe ama kifungu cha sita ama kifungu cha nane. Unapochomeka kwenye kifungu cha saba, kifungu cha saba kina mambo yake yanayojitoshesheza ambayo kwa namna yoyote ile huwezi kupachika haya maneno unayotaka kuzungumza.

Kufuatana na maandishi yako humu inaonekana nia yako ni kuleta kifungu kipya, sasa sijui ama ni kabla ama baada ya Kifungu cha saba lakini ni kifungu kipya kinachojitegemea, siyo ndani ya kile cha saba nafikiri tunakubaliana katika hilo. Kwa hiyo, unataka kiwe Namba nane, mimi nitakikubali kama pendekezo jipya la kwamba iwe nane.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, namba sabatumevuka. Hili ni pendekezo jipya la Kifungu kipya kitakachoitwa kifungu kipya cha 8.

*(Hapa Mhe. Hawa M. Chakoma alipiga kelele na kulia kwa sauti baada ya kuzungumza na simu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie ni habari tunadhani zinaweza zikawa za msiba wa karibu, tukipata taarifa tutawajulisheni. Naomba mtulie Waheshimiwa mtu akipata tatizo mkianza kumzonga wala

haipendezi wale waliokwishaenda nje wanatosha, wanatuwakilisha wengine wote.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nadhani umekipata au arudie pendekezo jipya hili la Mwalimu Bilago.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashauri Waheshimiwa Wabunge hizi simu tuwe tunazima tu.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu hii kila simu inaingia una *communicate* unaweza kupata taarifa yoyote ile.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu ziko aina mbalimbali za mikataba na maudhui tofauti. Sasa ukianza kuweka kwenye sheria watu watakaounda timu hiyo ya majadiliano kwa niaba ya Serikali umejifunga mno. Kwa hiyo, tulichokifanya tumekiboresha kile kifungu cha nane, ile Ibara ya nane tukampa mamlaka Waziri aweze kutengeneza kanuni za namna hata kuunda Kamati. Kinasema *parameters of negotiation, code of conduct* na kadhalika. Haya mambo ya timu iwe inafanyika *admistratively* yaani yanafanyika kiutawala tu, hayawezi yakawekwa kwenye sheria kabisa tangu mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukishafunga hivi ukagundua kwamba kuna watu wengine wanahitajika kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri Mwalimu Bilago hili tumelizingatia kwa maana ya Ibara Mpya, hii Waziri afanye na wanaweza wakati wanaunda hiyo timu unaweza ukapeleka hata mapendekezo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Bilago ukubaliane na mapendekezo ya Serikali katika suala hili.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa ziada Mwalimu Bilago, kwa mfano inatakiwa kufanyika *negotiation* ya suali linalohusu *air space*. Sasa niambie katika Wajumbe wako hapa nani anaelewa haya maneno? Ndiyo maana *negotiation team*

itategemeana na *subject* na kinachokuwa *negotiated*, kwa hiyo Serikali itaangalia sasa pale itengeneze akina nani kwa madhumuni yale. Ikija sijui ya kitu fulani wanawatengenezea akina nani kwa madhuni hayo, kwa hiyo ukiweka *fixed* hapa unakuwa umejifunga. Ndiyo najaribu kumuelewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwalimu Bilago. (*Makofi*)

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuelewa, nilichokuwa nakizungumzia hapa *whether* tunataja *a team or not* tuna *i-list down*. Lakini huelezwi kwamba kutakuwa na chombo, imekaa kichombo chombo hivi, sasa chombo, ni chombo gani kitakachoundwa na nani, ingeeleza basi pale angalau ionekane chombo fulani kitaundwa na Waziri mwenye dhamana kushughulikia masuala ya *negotiation* ingekaa vizuri tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninamuomba tu Mheshimiwa Bilago aweze kulielewa hili, kwanza ukiangalia katika mapendekezo yake yeye amejikita zaidi katika masuala ya maliasili tu.

Pili, ukiangalia katika mapendekezo ya Jedwali la Marekebisho ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria anataka kukitambulisha kifungu kipyua cha 8(2) kwenye mamlaka ya Waziri kwenye kutengeneza Kanuni, pale utaona *parameters* za *negotiation* zitakuwaje, utaona *code of conduct* ya watumishi wa umma au *members* watakaoshiriki katika majadiliano yatakuwaje.

Tatu, majadiliano haya siyo kwamba ndiyo yanaanza kufanyika sasa hivi, ukiangalia Serikalini kwa ujumla wake, katika mikataba mbalimbali tunazo *Government Negotiation Teams*, ikifika wakati husika kwa mujibu ya mkataba inaangaliwa *re-composition* iwe vipi, ndivyo inavyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba tu aweze kukubali na awe na imani kutokana na mazingira husika, madhumuni ya suala husika na suala lenyewe itategemea *composition* iwe vipi.

**MWENYEKITI:** Mwalimu tunakuomba utukubalie.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari baadaye lakini naomba hebu tupate *inputs* mbili tatu za Wabunge. Naomba kutoa hoja Wabunge waniunge mkono katika hili.

**MWENYEKITI:** Hukuungwa mkono Mwalimu, hili liko wazi tu. Mapendekezo ya Mheshimiwa Bilago hayakuungwa mkono kwa hiyo yamedondoka yenyewe. (*Kicheko/Makofi*)

Ibara ya 8

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mapendekezo yangu ya kifungu cha 8(1) yanayosema; "*Without prejudice to the generality of subsection (1) the regulations shall describe the code of conduct for public servants who are involved in the negotiations of investment agreements for natural wealth and resources.*"

**MWENYEKITI:** Hebu isome tena, unataka kesomekeje hicho kifungu cha 8.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongeza kifungu kidogo cha (1) ambacho kinasomeka; "*Without prejudice to the generality of subsection one, the regulations shall prescribe the code of conduct for public servant who are involved in negotiations of investment agreement for natural wealth and resources.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina maana kwamba tutunge katika *regulations* ambazo Waziri ataziweka kiwepo na kipengele cha *code of conduct* ambacho kitaangalia maadili, uadilifu, mwenendo, uwajibikaji wa *Government*



*Negotiation Teams* kwa maana ya wanasheria, wachumi na watu wengine ambao wataenda kuingia kwenye mikataba *over natural resources and wealth* kwa niaba ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Sasa umeeleweka kabisa Mheshimiwa Sabreena. Nikukumbushe tu kwamba siku hizi, kila anayepata nafasi fulani anaapa kwanza kiapo cha uaminifu, lakini ataongezewa. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Sabreena Sungura aosome mapendekezo ya Serikali ya Ibara hiyo kwenye maboresho. Tunazungumza kwamba Waziri; *without prejudice subsection (1) the Minister may make regulation on the following matters, (b) code of conduct for Members of Government Negotiation Team* ambao ni *wider* kuliko yake. Kwa sababu kwenye *negotiation team* siyo lazima wawe Watumishi wa Serikali wanaweza kuwa watu kutoka *private sector*, na wao wakaingia hapa wataapa na watatii. Kwa hiyo, nadhani hoja yake yeye ilikuwa *narrow*, sisi yetu ni *wider* kwamba hata asiyekuwa mtumishi wa Serikali maadam yuko kwenye *negotiation team from the private sector, from anywhere* atakuwa anabanwa na *hyo code of conduct*.

**SPIKA:** Naamini upo *comfortable* Mheshimiwa Sabreena.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa sababu mapendezo ya Mheshimiwa Waziri yamekuja *late* yamepitishwa muda huu. Kwa hiyo, nashukuru kwamba yako pamoja na kile ambacho nilikuwa nakifikiria, naomba tuendelee. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Isije ikaingia kwenye *Hansard* hivyo. Mapendekezo ya Serikali yamepita kwenye Kamati.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali Jipya

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge zima imemaliza kazi yake kwa Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikatoba ya Maliasili za Nchi wa mwaka 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017)*.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikatoba inayohusu Rasilimali na Maliasili za Nchi wa mwaka wa 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikatoba inayohusu Rasilimali na Maliasili za Nchi wa mwaka wa 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017)*, kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana na sasa nitawahoji kwa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi na Kuweka Utaratibu ambapo Wananchi Kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wataweza Kupitia na Kujadili Makubaliano na Mikataba yote inayohusu Rasilimali za Nchi kwa lengo la kujiridhisha endapo Masharti, Makubaliano na Mikataba hiyo haikinzani na maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla *(A Bill for an Act to Make Provisions for Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms of the Natural Wealth and Resources Contracts in order to provide for a mechanism where the people of Tanzania through the National Assembly can review relevant arrangements made by the government to ensure that terms and conditions of such arrangements or agreements are in line with the interest of the people and the United Republic.*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitamke tu kwamba Bunge limeshafanya kazi yake kwa Muswada huo kwa hatua

zake zote, kilichobakia ni Muswada huo kupelekwa mbele ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ili uweze kupata kibali chake kwa mujibu wa Ibara ya 97(1) ya Katiba yetu.

Baada ya kumaliza kazi ya Miswada hiyo miwili niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge ambao mlifanya kazi *tirelessly* (bila kuchoka kabisa) wakati wa *weekend* na kipekee niipongeze sana Kamati ya Pamoja chini ya Mheshimiwa Doto Biteko. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Miswada hii tulipeleka kwenye Kamati nne. Jambo ambalo kwa Bunge la Kumi na Moja ni mara ya kwanza na tulifanya hivyo kwa ajili ya kuongeza uelewa wa idadi ya Wabunge, maana yake ilifikia Wabunge siyo chini ya 100 hivi waliopitia kwa wakati mmoja kama Kamati kifungu kwa kifungu, hatua kwa hatua, pia niwapongeze wadau wote ambao waliweza kufika, hapa Bungeni Dodoma na kuweza kutoa maoni yao, yaliyotusaidia sana katika kuboresha Muswada huu. (*Makofi*)

Mwisho niipongeze sana Serikali, kipekee Mheshimiwa Waziri Profesa Palamagamba Kabudi kwa ushiriki wake mkubwa sana katika jambo hili na jinsi ambavyo yeye na timu yake wamefanya kazi usiku na mchana na mmeona Jedwali la Marekebisha lililokuja la Serikali, ni maeneo ambayo Serikali imekubali na kuyaona na kuboresha, kwa hiyo ni *spirit* nzuri sana ambayo tunaipongeze sana kwa upande wa Serikali kwa kukubali kusikiliza na kuwasikiliza Wabunge na kila ilipowezekana na kubidi tukaweza kurekebisha. (*Makofi*)

Miswada hii miwili ambayo inahusiana na suala la Umiliki wa Maliasili na Mikataba ya Majadiliano ni Miswada ambayo inaliingiza Bunge la Kumi na Moja katika historia ya kipekee kabisa, kwa hiyo kama Spika wa Bunge la Kumi na Moja kwa kweli najisikia faraja kubwa sana kwamba mimi na ninyi wenzangu tunaingia katika historia mpya ambayo tumeangalia maliasili ya nchi yetu, tukaweka sheria ya kuimiliki sisi wananchi wa Tanzania hiyo mali yetu, na

tukaweka taratibu za mikataba, mambo ambayo tumeyapigia kelele kwa miaka mingi sana. (*Makofi*)

Hii ni hatua kubwa, tunaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano hatua hii siyo ndogo hata kidogo, tunaamini kabisa jambo hili litatusogeza mbele. Kama tukiona matatizo kama Watanzania, naamini Serikali ipo na Wabunge tupo, tutakaa na kuzungumza kuona wapi panahitaji kuwekwa vizuri zaidi. (*Makofi*)

Baada ya hayo, nina matangazo mawili. Moja palitokea malalamiko asubuhi na wengine walienda mpaka kwenye vyombo vya habari wakawa wanalalamika kwamba majedwali yao ya marekebisho hayakupokelewa na Ofisi yangu, nitoe tu maelezo kidogo na wengine wameniandikia.

Kuna mmoja nazani atakuwa ni wa Kambi ya Upinzani ameniandikia lakini akasaini kwa niaba ya Mheshimiwa David Silinde, sahihi ile wala siyo ya David Silinde, ni mtu mwingine amechoronga tena pale juu, jambo ambalo siyo la utaratibu. Kama mtu ameandika jina lake na yupo Bungeni, basi ni vizuri yeye mwenyewe asaini mwenyewe ndiyo taratibu zetu. Lakini basi haina neno, alikuwa analalamikia jambo hilo.

Mheshimiwa Chenge alipokuwa Mwenyekiti hapa katika Bunge hili aliwahi kutolea ufafanuzi jambo hili, kwamba marekebisho, ukileta Jedwali lolote la marekebisho ya sheria haiwi jambo la siri wala kuviziana, linakuwa ni jambo ambalo linafanywa kwa nia njema kwa uwazi. Ninaposema kwa nia njema kwa uwazi nina maana gani. Maana yangu ni kwamba siku ambayo jambo husika liko kwenye *Order Paper*, kwamba linaingia hapa na Bunge limekwishaanza ile saa tatu kamili asubuhi ambapo Waziri anayehusika na jambo hili yuko humu Bungeni, wewe Mbunge uko nje unakuja saa nne, saa moja baadaye, nusu saa baadaye, uko nje unapeleka marekebisho kule ofisini, sasa huyu Waziri atayapataje yale marekebisho na atakapoletewa baadaye hapa wakati yuko humu Bungeni na mnajua haya

mambo yana-*consultation* lazima Waziri naye a-*consult*, hivi vitu vya Serikali siyo mtu anasimama tu yeye mwenyewe anarekebisha hapa, anahitaji na yeye a-*consult* kidogo.

Kwa hiyo, siyo uungwana Bunge limeanza wewe unapeleka marekebisho kule na Mheshimiwa Chenge alishaeleza kwa vile wengine tunakuwa hatupo, tupo, inawezekana watu siku hiyo hamkuwepo. Kwa hiyo, marekebisho kama yapo ya kesho ya lini, yapelekwe mapema Bunge linapoanza saa tatu ndiyo mwisho wa marekebisho yoyote yale. Yale yanayokwenda kabla ya hapo yanampa nafasi Waziri kuyapokea, kuyaona na kuya-*assign* kwa maofisa wake kama wapo, mchakato ule unaendelea, wakati ule wa maswali na nini mchakato unaendelea wanafanyia kazi jambo lako, kama ni kujiunga nawe, au kama ni kuchukua mawazo yako sasa wayaingize mle ili wao watengeneze *schedule* tena na wao na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tukielewana hivyo malalamiko haya mengine wala hayatakuwepo. Tutakuwa tunawapa tu wananchi tu picha ambayo siyo sawa, kwamba hapa kuna utaratibu wa kukandamiza wengine na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, kama umepeleka jedwali lako kabla ya saa tatu na likakataliwa, hapo ndiyo itakuwa ni hoja ambayo Spika anahitaji kualiriwa ili aweze kurekebisha jambo hilo haraka sana.

Waheshimiwa Wabunge, rafiki zangu akina Mheshimiwa Mnyika walikuwa wanalalamika asubuhi, hili jambo siyo sawa. Mheshimiwa John Mnyika yeye amepeleka pale kama saa 03:35 au 03:40 asubuhi na leo alikuwa amepiga *white*, amefuatana na Mheshimiwa wa Zanzibar Mr. *White* Mheshimiwa Salim Hassan Abdullah Turkey, eeeh! Wamepiga wote nyeupe isipokuwa viatu rangi tofauti. Kwa hiyo, hata mimi niliwaona na niliangalia saa yangu hawakuwa ndani ya utaratibu hata kidogo. (*Kicheko*)

Lakini tukija humu ndani ya Bunge, tunalalamika

tunawafanya wananchi wanaamini kabisa kwamba tunaonewa kumbe ni taratibu ambazo tumejiwekea hatuzingatii. Kwa hiyo, hilo ni la jambo la kwanza kwa wenye marekebisho ya kesho wahini mapema, hata kuanzia leo anzeni kupeleka kwa Katibu ili yaweze kufanyiwa kazi mapema, hakuna mtu anayeogopa rekebisho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili, kwa masikitiko makubwa naomba nisome maelezo au taarifa ya Spika kwenu, kuhusu vurugu alizofanyiwa Mbunge wa Viti Maalum Mheshimiwa Juliana Shonza leo.

Waheshimiwa Wabunge, leo Jumatatu, tarehe 03 Julai, 2017 baada ya shughuli za Bunge kusitishwa kwa mapumziko ya mchana, kuna jambo limetokea ambalo nimetaarifiwa kwenye lango la kuingilia Jengo la Utawala, hapa Ofisi ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika tukio hilo Mheshimiwa Juliana Shonza akiwa langoni hapo alikutana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani ambao walirushiana naye maneno na kumzonga zonga kwa nia ya kutaka kumpiga kutokana na utendaji wake kazi Bungeni...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**SPIKA:** ...hususani hoja yake aliyoitoa Bungeni tarehe 5 Juni, 2017 ya kubadilisha pendekezo la adhabu lililotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Ester Bulaya, hoja hiyo ya Mheshimiwa Juliana Shonza ilisababisha Bunge kuazimia kuongeza adhabu kwa Wabunge hao.

Waheshimiwa Wabunge, Sheria na Kanuni zetu zinatoa makatazo na zinaainisha vitendo mbalimbali ambavyo ni makosa na havitakiwi kabisa kufanyika katika maeneo ya Bunge. Mathalani Sheria ya *Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act*, Sura ya 296 katika kifungu cha 31(a) inatamka: *"Any person shall be guilty of an offence who –*

*(a) assaults, obstruct or insults any member or officer going to or coming from the precincts of the Assembly Chamber."*

Aidha, kifungu cha 31(d) nacho kinatamka kwamba; *"Any person shall be guilty of an offence who- (d) challenges any member to a fight on account of his conduct as such member."*

Waheshimiwa Wabunge, miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge wanaodaiwa kufanya vitendo hivyo vya kumzonga zonga na kutaka kumpiga Mheshimiwa Juliana Shonza ni pamoja na hawa wanane wafuatao:-

1. Mhe. Saed Kubenea;
2. Mhe. Joseph Selasini;
3. Mhe. Susan Kiwanga;
4. Mhe. Devotha Minja;
5. Mhe. Cecil D. Mwambe; (*Kicheko*)
6. Mhe. Frank G. Mwakajoka;
7. Mhe. Pauline P. Gekul; na
8. Mhe. Cecilia D. Paresso.

Waheshimiwa Wabunge, nimesema wanaodaiwa, yawezekana kuna utofauti wa uonekano au vipi, lakini inavyosemekana.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili kwa jinsi nilivyolipokea mimi ni suala la kijinai, na mara zote tumekuwa tukiwaelekeza kwamba Wabunge hata mnapokuwa ndani ya maeneo ya Bunge hamna kinga dhidi ya makosa ya jinai. Natumia fursa hii kuwajulisha kwamba Mheshimiwa Juliana Shonza ameniomba na nimempa kibali cha kulifikisha suala hili katika Jeshi la Polisi ili lifanyiwe kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu za kijinai. (*Makofi*)

Aidha, kwa kuwa suala hili pia ni la kimaadili na kwa mujibu wa sheria na Kanuni zetu masuala yote ya Maadili ya Wabunge yanafanyiwa kazi na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya



Nne ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 nalipeleka suala hili mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili ilifanyie uchunguzi na nini hasa kilitokea. Nani hasa walihusika na kisha kutoa maoni na mapendekezo kuhusu hatua za kuchukua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kwa kuwaomba kujiepusha sana na masuala ya makosa ya kijinai. Kama tulivyosema mwanzo sisi Kanuni zetu mambo ya kijinai hatushughuliki nayo, tunashughulika na mambo ya kimaadili. Kwa hiyo, kwa yale ya kijinai basi ingekuwa ni vigumu sana mimi kumzuia Mheshimiwa Juliana kwenda kwenye vyombo vya dola, ili kuona haki inatendeka, na kwa yale ya kimaadili kwa ratiba zetu zilivyo tutaangalia namna gani Kamati yetu itakavyofanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, niseme tena kwa upole mkubwa, ndugu zangu na tumesema mara nyingi, mimi mwenyewe binafsi na hata miongoni mwenu tumezungumza sana, suala la maadili, suala la kuishi kiutu, kwa pamoja kwa ushirikiano, lakini tukitofautiana pale ambapo ni lazima kutofautiana, tukiungana mkono pale ambapo ni lazima kuungana mkono. Jambo hili ni la kusikitisha sana, jambo hili ni la kukemewa, kwa sababu tu hatujui uhakika wa jambo lenyewe, hatuwezi kusema sana. Endapo ni kweli limetokea basi ni jambo la kutia aibu Bunge letu kwa mara nyingine tena.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo shughuli za leo zimekamilika, kwa jinsi hiyo masuala yanayohusu Mheshimiwa Hawa Mchafu tutayasemea kesho ili tuweze kuwa na hakika ya nini tunatangaza hapa ndani. Kwa hatua hiyo, kwa vile shughuli za leo zimekamilika, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1.17 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 4 Julai, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*